# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TANO

### Kikao cha Saba – Tarehe 8 Novemba, 2016

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Tunaendelea na Mkutano wa Tano, Kikao cha Saba, lakini kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyotangaziwa na Mheshimiwa Mwenyekiti, Mussa Azzan Zungu jana, kuhusiana na taarifa ya msiba. Tunaendelea kuomboleza msiba wa mpendwa wetu Marehemu Mzee Samuel John Sitta, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa. Msiba uliotokea jana huko Munich, Ujerumani.

Mazishi ya Spika Mstaafu yako kwa mujibu wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi ya 2006 ambapo Serikali ndiyo inayoratibu taratibu zote za mazishi hayo. Labda kwa ambao hawakumbuki vizuri niwakumbushe tu, kwamba mazishi ya viongozi yana-*categories* kubwa mbili; kuna mazishi ya kitaifa yanayowahusu viongozi wa juu , Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu Wastaafu au walioko madarakani na mazishi ya Kiserikali ni ambayo yanahusu Jaji Mkuu na Spika. Kwa hiyo, mazishi ya Mheshimiwa Sitta yatakuwa ni mazishi ya Kiserikali. Kwa hiyo, sisi Bunge tunaendelea kuwasiliana na wenzetu Serikalini kwa kuwa wao ndio waratibu wa mazishi hayo ya Kiserikali. Tutaendelea kupeana taarifa kuhusu taratibu za mazishi hayo na namna Bunge letu linavyoweza kushiriki katika kumuaga Marehemu mpendwa wetu.

Jana Tume ya Utumishi wa Bunge iliketi na kuandaa mapendekezo ya namna ambavyo Bunge linaweza likashiriki katika ratiba nzima ya mazishi hayo ya Kiserikali; na tumetuma maafisa wetu Dar es Salaam kwenda kuungana na maafisa wengine wa Serikali walioko kule kuwa katika timu inayoratibu shughuli nzima ya mazishi.

Ofisi ya Bunge ilikuwa ikigharamia matibabu yake Marehemu kuanzia alipokuwa hospitali nchini India baadaye tukalazimika kumpeleka hospitali za Uingereza na mwishowe hospitali za nchini Ujerumani ambako mauti yamemkuta. Hivyo Ofisi ya Bunge ndiyo itakayogharamia usafirishaji wa mwili wake kutoka Ujerumani na kurejea hapa nchini.

Mwili huo unatarajiwa kuondoka leo nchini Ujerumani kuja Tanzania na baada ya vikao ambavyo nimeshavielezea, vinavyoendelea hivi sasa ndani ya Serikali, tutajulishana namna bora ya ushiriki wetu.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mambo mengine niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba tunao utaratibu ambapo Mbunge mwenzetu akifiwa tuna namna ambavyo huwa tunafanya ushiriki. Tukumbuke katika msiba huu Mama Margaret Sitta ambaye ni Mbunge mwenzetu amefiwa na mume wake. Kwa hiyo, ule ushiriki ambao huwa tunaufanya katika taratibu zetu sisi kama Wabunge pia tutafanya katika jambo hili.

Lengo letu ni mwili huo pamoja na mambo mengine kuweza kuletwa hapa Bungeni Dodoma kabla Wabunge hatujaondoka ili Wabunge wote tuweze kupata fursa ya kumuaga Marehemu. Kama nilivyosema, tutaendelea kujulishana ratiba nyingine kadri tunavyozidi kupata habari na kadri tunavyoendelea na mipango ya mazishi. *(Makofi)*

Niungane nanyi katika kumuombea mwenzetu ili Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Katibu!

**RAMADHANI I. ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Swali la kwanza tunaelekea Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Neema Mgaya. Mheshimiwa Neema Mgaya.

Na. 69

### Tatizo la Ajira kwa Vijana Nchini

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Vijana wengi nchini wanakabiliwa na tatizo kubwa sana la ukosefu wa ajira.

Je, Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA:** alijibu:-

Mheshiwa Spika, kwa niaba wa Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti wa nguvukazi wa mwaka 2014, kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana ni asilimia 11.7. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imejipanga kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Ujuzi Nchini ambao umelenga kutoa mafunzo ya vitendo yatakayofanyika maeneo ya kazi. Aidha, ili kuwapa vijana wengi fursa za mafunzo Serikali imeanzisha programu maalum ya kutambua ujuzi uliopatikana kupitia mfumo usio rasmi na kuurasimisha kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wale watakaobainika kuhitaji na kuwapa vyeti.

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha hilo kwa sasa Serikali inaendelea kufundisha vijana 400 katika kiwanda cha *Took Garment Company Ltd.* lengo ni kufundisha vijana 1000. Mafunzo mengine yataanza mwezi Novemba, 2016 katika kiwanda cha *Mazava Fabrics,* Morogoro pamoja na *DIT* Mwanza ambayo ni kwa ajili ya kutengeneza viatu na bidhaa za Ngozi. *VETA* nchi nzima watafundishwa vijana 4000. Serikali inaendelea kujadiliana na taasisi nyingine zikiwemo kiwanda cha Karanga Moshi na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuwezesha vijana kuwa wajasiriamali kwa kuwatambua vijana na mahitaji yao katika ngazi mbalimbali na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi mbalimbali ya vijana.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuhamasisha vijana wenye utaalamu mbalimbali kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira hususani kilimo na biashara.

Aidha, Serikali itajikita zaidi kuhamasisha vijana na kuwawezesha kuwekeza kwenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili kufikisha lengo la

asilimia 40 ya nguvu za kazi nchini kuwa katika sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2020 kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuendelea kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao kupitia mfuko huo vikundi vya vijana 6,076 vyenye wanachama 30,380 vimepata mikopo yenye masharti nafuu ya kiasi cha shilingi takribani bilioni moja na milioni mia sita kupitia kwenye *SACCOS* zao za Halmashauri za Wilaya ili ziweze kuwakopesha vijana mikopo ya masharti nafuu na hivyo vijana waweze kujiajiri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia ratiba ya siku ya leo imejaa kweli kweli kutokana na kutoendelea kwa shughuli hizi jana. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki cha maswali watakouliza maswali ni wale wenye maswali ya msingi peke yao. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa tatizo la ajira ni kubwa na kwa kuwa tuna miradi mingi ya kilimo; kwa mfano kilimo cha chai kule Njombe, miwa Kilombero, kahawa, pamba kule Kanda ya Ziwa na katika miradi hii kuna fursa ya kuweka programu ya *outgrowers*.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua Serikali inatumia vipi hii fursa ya programu ya *outgrowers* kuwashirikisha vijana ili kuweza kutatua tatizo la ajira nchini?

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tatizo hili la ajira nimekuwa nikilizungumzia mara kwa mara takribani miaka sita tangu nilipokuwa ndani ya Bunge hili, tangu nilipokuwa Mbunge wa Vijana. Nilitaka kujua, Serikali iniambie imeweza kutatua kwa kiasi gani tangu nianze kuzungumzia tatizo hili?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Mavunde, na wewe mwenyewe ni kijana.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI AJIRA NA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameuliza namna gani Serikali tunaweza tukawashirikisha vijana kwenye fursa mbalimbali hasa za kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 mwezi uliopita kupitia Wizara ya Kilimo pamoja na sisi Wizara chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu tumezindua mpango maalum wa kilimo ambao utawashirikisha vijana. Lengo lake ni kuwaweka

vijana hawa katika makundi mbalimbali kutokana na mikoa yao waweze kushiriki katika kilimo cha nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu tunakwenda pia sambamba na mpango ambao upo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambao ni mpango wanaouita *ODOP (One District One Product)* na lengo lake ni kufanya kitu kinachoitwa *District branding* ya kila sehemu kwa nchini nzima ambako shughuli za kilimo pamoja na shughuli nyingine za ujasiriamali zinafanyika. Kuwepo na kitu cha utambulisho katika Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inatambua kabisa kilimo biashara ni kati ya eneo ambalo linaweza likachukua vijana wengi kwa wakati mmoja, na tumeweka msisitizo mkubwa kuhakikisha kwamba makundi makubwa ya vijana yanapata fursa ya kuweza kushiriki katika uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, katika swali lake ameuliza ni kwa kiwango gani sasa tumetatua changamoto hii. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba takwimu zinasema ukosefu wa ajira hasa kwa vijana nchini Tanzania umepungua kutoka asilimia 13.7 ya mwaka 2012 mpaka asilimia 11.7.

Mheshimiwa Spika, lakini ukilinganisha Tanzania na nchi nyingine za jirani kwa maana ya Kenya na Uganda; tatizo la ukosefu wa ajira kwa Kenya ni takribani asilimia 17.3, kwa Tanzania tumekwenda mpaka asilimia 11.7.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni dhahiri kwamba Serikali kupitia mipango yake mbalimbali imejaribu kutengeneza mazingira wezeshi kwa ajili ya vijana kutengeneza fursa mbalimbali na vijana wengi wameendelea kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, nimuondoe hofu kwamba tunayo mipango madhubuti ya kuendelea kusaidia kundi kubwa hili la vijana waweze kupata ajira na kuondoka katika adha hii ya ukosefu wa ajira.

Na. 70

**Ujenzi wa Barabara ya Kilometa 10 Ndani ya Mji wa Nzega**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali inakusidia kuanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya kilometa 10 ndani ya Mji wa Nzega kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi wakati wa kampeni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge wa Jimbo la Nzega Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua za awali za utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kilometa 10 za barabara kwa kiwango cha lami zimeshaanza, ambapo kazi zilizofanyika ni upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, kuandaa michoro na makisio ya kazi za ujenzi wa kilometa 10. Mtandao huo wa barabara utajengwa katika Kata ya Nzega Mjini Mashariki, sawa na kilometa tano na Nzega Mjini Magharibi kilometa tano zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, gharama za kutekeleza mradi huo ni shilingi bilioni 5.2 ambazo zitahusisha ujenzi wa mitaro ya barabara na makalavati ikiwemo mitaro mikubwa katika eneo la Samora, ujenzi matabaka ya barabara ya changarawe na ujenzi wa mtabaka mawili ya lami nyepesi.

Mheshimiwa Spika, makisio ya gharama hizo yatazingatiwa katika bajeti ya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kuanza utekelezaji kwa awamu.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Nilitaka kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shilingi bilioni 5.2 ni sawa sawa na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa zaidi ya miaka mitatu, na kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Nzega haina uwezo wa kifedha na ndio ilikuwa mantiki ya kumuomba Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na baadaye Rais John Pombe Magufuli kwamba miradi hii ya ujenzi wa kilometa 10 iende chini ya *TANROADS*.

Je, sasa Serikali iko tayari kuwaambia wananchi wa Jimbo la Nzega kwamba miradi hii ya kilometa 10 itajengwa chini ya utaratibu wa *TANROADS* na si kwa kutumia fedha za Halmashauri ya Mji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nafahamu Halmashauri ya Mji wa Nzega mapato yake ni madogo, na Mheshimiwa atakumbuka takribani wiki tatu na nusu au

wiki nne tulikuwa wote kule Nzega tukihamasisha shughuli za maendeleo. Nipende kumshukuru sana kwa juhudi kubwa anazozifanya katika Jimbo lake

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishieni kwamba hii ni *commitment* ya Serikali na ahadi ya Mheshimiwa Rais. Katika hivi ukiachia hata huo uchache wa mapato, hata ujenzi wa miundombinu katika maeneo mengine tunayoyafanya hivi sasa si kwamba Halmashauri hizo zinauwezo huo.

Mheshimiwa Spika, si muda mrefu tutaanza mchakato hata katika Mji wa Mpwapwa na maeneo mengine mbalimbali hapa nchini. Naomba nisema wazi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa makusudi imeamua kubadilisha miundombinu ya Manispaa na Majiji ya maeneo mbalimbali, na ndiyo maana utakuta katika miji mikubwa, Manispaa na Halmashauri za Miji sasa hivi mitandao ya barabara imeimarika.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Bashe amepata fursa kubwa, ambapo Mamlaka ya Mji wake vile vile tayari umesha-*qualify* sasa kuingizwa katika mipango ya ujenzi wa barabara za lami. Kwa hiyo, naomba nimtoe hofu, Serikali itahakikisha ahadi ya Mheshimiwa Rais inatekelezwa, tunajua mapato yenu ni madogo. Lakini pia ni *commitment* ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuhakikisha kwamba miji yote inajengewa barabara za lami. Ondoa hofu Serikali itatekeleza hilo kwa kadiri iwezekanavyo.

Na. 71

**Mabasi Yaendayo Kasi**

**MHE. KANALI (MST.) MASOUD ALI KHAMIS (K.n.y MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI)** aliuliza:-

Serikali imeanzisha mabasi yaendayo kwa kasi katika Jiji la Dar es Salaam lakini madereva wengi wamekuwa wakiendesha magari hayo kwa kasi kubwa; kiasi cha kuhatirisha maisha ya watu waendao kwa miguu.

(a) Je, ni lini Serikali itawachukulia hatua madereva ambao hawafuati Sheria za Barabarani?

(b) Je, ni muda gani magari hayo ya *DART* yamepangiwa kuanza kazi na kuda wa kumaliza kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Muheshimiwa Ibrahim Hassanali Mohammedali Mbunge wa Kiembesamaki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, (a), madereva wa *DART* wanapaswa kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani kama ilivyo kwa dereva yeyote. Tangu mabasi yaanze kutoa huduma madereva 20 wamepewa onyo kwa makosa ya usalama barabarani na wawili wamefukuzwa kazi. Aidha, madereva 40 wamekatwa mishahara kwa makosa mnalimbali kwa kukiuka sheria za barabarani.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti mwenendo wa mabasi, mabasi yamefungwa vifaa maalumu katika magari ili kutoa ishara kwa dereva anapozidisha mwendo ambao ni kilomita 50 kwa saa. Aidha, Serikali imeweka utaratibu wa kuwajengea uwezo madereva kupitia semina zinazoendeshwa na wataalam kutoka *NIT na VETA* na Askari wa Usalama Barabarani ili kuwakumbusha taratibu na maadili ya kazi ya udereva.

Mheshimiwa Spika, (b), kwa kuzingatia mazingira ya Jiji la Dar es Salaam kuhusu huduma za usafiri, mkataba baina ya *DART* na mtoa huduma ambaye ni *UDART* umeainisha kwamba huduma ya mabasi yaendayo haraka itaanza saa 11.00 alfajiri hadi saa 06.00 usiku.

**MHE. KANALI (MST.) MASOUD ALI KHAMIS :** Mheshimwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba kuuliza swali la nyongeza.

Je, mabasi haya yana idadi maalum ya kupakia abiria na kama hayana idadi ni kwa nini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza Mheshimiwa Waziri –TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza tuna mabasi ya aina mbili, yale mabasi marefu zaidi na mabasi mafupi, na mabasi haya kila basi lina idadi yake.

Kwa hiyo, nimuondoe shaka Mheshimiwa Mbunge, mabasi haya yana idadi maalumu isipokuwa wakati mwingine katika vituo mabasi yakifika watu huwa wanakimbizana kuingia ndani ya mabasi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu umewekwa kuhakikisha kuwa watu wanapanda mabasi hayo kwa kuzingatia idadi yake ili kulinda usalama wa raia katika suala zima la usafiri.

Na. 72

**Serikali ya China Kuchangia Matibabu kwa Wanaopata Ajali na Bodaboda**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali ya Watu wa Jamhuri ya China wasichangie huduma za afya kwa wananchi wanaopata ajali zinazotokana na waendesha bodaboda?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO** ajilibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Jimbo la Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa sasa kumekuwepo na ongezeko la ajali nyingi za bodoboda ambazo zinaongeza gharama za matibabu. Ongezeko la ajali hizi limekuwa likichangiwa na sababu mbali mbali ikiwemo vifaa hivi kutofanyiwa matengenezo ya mara kwa mara, madereva kukosa umakini, ulevi, uzoefu na miundombinu chakavu.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vinapoingia nchini kuna mamlaka mbalimbali ambazo zinasimamia uingiaji wake. Mamlaka hizi ni pamoja na ile ya udhibiti wa ubora yaani *TBS* na Mamlaka ya Mapato *(TRA)* ambapo hulipiwa ushuru kabla havijaingia sokoni.

Aidha, kabla mtumiaji hajaanza kutumia kwa biashara inamlazimu kukata leseni ambayo pia hukusanywa na Serikali. Sanjari na hilo ni vyema kufahamu kwamba pikipiki zinazoingizwa nchini zinatoka nchi mbalimbali na si China peke yake.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo ninatarajia kuiwasilisha hapa Bungeni, nimependekeza kuwa kila mwananchi awe na kadi ya bima ya afya ili e ndapo atapata ajali aweze kupata matibabu bila kiwazo chochote.

Mheshimiwa Spika, hata kama watu wote watakuwa na bima, suala hili la ajali za bodaboda halikubaliki na halivumiliki. Ninaomba wote tukemee vitendo vya uendeshaji mbaya wa bodaboda ili kulinda uhai wa wananchi wetu. Aidha, ninaliomba Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani kuendelea kulisimamia suala hili ili kupunguza ajali za barabarani zinazoweza kuepukika.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa napenda niishukuru Serikali kwa kukiri udhaifu mbalimbali ambao unaweza kuwa unasababishwa na ajali zinazoweza kuwa zinatokea ambazo zimeelekezwa kwenye swali la msingi ikiwemo ni pamoja na uzoefu na uchakavu wa miundombinu. Swali langu la nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba wote tunafahamu Tanzania na China ni nchi marafiki na bidhaa nyingi za biashara karibu asilimia 95 zikiwemo pikipiki za bodaboda zimekuwa zikitoka China.

Swali langu, je, ni kwa nini Serikali sasa isione namna ambayo inaweza ikafanya mazungumzo na Serikali ya China kwa kuangalia bidhaa ambazo zinaingizwa zikiwemo za bodaboda na vitu vinginevyo ili Serikali ya China ama kupitia makampuni yanayoagiza hizi pikipiki kuweza kuchangia katika zahanati zetu kama vile ambavyo wawekezaji wengine wanavyofanya katika kutoa huduma za jamii? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, pamoja na kuanzishwa na kuletwa hiyo Sheria ya Bima, je, Serikali haioni pamoja na hayo yote, kuiomba na kufanya mazungumzo na Serikali ya China pia katika kusaidia kuongeza vifaa tiba? Kwa sababu bima peke yake haimsaidii mwananchi aliyekatika miguu miwili ama mmoja kuweza kutibiwa na bima, bado atahitaji kununua mguu wa bandia na vitu vinginevyo na hospitali za Serikali yetu bado hazina uwezo katika wa kuwa na vifaa kama hivyo. Je, hawewezi wakafanya mazungumzo ili kuweza kupatiwa huduma hasa za afya ambazo zinaweza zikaenda moja kwa moja vijijini kwa wananchi wetu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, swali la kwanza nadhani lilikuwa ni la Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kama Waziri alilisikia; na swali la pili ni la Wizara ya Afya.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Watengenezaji wa pikipiki na magari yao yanakidhi viwango na *TBS* inathibitisha. Tatizo kubwa la ajali za bodaboda au hizi gari aina ya Noah ni kwa ajili yetu sisi watumiaji. Watu wanaendesha bodaboda wakiwa wamelewa,

wanapakiana watano mpaka sita, huwezi kumlaumu mtengenezaji. Hata chakula, ukila kilo 10 za pilau zitakudhuru. Kwa hiyo ni juu yetu sisi Watanzania tufuate masharti ya kutumia hivyo vifaa sio tatizo la Mchina. *(Makofi/kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kitaalamu ajali inaweza ikasababishwa na matatizo yanayoweza kujitokeza katika ngazi nne tofauti. Katika ngazi ya mtumiaji, katika ngazi ya chombo, lakini pia katika mazingira ambapo ajali imetokea kwa maana ya *design of the road* na vitu kama hivyo.

Sasa matatizo yote haya imeonekana kwa kipindi kirefu yanasababisha ajali za barabarani ambazo zinasababisha maumivu kwa watumiaji ama muda mwingine zinasababisha vifo. Yote haya ambayo ni madhara yanayotokana na ajali za barabarani mwisho wa siku yanakwenda ku-*impact* mfumo wa afya, yanaenda kuongeza mzigo wa gharama kwenye kutoa huduma za afya. Ndiyo maana Serikali sasa inakuja na mkakati wa kufikiria namna ya ku-*charge* gharama fulani kwenye kila chombo cha moto ambacho kitaingia barabarani kabla hakijaingia barabarani. Tozo hiyo itakuwa inatozwa kila mwaka, lakini bado tuna mazungumzo ndani ya Serikali kuona kama jambo hili litakubalika ili tuweze kulileta sambamba na mapendekezo mengine kwenye Sheria ya *Single National Health Insurance* ambayo tunatarajia kuileta hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo yetu ni kwamba wote wanaopata ajali wawe na bima za afya ili waweze kupatiwa huduma pale ambapo inajitokeza wamepata matatizo yoyote ya kiafya. Lakini hatuwezi kuchukua mzigo wa magonjwa ya watu wetu tukaurundika kwa Wachina eti kwa sababu wanaunda vifaa vya moto, hapana. Jukumu la kutoa huduma za afya zilizo bora kwa Watanzania ni la Serikali yao na hatujalishindwa bado.

**SPIKA:** Ahsante sana, bado tupo Wizara hiyo hiyo ya Afya sasa swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Mkoa wa Dodoma.

Na. 73

**Tatizo la Ukeketaji Katika Baadhi ya Jamii Nchini**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Tatizo la ukeketaji katika jamii nyingi nchini bado ni kubwa na sasa ukeketaji huo unafanywa kwa usiri mkubwa hasa baada ya jamii hizo kugundua kuwa ipo sheria dhidi ya ukeketaji.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia ukatili huu wanaofanyiwa watoto wachanga na kuhatarisha maisha yao?

(b)Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru watoto wachanga dhidi ya ukatili huu wa ukeketaji unaofanywa na baadhi ya jamii nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, (a) Serikali katika kufuatilia ukatili wa watoto wachanga imekuwa na mikakati mbalimbali ikiwa ni pamona na kuwa na vikundi vya uelimishaji kupitia mangariba, kuanzisha madawati zaidi ya 417 ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi, kuanzisha mtandao wa huduma ya mawasiliano ya kusaidia watoto namba 116 *(child helpline)* pamoja na uanzishwaji wa timu za ulinzi wa mtoto katika Halmashauri mbalimbali ili kukabili tatizo la ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuongeza msukumo zadi katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuachana na mila zilizopitwa na wakati pamoja na ufuatiliaji kupitia wauguzi toka mtoto alipozaliwa hadi anapotoka hospitalini.

Mheshimiwa Spika, (b), Serikali inaendelea na mkakati wa kutoa elimu ya uzazi salama kwa wakunga wa jadi, akina mama na wauguzi katika zahanati na vituo vya afya kubaini na kutoa taarifa kuhusu mtoto aliyekeketwa ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya mzazi huyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, mikataba ya kimataifa na ya kanda kuhusu haki na ustawi wa mtoto na Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009; na pia kutekeleza Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2012, kifungu cha 169(1)(a) pamoja na Mpango wa Taifa wa Mwitikio na Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto wa mwaka 2013 hadi 2016.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeandaa mpango kazi wa Taifa wa kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaoanza mwaka 2017 hadi mwaka 2022 utakaozinduliwa Novemba, 2016, ambapo masuala ya ukatili hasa utokomezaji wa mila na desturi zinazopelekea ukeketaji zitashughulikiwa ipasavyo.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali imeandaa utaratibu wowote wa kuwakagua watoto ambao wapo chini ya umri wa miaka mitano katika kliniki au wasiohudhuria kliniki ili kuweza kupata takwimu sahihi za watoto ambao wamekeketwa chini ya miaka mitano ili kufahamu ukubwa wa tatizo ukoje? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba katika mfumo wa kutoa huduma za afya nchini watoto wote chini ya umri wa miaka mitano wanapaswa kuhudhuria kliniki ya *RCH* ili wapate chanjo mbalimbali lakini pia wazazi wao waweze kufikiwa na elimu mbali mbali ambazo zinatolewa kila siku kabla ya kuanza kwa kliniki hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na utaratibu huo watoto wote wachanga sasa hivi kuna mpango maalum chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa kuwaelimisha wauguzi wote nchini kufanya ukaguzi maalum wa watoto hususani wa kike kuhusiana na mambo ya ukeketaji ili tuweze kuwabaini wazazi ambao wamewapeleka watoto wao wachanga kufanyiwa ukeketaji.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo huduma hiyo sasa ipo na inaendelea kutolewa nchini. Nitoe onyo kwa wazazi wote ambao wanaendelea na vitendo hivi, kwamba wakikamatwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao kwa sababu kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi utaratibu umehama badala ya kuwakeketa mabinti wakubwa, sasa hivi wazazi wamegundua kwamba wawakekete watoto wachanga. Jambo hili halikubaliki na tutachukua hatua kali, na ndiyo maana tumeweka sasa mkakati wa kutoa elimu kwa wauguzi wafanye ukaguzi maalum kwa watoto wa kike kama wamekeketwa ama la, kwa hiyo utaratibu upo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hiyo hatari kubwa hiyo. Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe Augustino Manyanda Masele.

Na. 74

**Maeneo ya Nyakafuru na Kenegere Kugawiwa kwa Wachimbaji Wadogo**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Mbogwe limejaaliwa kuwa na madini ya dhahabu na utafiti umekuwa ukiendelea bila uchimbaji kufanyika katika maeneo ya Nyakafuru, Kenegere na kadhalika.

Je, ni lini Wizara ya Nishati na Madini itayaachia maeneo haya na kuyagawa kwa wachimbaji wadogo wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Nyakafuru lenye leseni ya ukubwa wa kilometa za Mraba 17.53 linamilikiwa na kampuni ya *Mabangu Mining Limited* ambayo ni kampuni tanzu ya *Resolute Tanzania Limited* kupitia leseni PL 5374 ya 2008, leseni hii imeisha muda wake tarehe 23 mwezi wa 10 mwaka huu na kuombewa *extension*. Hadi sasa mashapo yamefikia tani milioni 3.36 zenye wakia 203,000 za dhahabu yamegunduliwa, na jumla ya dola za Marekani milioni 1.83 zimetumika kufanya utafiti katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, eneo la Kenegere lina leseni ya utafiti PL 4582 ya 2007 ambayo imeombewa pia *extension* kupitia PL 6748 ya 2010. Lakini kuna PL 8329 ya 2012 zinazomilikiwa na kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* ambapo mradi huo kwenye ukubwa wa kilometa za mraba 13.18 upo katika hatua ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, kampuni hiyo imetumia zaidi ya dola za Marekani milioni 23 kufanya utafiti na imeainisha mashapu ya dhahabu tani milioni 13 zenye wakia 545,000.

Mheshimiwa Spika, pia eneo la Kanegele lina lesni ya utafiti wa madini PL 10159 ya 2014 yenye ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 6.39 pamoja na leseni ya kuhodhi eneo RL 0014 ya 2014 yenye ukubwa wa kilometa za 2.94, kampuni pia inamiliki na leseni ya kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* kupitia kampuni yake tanzu ya Mabangu. Mipango ya uendelezaji wa mgodi katika

eneo hilo inaendelea kwa kuzingatia mwenendo wa bei ya dhahabu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, ili kutohodhi shughuli za utafutaji zinazoendelea katika eneo hilo Wizara ilishauriana na uongozi wa Wilaya ya Mbogwe tarehe 20 Aprili, 2015 na kuamua kutenga maeneo ya Shenda kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Aidha, Kampuni ya *Resolute Tanzania Limited* imeridhia kutoa leseni ndogo tatu katika eneo la Bukandwa.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa kampuni ya *Resolute* imekuwa ikifanya utafiti kwa muda mrefu ni lini sasa Serikali itaitaka kampuni hii iweze kufungua mgodi kwa ajili ya manufaa ya Wilaya hii ya Mbogwe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, yapo mazungumzo baina ya Serikali pamoja na kampuni yanayoendelea kuhakikisha kwamba kampuni hii inaachia eneo la Kanegere ili kusudi wananchi waweze kupata maeneo ya kuchimba dhahabu. Ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atatembelea Mbogwe kuweza kuhakikisha kwamba jambo hili linaafikiwa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Kampuni ya *Resolute* imekuwa ikifanya utafiti kwa muda mrefu na sasa hivi shughuli za utafiti kimsingi zimekamilika na hatua inayofata sasa ni kufungua mgodi. Kulingana sasa na taratibu za ufunguaji mgodi kampuni iko tayari kuanza kufungua mgodi miezi sita ijayo kutegemea sasa na bei ya soko la dhahabu pamoja na upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kutembelea eneo, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Masele anavyowatafutia maeneo wachimbaji wadogo. Hivi sasa katika eneo la jimbo la Mbogwe, Wizara imeshatenga maeneo yanayoitwa Shenda Kaskazini ambayo yana ukubwa wa hekta 990.99 na eneo hilo litapatiwa leseni 100 kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hatua hiyo bado Wizara pia imezungumza na mwekezaji na kupata eneo lingine la Kanegere namba mbili ambalo litakuwa na ukubwa wa hekta 177 ambazo pia zitapatikana leseni 18.

Lakini kadhalika eneo la Bukandwe ambalo Mheshimiwa amelizungumzia pia kampuni imeachia eneo la ukubwa wa hekta 300 ambapo pia zinapatikana leseni kama 10.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Masele nimshukuru sana kwamba, wachimbaji wake watapata maeneo mengi na nitatembelea huko mara baada ya Bunge hili kuahirishwa.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, sana tunaendelea swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mbinga Vijijini Mheshimiwa Msuha popote pale ulipo.

Na. 75

**Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini – Mbinga**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

Wananchi wa Mbinga wanaishukuru Serikali kwa mradi wa kusambaza umeme vijijini kwani wana imani mradi huo utasaidia kuinua hali za maisha. Hata hivyo ni vijiji 34 tu ndiyo vimepatiwa umeme kupitia mpango wa usambazaji umeme unaotekelezwa na *REA* Awamu ya Pili.

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika vijiji 118 vilivyosailia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Martin Alezander Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali itapeleka umeme katika vijiji 118 vilivyobaki vya Wilaya ya Mbinga kupitia mradi kabambe wa *REA* Awamu ya Tatu. Ujenzi wa mradi huu utaanza mwezi Disemba, 2016 na kukamili katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kukamilika kwa taratibu za kuwapata wakandarasi watakaohusika na ujenzi wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovolti 0.4 yenye urefu wa kilometa 471, ufungaji wa transfoma 246 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 19,185. Kazi hii itagharimu shilingi bilioni 18.1.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Spika, asante pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, mpango wa *REA III* una-*cover* mwaka 2016 mpaka 2019/2020. Serikali ina mpango gani kushirikisha Waheshimiwa Wabunge katika kupanga maeneo ya kupeleka umeme katika miaka hiyo husika kuzingatia kwa bajeti ya kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mkoa wa Ruvuma haujaunganishwa bado na umeme wa Gridi ya Taifa. Ni lini sasa mradi wa umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Makambako kwenda Songea utakamilika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kabisa Mheshimiwa Mbunge ametukumbusha kwamba tuwaambie Waheshimiwa Wabunge. Kwanza kabisa niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, mradi wa *REA* Awamu ya Tatu unaoanza sasa tunatumia utaratibu ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, wakandarasi watakapokuwa wanaingia *site* kuanzia Disemba mwaka huu, hatua ya kwanza itakuwa ni kukutana na kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge kabla hawajaanza kazi kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe tu angalizo lingine, kwamba tumeweka utaratibu sasa mahali ambako kuna Ofisi zetu za *TANESCO* tumeandaa kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa kuweka vituo rasmi ili wananchi wasiende kwenye Ofisi za *TANESCO* ila wafanyakazi wa *TANESCO* wakae kwenye vituo ambavyo Serikali za Mitaa zitakuwa zimetambua.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wabunge pamoja na Diwani watashirikishwa sana kabla ya utekelezaji wa mradi huu kuanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mradi wa Makambako – Songea, mradi wa Makambako – Songea una sehemu tatu za utekelezaji. Sehemu ya kwanza ni ujenzi wa *distribution line* ambao inachukua urefu wa kilomita 900 kwa maeneo yote ya Mbinga, Songea na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulianza mwaka juzi na unakamilika mwakani mwezi Julai. Sehemu ya pili ni kujenga *transmission line* ambayo imeanza mwaka jana na hivyo itakamilika mwezi Septemba, 2018. Hatua ya tatu ni kujenga *substations* tatu, moja ikiwa Makambako, nyingine Songea na nyingine eneo la Madaba, kwa ujumla wake kazi zote zitakamilika mwezi Mei, 2018. (*Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hili ni la muhimu sana hawa wakandarasi wakifika huko kwa kweli wawaone Waheshimiwa Wabunge, muhimu sana. (*Makofi)*

Na. 76

**Tatizo la Soko kwa Bidhaa za Kilimo na Mifugo**

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI** aliuliza:-

Wakulima na wafugaji wa Tanzania hawajawahi kuwa na uhakika wa bei ya mazao yao hasa katika msimu wa mavuno ya kutosha badala yake wanageuka watumwa wa mazao yao wenyewe kwa kukosa masoko, maghala na bei zuri ya mazao.

Je, ni lini tatizo hili litaisha ili kuwezesha Watanzania wengi zaidi kujiingiza kwenye kilimo na ufugaji?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Gibson, uhakika wa bei na masoko ya mazao ya kilimo umekuwa ni changamoto kwa wakulima na wafugaji wetu. Kwa kutambua hilo Serikali ilibuni Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo mwaka 2008 mahususi kwa kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao nchini. Aidha, mkakati unganishi wa maendeleo ya viwanda wa mwaka 2020 *(intergrated industrial development strategy 2020 – IIDS)* na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye lengo la kujenga uchumi wa viwanda umezingatia kwa dhati uongezaji thamani wa malighafi za kilimo ili wakulima wapate masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kipaumbele vinavyolengwa katika mkakati na mpango huo ni pamoja na viwanda vya kusindika mbegu za mafuta, kutengeneza nguo na mavazi, kubangua korosho, kutengeneza ngozi na bidhaa zitokanazo na ngozi, viwanda vya nyama, viwanda vya maziwa, uzalishaji wa sukari na usindikaji wa matunda na mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, aidha, ili kufanikisha uhakika wa ubora, wingi wa malighafi na bei nzuri kwa wakulima, Serikali inaendelea kuimarisha Mfuko wa Stakabadhi za Ghala ambao unawezesha mazao kutunzwa na kupunguza uharibifu wa mazao baada ya kuvuna *(post harvest loss)*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango iliyotajwa hapo juu itatuwezesha kutengeneza masoko ya uhakika na bei nzuri kwa wakulima na wafugaji. Kama ambavyo tumekuwa tukihimiza mara kwa mara tutashirikiana na kuiwezesha sekta binafsi kujenga viwanda.

Mheshimiwa Spika, Maeneo mengine ya ushirikiano ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya masoko kama vile maghala ya kuhafadhia mazao, barabara za vijijini na utoaji wa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa uzalishaji wa tija.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul maswali ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Meiseyeki.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa Tanzania wanaelekea sasa kwenye msimu mwingine wa kilimo ikiwa mazao yao bado wanayo manyumbani hawajauza. Tuliona wakulima wa nyanya, mbaazi, mahindi na mazao mengine, na Serikali ilitoa kauli katika Bunge hili kwamba wanatafuta masoko nje ya nchi nilijibiwa na Naibu Waziri wa Kilimo. Naomba nifahamu mchakato huo umefikia hatua gani maana wakulima mpaka sasa wana mazao yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, majibu ya Waziri ni kwamba, wanaanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuchakata mazao ili mazao haya yapate soko na mtawezesha sekta binafsi na Serikali haitoi moja kwa moja fedha kwa ajili ya viwanda hivyo watu binafsi waanzishe. Wakulima wa Tanzania wasubiri kwa muda gani mpaka hivyo viwanda vianzishwe ili mazao yao yapate soko? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nianze na hili ambalo ni rahisi. Wananchi wasubiri kwa muda gani kuanzisha hivyo viwanda?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunajenga viwanda. Lengo la kujenga viwanda ni kuongeza thamani na kupunguza uharibifu wa mazao *(post-harvest loss)*. Jambo la kufanya Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote na

Watanzania nendeni *SIDO,* na nimekuwa nikilisema, kusudi waweze kutambua na Naibu Waziri wa Ajira alizungumza hapa, kuna kitu kinaitwa *ODOP (One District One Product)* inalenga kuangalia katika eneo lenu tatizo ni nini, fursa ni ipi.

Mheshimiwa Spika, sasa watakuongoza wale na watakuvuta mpaka uje ufikie kwangu tuweze kupatia suluhisho lakini mimi nina imani na Watanzania wakielekezwa, wakiongozwa wanauwezo wa kuwekeza. Kwa hiyo suluhisho ni tutaanza lini, tumeshaanza sasa hivi tunajenga viwanda. *(Makofi)*

Tatizo lake Mheshimiwa Mbunge nenda kamuone Meneja wa *SIDO* kama ukiwa na wepesi njoo unione mimi nitaweza kukupatia suluhisho.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; tatizo la nyanya na tatizo la mbaazi. Tanzania kama Taifa tumepata tatizo kubwa la bei ya mbaazi na ndiyo maana wananchi unao wazungumzia wameweka mbaazi zao. Mwaka jana kilo ya mbaazi ilikwenda mpaka shilingi 2,000 lakini bei ya soko la mbaazi imeshuka mpaka shilingi 500 tatizo tunalijua.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, tunawasiliana na Serikali ya India ili tuwe na makubaliano ya moja kwa moja kuuza mazao hayo ya mbaazi kwa kushirikiana na Serikali ya India. Tanzania tulikuwa tunauza tani laki moja ya mbaazi, Mheshimiwa Mo ametupa *order* ya tani milioni mbili nina uhakika tutafanikiwa kuwapa majibu Watanzania. (*Makofi)*

Na.77

**Kuhalalisha Viwanda vya Kutengeneza Gongo Nchini.**

**MHE.GIMBI D. MASABA** aliuliza:-

Kutokana na mpango wa Serikali kuhakikisha ifikapo mwaka 2025, Tanzania inafikisha uchumi wa kati.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha na kuhalalisha viwanda vya kutengeneza pombe aina ya gongo ili kuchochea uchumi wa nchi?

(b) Pombe hii aina ya gongo inapendwa kunywewa zaidi na watu wa vijijini. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuwaendeleza kielimu zaidi wataalam hao wanaotengeneza pombe hiyo ili wapate ujuzi kwa maslahi ya Taifa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viwanda anavyosema Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba ni tabaka la viwanda vidogo sana na viwanda vidogo. Viwanda hivi ni fursa ya sekta ya binafsi kuwekeza. Serikali inalenga viwanda vikubwa sana na miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhalalisha pombe aina ya gongo kama ilivyo sasa ni jambo ambalo haliwezekani, ila sekta binafsi inashauriwa kuanzisha viwanda vitakavyotumia malighafi zinazotengeneza kinywaji hicho kwa lengo la kuzalisha kinywaji kinachokidhi viwango vya usalama na ubora wa chakula.

Naomba nirudie, kinywaji hicho kwa kuzingatia ubora na usalama wa mnywaji.

Mheshimiwa Spika, moja ya kigezo muhimu cha kuanzisha kiwanda ni uwepo wa soko. Kutokana na wananchi kupendelea kinywaji hiki, nitumie fursa hii kuwashauri wadau wa sekta hii kuwasiliana na ofisi za *SIDO* ambazo zinapatikana mikoa yote ili kupata mwongozo juu ya uanzishaji viwanda bora na salama vya aina hii.

Kwa upande wa Makampuni makubwa ya pombe nawashauri wachangamkie fursa hii kwa kutengeneza pombe yenye ladha ya gongo kwani baadhi ya wateja ni ile ladha inayowavutia na kupendelea kinywaji hicho. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hili swali kwa upendeleo maalum litapata maswali ya nyongeza. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE.GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Serikali ipo tayari kufanya utafiti ili kubaini faidi na vitu muhimu vinavyohitajiaka katika suala zima la pombe hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa vile Tanzania inahitaji uchumi wa viwanda Serikali ipo tayari kuwapeleka wajasiriamali hawa China, Japan na Afrika Kusini ili kujifunza zaidi na waweze kutengeneza kitaalam zaidi kama ilivyo pombe ya konyagi? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, faida za kinywaji hiki gongo zinafahamika. Wataalam wangu wana uwezo na faida za kinywaji hiki, tatizo letu ni usalama. Kwa hiyo, mimi nitawaelekeza wataalam wangu waje kwenye jimbo lako Mheshimiwa Mbunge kusudi wahakikishe kwamba kile kinywaji kama kinatengenezwa kitengenezwe salama.

Lakini kwenye jibu langu nilikuambia watu wengi wanaokunywa gongo hawapendi gongo wanapenda ile ladha yake. Sasa tutatafuta ladha tuwatengenezee kinywaji salama chenye radha ya gongo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwapeleka Watanzania kwenda China, nikimjibu Mheshimiwa Dotto napenda nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu tarehe 7 mpaka 11 Disemba, 2016 nimewaalika watengeneza viwanda wote na wenye viwanda kwenye uwanja wa Sabasaba kusudi wawaoneshe Watanzania mitambo mbalimbali ambayo ni viwanda na namna ya kuitumia.

Kwa hiyo, badala ya kuwapeleka China, na Watanzania ni milioni 53 sina nauli ya kuwapeleka, njooni Sabasaba kila mtu uangalie kiwanda anachopenda, korosho, kahawa na kila kitu kitakuwa pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kuwa gongo imeathiri sana wanaume wa Wilaya ya Rombo hadi akina mama wakaandamana, Mheshimiwa Selasini swali la nyongeza tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana lakini napenda kukuthibitishia kwamba niko sawa sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kila kabila hapa nchini lina aina fulani ya pombe ya asili ambayo inapendwa. Kule kwetu Rombo viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya pombe za aina mbalimbali viko vingi tu. Niliwahi kuomba hapa Bungeni; ni lini Serikali badala ya kupiga vita viwanda hivi ikatuma wataalam wake wa *TBS* na *TFDA* wakafanya ukaguzi na wakapima aina ya pombe ambazo zinapatikana huko; na kwa sababu sasa hivi tunajenga Taifa la viwanda tukawa na viwanda ambavyo vinaweza vika-*improve* zile pombe za asili kwa faida ya watu wetu na kwa ajili ya kuongeza mapato na ajira ya maeneo husika?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imegawana mikoa yote ya nchi hii katika makundi manane, na nitawaagiza timu itakayokwenda Mkoa wa Kilimanjaro kwenye Jimbo la Rombo kwamba wafuatilie suala hilo namna gani tunaweza kutengeneza viwanda vya kuzalisha ile pombe wanayoipenda wananchi kwa kuzingatia ubora na afya; nitazingatia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Simanjiro nilikuona swali la mwisho la nyongeza.

**MBUNGE FULANI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**SPIKA:** Aah, sawa sawa endelea na swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, kuna jambo moja nataka tuliweke kwenye rekodi lakini pia swali langu kwa Mheshimiwa Waziri; kwa sababu kwa muda mrefu Serikali ilikuwa ikitangaza kwamba gongo ni pombe haramu kama ambavyo umeona watu wengi swali hili wakiliuliza, lakini kuna pombe mbalimbali zinazotengenezwa kutokana na mazao.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kuna pombe inatengenezwa nipa ndiyo hiyo hiyo gongo inatokana na mabibo makavu lakini pia ni sehemu ya kuongezea wakulima kipato.

Je, Serikali haioni sasa kama hawataki wakulima wale wapike gongo kwa kutumia zile malighafi zao ambao ni sehemu ya korosho kwa nini sasa isinunue wakaenda kufanya hata chakula cha mifugo kwa nia ya kuwaongezea wakulima kipato? (*Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza kwenye suala la Mheshimiwa Selasini, suala linalotukwamisha, na ndiyo maana watu wengine kwa kutokujua wanaichukia *TFDA*, hoja ni kwamba kinywaji kile kinatengenezwa vipi? Kinakuwa *packed* vipi? Na kinapimwa kuthibitisha huo ubora, na nimeshaahidi, na niwaeleze wataalam wangu watakao kwenda Mikoa ya Lindi kafuatilie kinywaji hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini nikutake wewe Mheshimiwa Mbunge rafiki yangu Bwana Mwambe na wewe ni rafiki yangu na unajua. Njoo unieleze wazo hilo tutumie wawekezaji wa ndani hata wa nje tuweze kutengeneza kinywaji kizuri hicho tuweze kuuza Tanzania na masoko ya nje.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi linaulizwa na Mheshimiwa Salma Mwambe.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mimi naitwa Salma Mohamed Mwassa.

**SPIKA:** Salma Mwassa.

Na. 78

**Mabarza ya Ardhi na Nyumba**

**MHE. SALMA M. MWASSA** aliuliza:-

Je, ni nini umuhimu wa kuwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 78 la Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya hapa nchini yanaundwa na kusimamiwa na kifungu cha 22 cha Sheria ya Mahakama ya Ardhi Namba 2 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kipekee wa Mabaraza haya ni suala zima la utatuzi wa migogoro yote itokanayo na matumizi ya ardhi nchini kwa karibu zaidi ukilinganisha na vyombo vingine vya kutatua migogoro. Hivyo, Mabaraza haya yana umuhimu mkubwa sana katika kuleta amani na muafaka katika maeneo mengi yenye migogoro ya watumiaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, umuhimu mwingine ni kutatua migogoro yote ya ardhi kwa haraka na kwa njia rafiki na shirikishi kwa kuwa Mabaraza haya yako karibu na wananchi wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, umuhimu huu umejidhihirisha katika utendaji wake. Kati ya Oktoba, 2004 mpaka kufikia Oktoba, 2016 jumla ya mashauri 131,470 yalipokelewa na kati yake mashauri 100,744 yameamuliwa na mashauri 32,176 bado yanaendelea.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na majibu ya kuleta matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika Sheria hii ya Mabaraza ya Ardhi inasema kwamba; Baraza la Ardhi la Wilaya lisiongelee kesi inayozidi au kiwanja kinachozidi thamani ya shilingi milioni 50, na Baraza la Nyumba la Kata lisiongelee kiwanja au nyumba inayozidi shilingi milioni tatu.

Meshimiwa Spika, kwa mikoa kama Dar es Salaam, Mwanza, maeneo yoye ya mijini Nyumba nyingi zimezidi thamani ya shilingi milioni 50. Sasa kutokana na sheria hii kutokukidhi matakwa halisi ya mwenendo wa thamani ya ardhi iliyopo mijini kwa sasa, ni lini sheria hii itarekebishwa au iletwe hapa Bungeni irekebishwe au ifanyiwe *amendment* ili iendane na hali halisi ya sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, migogoro mingi ya ardhi ya ardhi nchini inasababishwa na ardhi kutopimwa na kumilikishwa kwa ufasaha, na hii inasababishwa na gharama kubwa na mlundikano wa kodi ya umilikaji wa ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kodi ya *premium* katika umilikaji wa ardhi ambayo ni asilimia 7.5 ni kubwa mno kwa sasa, ni lini kodi hii itashushwa au itafutwa ili kuwaletea tija wananchi au kuwapunguzia mzigo wananchi katika kupata haki yao hii ya kumiliki ardhi kwa sasa? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Salma Mwassa, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anazungumzia sheria kutokidhi kwa mana ya kwamba viwango vilivyopo kwa sasa na hasa mijini ukiangalia kwa Mabaraza ya ardhi kiwango chake ni shilingi milioni 50 lakini nyumba nyingi zimezidi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu haya masuala yanakwenda kisheria, na kama hitaji linaonekana kwamba sheria imepitwa na wakati nadhani ni wakati muafaka pengine wa kuweza kupitia upya na kuweza kuangalia kwasababu kadri siku zinavyokwenda ndivyo jinsi na majengo yana-*appreciate value* zake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ni wazi kweli anavyolisema limepitwa na wakati, lakini bado pale inapoonekana kwamba viwango, au kiwango cha kesi husika kinazidi Mamlaka ya Baraza husika kesi hiyo huwa inapelekwa kwenye

mahakama ya juu. Kwa hiyo bado linaweza kufanyika wakati bado tunasubiri kubadilisha sheria hii.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la viwango. Tukumbuke katika bajeti nadhani ya mwaka 2015/2016 kiwango cha *premium* kilishuka kutoka asilimia 15 kwenda kwenye asilimia 7.5. Sasa tuna miaka kama miwili tu toka hii imeanza kutumika na bado inaonekana ni kubwa. Lakini tukumbuke pia kwamba viwango vingi vya ardhi ambavyo vilikuwepo vilishushwa ikiwepo hata ile ya upimaji wa ardhi kwa kiwanja kutoka shilingi 800,000 kwenda shilingi 300,000. Kwa hiyo, haya yote ni mapitio yanayofanyika kulingana na muda jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hili nalo bado linaonekana ni tatizo siwezi kuahidi hapa ni lini tutaleta sheria hiyo kwa sababu ndiyo kwanza imeanza. Lakini tutazidi kufanya utafiti wa kina na kuweza kujua kama kweli ni kikwazo kikubwa tuweze kuona namna gani tutapitia tena viwango vyetu ili wananchi ambao tunategemea wanufaika wa ardhi hii ambayo sehemu kubwa haijapimwa waweze kunufaika na kupata ardhi zao na kuweza kupata hati ili waweze kufanya shughuli zingine za maendeleo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana, kwa leo tuishie hapo. Moja kwa moja naenda kwenye tangazo, nanalo tangazo moja tu, naomba tusikilizane, nalo linatoka Utawala, Bunge. Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba leo tarehe 8 Novemba, 2016 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu ugonjwa wa kifua kikuu na maambukizo mseto ya kifua kikuu na UKIMWI katika ukumbi wa Bunge kuanzia saa saba mchana. Kwa hiyo, semina hii nadhani itafanyikia hapa hapa. Kutakuwa na semina baada ya kuahirisha mambo haya saa saba mchana, naomba wote mkumbuke jambo hilo muhimu.

Jambo la pili ambalo ningependa kusema hapa ni kwamba toka tumeanza Mkutano huu wa Tano nilikuwa sijaja hapa mezani lakini Wasaidizi wangu Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti Chenge, Mwenyekiti Zungu na Mwenyekiti Najma Giga wamefanyakazi nzuri sana ya kuliongoza Bunge hili. Ningeomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana, sana, sana na kuwatia moyo kwamba waendelee kufanya kazi hiyo nzuri na mimi niko nao. *(Makofi)*

Mkiangalia *order paper* mtaona tunazoshughuli nyingi kidogo ambazo inabidi zifanyike kwa ufanisi mkubwa kwa siku ya leo na uendeshaji wa kisayansi.

Kwa hiyo, ili mambo haya yaweze kwenda vizuri nitamuomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, atutolee hoja ya kutengua kanuni ili mambo yetu yaweze kukaa vizuri tuweze kwenda vizuri zaidi, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE WALEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya hoja ya kutengua kanuni za Bunge chini ya kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa yaani kikao cha leo tarehe 8 Novemba, 2016 ni mjadala kuhusu Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya na kushughulikia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba 3 wa mwaka 2016 na kuupitisha katika hatua zake zote na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1)(a), muda wa kusema Bungeni kwa kila Mbunge anayejadili hoja ni dakika zisizozidi 15, na kwa kuwa Kamati ya uongozi katika kikao chake kilichofanyika jana tarehe 7 Novemba, 2016 iliafiki kwamba muda wa kuchangia kwa kila Mbunge atakayepata nafasi iwe dakika 10 ili kupata wachangiaji wengi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge zilizopangwa kwa ajili ya kikao cha leo tarehe 8 Novemba, 2016, naomba kutoa hoja kwamba kanuni ya 62(1)(a) itenguliwe ili muda wa kila Mbunge kuchangia iwe dakika 10 badala ya dakika 15, Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kwa shughuli za leo tutaenda kwa dakika kumi, kumi, nitawaomba sana wale waliojipanga na waliojiandaa kuchangia shughuli za kutwa nzima ya leo basi tuende kwa dakika kumi, kumi. Wachangiaji majina nitayapata kupitia utaratibu wetu wa vyama vyenu, Kambi zenu kwa ujumla wake. Kwa jinsi hiyo tuendelee.

Katibu!

**NDG.RAMADHANI ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

**MKATABA WA UBIA WA UCHUMI BAINA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI NA UMOJA WA ULAYA (*EAC-EU EPA)***

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba, Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kina madaraka kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyote katika utekelezaji wa majuku yake. Tarehe 6 Novemba, 2016 mtakumbuka kulikuwa na Semina ya Wabunge wote ambapo tulipatiwa uelewa kuhusiana na suala la Mkataba wa *EPA* katika ukumbi huu huu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane! Waheshimiwa Wabunge, jana tarehe 7 Novemba, 2016 Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji aliwasilisha mezani Mkataba huo na kwa mujibu wa Kanuni ya 37(4), Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa hoja kuomba Bunge lijadili mkataba huo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo basi muda si mrefu ujao nitamuita Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles John Mwijage awasilishe maelezo mafupi sana ambayo yatatusaidia kufungulia mjadala wetu na baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge mtapata nafasi ya kuchangia kwa lengo la kutoa maoni na ushauri ili kwa niaba ya wananchi Bunge liweze kuishauri Serikali ipasavyo kuhusiana na Mkataba tajwa.

Waheshimiwa Wabunge, ili kuhitimisha suala hilo Kibunge, mwishoni wa mjadala huu itabidi niwahoji ili Wabunge wanaoafiki kwamba Serikali isisaini Mkataba huo waseme ndiyo na wale ambao watakuwa hawaafiki waseme siyo. Nadhani maelezo yangu haya yamesaidia katika kuwaweka sawa kuhusu utaratibu wa jinsi tutakavyoenda na jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivosema majina tayari ninayo kupitia Vyama vyenu, na kama kuna ambao wanajisikia kabisa kwamba ni vyema wapate nafasi ya kusema humu ndani basi waniandikie nitaangalia hali halisi ya muda unavyoenda hapa mezani kwangu.

Kwa jinsi hiyo, namuomba Mheshimiwa Charles Mwijage aongee baada ya hapo Mheshimiwa Kangi Lugola utafuatia na Mheshimiwa Livingstone Lusinde na tutaendelea na orodha yetu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako tukufu kwa niaba ya Wananchi, lipokee, lijadili na kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu mkataba tuliouwasilisha mezani kwako wa Ubia wa Uchumi baina ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa utangulizi huo mfupi sana. Mheshimiwa Kangi Lugola sasa, Mheshimiwa Lusinde ajiandae, Mheshimiwa Saed Kubenea atafuatia.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuwa mchangiaji wa siku ya leo kuhusu mkataba wa Ubia wa uchumi baina yetu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya Nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu ambao mimi nimeushika hapa mkononi ni miongoni mwa mikataba ambayo ni mibovu, ni miongoni mwa mikataba ambayo ni mibaya, ni miongoni mwa mikataba ambayo inanikumbusha enzi za miaka ya zamani. Mikataba kama hii ndiyo ambayo tulisoma kwenye historia ya akina *Carl Peters* na kwamba Wazee wetu wakiwemo wakina Mangungu waliweza kusaini mikataba mibovu na ya ajabu kama huu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Jemedari John Pombe Magufuli ambaye kwa kutumia mkono wake alikataa kabisa mkono wake usitumike katika kusaini mkataba mbovu huu katika Ikulu ya Tanzania, mjini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema mkataba huu ni mbovu? Niliwahi kuja Bungeni hapa nikiwa na *semi-trailer* ambalo nilishindwa kuliingiza humu ndani nikaliacha pale nje lilikuwa limesheheni bidhaa mbalimbali vikiwemo vijiti vya kutolea nyama kwenye meno, chaki, vikiwemo vitambaa, zikiwemo peremende.

Mheshimiwa Spika, kama nchi yetu imekuwa na bidhaa ambazo zimezagaa na kusababisha sisi tusiweze kuimarisha na kujenga viwanda vyetu, tukisaini mkataba wa namna hii nchi yetu itakuwa ni dampo la bidhaa nyingi za ajabu na matokeo yake dhamira njema ya Mheshimiwa Rais ya kutaka nchi hii sasa iwe ni nchi ya viwanda hakika hatutaweza kufanikiwa kama tutasaini mkataba wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu ambapo katika aya zake 146 zaidi ya vifungu 20 ni vifungu ambavyo vina matatizo, na Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi kwa sababu ya muda sina sababu ya kuvipitia tena. Vifungu hivi vina matatizo, vifungu hivi vinatufanya tukisaini mkataba nchi yetu ya Tanzania haitakuwa na nafasi ya kujitanua katika ku-*negotiate* tutakuwa tumefungwa. Tukisaini mkataba huu kwenye vifungu ambavyo vinahusu masuala ya kilimo, masuala ya mifugo, masuala ya miundombinu tutakuwa tunasaini mkataba ambao kwa kweli nchi yetu itaingia kwenye matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika masuala haya ya nchi za Ulaya kuwinda nchi zetu katika umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wanajua kabisa kwamba nchi ya Kenya ambayo wamepiga hatua kiviwanda, sote tunajua viwanda vya nchi ya Kenya viwanda vingi ndivyo hawa hawa ambao wanatoka kwenye Jumuiya ya Ulaya. Kwa hiyo, leo hii tukisaini mkataba kama huu ambapo tunashirikiana na nchi ya Kenya kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa vyovyote vile tutaingia katika matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano ambayo iko hai. Sisi tulipoanzisha *General Tyre* wakati ule tulijua kabisa kwamba tutakuwa na soko zuri na tutaweza kuwa na viwanda ambavyo vitatusaidia, lakini Kenya hawa hawa ambao walitumiwa na nchi za Jumuiya ya Ulaya waliweza kuanzisha Kiwanda cha *Fire Stone,* leo hii kiwanda chetu cha *General Tyre* kimekufa. Kwa hiyo, tukisaini mikataba kama hii kwa kweli tutaendelea kuwa na matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika niseme, wenzetu wa Kenya ndiyo hata miaka ya nyuma wakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikuwa ni chanzo cha kuua Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo tuliianzisha wakati ule. Leo nina wasiwasi tukiendelea na Mkataba huu tukiwa tunashirikiana na Wakenya kwa vyovyote vile Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki ambayo tumeianzisha kwa nguvu kubwa, kwa nia njema lazima Jumuiya hii matokeo yake itaenda kuvunjika tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo viongozi wetu wa Serikali, Wizara ya Afrika Mashariki, Wizara ya Viwanda na Biashara na Uwekezaji, hakikisheni kwamba wataalam wetu waendelee kuuchambua mkataba huu ili maeneo yote yale ambayo yana matatizo yaweze kufanyiwa kazi. Na niseme bayana, lazima katika *negotiation* nchi yetu itakapofanya uchambuzi waweze kuwa na *negotiation framework* ambayo imetokana na mawazo ya Wabunge waweze kuboresha mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba mkataba huu kuna maeneo ambayo ni mazuri, lakini kwa sababu maeneo makubwa yana matatizo, hatuwezi tukaingia kwenye *risk* kwa sababu tu kuna mambo ambayo ni mazuri wakati mambo makubwa ndiyo mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo sisi tuna Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye *EALA* lazima Wizara ya Mambo ya Nje na Afrika Mashariki iweze pia kushirikisha Wabunge kwa *Chapter* ya Tanzania na wenyewe wajaribu kuchambua katika Bunge lao, waende kupiga marufuku muswada kama huu kuendelea kusainiwa ukiwa mbovu namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuna Mabunge mawili, Bunge letu hili kwa leo mimi kama Mbunge wa CCM, Mbunge ambaye naamini Serikali yetu inahitaji mkataba wa kufanya biashara na nchi za Ulaya, lakini hatuwezi kukubali Serikali ya CCM ikaingia mkataba ambao ni mbovu, ambao ni *fake* kama huu.

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, bila kujali itikadi zetu, lazima nchi hii tuitendee mema, lazima mkataba huu tuukatae, Mkataba huu ni mbovu, urudi uchambuliwe halafu lazima Bunge hili baadaye lishiriki tena kuangalia ile *negotiation framework* ili tuone kwamba sasa tunaweza tukaenda kusaini mkataba ambao ni mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mikataba mingine kama hii, humu humu ndani mimi nimesoma vifungu vingine vinajaribu kuwa na mwelekeo pia wa kutuletea mambo mengine ya ushoga kama ambavyo mikataba mingine inaleta mambo ya ushoga. Kwa hiyo, lazima Wabunge tuwahurumie Watanzania na hasa Watanzania ambao ni wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa macho, sehemu zao nyeti zinaweza zikaingiliwa kwa sababu ya mikataba mibovu kama hii. Hatuwezi sisi tukakubali. Lazima tulinde haki za binadamu sisi kama Wabunge wa Bunge hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninakushukuru sana. Nitawashangaa Wabunge wenzangu ambao tumepata semina hapa nzuri ya maprofesa na madokta waliobobea halafu matokeo yake Mbunge unasimama, unakuja kuupongeza na kusema tupitishe mkataba wa namna hii. Nitakushangaa sana, na ndiyo maana hii mbingu mnayoiona hii yuko Mwenyezi Mungu anatutazama, analitazama Bunge hili namna gani mlivyo na huruma na uchungu na wananchi ambao ni watu wa Mungu. Mkisaini mkataba huu nawaambieni itakuwa ni vigumu sana hata ninyi kuuona ufalme wa Mungu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. Siungi mkono kupitisha mkataba huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola. Mheshimiwa Saed Kubenea, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, leo Bunge hili linakutana kwa pamoja kuamua kusitisha au kusaini Mkataba wa *EPA*. Lakini juzi wakati tunapata semina juu ya mkataba huu baadhi ya Wabunge tuliomba tuletewe watu wengine ambao waliufikisha mkataba huu mahali hapa ili waje kueleza uzuri wa mkataba huu. Ni bahati mbaya sana kwamba kilio hicho hakikusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka hapa tulipofika, mambo yote haya yamefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Leo hii kutuambia kwamba huu mkataba ni wa ajabu, ni mbaya, ni mchafu, ni wa kikatili na hili lenyewe nalo ni la ajabu. Ndiyo maana tunasema kwamba baadhi ya watu wanaposema kwamba Chama cha Mapinduzi kimechoka, kimezeeka, wanasema kwa sababu ya mambo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwamba mkataba huu ukawa ni mbaya, lakini kuna faida kubwa kwenye mkataba huu ambazo hazijaelezwa na watoa mada. Kwa mfano, mkataba huu unatupa sisi kama nchi upendeleo maalum wa kupeleka bidhaa katika nchi za Ulaya bila kulipa kodi. Jambo hili halielezwi mahali popote na watu waliotoa mada. Binafsi inawezekana tukawa na maoni yanayokinzana, na ndiyo mjadala. Hoja ya msingi hapa ni nani aliyefikisha mkataba huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba huu ulijadiliwa katika Kikao cha Baraza la Mawaziri cha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kabla mkataba kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, ulipitia kwenye Kikao cha Makatibu Wakuu, baada ya Kikao cha Makatibu Wakuu mkataba uliingia kwenye Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Huu mkataba kabla ya kwenda katika Baraza la Afrika Mashariki ulipitia katika Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa watu wanakuja hapa leo kusema mkataba mbaya, mchafu kana kwamba nchi hii ndiyo kwanza inaanza upya, si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwamba Bunge hili likaelezwa taarifa sahihi kutoka pande zote mbili. Upande unaopinga mkataba na upande

unaotaka mkataba ili maamuzi sahihi yafanyike kwa manufaa ya Taifa letu. Tusifanye mambo ya ushabiki hapa. Tulipitisha miswada na sheria mbalimbali hapa za kuuza mabenki yetu, tukauza mashamba, tukabinafsisha lakini hao hao waliobinafsisha wamerudi wamesema uamuzi ule haukuwa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima na ni muhimu sana kabla ya Bunge lako Tukufu halijaingizwa katika mgogoro huu, wapatikane watu wa upande wa pili, wakaeleza uzuri wa mkataba huu ili Bunge hili liweze kuamua kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge limeelezwa kwamba nchi za Afrika Mashariki ikiwemo Kenya na Rwanda, taarifa zinasema hata Rwanda wameshasaini mkataba huu. Sasa kama sisi tuko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kenya na Rwanda wameshasaini mkataba, sisi ndani ya Jumuiya hiyo tunabaki wapi kama kisiwa? Nchi za *SADC* ambazo zimeshasaini sehemu ya mkataba huu na sisi tumo katika Jumuiya ya *SADC* kama washirika wa biashara, tunakuwa wapi kama nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni jambo muhimu sana kwamba kabla ya uamuzi wa kufunga, kusaini au kutokusaini kwa mkataba, ni muhimu kwa maoni yangu kwamba huu mkataba haiwezekani wote huu kama ulivyo ukawa mbaya, haiwezekani. Haiwezekani kwamba dudu lote hili likawa baya kwa sababu watu wetu, wazalendo kabisa walitumwa kutoka Serikalini kwenda kushiriki kwenye vikao vya majadiliano hadi wakatengeneza kitu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Bunge hili lingetoka na Azimio kwamba kabla ya mkataba huu kusainiwa vile vifungu ambavyo ni vibaya viondolewe tukajadiliane, vile vifungu ambavyo havifai viondolewe tukajadiliane, si kusema kitu chote hiki ni kibaya, tutaonekana watu wa ajabu duniani, yaani hata sisi kupeleka bidhaa zetu nje likawa jambo baya? Kwa nini tumejiunga na *AGOA*? Kwa nini kila mwaka tunapeleka maafisa kwenye mikutano ya *AGOA*? Ni kwasababu kuna vitu vizuri vimo humu ndani ya mkataba. Hivyo vitu vizuri hivyo, tuiagize Serikali ikafanye majadilinao upya ili vile vizuri tuvichukue na vibaya tuvitupe, si kusema kila kitu kibaya, haiwezekani. Haiwezekani kwamba vitu vyote vilivyomo humu vikawa vitu vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo rai yangu ni kwamba Serikali ambayo iliingia mkataba huu, watalam ambao walishiriki mkataba huu, Baraza la Mawaziri ambalo limeshiriki mkataba huu mpaka kutufikisha nchi mahali kwenye njia panda, Mabunge ya nchi za wenzetu yamesharidhia, sisi tukiwa tuko nyuma hawa watu waliotumwa kwenda kusaini mkataba huu ni lazima wawajibike.

Waliokwenda kufanya mazungumzo ya mkataba huu, kama mkataba huu ni mchafu ni lazima wawajibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili lisichukuliwe kwa ushabiki. Sote hapa tunaweza tukawa Wazalendo, na hakuna mtu asiependa nchi yake lakini ni lazima tupime uzuri na ubaya.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Ahsante sana, Taarifa Mheshimiwa Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda tu kumpa taarifa mchangiaji anayesema kwamba mchakato wa kujadili mkataba huu umeanza siku nyingi kama anavyosema kwenye ngazi za wataalam toka mwaka 2007 na matakwa ya mkataba huu yalipaswa kuwa Afrika Mashariki kama Jumuiya, kwa pamoja tusaini mkataba na Jumuiya ya Ulaya na si nchi moja moja isaini. Sasa unapoona wenzako wamesaini wao bila kusubiri makubaliano yakawa ni ya pamoja, lazima kama una akili timamu utafakari na ufanye uamuzi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ni kwa msingi huo ndiyo maana msimamo wa Tanzania umekuwa ni wa kusita ili tutafakari kwa kina na ndiyo maana tumefikia hatua hii kushirikisha Bunge letu ili tuweze kufanya uamuzi sahihi kabla hatujaingia mkenge.

Kwa hiyo, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba wataalam wa Serikali wamekuwa wakitafakari kwa kina wakiangalia maslahi ya Tanzania kwenye mkataba huu yatakuwa nini kabla ya kukurupuka kwenda kusaini, na ni vyema angewapongeza badala ya kuwabeza. *(Makofi)*

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Spika, naona hiyo taarifa ni ya kwako na hiyo ni sehemu ya mchango wake. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na Mheshimiwa Hamidu Bobali aendelee kujiandaa, lakini nataka tu kukumbusha tulikotoka na tulipo. Kwenye Bunge lililopita nilipata *pressure* kwa baadhi yenu kutaka kwamba tuahirishe shughuli za Bunge tujadili jambo hili, kama mtakumbuka.

Nikawatuliza Wabunge kwamba tulieni, tutawasiliana na Serikali ili kabla hawajafikia mahali pa kusaini au kutokusaini Bunge hili lipate nafasi ya kuupita mkataba huo na kuishauri Serikali.

Kwa hiyo, mkataba huu kuja hapa inafuatia ombi lenu kwangu na mimi kutoa ombi hili kwa Serikali, kwa hiyo fursa tuliyoiomba sasa tunayo ambayo ni vizuri tuitumie vizuri kwa kushauri upande wowote ambao mtu una msimamo nao halafu mwisho wa siku tutahoji tupate tunaishauri Serikali yetu itueIekeze wapi. Lakini jambo hili ni kutokana na maombi yetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru….

**SPIKA:** Baada ya Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia juu ya mkataba huu wa *EPA*.

Mheshimiwa Spika kwanza nieleze msimamo wangu. Msimamo wangu mimi binafsi, serikali isiusaini huu mkataba. Ninazo sababu za msingi za kusema lakini pia nina maangalizo mengi kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunahitaji kusaini mkataba huu au tunautazama mkataba huu, kuna haja ya kuangalia Mkataba wa *Cotonou (Cotonou Agreement)* ambao tulisaini.

Mheshimiwa Spika, ukisoma faida ambazo nchi za Afrika tumezipata kwa kusaini Mkataba wa Cotonou, unaona kwamba tulipata faida moja wapo kubwa ilikuwa ni kwamba tuliweza kuingiza bidhaa zetu katika soko la Ulaya na tukaweza kuokoa zaidi ya *Euro billion 1.4* ambayo ilikuwa ni *duty and tariff* ambayo kama si mkataba ule hizi pesa maana yake tulitakiwa tuzilipe.

Mheshimiwa Spika, tunaposema *EPA* kwetu sisi haitufai kwa sasa ni kwa sababu moja kubwa. Wenzetu wameweka kifungu cha *import duty* kuwa *free,* tujiulize kwetu sisi kama Taifa tuna bidhaa ambazi zinakidhi viwango kuingia kwenye soko la Ulaya? Hili ni swali la msingi sana na je, wenzetu wa Ulaya wanazo bidhaa ambazo zinaweza kuingia zikakidhi vigezo katika soko letu la Tanzania? Hili ni swali la msingi sana la kujiuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tujiulize, ikiwa tutaondoa ushuru kwa bidhaa zinazoingia, tutapoteza mapato ya kiwango gani katika bandari yetu ambapo tunategemea *import* kwa kiwango kikubwa kutoka kwenye hayo mataifa ambayo leo tunaingia nayo mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi kuangalia; tunawalaumu wenzetu Kenya kwamba wameharakia, Kenya wenzetu wameandaa *facilities* na wana bidhaa za kwenda kuuza Ulaya, tayari wanazo. Suala sio kuwalaumu, suala tunatakiwa na sisi tujiandae ili tuweze kuwa na bidhaa zitakazofikia viwango vya kuviuza Ulaya. Kwa hiyo, angalizo ninalolitoa mimi, si tu tunawalaumu Kenya, ni kweli, hatuwezi ku–*compete* na wenzetu lakini tujione kwamba tumechelewa kwasababu ya uzembe wetu sisi wenyewe. Tumeshindwa kujipanga.

Leo tunakuja kuwalalamikia wenzetu, tuwaache wenzetu waende lakini sisi kama Taifa nasema kwa maslahi mapana ya Taifa hili hatuwezi leo kuusaini kwasababu hatuwezi kushindana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna sifa ya kusaini mikataba mingi. Ukisoma mikataba, *Lome Convention, Cotonou convention* - tulisaini lakini maeneo mengi ya vifungu ambavyo tulikubaliana navyo vingi tukashindwa kuvitekeleza, na kimoja wapo cha kifungu ambacho tulisaini kwenye *Cotonou Convention* ilikuwa ni suala la *impunity* pamoja na *rule of law* ambavyo hivi vyote vilikuwepo kwenye *Cotonou Agreement,* tulishindwa kama Taifa kuvitekeleza, sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati mwingine tunaposaini mikataba sisi wenyewe tunakuwa hatujajitengenezea mazingira ya kuweza kuendana na mkataba husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi kwa niaba yangu na nashukuru sana kwamba hata chama changu, Chama cha Wananchi CUF kimetuagiza kwamba huu mkataba tuukatae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, chama chetu kimefanya *analysis* ya kutosha, na mara nyingi chama chetu kimekuwa na watu makini na tukifanya misimamo mizuri. Mkataba huu, msimamo wa chama chetu tunaukataa.

Kwa hiyo tunaomba Serikali, Mkataba wa Cotonou usiusaini kwa sababu tumechelewa, wenzetu wametuacha sana. Jukumu pekee ambalo tunapaswa kulifanya ni sisi kujipanga kwa sababu wenzetu duniani wanakimbia, tusiendelee kutambaa, ndilo suala la msingi la kulifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba yetu, kazi tunayofanya hapa ni kazi ya Kikatiba. Naomba nimalizie kwa kutoa wito, ipo mikataba pia ambayo kama Taifa tumesaini ambayo yenyewe ina *mpact* kubwa kwenye nchi yetu ikiwemo na Mikataba ya Gesi na Madini.

Mheshimiwa Spika, tengeneza jina, tunaomba mikataba hiyo ya gesi tuilete ndani ya Bunge na yenyewe tuje kuijadili kwa sababu inakwenda kugusa maslahi mapana ya Taifa letu. Nakushukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama mbele yako kwanza, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kumshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kunipa afya kuweza kusimama na kuchangia katika mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuanza kwa kumwomba Rais wangu kipenzi, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, asiusaini mkataba huu kwa manufaa ya Watanzania. Tunamwomba sana kama Wabunge, kwa sababu mkataba huu hauna manufaa hata kidogo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kutokusaini huu mkataba hatuwi wa kwanza na wala hatuwi kituko. Kwa upande wa *SADC,* Angola hawajasaini; kwa upande wa *ECOWAS,* Nigeria na Gambia hawajausaini mkataba huu. Kwa hiyo, sisi hatuwi wa kwanza kuukataa mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba huu hauna manufaa yoyote na Watanzania kwa sasabu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa mujibu wa takwimu za Benki Kuu, nchi kumi ambazo Tanzania tunafanya nazo biashara, nchi ambazo sisi tunachukua bidhaa, tuna-*import* kutoka kwao, ya kwanza ni Saudi Arabia; ya pili, ni China; ya tatu, ni India; ya nne, ni Falme za Kiarabu; ya tano, ni Afrika Kusini; ya sita, ni Uswiss; ya saba, ni Japan; ya nane, ni Marekani; ya tisa, ni Kenya; na ya kumi ni Andorra. Katika hizo nchi kumi, nchi za Ulaya ni Uswiss peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kuangalia katika nchi ambazo sisi tunapeleka bidhaa zetu katika zile *top five;* ya kwanza ni China; ya pili ni India; ya tatu, ni *South Africa*; ya nne, ni Saudi Arabia; na ya tano, ni Kenya. Hakuna nchi yoyote ya Ulaya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia katika *FDI;* ya kwanza ni Uingereza ambayo na yenyewe ni inajitoa kwenye Jumuiya ya Umoja wa Ulaya; ya pili, ambayo ndiyo itakuwa ya kwanza, kwa sababu Uingereza inatoka katika Jumuiya ya Ulaya, ni India; ya tatu ni Kenya; ya nne, ni Netherland; inafuata China, Marekani, Afrika Kusini, Canada, Ujerumani na Oman. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nchi zenyewe za Ulaya unaziona ni kama mbili tu. Kama tunataka kuua biashara zetu, kama tunataka kuua viwanda vyetu, tuingie katika huu mkataba. Wanachotaka hawa ni kutaka kuchepusha mfumo wetu wa biashara. Wanataka kututoa tusifanye biashara na Saudi Arabia, China na India; na kwa sasa hivi, masuala ya biashara wanaotawala duniani ni China, India na Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa Jumuiya ya Ulaya wanataka kuturudisha tena tulikotoka. Wanataka tena *scramble for Africa,* hatuko tayari. Pia wanachokifanya Jumuiya ya Ulaya, kwa sababu makubaliano ya *EPA* ni kusaini Jumuiya ya Afrika kama nchi moja na sio mmoja, mmoja. Kwa hiyo, wanachotaka ni kuvunja Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Tuwaambie kabisa, Jumuiya ya Ulaya kwa kuanza kusaini na nchi moja moja badala ya kanda nzima kama Afrika Mashariki, wanataka kubeba dhima ya kuuwa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena, namwomba Mheshimiwa Rais, kwa kweli asisaini mkataba huu. Kuna mtu amesimama hapa akasema tusomewe mazuri yaliyoko katika mkataba. Mkataba tumekabidhiwa, angeusoma huu mkataba akatueleza yeye mazuri. Yeye anasimama, anasema tusaini, lakini hajasema hata moja zuri, anakusudia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimuunge mkono Mheshimiwa Bobali aliyesema hivi sisi, tuna kitu gani tunachoweza kwenda kuuza Ulaya? Sana sana sisi tunategemea malighafi; tunategemea kuuza nyama, samaki, lakini je, tuko tayari? Tunao uwezo wa kushindana na bidhaa kutoka Ulaya au sisi tunataka kufanywa soko la kuja kutupa bidhaa zao za kuja hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi za Caribbean ambazo zilijiunga, tafiti zinaonesha zimepoteza mapato yao kuanzia mwaka 2009 hadi 2013, wamepoteza zaidi ya *Euro* milioni 74.

Mheshimiwa Spika, narudia tena, tusisaini mkataba huu, hao wanaoshabikia, ndio wafadhili wao. Sisi hatuko tayari kusaini mkataba ambao pia katika kifungu cha 96 cha Cotonou ambacho kinaoanisha na Ibara ya 136

ya *EPA* pia haki za binadamu zimo, ambamo ushoga umo. Tuko tayari sisi kuingizwa kwenye ushoga kwa kupitia hii biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema siungi mkono hoja. Mkataba huu Mheshimiwa Rais tunakuomba usiusaini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nilishamtaja Mheshimiwa Anatropia, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tunachojadili hapa tatizo letu ni mkataba au ni *terms* za mkataba? Tukigundua tofauti, kama tunaona *terms* za mkataba hazitu-*favour*, tunafanya nini tuwe na *terms* zinazotu-*favour?* Tatizo letu ni kukataa au tatizo letu ni ku-*argue? Are we arguing or we are complaining? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachofanya tujitambue kama Taifa, *are we in a position to set terms* tunazozitaka? Hicho ndicho tunachopaswa kufanya kama Wabunge. Tusitake kukaa hapa kwa vile watu wamekuja, wakatuambia mkataba ni mbovu, basi kila anayesimama anasema mkataba ni mbovu. *Let us talk of the issues,* mkataba ni mbovu katika lipi? Mkataba ni mzuri katika lipi? Hapo tuta-*set* tofauti ya kuwa na Mbunge na kuwa shabiki wa kuambiwa sema moja, mbili, tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili tunayopaswa kujua, huu mkataba unasainiwa *between blocks;* tunaweza kuongea na *member states wetu* katika *block* yetu ya *East African countries* tuka-*negotiate the terms.* Wanashindwa kukaa kuongea na sisi kwa sababu *we always have fear of the unknown.* Tuna-*fear,* tuna-*complain,* hatuko *comfortable* hatujielewi. Kenya ikiongea tunajua wanashirikiana na mabepari kwa ajili ya ku-*colonize*. Taifa lingine likiongea sisi hatuwezi kujisimamia kama nchi? Tutaanza lini kujisimamia? Tuwashawishi sasa *member states, the East African blocks* twende *forward* tuwaambie *these terms so far are not favourable, we want (a), (b), (c)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, swali ambalo tunapaswa kuongea leo, tuna *bilateral relationship between* Kenya, Uganda na nyingine *East Afican States,* tunakaa humu ndani, tunawa-*brand* Kenya kama watu wanaotaka watu-*colonize* halafu Mheshimiwa Rais anaenda kushinda Kenya, anasema *those are our brothers and sisters. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka katika hii *summit* ya *East Africa*, Museveni aliwaambia, *let us not punish the Kenyans simply because they are one inch taller.* Tutakuwa tunafanya makosa. Tuongee na Kenya *with terms, you guys*

*look here,* kwa kusaini huu mkataba, sisi tutapoteza kwa kiwango hiki, mnaonaje? Tunaweza ku-*negotiate* vipi tu-*compensate* hii *deficit? Instead of arguing,* tuna-*complain* humu ndani. Tujipime upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukataa kwa matusi na vijembe, vinahatarisha hata urafiki wetu na Kenya, Uganda, Rwanda na bado hatuna *terms* tunaleta mezani, tunataka moja, mbili, tatu. Niambieni tunataka nini zaidi ya ku-*complain? (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tukimaliza sasa tujiulize swali, tunagombana na Kenya au tunagombana na *Europen Union?* Tukikaa sasa kama *block* ya *East Africa* ndiyo tutaenda kupambana sasa na *European Union between the terms we want to have. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo tofauti tunayochangia hapa, tuseme tuna-*complain* kuhusu mkataba; tunasema tusaini mkataba au tusaini *terms?* Tusisaini *terms;* tusisaini mkataba, tusaini *terms*. Tuwaambie *we want* (a), (b), (c). Tukizileta hapa, tutasaini na siyo mkataba tunaousema.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Wewe unataka nini?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nadhani watakuwa wameelewa. Tutofautishe ushabiki na *issues. Let us talk of the issues,* tusiongelee *propaganda*.

**MBUNGE FULANI:** Wewe tuambie, unataka nini?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Nenda kwenye vifungu wewe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Bashe ndio mchangiaji anayefuata. *(Kicheko)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Labda kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara na Serikali kwa ujumla kwa kuleta mjadala ndani ya Bunge wa kujadili mkataba ambao Taifa letu

lingeingia. Naiomba Serikali, *spirit* ya kuleta mikataba Bungeni na uangalie namna gani unaweza kutusaidia kupitia ofisi yako, mikataba ikawa inaletwa ili kupata *mandate* ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nianze kujenga hoja yangu; kwa nini Watanzania tunahoji juu ya mkataba wa *EPA? From the business perspective,* mahali ambapo mnaenda kushindana hakuna kuaminiana, ndiyo maana tunayoosheana vidole. Tatizo la mkataba huu, hali-*recognize state as an individual* lina-*define parties as a group.* Hili ni tatizo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningesema na ushauri wangu kwa Serikali, kwa sababu *section 143* ya Mkataba wa *EPA,* kama hawa wazungu wana nia njema na uchumi wa nchi yetu, tupeleke *amendment;* kwa sababu *section* 143 inaruhusu kupeleka *amendment.* Tupeleke *amendment* ku-*redefine parties,* kila nchi iingie mkataba na *EPA* kivyake kwa kuangalia maslahi yake. Bila hivyo, hatuna sababu ya kusaini mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Ukiusoma mkataba huu unanikumbusha wakati nasoma *form three* historia; *triangular trade. This is another triangular trade in a different way.* Ni mkataba ambao unatujenga sisi kuwa *producers* wa *raw material and become a market for them. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya pili, mkataba huu unapingana na *dream* ambayo Tanzania imekuwa nayo toka tulivyopata Uhuru. Mwaka 1964 tuli-*develop thinking* ya kuwa na *industries,* tuka-*fail*. Vilevile *mistrust* kati yetu na Kenya jamani tusisahau. Mwaka 2015 kabla ya Bunge, Mawaziri wetu walienda kukaa kwenye *East Africa,* wakakubaliana mambo ya msingi kama *block*.

Moja, walikubaliana kuweka kodi kwenye *transit goods;* sisi tumekuja kuweka, Wakenya wamefuta. Kwa hiyo, *how can we trust them? We will never trust them* kwa sababu ya historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo tumekubaliana na wao toka tuna Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kwanza, Jumuiya ya Afrika Mashariki ya pili, wenzetu wameshindwa ku-*honour* kwa kuangalia maslahi yao. Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi sana ambalo tunatakiwa tulione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ukisoma *Article 20* kwenye mkataba huu, unazungumzia *issues* za *tax; import duties,* kutoa uhuru na kufungua *borders without restriction.* Wanakuwekea *conditions* kabisa kwamba ukitaka kufanya *protection on your internal market or internal development,* lazima upate *approval* kutoka kwao. *Who are they? Are we not free country? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili ujue mkataba huu ni shida, wanazungumzia *compensation framework* ambapo hawatoi *commitment. They know we are going to lose money; we are going to lose our development truck,* lakini hawaweki *commitment, this is the problem.* Kwa hiyo, ndiyo maana nasema, tusiseme kwamba tuko kisiwani, tuko kwenye dunia; lakini mkataba lazima uwe *win win situation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nataka kumshauri Waziri wa Viwanda, kwa kuwa *section 143* inatoa ruhusa ya kufanya *amendment; proposal* ya kwanza, *redefinition of parties, "this has to be a country between EU and Tanzania, not EU with East Africa, that is number one. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *number two,* tukubaliane, *we have raw material, they have capital, they have technology;* tukubaliane kwamba chochote wanachotaka kuuza kwenye soko lao, viwanda vyao wahamishie kwetu, tu-*produce* ndani. *If they want, they sing our song, not their song. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa *protective*; tusipokubali kama nchi ku-*protect interest* zetu za ndani, nataka niwahakikishie, tunaletewa; amesema mama yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia *this is a second scramble of Africa,* tunageuka wazalishaji wa *raw materials* kama wakati ule tulipokuwa wazalishaji wa watumwa.

Mheshimiwa Spika, ukisoma *Article 75* kwenye huu mkataba, unazungumzia *issue* za *economic development*. Vilevile, wameorodhesha *items,* wame-*avoid* kitu kimoja, *they know, there is no development, without industrialization. There is no anywhere* kwenye huu mkataba mimi nimeusoma *page by page*. Wanako-*require* na kukubali kwamba katika *transfer of knowledge we will transfer* teknolojia za viwanda kwenye nchi ambazo tunaingia nazo kwenye mikataba, lakini *EPA Agreement* wametugawa kama Afrika. *EPA Agreement content* zake kwenye West Afrika, hazifanani na East Africa. Kwa hiyo, wametugawagawa kwa maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niishauri Serikali, hamjakosea kutokusaini na niipongeze Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais kutokusaini mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu uende uwe ni mkataba kati ya Tanzania...

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Kangi Lugola.

**TAARIFA**

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa nzuri sana Mheshimiwa Bashe, pale ambapo ametukonga Bunge hili kuhusu nchi kuingia moja moja na nchi kuingia kama *block*. Ndiyo maana katika mkataba huu ukiangalia *page* ya pili, sisi wametuingiza nchi zote kama *block* moja, *East Africa,* lakini ukienda *page* ya tatu wazungu walivyo wajanja wameingia nchi moja moja halafu wakamalizia tena *and European Union*. Kwa hiyo, wao wameingia nchi moja moja, halafu wakaingia kama *block* tena.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliona Mheshimiwa Bashe ametukonga, tumpe hii taarifa, ni nzuri sana. Ni wajanja sana hawa. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa yake. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kitu kimoja, *East African Community* ni *historical*. Ilikufa kwa sababu ya *mistrust* na kwa sababu ya *economic interest* ya *individual state members*. *There is no shame* kwa nchi kuingia kwenye *block* na kujitoa. *There is no shame* kwa nchi kuingia kwenye *block* na kulinda maslahi ya watu wake na kuachana na wenzake. Watu huachana na wake zao, huachana na wazazi wao, kwa kuangalia maslahi na yale wanayoamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwatie moyo Serikali, *EPA Agreement, if they will not follow our interest we can't,* kuna *Far East*, kuna *Middle East;* kwanza leo tumbaku inadhalilishwa na wazungu; leo hii mazao yetu yanadhalilishwa na wazungu, *we should think of another way*. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bashe. Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, juzi nilisema hapa kwamba biashara ni vita. Nasikitika sana kwamba *nature* ya mjadala ambao unaendelea Bungeni ni kama watu ambao tunaenda vitani, halafu tunanyoosheana silaha.

Mheshimiwa Spika, inapokuja kwenye masuala ambayo nchi inakwenda kupambana na wengine, jambo la kwanza ambalo ni lazima tulifanye, wote lazima tuwe kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siridhishwi kabisa na *nature* ya mjadala, kwa sababu hatuoni aibu kutofautiana katika jambo ambalo huko tunakokwenda tunakwenda kupigwa na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitawaambia kitu kimoja, *why Kenya has signed?* Kwa wale ambao labda mtakuwa hamfahamu, *why Kenya has signed an EPA* kinyume na maagizo ambayo Wakuu wa nchi wa Afrika Mashariki wamekubaliana? *Why has they signed?* Maua! Biashara ya maua ndiyo imewafanya Kenya waseme *to hell with EAC,* sisi tunasaini. Maua tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama una nchi kama Kenya yenye uchumi mkubwa zaidi ya Tanzania, inakuwa tayari kuhatarisha *EAC* kwa sababu ya maua, lazima tujiulize mara mbili mbili. Hii mnarushiana mishale hii, hili siyo jambo la chama kimoja hili. Siyo jambo la CCM, siyo jambo la CHADEMA, siyo jambo la CUF, siyo jambo la ACT-Wazalendo, hili ni jambo la Tanzania. Kwa hiyo, naomba tutakapoendelea na mjadala huu tuitazame nchi, tusijitazame sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo sita muhimu ambayo yanatufanya sisi kama Tanzania tusite kuingia kwenye mkataba huu. Jambo la kwanza wanaita ni *asymmetrical liberalization. EU* wanasema sisi tuna-*liberalize* bidhaa zenu zote; nanyi tunawaruhusu kidogo kidogo, mta-*liberalise* asilimia 90 ya bidhaa zote na asilimia 10 ya bidhaa za kilimo. Wazungu wanasema, *devils is in the details.* Hiyo asilimia 10 ya bidhaa za kilimo ni nini?

Mheshimiwa Spika, ukienda kuangalia kwenye mkataba unakuta kwamba sisi tunaweza tukauza kila kitu kule, tukawabana wao waingize asilimia 10 tu, lakini ndani ya zile bidhaa 10 kuna bidhaa za mazao ya mihogo. Mazao ya mihogo ni nini? *Starch* kwamba sisi leo tunaweza tukawauzia wao mihogo *(raw),* wao wakatuletea *starch.* Ndivyo mkataba ambavyo upo. Kuna mazao mengi sana, ndiyo maana nasema, *devils in the details.*

Mheshimiwa Spika, wanatuambia kwamba hakuna *export taxes,* nini maana ya hii? Maana yake ni kwamba leo mkitaka msiuze korosho ambayo ni ghafi, mnataka muuze korosho iliyobanguliwa, *EU* wanasema usiweke kodi kwenye korosho ghafi. Sisi sera yetu ya kibiashara ni kwamba ili kuhakikisha watu wanabangua korosho, tunaweka kodi kwenye korosho ghafi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba huu, ili tufanye hivyo, lazima kwanza tuombe ruhusa kwa *European Union. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni ngozi. Ni kwa nini nchi ya Ethiopia imekataa katakata hata ku-*negotiate* na *European Union?* Kwa sababu Ethiopia wamesema sisi tunataka kujenga kwanza uwezo wetu wa ndani, tukishaweza kushindana na ninyi, tutakuja ku-*negotiate* tuweze kuwa na mkataba, hiyo ni *Article 14.2. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo hapa ambalo limekuwa likiongelewa, lakini haliwekewi *details; revenue loses.* Kwa sababu, unapozuia *export taxes* na unaporuhusu bidhaa za *European Union* kuingia nchini bila kodi, maana yake ni kwamba, hutakuwa tena na *import taxes* ya bidhaa zote zinazotoka *European Union,* huta-*charge excise duty* kutoka bidhaa zote zinazotoka *European Union,* hauta-*charge VAT* kwenye bidhaa zote zinazotoka *European Union*…

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba niongezewe muda kidogo. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Najua ni ya kwanza, lakini nina *point* sita.

**MBUNGE FULANI:** Unataka msaada huku?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kitakachotokea tutapoteza. Hata kwa *East Africa* nzima tutapoteza *Euro* bilioni 3.6, zaidi ya shilingi trilioni nane. Kwa Tanzania peke yake tutapoteza dola milioni 853. Hesabu hizi zimefanywa na *European Union* wenyewe. Sasa nini ambacho kilitakiwa kifanywe?

Mheshimiwa Spika, kulitakiwa kuwe na mfumo wa kuweza kufidia hiyo *loss. EU* wamekataa huo mfumo wa kufidia *loss. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba nipendekeze baadhi ya vitu. Moja, itakuwa ni faida kubwa kwa nchi yetu, kama mkataba wa namna hii ukisainiwa na Afrika nzima yaani kuwe na *Continental Free Trade Agreement* ambayo ndiyo iingie mahusiano na *European Union.* Kwa hiyo, nilikuwa nataka katika moja ya mapendekezo yetu, ushauri wetu kwa Serikali ni kwamba Tanzania itumie nguvu yake ya kidiplomasia ku-*rally* nchi nyingine za Kiafrika ili

mkataba huu uondoke kwenye *individual regional groups* ambazo tayari zimeshasambaratika, tuwe na *continental approach* dhidi ya *European Union.* Faida yake kubwa hii ni kwamba, itasababisha tuwe na *free trade area within Africa* na tuwe na mahusiano na nchi hizo tukiwa na ukubwa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni lazima tu-*negotiate;* yaani moja ya maagizo ambayo Bunge linatakiwa litoe kwa Serikali, ni ku-*negotiate compensation mechanism* ya *revenue losses,* kwa sababu ukiingia mkataba wa namna hii, kuna *trade diversion.* Zile bidhaa ambazo tungeweza kuziagiza kutoka nchi nyingine, zikipewa *preferential treatment,* bidhaa za *EU* maana yake ni kwamba zinapotea. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na *compensation framework.* Bila hiyo *compensation framework,* sisi ndio ambao tutaingia kwenye shida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Mawaziri wamshauri Mheshimiwa Rais kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hii *point* ya mwisho tu.

**MBUNGE FULANI:** Malizia tu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Mawaziri wamshauri Rais. Kwa kuwa sasa hivi tupo kwenye hali ya juu sana ya majadiliano ya jambo hili, tunahitaji *a political commissar* ambaye akilala, akiamka anaangalia hii mikataba ya kibiashara ya Kimataifa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wizara ya Viwanda na Biashara ina Waziri tu, haina Naibu Waziri. Waziri akihangaika na kututafutia viwanda, atapoteza *focus* ya kuhangaika kwenye *negotiation.*

Kwa hiyo, tuiombe Serikali, sisi hatuna mamlaka ya kumwagiza Rais, lakini tumshauri kwamba tunahitaji msaidizi wa Mheshimiwa Mwijage pale *(political commissar)* ambaye kazi yake yeye na apewe *instrument* maalum ya ku-*deal* na hili jambo ili kuhakikisha ya kwamba *at all time* tuna mtu ambaye yuko *dedicated* kwenye jambo hili tu, wakati Waziri anaangalia kwa ujumla wake masuala mengine ya viwanda na kadhalika, ili tuweze kuwa na nguvu ya kuweza kwenda kushindana na kujadiliana na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto. Mheshimiwa Khatib Said Haji, halafu Mheshimiwa Peter Msingwa na Mheshimiwa Lusinde wajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nianze kwa kusema kwamba, wakati tuna msiba mkubwa uliolipata Taifa kwa kuondokewa na kipenzi chetu, nasikitika kwamba tunaletewa tena msiba mwingine ambao ni mkataba usiofaa hata kuujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo leo nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimesimama hapa kama mzalendo wa Tanzania. Katika mambo ya kinchi, katika mambo ambayo yataleta tija au hasara kwa nchi hii, na mimi nakubaliana, lazima tuwe wamoja. Naupongeza sana uongozi wa juu wa chama changu kwa kuliona hili na kutuletea mawazo ambayo siyo lazima, lakini kutuelekeza katika njia ya kwenda katika mjadala huu ambao ni hasara kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kutafuta nondo zangu hapa, kila nilivyoangalia sizioni, lakini nina wasiwasi ndugu yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe kazichukua. Kwa sababu yale niliyopanga kuyasema hasa, ndiyo yale ambayo ameyawakilisha. Hongera sana Mheshimiwa Zitto Kabwe. Ametupa somo na funzo zuri ambalo tunafika mahali kama Taifa lazima tukubaliane katika mambo ya msingi kama hili ambalo tunalo sasa hivi mbele ya meza yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, binafsi kuna kipengele katika mkataba huu kinachosema kwamba tutakaposaini mkataba huu hatutakuwa tena na uwezo kama nchi kuwa na ushirikiano na nchi nyingine, hii ni aibu! Hii ni aibu kwa sababu Tanzania ni Taifa huru. Hautakuja mkataba wowote ambao utatuzuia kuwa na ushirikiano wa kibiashara, ya kiuchumi au ya kisiasa na nchi nyingine, mkataba huo ukawa na una manufaa kwa nchi hii, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kifungu kingine kinasema kwamba tukishaingia katika mkataba huu, suala la kupandisha kodi kwa bidhaa itakuwa halina tena nafasi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hii kila mwaka unaona kodi zetu ni hizo za sigara, bia, vilevi na kadhalika. Hizo ndiyo kodi; *revenue* kubwa inatokana na hayo. Leo tukisaini mkataba huu, hayo mambo yatakuwa hayapo. Kuingiliwa uhuru wa nchi yetu kwa namna yoyote ni janga ambalo mzalendo wa ukweli haifai kulishabikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isionekane kwamba wapinzani ni watu wa kukataa kila kitu. Niwahakikishie, likija jambo lenye maslahi tutakuwa pamoja na hatutaangalia chama, lakini niwatahadharishe wenzangu, hasa upande huo, likija jambo la ovyo ovyo kama vile ulivyokuwa Muswada wa Habari, tutaukataa mpaka mwisho wa kiama. Tuambiane ukweli, mkileta lenye manufaa ni kama mnavyotuona, lakini mkija na mambo ya ovyo hatutakuwa pamoja, lazima muone mawazo yetu na muelewe kwamba sisi tupo kwa ajili ya Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mashaka sana. Jamhuri ya Kenya ni watu ambao wakati mwingine sijui wanatuona sisi Watanzania tukoje. Wamekuwa ni watu wa ku-*beep, beep* tu. Hii Afrika Mashariki haikuja kwa lengo la kunufaisha nchi moja katika Afrika Mashariki na nchi nyingine ziwe mashahidi, haiwezekani. Leo wenzetu Kenya kwa sababu katika mauzo ya nje wana karibu asilimia 90 na kitu, kwa hiyo, wao ni haraka sana kusaini katika hili; na wamekimbilia sana katika hilo, lakini hawatuangalii sisi. Nao ni miongoni mwa zile nchi zilizojifanya wako tayari katika kila jambo. Kwa hiyo, kama hili wako tayari, watakwenda peke yao, sisi bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika; Mheshimiwa Spika, umekuwa mtoro sana siku hizi mpaka tunakusahau. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kenya hao hao tuliokaa nao katika makubaliano ya *single custom territory,* ndio hao wametuacha kwenye *junction.* Sisi tumekwenda, wao wamechomoa. *VAT on transit goods,* hao hao Wakenya tulikubaliana, wakati wa kusaini, sisi tumeingia kichwa kichwa, wao wamechomoa. Mpaka lini Kenya watatuona sisi ni watu ambao ni kama wa kututumia *rubber stamp* ya kuendeleza mambo yao na sisi kutuacha nyuma. Haiwezekani, lazima tujiangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inatupa funzo moja kubwa sana. Waheshimiwa, Serikali hii ya CCM hebu sasa fikirieni, dira na sera zetu za kiuchumi zinatuelekeza vipi? Haya ndiyo matatizo makubwa tunayoyapata; kuna mjuvi wa maneno mmoja au mjuaji wa kusema mmoja, alisema kwamba nahodha bora ni yule anayejua bahari anayokwenda. Kwa nahodha asiyejua bahari anayokwenda, hakuna upepo utakaokuwa muafaka katika safari yake, hakuna. Kwamba nahodha ni yule anayejua nchi yangu hii Tanzania, Serikali yetu; sera zetu za kiuchumi zinapelekea sasa wenzetu kuweka mikataba hii na kutuletea kuona kwamba sisi kwa sababu ya dhiki zetu, kwa sababu ya njaa zetu, wao watuletee lolote na tutakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema kwamba ni afadhali tufe na dhiki zetu kuliko kukubali mikataba ya ovyo ovyo kama hii. Hatutakuwa tayari kufungiwa ngulai na kwa sababu eti ni nchi maskini tuendelee kukubali. Sasa umaskini huu ni lazima tuwaulize watawala wa miaka 50 mlioitawala nchi hii, kwa nini nchi yetu inaendelea kuwa maskini wakati sera nzuri na mambo mazuri mnayataja kwenye mikutano, lakini kwenye utekelezaji tunakuwa *zero? Why? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima sasa mtimize wajibu wenu. Nakiomba sana chama kizee cha CCM, wengine wanaposema chama kizee wanaona kama ni kejeli; uzee ni busara. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi ninapokiita chama kizee, naamini kuna busara. Niliwaambia bahati nzuri sana Bunge hili asilimia karibu 60 ni vijana na wengi ni ninyi, tusifike mahali tukaona wale wazee waliokuwemo kwenye Bunge hili ni bora kuliko vijana ninyi mlio na mawazo ya kizee kupita kiasi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khatib Said Haji. Amewatania CCM. CCM nao wakawa wananiandikia hapa wanasema, hivi CUF bado ipo? *(Makofi/Kicheko)*

Nilimtaja Mheshimiwa Mchungaji Msigwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatia.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *In principle,* nakubaliana na mawazo ya Serikali kwamba mkataba huu tusiusaini, lakini kuna mambo ambayo kama Wabunge na kama wawakilishi wa wananchi lazima tuyajadili kwa pamoja tuone faida na hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napingana sana na wenzangu wanaofika hapa wanasema kwa sababu Mheshimiwa Mkapa amesema, Mheshimiwa Magufuli amesema, kwa hiyo, hatuusaini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Si tunapeana zamu ya kuzungumza jamani! Si mnisikilize! Si ndiyo zamu!

**MBUNGE FULANI:** Amesema!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Si zamu kuongea jamani. Mbona mna…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ninyi mna busara…

**SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa, ongea na Spika.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, wajibu wetu sisi kama Wabunge hapa na hii ndiyo tabia ya Watanzania wengi, hatupendi kuhoji, hatupendi kudadisi, hatupendi kubishiwa. Hiki kitu kimekuja hapa, tuna haki ya kuhoji, kudadisi na kuuliza ili tukubaliane. Sisi siyo nyumbu kwamba tuingie tu mtoni, kwa nini mnataka tusidadisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu mkataba wataalam walipokuja juzi hapa, Profesa Kabudi alifafanua vizuri sana, lakini katika *article* 140 na kitu, alizungumza *article* karibu 20 au 15. Alizijadili hapa vizuri sana kwa weledi. Sisi kama Taifa amezungumza vizuri sana dada yangu hapa, tuna tabia ya ku-*complain,* tuna tabia ya kulialia! *Complainers attract complainers.* Kila wakati tunalalamika. Nakubaliana kabisa kwamba hii ni vita. Kila mtu anataka kupata hii keki ya uchumi duniani; kwa nini mnadhani Kenya wakubaliane na sisi kama wao hawapati maslahi? Kwa nini mnafikiri *Europeans* waje hapa kufanya mikataba kama wao hawana maslahi?

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu sisi kama Taifa kutengeneza mazingira ambayo na sisi tuta-*capitalise* kupata faida. Siyo kila saa tunakuja hapa tunalialia, Kenya wametuzidi, Kenya wametuzidi. Kama wewe ni mpumbavu, upumbavu wako hauwezi kutoka kwa sababu unamchukia mwenye akili. *We are responsible* kujifunza kwa nini Kenya kila siku wanakuwa *pro-active* na sisi tunachelewa ku-*capitalise* huko mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu tunalia nao hapa kwamba wana mazingira mazuri. Sisi hapa tunalalamika; Mzee wa *sound* hapa kila siku ana viwanda vya kwenye mabegi. Sasa kama tuna viwanda vya kwenye mabegi, tutaenda kuuza nini Ulaya? Kutokuwa na kitu cha kuuza Ulaya *is that their problem or is our problem?* Badala ya kwamba sisi tukae hapa tujadiliane ni kitu gani tutapeleka Ulaya, tunalaumu kwa sababu hatuna kitu cha kuuza Ulaya. *Is that their fault? That is our fault. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumza kwenye bajeti iliyopita, tumelalamika sana jinsi ambavyo Wizara ya Mambo ya Nje, imekuwa dhaifu katika masuala ya diplomasia ya kiuchumi. Ni kwa sababu hatuna wataalamu ambao wanaangalia mbele kuangalia Tanzania tunahitaji nini.

Mheshimiwa Spika, amezungumza dada yangu hapa, ukianza kujiuliza kaka yangu Mwijage hivi tunahitaji nini? Kwenye *East Africa* tunataka kupata nini? Tunataka kufanya biashara ipi? Iko kwenye makaratasi hapa halafu mnataka kutuambia Waheshimiwa Wabunge tukienda kwa wananchi...

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, upande gani?

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Kutoka hapa.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mwongeaji. Namheshimu sana Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, lakini ni vizuri pia akakumbuka historia kwamba watawala kwa maana ya wazungu walikuwa wanatumia Tanganyika kwa ajili ya kuzalisha *raw material* wakajenga viwanda Kenya. Kwa hiyo, siyo kwamba ni sisi tumetaka, ni watawala. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nakushukuru kwa taarifa, lakini wazungu sio watawala wa Kenya. Kenya inatawaliwa na Uhuru Kenyatta ambaye ni Mswahili. Kama wenzetu wametuzidi akili...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hili suala la *blame shift*, kila siku tuna-*blame* wengine tunashindwa kuwa *responsible* kwa uchumi wetu, hebu tuliache. Kwa sababu Wizara ya Mambo ya Nje ina udhaifu mkubwa sana katika nchi hii katika masuala ya diplomasia ya kiuchumi.

Mhemiwa Spika, nimemuuliza ni kitu gani tunataka kama Taifa upande wa Afrika Mashariki, ni kitu gani tunataka *SADEC?* Tunakuja hapa tunalialia tu, lakini hatujui tunataka nini. Hebu tuambie kwa mfano Wabunge tunataka tufanye biashara vipi na Afrika Mashariki, Ulaya, Marekani, Afrika ya Kusini au na Brazil? Tunataka tufanye biashara gani? Tunayo mikataba.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, la pili, tumezungumza juzi kwenye ripoti ya …

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**SPIKA:** Naomba Waheshimiwa Wabunge, tuvumiliane, nina majina mengi ya wachangiaji. Tusipoteze muda watu wamalize, maana ni dakika kumi haraka haraka.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, naomba unilinde kwenye muda wangu, naona wanani-*disturb* sana.

**SPIKA:** Atajibiwa tu hoja zake. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kwenye ripoti ya *GCI* imezungumza sana jinsi ambavyo mazingira hata ya kufanya biashara katika nchi yetu ni magumu sana; mojawapo ya mazingira magumu ni kwamba Tanzania hatuna utaalam hata wa TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, nchi za nje zinashindwa kufanya biashara na sisi kwa sababu hatuna utaalam huo. Mazingira ya rushwa, ufisadi na urasimu katika kufanya biashara, haya mambo hatu-*deal* nayo, matokeo yake tunaanza kuwalaumu Kenya, tunailalamikia Kenya, Kenya wanatuzidi, wametutangulia. *Is that their problem or our problem?*

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya mambo yote ambayo Serikali ilileta wataalam hapa ambayo nakubaliana nayo kwamba lazima tuwe waangalifu, lakini lazima tuji-*position* mahali ambapo tuwe na uwezo wa ku-*compete* Kimataifa, siyo kulialia. *We are like babies*, *every time* tunalia, Kenya wametutangulia. Kwani wewe kutanguliwa unaona tatizo gani? Tulipata uhuru kwa pamoja; kila siku tunalialia Kenya wajanja, Kenya wajanja. Hapa Tanzania tunalalamika, Kenya wajanja; ukienda kwenye *aviation,* Kenya wanatuzidi; hata hapa Tanzania, wao wako zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *tourism,* Kenya wametuzidi. Tunalialia. Hatuandai watu wetu, hamweki mipango madhubuti ya kuandaa watu wetu kwenye mazingira ya kibiashara, tunabaki kulialia, mwisho wa siku tunakuwa kwenye mkia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Kaijage. *(Kicheko)*

Si Kaijage jamani!

**MBUNGE FULANI:** Mwijage! *(Kicheko)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwijage, nakushauri, hivi viwanda vyako vya kwenye mabegi na kwenye mifuko ni kweli hatutapeleka bidhaa Ulaya, haiwezekani. Ni lazima tutengeneze mazingira. Mnalalamikia Kenya eti viwanda vya Wazungu viko Kenya, kwa nini nyie msilete viwanda vya wazungu hapa? Kwani si Watanzania wataajiriwa? Hiyo Dangote ni ya Mtanzania? Si ni Mnaigeria amekuja hapa Watanzania wanaajiriwa? Tusitafute visingizio tunashindwa kujipanga wenyewe, tunashindwa kutengeneza mazingira mazuri, halafu inapokuja mikataba hii tunaanza kulaumiana.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, nimemwona Mheshimiwa Hawa Ghasia hapa, mazungumzo mengine anayozungumza siyo ya kidiplomasia; ya kusema watu wengine tuna- *support* kwa sababu ya ushoga, hii siyo lugha za kidiplomasia. Tanzania siyo kisiwa, tunahitajiana vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo tunatakiwa tujue, kwa nini Kenya wamesaini? Lazima tujue kwa nini Kenya wamesaini? Haya masuala ya kidiplomasia ni vizuri tukatoa michango ya kidiplomasia kwa sababu tunahitajiana na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wakenya wamesaini, Watanzania tunakaa pembeni; lakini kumbuka kuna siku kutakuwa na jambo ambalo Watanzania tutakuwa na faida nayo kubwa, lakini kuna uwezekano tukamhitaji Kenya au Rwanda. Wao watakapochomoa, itakuwaje? Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo ni lazima tujadiliane kama Taifa, siyo tukiwa *blind;* lazima tujadiliane tu-*dialogue*.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Unaunga mkono au unapinga mkono? Ahsante sana. Mheshimiwa Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Zungu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mungu kwa kutupa nafasi nzuri kabisa ya kujadili juu ya huu Mkataba wa *EPA*. Vilevile sina budi nichukue fursa hii katika Bunge hili kumpongeza sana Profesa Kabudi kwa namna alivyotufumbua macho. Profesa Kabudi ni moja ya Watanzania wenye uwezo wa walichonacho kuwasaidia na wengine waweze kuelewa. Hilo ni jambo zuri sana na kwa kweli tunajivunia sana kwamba elimu yako inawafaa wengi na inaifaa nchi. Hongera sana Profesa Kabudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ngumu sana kusimama hapa kuutetea huu mkataba na ndiyo maana unaweza kuona kuna baadhi wanaojaribu wanapata shida sana. Hauna namna yoyote ya kuuzungumzia uzuri wa Mkataba huu, hata kama umeandaliwa au umejiandaa; ni jambo gumu sana. Ndiyo maana umeona hata waliojaribu kufanya hivyo, wamejikuta wao wenyewe wakipata shida sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Khatib, ameonyesha kwamba isiyo kongwe haivushi, kwamba ukongwe wa CCM ni jambo zuri na inaendelea kuvusha nchi hii. Amesema chama hiki ni kikongwe. Ukishasema kikongwe, maana yake hicho ndicho chenye uwezo wa kuvusha baadhi ya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama umewasikiliza wazungumzaji wachache waliotangulia, nataka niungane nao kwamba hata kuchukua muda mwingi kuujadili mkataba huu ni kutumia tu fedha za Watanzania vibaya, huu mkataba haukustahili hata kufika huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni moja ya mikataba mibovu kabisa ambao pengine nimsaidie hata mzungumzaji aliyepita, kwa nini Kenya wamesaini? Wamesaini bila kuutafakari kwa makini. Wangetafakari kwa makini; na nikubaliane na Mhesimiwa Zitto kwamba wamesaini kwa ajili ya kufanya biashara ya maua, siyo kwa ajili ya usalama wa mkataba wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 140, hakiruhusu nchi moja kujitoa baada ya kuingia. Mimi nataka niseme, Jumuiya yetu ya *East Africa*, kama kuna jambo mmetuangusha ni katika jambo hili. Kwa nini msingekaa wenyewe kwanza mkaupitia huu mkataba? *Secretariat* ya Jumuiya ya *East Africa* mkakaa mkausoma kwa pamoja kabla ya kuruhusu nchi moja moja kwenda kujisainia yenyewe? Kwa hiyo, hapa tunaanza kona kuna *problem* kwenye Jumuiya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki iwe inakaa pamoja kwenye mambo ya muhimu na mazito kama haya, leo tusingeona aibu ya Kenya kutangulia kusaini kama mngekaa pamoja mkashauriana, kwamba jamani hivi unaingiaje kwenye mkataba ambao unakuchagulia rafiki? Unaingiaje kwenye mkataba ambao unakulazimisha kushirikiana na adui? Huu mkataba kadri unavyousoma, kuna sehemu unakuchagulia rafiki wa kufanya naye biashara na kuna sehemu unakulazimisha kukaribiana na mtu ambaye wakati huo humhitaji.

Mheshimiwa Spika, ukitazama kwa makini mkataba huu wa *EPA,* ni sawa sawa na mzee wangu pale kijijini kwenda kupelekewa zawadi ya kuku halafu akachukuliwa ng'ombe wake kumi; kitu ambacho hakiwezi kukubalika!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni moja ya mikataba mibovu kabisa. Nasi tunapoukataa mkataba huu na kuitaka Serikali, isiusaini, tunaukataa ili kuwaonesha Jumuiya ya Ulaya kwamba Afrika sasa inao wataalam, wanajitambua na wanaweza kufanya biashara huria na mtu yeyote. Sisi sio watu wa kupangiwa na kuletewa mikataba ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niishauri Serikali; kwa mkutadha huu, huu mkataba haufai kusainiwa hata kidogo kwa sababu una vipengele vingi vinavyodhalilisha Afrika.

**TAARIFA**

**MHE. JAMES K. MILLYA:** *Mheshimiwa Spika, natambua kabisa kwamba Mheshimiwa Lusinde yeye siyo mwanasheria na kwamba haelewi hata anachokiongea sana;* ukisoma Ibara ya 140…**[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**SPIKA:** Mheshimiwa Millya, nakuomba ungetoa maneno hayo ya kwamba haelewi anachokiongea kwa sababu huyo ni Mbunge mwenzako. Unaweza ukatofautiana naye, lakini huko ulikofika ni mbali kidogo. *(Makofi)*

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, naondoa hayo maneno, ni kuteleza kwa mdomo.

Mheshimiwa Spika, *article 140(1)* inasema hivi; *a party to this Agreement may give written notice to the other of its intention to denounce this Agreement; (2) Denunciation shall take effect after one year*. Maana yake ni kwamba unapotaka kuondoka lazima uandike...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila utaratibu)*

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Hicho cha pili, *denunciation shall take effect one year after notification.* Maana yake ukitaka kuondoka, hujafungwa moja kwa moja kwamba huwezi kuondoka. Unaweza ukatoa *written notice* na baada ya mwaka mmoja ukaondoka. Kwa hiyo, usitudanganye hata kidogo kwamba hatuwezi kuondoka. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, tafadhali taarifa hiyo.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru na namheshimu sana Mheshimiwa Millya, lakini ni mmoja wa watu wachache ambao wamerubuniwa na wazungu. Hawa wazungu waliokuja wamemwona Millya. Maana hapa hatutakiwi kutafuna maneno; kuna baadhi ya Wabunge wamewaona, inawezekana na Mheshimiwa Millya akawa ni mmojawapo kati ya waliowaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hukatazwi, unawezaje kutoa *notice* halafu mwaka mzima ukaendelea kubaki mle? Unabaki humo kwa sababu zipi? Khah, maana wewe mwenyewe unasoma, halafu unajijibu. Bahati nzuri wewe mwanasheria na pengine unaelewa zaidi, lakini umepata majibu kwamba ukishatoa *notice,* mwaka mzima unaendelea kubaki mle. Ukifanya nini kama unao uhuru wa kutoka moja kwa moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie, hili ni jambo letu wote kama Bunge, tusianze kushindana humu. Tukubaliane kwamba mkataba huu haufai, maana ndani una vi-*package* vya ushoga, una vitu vya ovyo ovyo vimefichwa humo, Watanzania watatushangaa sana.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuwezi kuburuzwa na nchi yoyote, sisi ni Taifa huru! Iwe wamasaini nchi nyingine ambazo pengine wao wanavutiwa na ushoga, sisi hatuvutiwi nao. Kwa hiyo, hatuko tayari kukubaliana na jambo hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi naomba sana, mtu yeyote mwenye taarifa kwa kweli iwe taarifa ya maana. Vinginevyo mtalifanya Bunge hili lifike mahali ambapo sipo. Haya mwenye taarifa yake!

**TAARIFA**

**MHE. AUGUSTINO V. HOLLE:** Mheshimiwa Spika, nilitaka niende kwenye hicho kifungu cha *denunciation*, ukienda ile *article* ya 140, pale namba (1) inasema, "*a party to this Agreement may give written notice to the other of its intention to denounce this Agreement." A party; not a country.* Kwa hiyo, hapa siyo nchi inayotoka, ni *block; the entire block!* Eeh! Nataka nimpe taarifa aliyempa taarifa Mheshimiwa Lusinde, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hiyo taarifa kwa kweli alitakiwa apewe Mheshimiwa Ole-Millya zaidi. Mheshimiwa Lusinde endelea.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, hiyo itakuwa imetusaidia wote, lakini zaidi sana, Mheshimiwa Millya ameelewa kwamba ni ile *block* ndiyo inatakiwa kuomba kutoka lakini siyo nchi moja ambayo imezuiwa na mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, tuseme tu kwa kifupi, mkataba huu haufai. *East Africa* wawe makini na mikataba ya namna hii, waipitie wao wenyewe kama Sekretatieti na wao na uchungu na nchi zao kabla ya kuangalia manufaa watakayopata. Kwa sababu wakati mwingine kuna hadithi moja; watu waliwahi kushangilia kwenda kufanya kazi kwa Mfalme, wakati huo huo kulikuwa kuna agizo kwamba ili ukafanye kazi kwa Mfalme, ni lazima uhasiwe kwanza ndiyo uruhusiwe kufanya kazi kwa Mfalme. Kuna watu wakashangilia, walipofika pale kukuta masharti, yakawa magumu kwao. Kwa hiyo, kila mikataba ya kimataifa inapokuja, tuwe na Sekretarieti zinazotazama kwa makini, siyo kukurupuka! Tutakuja tuingie kwenye matatizo makubwa na tuziingize kwenye shida kubwa. Tutakuja kupata adhabu ambazo hazina msingi. Maana kadri unavyousoma unakutana na sehemu inasema *EU* inaweza kuchukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza kuona ambayo tunaweza tukaingia kwenye matatizo makubwa ya kuchukuliwa hatua na uhuru wa nchi zetu ukawa unatekwa bila sisi wenyewe kuelewa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono mkataba usisainiwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde. Mheshimiwa Zungu halafu Mheshimiwa Profesa Muhongo.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua nafasi hii kukushukuru, lakini vilevile lazima kwanza tukubali. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna alivyouona na namna alivyoshaurika. Namshukuru Mheshimiwa Mkapa, Mheshimiwa Msigwa kasema tusikatae kwa sababu tu kuna watu wamesema tuukatae. Tunaukataa kwa sababu mkataba huu ni *non starter* kwa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *if you don't deal with the problem, the problem will deal with you*. Hili ni tatizo kubwa sana. Sasa kuna mjumbe amesema tunaukataa kwa sababu kuna watu, viongozi wetu wamesema. Ni kweli viongozi wamesema na wamesema sahihi. Sasa hapa kuna kiongozi kwenye Bunge *EU* kuna kamati mbili; *International Trade* na *International Development*. Hizi kamati nazo hazielewani kuhusu mkataba huu. *International Trade*

wanaushikilia mkataba huu na *International Development* hawautaki mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna mtu kasema tunawasikiliza watu, tumsikilize Mbunge wa *European Union* anachokisema kuhusu mkataba huu. Anasema: *"the agreement to pose a risk to regional economies as their infant industries will face unfair competition due to products from the European Union. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu ni Mbunge wa *European Union,* siyo Mtanzania wala hatoki *East Africa.* Anasema, *she point it out that the European Union had pushed a hard bargain in the deal large by arm twisting Kenya."* Wamewafuata Kenya wakawapinda mkono. Anaendelea kusema, *"I think this kind of agreement is unfair for the East African Region; Europe is pushing very hard stance and they have taken Kenya as a leader. Kenya is the only one that has interest in this trade agreement, because they are not a list development country."* Kenya ni *non list development country.* Siyo *list* kama sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anasema, *Kenya need this agreement to maintain acces to the European Union.* Anaendelea kusema; *"if the agreement goes through, you East Africans;"* anatuambia sisi, hawaambii Kenya, anatuambia wote *block*, *"have no more preferences; you will receive all products coming from Europe in your market which will promote unfair competition. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *European competence is high,* ni kweli! Hivi maziwa ya salsa yatakuja hapa, wanakuta maziwa yametoka Ulaya ya dola moja badala ya haya ya kwetu ya dola moja na nusu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili jambo wenyewe wanatutahadharisha. Wanaendelea kusema, *so far they have been able to guarantee Kenya access to the EU market without even this agreement*.

Mheshimiwa Spika, umeona tunapopelekwa? Kenya kusaini huu mkataba au wasiusaini, tayari wana soko *EU.* Kwa hiyo, *they don't need this agreement. We have guarantee* Kenya! Hao ni *EU* wanasema, *that we still have access to the European market and to help their market in internal African Market.*

Mheshimiwa Spika, mengi tutayasema, nchi hii tukiingia kwenye mkataba huu, tumeua *industries* ambazo sasa hivi Serikali inataka kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni mmoja wa watu ambao wameijengea heshima kubwa sana nchi hii. Kwenye mikutano ya *EUSP - Brussels,* ndio ulikuwa unasimama na kutuongoza sisi kupinga kitu hiki cha kutuingiza katika matatizo

makubwa sana. *It goes without saying.* Tukisaini mkataba huu, *we are done. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *illegal fishing* inayofanywa kwenye bahari zetu. Tuna-*lose 250 million Euros* kwa kila mwaka kwa samaki kupelekwa Soko la Ulaya. Samaki hawa wanaibiwa katika bahari zetu, samaki hawa wakifika kwenye Soko la Ulaya wanatozwa kodi kule; na kodi hiyo inabadiki kutumika kwa wananchi wa *European Union*, sisi hatupati chochote. Nilitegemea kwanza angesema wange-*deal* na samaki zinazoibiwa kwetu kabla hazijapelekwa kwao kutumia kwa watu wao.

Mheshimiwa Spika, mkataba huu unasema, kukiwa na *loses* za *revenue* wataweka mfuko. Hebu tujiulize Waheshimiwa Wabunge, zipo nchi zimeshasaini mkataba huu; *Caribbean countries*; Mauritius hapa Afrika na kuna nchi za Afrika Magharibi zimeshaanza ku-*lose revenues.*

Mheshimiwa Spika, masuala ya *industries* katika nchi zao zimeshaanza kupotea. Mfuko huo walisema unaanzishwa, haujaanzishwa, haupo kwenye bajeti na hakuna popote katika nchi hizi zinazosaidiwa. Sisi wa tatusaidia lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mkataba ni mzuri sana, kwa lugha nzuri iliyoandikwa kisheria, lakini *it is a non starter* kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge, nchi hii tusimame pamoja kwenye suala hili; *one Nation under one God,* tusikubali kusaini mkataba huu. Kama kuna nchi imesaini, wana *interest* zao.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi nyingine hawana *interest* za Kitaifa, wana *interest* zao binafsi. Tunajua nchi zilizoingia kwenye mikataba hii wanafanya biashara *individually,* lakini tuulize, soko la maua pesa ngapi zinarudi Kenya na pesa ngapi zinabaki huko zinapopelekwa? Hatutaki kuingia kwenye matatizo kama ya Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote haya tunavyosema hapa kwamba Kenya inatumika *as a front as a leader* ni kuhusu malighafi ambayo Tanzania inayo, *nothing else.* Na wewe uliwaambia Brussels mkitaka madini yetu, jengeni viwanda kwetu. Tatizo liko wapi? Badala ya kusafirisha madini kutoka hapa kuyapeleka Ulaya, walete viwanda hapa, tuta-*promote jobs,* tutaweza kupata *revenues* za kutosha na kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kusema mengi, hili suala linafahamika, na yule anayepinga hili, analipinga tu kuonesha kwamba anasimama, anapinga. Hawana hoja ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mjono hoja, tusisaini mkataba huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saada Mkuya, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. SAADA MKUYA SALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata fursa hii na mimi nichangie katika mjadala uliopo mbele yetu. Na mimi naunga mkono hoja hii ya Serikali kwamba tusisaini mkataba huu kama ulivyo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea mbele naomba ku-*quote* maneno ya Rais Mstaafu ambayo yalikuwa *posted* kwenye gazeti la *East African,* Mheshimiwa Mkapa alisema kwamba *EPA is bad news for entire region. It is just bad news for entire region* wala siyo *for Tanzania, but for entire region. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba kama huu kama ungekuwa una *terms* nzuri, basi nadhani ingekuwa faida kwa *region,* lakini faida vilevile kwa Tanzania. *Terms* zake hazifanani na haziendani. Mheshimiwa Rais Mkapa alisema vilevile kwamba *the EPA for Tanzania and the EAC never made sense, the maths just never added up* yaani zile hesabu zake haziendi kutokana na hali yetu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pengine ingekuwa sisi kama *East Africa* tunahitaji zaidi *EU* wana soko la watu karibu milioni 700, *East Africa* tuna watu karibu milioni 300 *plus,* tungekuwa tunawahitaji zaidi kama angalau kungekuwa kuna ule uchumi unaoendana, lakini hatufanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isipokuwa tumeuleta huu mkataba hapa na tutaukataa kabisa, lakini tuchukue hii kama ni nafasi ya Tanzania kuweza kujijenga zaidi.

Kwanza, kwenye viwanda, lakini pili pengine Mheshimiwa Waziri ulichukue hili iwe ni changamoto, ingekuwa vyema kwamba huu mkataba tunaukataa, lakini wataalam wetu watuletee *alternative,* yaani zile *terms* zinakuja, hizi haziwezekani, *what do we want?* Tunakoelekea *regional integration* ndiyo itakuwa inapata nafasi zaidi kuliko *bilateral cooperation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hatuuhitaji mkataba kama huu lakini ninaamini sera yetu ya kujenga viwanda itakapokuwa imefanikiwa, tutakuwa tunahitaji mikataba ya aina hii. Kwa maana hiyo, tutakapokuwa tunakwenda, tuone ni jinsi gani tunaweza kujenga uwezo wa watu wetu, kwanza, kuangalia *critically* mikataba ya aina hii, lakini *secondly* iendane na *policy* zetu ambazo pengine tungeweza ku-*compete* zaidi na mikataba mingine au na masoko ambayo yanaambatana na mikataba kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkataba kama *EPA* unamaanisha nini? Tunakokwenda *development cooperation* inapungua na badala yake inakuja *trade cooperation.* Kwa maana hiyo, kama leo tutakuwa tunategemea zaidi *development cooperation,* kwa maana ya nchi matajiri kusaidia masikini, lakini kesho na nchi matajiri na wao zitataka ku-*benefit* kutoka kwa nchi masikini kama ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ni changamoto kwetu sisi. Tutakuwa tumeshinda leo, lakini ninaamini kwamba ni nafasi nzuri ya kujiweka vizuri zaidi kuona kwamba tutakapokuwa tunakwenda mbele, watakuja wengine na mikataba kama hii, tutaweza ku-*face* vipi? Hatuwezi kukataa kila siku, lakini ninaamini kwamba tunaweza kuchukua fursa hii kama changamoto na tukajiweka vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako namuomba Mheshimiwa Waziri, ninaamini kwamba mkataba huu utakwenda kuathiri *development cooperation* na *EU.* Nadhani tumekuja mwaka 2013, Mheshimiwa Waziri wa Fedha *by then,* tulikuja tukataka ridhaa ya Bunge kwa ajili ya kuridhiria *Cotonou Agreement* ambapo ndani yake tunapata misaada mbalimbali. Sasa kama sasa hivi tunakataa huu mkataba ambao ni *trade related,* sina uhakika wala hatuombi, lakini inawezekana tukaathiri *aid cooperation* na *EU,* wanatusaidia!

Mheshimiwa Spika, sasa namuomba Mheshimiwa Waziri, mkataba huu ambao tutaukataa hapa Bungeni leo, ninaamini afanye namna atakavyofanya aende akawaelimishe wananchi wa Zanzibar kupitia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu ninaamini nao watafurahia jambo hili ambalo limekuwa *decided* na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanapaswa kufahamu jambo ambalo linaendelea ambalo lina maslahi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri, Baraza la Wawakilishi linaketi mwisho wa mwezi huu, aende akawape semina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili na wananchi wa Zanzibar na wao waweze kuona kabisa kwamba

Serikali pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limefanya jambo la maana kabisa kutoku-*rectify* mkataba kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, hii inakwenda zaidi kwenye *regional integration.* Na sisi tunahitaji zaidi tu haya mahusiano. Sasa kwenye hili, pamoja na mambo mengine kama nchi tufanye jitihada zetu kuweza sana kuhimiza *South South Cooperation,* yale mahusiano yetu na nchi ambazo tunafanana nazo kiuchumi, kimazingira na kiitikadi ili tuone kwamba hatuendi tu mbele tukawa tuna mahusiano na *European Union* watu ambao tupo tofauti kiuchumi hata kiitikadi, lakini vilevile tuwe tuna sera madhubuti ya kuweza kuimarisha uhusiano wetu na nchi ambazo Kusini Kusini, yaani tunaita *South South Cooperation*. Mheshimiwa Waziri hilo nakuomba sana ulichukue.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri la tatu; kwa vile tunategemea athari kubwa itatokana na kutoku-*rectify* hapa, bajeti yetu itakayokuja tuhakikishe kwamba ile miradi ambayo ilikuwa inafadhiliwa na *EU,* tuiwekee mikakati ili Serikali yetu iweze kuibeba iende ikafadhiliwe na Serikali yenyewe, ama angalau tutafute *alternative*. Zanzibar tumefaidika sana na *Cotonou Agreement;* tumejengewa bandari, vilevile kuna miradi mingi ya maji ambayo *EU* imesaidia, lakini vilevile kuna miradi mingi ya utawala bora kupitia *NGOs* imesaidiwa. Tunaomba sana Serikali ijipange ili tuweze kutafuta mbadala wa nani na vipi itasaidia kuweza kuendeleza miradi kama hii.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, naunga mkono hoja. Yangu yalikuwa machache sana, kwamba Serikali isisaini, lakini tuchukue hii kama changamoto kuweza kusimama zaidi, kujiimarisha zaidi na watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa zaidi kwamba kama unakuja mkataba huu tunaukataa, lakini angalau kungekuwa na mapendekezo mbadala, yaani tuseme kifungu hiki hatukiwezi, hatukitaki, basi tuwe na kifungu kama hiki ili tuendane nacho. Kwa maana na sisi kama *block* tunawahitaji wenzetu. Leo huu ni mkataba, siyo mzuri, lakini ninaamini wakati ambapo sera zetu zitakaposimama sawasawa na kufanikiwa, tutawahitaji wao na wengine.

Kwa hiyo, naomba zaidi tuwe tunafanya kazi ya ziada. *Technical Committees* zinapokaa ziwe zinafanya kazi ya ziada na siyo kukataa, lakini vilevile walete mapendekezo kwamba ingekuwa bora jambo kama hili lingekuwa limekaa namna kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri, tunasubiri semina kule Zanzibar ili hili liweze kujadiliwa, lifahamike na wananchi nao wapate kufaidika kutokana na maelezo haya. Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Ole Millya halafu Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo kwenye mkataba ambao upo mbele yetu. Kwa sababu mengi yameshazungumzwa na wenzangu, nitazungumza machache sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza linapokuja suala la maslahi ya Taifa lazima tusimame kama Taifa. Japokuwa tuna Umoja wa *East Africa,* lakini kila nchi ina *levels* zake za maendeleo ambayo ime-*move*. Kwa hiyo, tunapoenda kuangalia suala la maslahi ya Tanzania tuasianze kusema kwa nini fulani kasaini, kwa nini Uganda kasaini, kwa nini Kenya kasaini? Yapo mambo ambayo yamemvutia yeye kusaini huo mkataba. Kwa hiyo, kwenye masuala ya maslahi ya Taifa tusimame kama Taifa kuangalia maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba mkataba ambao upo mbele yetu ukiusoma vizuri unaturudisha nyuma karibu miaka 50 tuliyotoka. Unakwenda kutupangia masharti wakati tumepigana angalau miaka 50 tunaanza kuweka sera za uchumi, sera za mapato na sera mbalimbali nzuri, inatuambia sasa kwamba tuache sera zote pembeni tufuate masharti ya *EU*, hatukubaliani na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunazo sera ambazo sahihi jinsi ya kukusanya mapato. Mkataba unachambua, zipo changamoto na hasara ambazo tutazipata kutokana na kuingia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, nasema ili muweze kuondokana na hasara hizo, lazima mkae mrekebishe sera za mapato ndani ya nchi zenu, hivi kweli tupo sawa sawa? Cha kusikitisha sana, pia wanatuambia ili muweze kufidia hasara zitakazotokana na kuruhusu biashara *free* kuingia nchi yetu bila ushuru muweze kukaa muongeze *VAT* kwenye bidhaa ndani ya nchi yenu ili muweze kufidia hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiongeza *VAT* kwenye bidhaa zetu, tunamuumiza nani? Tunawaumiza wananchi wetu, kwa sababu vyote wanaenda kulipa wananchi wetu. Kwa hiyo, tunalazimishwa sasa kwenda kuwabana zaidi Watanzania kwa sababu tu ya kukidhi matakwa ya Mkataba nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala kama hili kiukweli ni lazima tuwe makini, tuwe makini sana jamani. Juzi tulikuwa na bajeti mwezi wa sita, tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda; ni nchi gani duniani ambayo imeweza

ku-*move* kwenda kwenye *industrialization* bila kulinda viwanda vya ndani? Hakuna. Hata hao Ulaya ambao leo tunaona wame-*move,* walilinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza sisi mpaka hapa tulipo bado ni soko la bidhaa za wenzetu, ni soko la pamba-*stick*, ni soko la Wachina, ni soko la Wakenya, ni soko la wengine. Haitoshi tu tukafungue wazi, sisi tuwe kazi ni kuzalisha na kupeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunataka ku-*move* na mikataba kama hii na mikataba mingine naomba, kama Taifa lazima tuje tuwe na watu ambao tunapokuwa na mikataba kama hii waende ku-*negotiate; negotiators* wenye uwezo mkubwa. Kwa sababu mkataba kama huu haukutakiwa hata sisi kuja kuujadili; ulitakiwa uishie huko huko! Baada ya kuona kwamba hatuna maslahi nao, wanapiga pembeni, tunasonga mbele kwenda na mambo mengine ambayo yana maslahi kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima sisi Wabunge tuisimamie Serikali vizuri, tuje tuwe na watu wenye uwezo, *capacity thinking* nzuri ya kuweza kuwa *negotiators* kwenye mikataba kama hii hasa ya kitaifa ambayo tusipoiangalia vizuri, kipengele kimoja tu kinaweza kutu-*switch* tunajikuta kwamba tunaenda kuwa watumwa wa nchi nyingine badala ya ku-*move* kwenda mbele kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu Wabunge wengine wote kwamba mkataba kama huu hautufai na hata kama utatufaa, ni huko mbeleni. Pengine miaka 50 ijayo tuwe tume-*move* kidogo tumekuta wenzetu. Kama Wakenya, leo Kenya ni nchi ndogo, lakini kila nchi pia ina *factors* zake. Leo Tanzania tupo karibu milioni 50. Wakenya wenyewe ni wachache, lakini pia sera zinatofautiana. Kwa hiyo, lazima tuangalie *factors* nyingi nyingi kuhakikisha kwamba mikataba ya Kimataifa kama hii tunaipitisha. Kila mkataba unaopitishwa, tuangalie maslahi yetu, tusiangalie *East Africa* kwa sababu kila mmoja anapambana kwenye uwanja wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Millya, na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niweke msimamo kwamba na mimi pamoja na Kambi yetu Rasmi tunakubaliana kimsingi kwamba mkataba huu kwa muda huu usisainiwe na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hilo lisitunyime nafasi ya kuweza ku-*criticize* mkataba mzima *objectively*. Maprofesa watatu walikuja Jumamosi, ninawaheshimu sana. Mheshimiwa Profesa Kabudi, ni mwanasheria nguli, ni mwalimu wetu kwa namna yoyote, lakini walipowasilisha upande mmoja wa shilingi, kisomi haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *article 101* pale inaposomeka; "*resources mobilization*." Nataka tu niwaoneshe faida ya mkataba huu pamoja na madhaifu yake mengi, lakini kuna faida fulani.

Mheshimwa Spika, nenda kifungu cha pili; "*The objective of joint resource mobilisation is to complement, support and promote in the spirit of interdependence, the efforts of the East African Community Partner States in pursuing alternative sources of funding to support regional integration and the development strategies, in particular the EPA Development Matrix*." Hiyo *matrix* hatujaletewa.

Mheshimiwa Spika, Maprofesa wangetuonyesha Waheshimiwa Wabunge hiyo *development matrix* ni kitu gani? Tunapoungana na *EU* tunakuwa na nafasi kubwa ya ku-*negotiate for funding* kwa ajili ya miradi ya maendeleo; mkataba huu unasema hivyo. Mkataba huu kwa kiwango chochote una madhaifu makubwa lakini sisi kama nchi tusifikie mahali tukawa ni watu wa kukataa siku zote.

Mheshimiwa Spika, alipoanza Profesa siku ile, alisema kitu kimoja kwamba nchi ya Tanzania na Afrika ya Mashariki kwa ujumla, itapoteza *revenue*.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe kitu kimoja, mwaka 2004 tuliingia mkataba wetu na Kenya na Uganda; *East African Customs Union Protocol.* Tuliwaachia nchi ya Kenya kwa miaka mitano walipe kodi.

Mheshimiwa Spika, mkataba huo uliisha mwaka 2009. Mwaka 2009 Kenya ikaanza kuingiza bidhaa zake bila kulipa kodi Tanzania, baada ya Tanzania na Uganda kuruhusiwa kuingiza Kenya bidhaa zao wanazotengeneza kwa miaka mitano bila kodi yoyote.

Mheshimiwa Spika, tujiulize kama nchi, hivi baada ya ule mkataba mwaka 2009, viwanda vingapi Mheshimiwa Mwijage tumeanzisha kuanzia siku hiyo? Tumepeleka nini Kenya? Leo hii mnatutuhumu wengine, tumepeleka kabichi, nyanya na vitunguu lakini hatujaanzisha viwanda vya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, wengine mnasema tunautetea mkataba huu kwa sababu tuna maslahi binafsi na nchi za Ulaya, wala siamini hata kidogo. Mimi ni mzalendo na ninaamini ni mzalendo, lakini hivi mfano Tanzania, Waziri wa Fedha anajua, kati ya mataifa matano makubwa yanayochangia Tanzania bajeti yake, ni nchi zipi? Kama kati ya tano hizo, Ulaya zipo nchi tatu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wakati tunakataa mkataba huu, tujiulize maswali ya msingi, moja, hivi ni viwanda gani hivyo ambavyo tunavitetea kwamba tukiingia kwenye mkataba huu tunapoteza bidhaa?

Pili, kwa muda gani nchi yetu ya Tanzania itaweza kujenga viwanda vyake peke yake na kuweza kushindana na masoko haya mengine ya *East Africa* na Ulaya pia, itatuchukuwa muda gani kujenga viwanda kwa sababu viwanda vingi vipo mfukoni.

Tatu, kama hatutaanzisha viwanda kama nchi, hivi hamuoni kwamba Ulaya wakiingiza bidhaa zao kwenye uchumi kuna kitu kinachoitwa *basket of goods,* kwa sababu vitaingia kwa bei rahisi mwananchi wa kawaida atakuwa na uwezo wa kuvinunua kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunapata kutoka China tunavitoza kodi ambavyo ni vya hali ya chini kweli, lakini wote tunafahamu, leo ukiletewa bidhaa kutoka Ulaya na China, wote ambao mmesafiri humu duniani, mtakubaliana na mimi kwamba bidhaa ya China na Ulaya vinatofauti kubwa, *quality wise, I will go for European goods for sure!*

Mheshimiwa Spika, nne, naomba pia nishauri badala ya kukutaa mkataba huu, Bunge tumshauri Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais kwenye kikao cha mwisho cha Marais wa Nchi za Afrika Mashariki -*Summit* ya juzi Arusha au Kenya kikao kimoja cha mwisho, ndiye aliyewaomba wenzake kwamba jamani mkataba huu sisi hatujapitia, ninaomba niunde *Technical Committee* ambayo itapitia mkataba huu itushauri kama nchi.

Mheshimiwa Spika, *Technical Committee* ndiyo ile nafikiri ambao wamewasilisha upande mmoja wa shilingi nafikiri siyo vema sana tukawa ni nchi ya kususa na kukataa wakati hatuchukuii hatua madhubuti ya kuweza kubadilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nishauri kitu kimoja…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, hili naona nisilinyamazie, nimpe taarifa rafiki yangu. Taarifa ya timu ya watalaam wa Serikali inaongozwa na timu ya Wizara ya Viwanda na Biashara na *Foreign Affairs.* Hawa waliokuja hapa, timu ya watalaam wasomi wa Tanzania walialikwa na Bunge. Timu yangu ipo na imetengeneza taarifa zake na kimsingi mambo yote ninayoyasema ndiyo wananiwezesha. Kwa hiyo, usichanganye vitu viwili.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Millya tuendelee.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nipokee taarifa hiyo kwa nia njema kwamba anajaribu kuniambia kwamba ni kweli Mheshimiwa Rais alivyoomba kwamba iiundwe *Technical Committee* ya kuishauri Serikali imeundwa, lakini bado haijawasilisha mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, hilo halitunyimi fursa kama Bunge kuiomba Serikali, mkataba huu kwa sasa usitishwe lakini tusikatae moja kwa moja. Uende ukapitiwe tena tuangalie kama *negotiating team* ya Tanzania inaweza ikabadilisha baadhi ya mambo ambayo tunayataka na bidhaa ambazo tunataka kuzitetea kwa muda na baadaye urudishwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaomba Serikali yetu badala ya kupiga kelele ya kusema tunaandaa viwanda, sasa ifikirie ni muda sahihi wa kuwekeza kwenye viwanda. Hili jambo la kukimbia na kuwa na *protection policy* kila saa hautatufikisha mahali. Waingereza wanasema, *you better run the hard way* kwa sababu *the easy way you do not go it,* kwa sabubu ninyi hamuwezi hata kidogo. Tukiwaachia hata miaka 100 humuwezi kuanzisha viwanda vya kushindana na Ulaya. Ni changamoto kama nchi kwamba, ni lazima kwa muda huu tuamue wote kama jamii tuungane tuwaambie Mawaziri hawa wenye viwanda mifukoni, walete viwanda ili tusiwe wapiga kelele kwenye soko la Afrika Mashariki.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Arusha ukienda kwenye maduka yote vifaa vya Kenya vimejaa, ukiuliza tunapeleka nini Kenya? Utaambiwa maembe na machungwa ya Tanga na unga wa Azam.

Mheshimwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba mkataba huu usisainiwe, lakini kama nchi tuangalie faida ambazo tunaweza tukazipata kutokana na mkataba huu, badala ya kuanza kulialia na kupiga kelele kwamba

sisi hatuwezi, hatuwezi siku zote! Muda unatosha ni muda sasa wa kushindana na Mataifa mengine kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeingia kwenye *AGOA,* mmesikia jana Mheshimiwa Mwakyembe amesema tumeuza asilimia nne soko la Marekani, wakati Kenya wameuza 98% *they are taking advantage of their industrial power* na Tanzania tunabaki kulalamika ni nchi ya kulalamika tu Kiongozi analalamika, wananchi wanalalamika, kama alivyosema Mheshimiwa Lowassa wakati fulani.

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana! Mheshimiwa Cosato Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nami kupata nafasi hii ya kuchangia jambo hili.

Awali ya yote, pamoja na kuwa muda ni mchache nitumie pia fursa hii kuwapa pole wananchi wa Mafinga hasa pale Jambeki kutokana na lile janga la moto na pia janga la moto lililowakumba pale *stand* ya Mafinga, nawapa pole sana! Na ninawatia moyo kwamba Serikali itaendelea na jitihada za kututafutia gari la zimamoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, baadhi ya wachangiaji wamesema kwamba tunalalamika tu, tumekuwa watu wa ku-*complain*. Mwingine amesema tunagombana na *EU,* tunagombana Kenya, tunagombana na Uganda. Mimi niseme jambo moja kwanza, hatulalamiki, pili, hatugombani na yeyote isipokuwa tunalinda maslahi ya Taifa letu. Mwingine amesema kwamba tumechukua muda mrefu sana ku-*negotiate* jambo hili, ndiyo *negotiation* zilivyo za Kimataifa. Kuchukua muda mrefu wala siyo tatizo leo hii Uturuki bado inaendelea ku-*negotiate* na *EU* ili iweze kuingia. Pia kushiriki *negotiation* na kutosaini ni mambo ya kawaida katika masuala ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, Mkataba wa Roma huu ulioleta *ICC,* Marekani alishiriki lakini hakusaini, kwa hiyo, siyo dhambi kutosaini, wala sisi siyo watu kwanza. Pia hata katika *negotiation* kwanza kuna *stage* ya kwanza una-*negotiate,* pili, unarudi je, tume-*achieve* katika ile *negotiation*? Baada ya pale ndiyo unaamua usaini au usisaini. Sasa watalaam wame-*negotiate* wamekaa

chini wameona kwamba katika mkataba huu hatujakidhi matarajio ya yale ambao tunajarajia ku-*achieve,* wameshauri tusisaini. Haya ni mambo ya kawaida kabisa katika taaluma za mambo ya Kimataifa na mambo ya mikataba ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, pia kuna kitu kingine ambacho watu wengi wameshindwa kukitazama; kuna kitu kinaitwa *EBA,* kirefu cha *EBA* ni *Everything But Arms.* Sasa *Everything But Arms* ni nini? Kwa lugha nyepesi katika *EU-EBA* inasema kwamba *The EU will offer quarter and duty free market access to all products originating from the LDCs with the exceptional of arms, everything but arms.* Sisi ni *LDCs - Less Developed Country.* Maana yake ni kwamba *with EU-EBA* mpaka hapa tulipo tunaweza kuingiza chochote katika Soko la *EU,* isipokuwa silaha, lakini *free of duty. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu Kenya, wao tayari wameji-*pronounce* kwamba ni *middle income country,* chochote wanachofanya kule wanachoingiza kule katika Soko la *EU* lazima wachajiwe ushuru usiyo pungua asilimia 10, sisi *with EPA, without EPA* kwa yule *EU-EBA* tayari tunayo hiyo haki ya kuingiza chochote kule bila ushuru. Sasa ndiyo maana tujiulize kwa nini wenzetu wamesaini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Zitto amesema hapa kuhusu maua. Kenya wanauza maua yasiyopungua thamani ya dola 500,000 kwa mwaka, pia *export* ya Kenya katika *EU* pamoja na *UK* ambayo imejitoa kwa mwaka ni wastani wa *1.5 billion USD.* Sasa kwa kuwa wanalazimika kulipa ile asilimia 10 wanalipa siyo chini ya milioni 100 kwa mwaka kama ushuru wanapoingiza zile bidhaa. Lakini ni nani anayemiliki maua, ile *industry* ya maua katika nchi ya Kenya? Kenya tofauti na Tanzania hapa hata mimi Mtoto wa Mama Cosata leo hii ni Mbunge, *in* Kenya *that cannot be possible.* Mtoto wa malalahoi ukaja kuwa Mbuge kama tulivyokuwa sisi humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *industry* ya maua ya Kenya wanao-*dominate* ni ma-*giant* ambayo ni ma-*ruling class* na ndiyo maana haraka haraka wame-*ratify* huu Mkataba ili kusudi uwape hiyo *favour*. Kwa hiyo, haya mambo ndugu zangu tunapojadili kama alivyosema Ndugu yangu Khatib maslahi ya kitaifa tuyatazame mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili kwa nini tunakataa kusaini? Mimi nampongeza Mheshimiwa Rais na ninaipongeza Serikali kwa kuitika wito wa kuleta jambo hili hapa na sisi tuseme lolote. Kwa nini tunakataa? Madhara yake moja, tutapoteza ushuru,ambao mpaka sasa tunatoza hizo bidhaa wanazotuletea. Tukipoteza ushuru maana yake ni nini? Kupitia ushuru huo ndiyo

tunatarajia tujenge nchi yetu, tuhudumie watu wetu, tufanye elimu bure, tulipe mikopo ya wanafunzi, tujenge zahanati na kadhalika, sasa hicho tunakiondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, tukikubali jambo hili ita-*damage* jitihada zetu za kujenga uchumi wa viwanda. Kwa sababu tutakubali sasa tuwe tu ni soko.

Mwisho, tujiulize kwa nini wenzetu tunasema jambo hili lazima tusaini *as block* wao wamesaini, tumeshasema mfano huo wa maua Mheshimiwa Zitto amesema. Pia tuendelee kutafakari kwa kina tunapojadiliana na wenzetu ndani ya *East Africa,* unafiki huu mwisho wake nini na nini hatima ya *East Africa Community* na kwa mwenendo na *trend* ya unafiki wa namna hii?

Kuna watu wamekuwa na mashaka kwamba kwa kutusaini ita-*damage* mambo mengi, mojawapo wanasema *Foreign Direct Investment (FDI)* kwamba tutakosa kupata kuvutia mitaji kutoka *EU,* siyo kweli. Mheshimiwa Hawa Ghasia ametoa takwimu hapa katika *FDI* nchi ambazo zinaongoza mpaka sasa hivi kuwekeza mitaji yao hapa kwetu ni China, India, Kenya ikifuatia na nyinginezo. Katika nchi 10 ni mbili tu ndizo zinatoka *EU,* huu mkataba ukisaini maana yake ni kwamba una-*discourage FDI* kutoka kwingine. Je, tuna uhakika gani hawa watu tukisaini nao kweli wataendelea kutuletea mitaji, ambapo hadi sasa hivi ni nchi mbili tu kati ya 10 ambazo zinaleta hapa hiyo *FDI? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine watu wengine wana mashaka kwamba ita-*damage* mahusiano yetu ya kidiplomasia, siyo kweli. Hii siyo dhambi kutosaini. Leo hii Norway haiko katika *EU* kwa sababu inalinda maslahi yake. Uturuki inataka kuingia kwa sababu inadhani itanufaika zaidi, Norway haitaki kuingia kwa sababu inalinda maslahi yake, hata Sweden imeingia mwaka 1995 pia kwenye ile *Euro Zone* kwa maana ya *currency* hawapo kwa sababu wanalinda maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini *way forward,* katika biashara yoyote kitu muhimu ni soko na ndiyo maana tumeleta Jumuiya ya Afrika Masharika, ndiyo maana tuna *SADC*, lakini pia ndiyo maana tunafikiria kuangalia namna gani tutaunganisha *COMESA, SADC* na Afrika Mashariki ili tuwe na soko kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia hata katika Afrika tunajadili sasa hivi kuwa na *continental free trade area* ili tupanue soko. Kwa hiyo, ushauri wangu wakati tunajadili haya naipongeza Serikali, lakini naendelea pia kushauri wakati tunakataa kusaini Mkataba huu na tuendelee kuboresha mazingira yetu ya

kuwezesha kuvutia mitaji ili dhana ya kujenga uchumi wa viwanda iweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninashauri, tupende kujihabarisha Waheshimiwa Wabunge. Mkasome ile *article* ya Mzee Mkapa, ina *some details* kwa lugha nyepesi sana. Tutaweza kujifunza na kuona, lakini na kuwaelimisha watu wetu huko nje, kwa nini tumekataa kusaini, madhara yake ni nini?*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuipongeza Serikali kwa kutosaini. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Mkataba huu wa ubia baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niwapongeze waliotangulia kuupinga huu mkataba kwa nguvu kubwa na maneno mazuri yalio-*base* kwenye *content* nikianzia na mchangiaji wa mwisho Cosato Chumi aliyechangia kabla ya mimi, michango ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Azzan Zungu, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Hussein Bashe na wengine wote, wameenda vizuri sana kwenye *content,* na Mheshimiwa Hamidu Bobali na chama chake na Mheshimiwa Khatib Said Haji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakwenda kwenye *content* nitagusa mambo ya jumla ambayo ninadhani jumba lako hili Tukufu ni vema likajua ili tuweze kwenda katika mtiririko mzuri. Kuna watu wamesema hapa, nakubaliana Tanzania siyo kisiwa na wengine wamesema tusiikimbie hii ndoa, hii ndoa ni muhimu ni nzuri ina mazuri yake ni vema tukayatafuta mazuri yaliyoko sirini yasiyoonekana ili tuone kuna nia njema ndani ya hili. Naomba niseme machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote inapoamua kufanya urafiki na Taifa lingine lolote, kuna mambo inapoteza kama Taifa na kuna mambo inayapata kama Taifa, kwa maneno mepesi, mahusiano yoyote baina ya mataifa yanaunganishwa na *principle* ya *statism, principle* ya *self-help* na *principle* ya *survival.* Katika mazingira yoyote yale unapoingia kwenye makubaliano na Taifa lolote lile, kanuni ya kwanza inayopaswa kuku-*guide,* una *interest* gani kama Taifa kwenye ule mkataba.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, unalopaswa kuliangalia, utanufaika kwa kiwango gani katika ule mkataba? Lakini kuna mazingira mengine, unaweza usinufaike, ila ule mkataba ukakusaidia kuishi uione kesho yako, labda kuwakimbia maadui hiyo ndiyo inayoitwa *national survival.*

Mheshimiwa Spika, yawezekana kuna wengine wanayatafuta mazuri kwenye Mkataba huu kwa sababu tu ya ule woga katika makubaliano kuna mchawi asiyeonekana, yaani wanatafuta ku-*survive* sehemu ambayo hakuna *survival.* Niwaombe ndugu zangu Wabunge, historia ya nchi yetu tumeshirikiana na mataifa mengi katika nyakati tofauti. Kuanzia karne ya tano tuliposhirikiana na nchi za Mashariki ya Mbali na nchi za Uarabuni mpaka kipindi nchi za Ulaya zilipoingia, kipindi cha ukoloni na mahusiano baada ya uhuru. Wote mmeona kila Tanzania tulipojikwamua kutoka kwenye makucha ya kutaka kuendelea kumekuwa na uhusiano wa mjomba wa kuturudisha nyuma.

Mheshimiwa Spika, tumetoka kuanzia mwaka 1961 mpaka leo tunaongea mwaka 2016, kuna mikakati mingi sana tumeipanga kama Taifa, kuna mikakati mingi sana tumeipanga kama nchi na majirani zetu, kuna mikakati imefanikiwa na mikakati haikufanikiwa. Ni jukumu letu sasa kujiuliza kama Taifa, haya mahusiano tuliyowahi kuyafanya nyuma yalitusaidia kwa kiasi gani? Na haya mahusiano tunayotaka kuyafanya sasa yana tija kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbusheni ndugu zangu Wabunge, tulishawahi kugawanywa katika *block* mbili, *block* ya *East* na *block* la *West.* Mnakumbuka kipindi cha *cold war.* Nchi yetu kama Taifa ilisimama ikasema hatutageuka kulia wala kushoto tutakwenda katika mfumo ambao tunaona nchi yetu ina maslahi nayo, hatukugombana na Wamarekani na Waingereza na wala hatukugombana na marafiki zetu wa Urusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunavyokwenda kuujadili mkataba huu, ni mkataba wa kwanza ndani ya nchi yetu kuwekwa fungu moja *as a bargaining block against European Union.* Haikuwa kutokea huko nyuma na wala hatukuwahi na *experience* ya kundi zima tukawa na *interest* sawa, tukawa na *historical background* sawa, tukawa na matamanio sawa, tukawa na ndoto sawa, leo tukae kwenye meza ya majadiliano *against a huge block - European Union. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaona kuna tatizo, kuna matatizo mawili; tatizo la kwanza si mahusiano yetu na Jumuiya ya Ulaya na wala siyo mahusiano yetu na majirani zetu wanaotuzunguka, tuna tatizo la kwanza la *content,* mambo yaliyopo ndani ya mkataba ambayo tunayapinga. Kwa bahati mbaya sana kwa hatua tuliyofikia, hatuna fursa ya kuchambua kifungu kimoja baada ya

kingine, tuna fursa moja tu sasa hivi ya kuukataa, kwa sababu ya kukubali hatunayo. Baada ya kukataa hayo mazuri msiyoyaona hapa mnayodhani yapo, ndiyo yatakuja.

Mheshimiwa Spika, leo hii hapa tujadili nini, tu-*suspend,* uende halafu urudi, hapana. Hatuna fursa hiyo, tuna fursa leo ya kusema Serikali isaini mkataba au Serikali isisaini mkataba. Kutokana na hoja zote zilizotolewa ndani humu na Wabunge, nakubaliana na ninaiomba Serikali isisaini mkataba huu. Kwanza, haujatupa *room* ya kufanya marekebisho, kama kutaonekana huko mbele kuna haja ya kurekebisha vifungu tutakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna marafiki zetu wametangulia, ndugu zetu Walatini wana msemo *amicorum omnia communia* wakimaanisha *between friends all is common* au wakimaanisha *for friends all things are shared.* Sasa kwa *style* ya wenzetu wanavyokwenda tunaona ile *principle* ya *amicorum omnia communia* haipo, hatuoni kitu hapa kinachoenda *in common.* Walishakaa Wakuu wetu wa nchi wakasema tujipe muda wa miezi mitatu, wenzetu wamekwenda *speed*.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema machache yafuatayo; umefika wakati sasa kwa Watanzania kutoka kwenye giza nene la urafiki wa kinafiki wenye lengo la kudidimiza na kuua ndoto ya Tanzania kuwa na viwanda. Umefika wakati sasa kwa Tanzania kutoridhishwa na aina hii ya urafiki mpaka pale mishipa yetu ya fahamu itakapojiridhisha kwamba urafiki huu haufanani na ule urafiki wa paka na panya kukumbatiana na kubusiana ilhali shimo la panya la kutorokea liko mbali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika kwa Watanzania kutokuwa na kiu ya kutaka kunywa maji ambayo yako kwenye kikombe cha mateso, uchungu na maumivu makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya, siungi mkono hoja na ninaiomba Serikali isipitishe na isisaini mkataba huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sixtus Mapunda, mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Kitandula.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, sijajua kama ni Mheshimiwa Kakunda au Mheshimiwa Kitandula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye mada ya leo. Nilipokuwa ninausoma mkataba hisia zikanipeleka kwenye historia. Miaka takribani mia moja iliyopita na zaidi walikuja wazungu na mikataba, lakini kabla ya kuja wazungu na mikataba wazungu walisitisha biashara ya utumwa na katika tangazo la kusitisha biashara ya utumwa ukisoma *verses* zilizokuwemo mle ni pamoja na kusema kwamba hii nguvu kazi ambayo tulikuwa tunaichukua tunaisafirisha ibaki kulekule ili izalishe kwa ajili ya viwanda vyetu. Baada ya hapo walifungua mashamba makubwa, mashamba yale yalikuwa ni kwa ajili ya kuzalisha malighafi zilizokuwa zinahitajika kwenye viwanda na wakati ule ndiyo ilikuwa mapinduzi ya viwanda yanafanyika Ulaya. Kwa hiyo, dalili zote za mfanano wa mikataba ya wakati ule imo kwenye huu mkataba, kwa hiyo mkataba huu una harufu ya ukoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi na wenzangu na mimi nirejee kwamba hakuna mkataba mbovu ambao nimewahi kuushuhudia kama huu kuanzia mwanzo tu. Pale kwenye kurasa za mwanzo kabisa ukisoma jinsi nchi zetu zilivyoorodheshwa, zimeorodheshwa kama *block* moja kwa moja, lakini walivyokuja kuorodhesha nchi zao wakaorodhesha moja moja halafu baadaye wakasema *and the EU,* hii aliisema mwanzoni kabisa Mheshimiwa Lugola. Mimi kuanzia hapo tu nilipata wasiwasi na nikapata wasiwasi zaidi hata wataalam wetu ambao walikuwa wanakwenda ku-*negotiate* tangu miaka ile ya 2007 mpaka juzi, nilipata wasiwasi kama kweli walikuwa wanajiandaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwango vilivyomo humu vya *terms* kwa asilimia zaidi ya 80 ni vya ukandamizaji, kutukandamiza sisi na mengine yamo humu yanalazimisha kwamba tukisaini mkataba huu ndiyo tutapata hata masuala ya *development cooperation.* Sasa suala hili limenisumbua sana kama ambavyo limewasumbua Wabunge wengine, ninaomba niunge mkono wale wote ambao wametoa wito, Serikali isikubali kusaini mkataba huu mpaka pale marekebisho makubwa yatakapokuwa yamefanyika ikiwemo kuruhusu nchi mojamoja kujitoa wakati wowote inapoona kuna hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningezungumza mengi lakini mengi yameshazungumzwa itakuwa ni kurudia, ninaomba niishie hapo, wote tuunge mkono kukataa kukataa mkataba huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Kitandula kwa kifupi tafadhali.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nimshukuru Mungu sana kwa siku ya leo kufika, kwa sababu ni siku ambayo niliitarajia na niliitegemea sana. Nasema haya kwa sababu nimepata bahati ya kushiriki makongamano ya kitaalam ya jambo hili, mwaka 2013 kule Rwanda na mwaka 2014 kule Brussels, Ubelgiji.

Mheshimiwa Spika, kiufupi mkataba huu ni hovyo! kiufupi wenzetu hawana nia njema kupitia mkataba huu. Mkataba huu umejadiliwa kwa miaka 12, miaka 12 nchi zetu zimekuwa kwenye majadiliano ya mkataba huu *and yet* tuna mkataba mbovu kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni mkataba ambao nchi yetu imeamua kuchukua njia ya kidiplomasia kusema kwamba inajitoa kwa sababu Uingereza inajitoa kwenye *European Union,* kauli ya kidiplomasia, lakini nchi ya Tanzania tumeheshimika duniani kwa kusimamia tunachoamini, tusijifiche kwenye diplomasia hii, tuwaambie ukweli hawa wenzetu ambao hawana nia njema na sisi. Tuwaambie ukweli kwamba tunathamini Utanzania wetu, tuwaambie ukweli kwamba tunajiheshimu na hatuko tayari kupuuzwa kupitia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamesemwa, *loss of revenue,* kulinda viwanda vya kati na vidogo, yamesemwa kuhusu *rendezvous clause,* mimi nataka niya-*sum up* kwa mambo haya machache nitakayouliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikisoma mkataba huu najaribu kujiuliza hivi mkataba huu unakusudia kutuongezea uzalishaji katika nchi zetu? Jibu ni hapana. Hivi mkataba huu unatuhakikishia usalama wa chakula? Jibu ni hapana. Hivi mkataba huu unatuongezea fursa za ajira zenye staha katika nchi zetu? Jibu ni hapana. Hivi mkataba huu unatuwezesha kutoka katika uchumi wa kutegemea *natural resources exportation* na kwenda kwenye *production of sophisticated products*? Jibu ni hapana. Lakini kilichowazi ni mkataba wa kutweza utu wetu, tufike mahali tuwaambie mchana kweupe macho makavu, kwamba hatutakubali kudhalilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuupinge mkataba huu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani baada ya mjadala huu tumefika mahali ambapo sasa tufanye uamuzi wa kuishauri Serikali ipasavyo kwa taratibu zetu za Kibunge. Majina ya waliotaka kuchangia mjadala huu ni mengi na wengi wenu hamkupata nafasi, lakini basi waliopata nafasi wamewawakilisha, kwa muda uliopo tusingeweza kuongea wote.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo kilicho mbele yetu ni kama nilivyoeleza mwanzoni kwamba sasa nimefika mahali pa kuwahoji na hojaji yangu itakuwa kama ifuatavyo:-

Nitawauliza Wabunge wanaoafiki kwamba Serikali isaini mkataba huu waseme ndiyo, mtajibu, na wale wanaotaka Serikali isisaini mkataba huu, waseme hapana.

Wanaoafiki Serikali isaini Mkataba huu waseme ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Wanaoafiki Serikali isisaini Mkataba huu waseme hapana.

**WABUNGE FULANI:** Hapana.

**SPIKA:** Nadhani Wabunge waliosema hapana Serikali isisaini Mkataba wameshinda. *(Makofi)*

*(Bunge Lilikataa Serikali Isisaini Mkataba wa Ubia wa Uchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya ( EAC -EU EPA)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyosema Waheshimiwa Wabunge jambo hili ni la maslahi ya Taifa, ni jambo letu sote kabisa na kipekee nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuitikia wito ambao niliutoa wakati tunapoahirisha Mkutano wa Nne uliopita wa Bunge kuomba kwamba jambo hili Wabunge wapate nafasi ya kulifahamu na nafasi ya kuishauri Serikali kabla haijafika mahali pa kufanya maamuzi ya mwisho kabisa. Kwa hiyo, tuliomba tupate nafasi ya kutoa ushauri nafasi hiyo tumeipata na tumeitumia vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru wote kwa michango yenu mliotoa na matazamio mliyoyatoa na ushauri wenu kwa Serikali. Kwa kweli inahitaji uwe na utaahira fulani kusaini mkataba huu kwa jinsi ulivyo hivi sasa, labda kama una mabadiliko, lakini kwa jinsi ulivyo hapana, haiwezekani.Kama walimfanyia hivyo Chifu Mangungu mbona miaka mingi imepita sasa. Hawawezi kutufanyia hivyo tena kwa mara nyingine. Kuhusu majirani zetu, tuwazoee tu, ukishakuwa na jirani yako hakupi homa, unakuwa unamjua kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaambia tangu mwanzo kwamba mambo ni mengi, nitaomba tutumie vizuri muda uliobaki huu wa nusu saa kwa kushughulikia lile jambo lingine kwenye *Order Paper.* Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MUSWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Ammendments (No. 3) Bill, 2016)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Moja kwa moja nimuite Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Ammendments (No. 3) Act of 2016)* sasa usomwe kwa mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitishe muswada huu kuwa sehemu ya sheria ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha maudhui kuhusu muswada huu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutimiza mwaka mmoja katika Utumishi wa umma kwa nafasi hiyo kama Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu katika muda huo ameweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ipasavyo, namtakia kila la kheri katika utumishi wake kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza kwa ufanisi ipasavyo Bunge letu. Nalipongeza Bunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa Kikatiba wa kutunga sheria, lakini pia kwa kuishauri na kuisimamia Serikali inapotekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Kwa ujumla, nawashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na muswada uliopo mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa namna ya kipekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, kwa ushirikiano waliotupatia wakati wa kuwasilisha maelezo kuhusu muswada huu mbele ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba na Sheria imefanya kazi nzuri ya kupitia muswada huu, kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau walioitwa kwenye Kamati hiyo na kisha kutupatia mapendekezo kwa nia ya kuuboresha muswada huu. Maoni na ushauri wa Kamati hiyo vimetusaidia kuuboresha muswada huu kama inavyoonekana katika majedwali ya marekebisho ambayo tumeandaa na kuyawasilisha katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Ndugu Gerson J. Mdemu, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, tunawashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaotupatia kwa njia mbalimbali ikiwemo ushauri, maombi, taarifa muhimu na kadhalika katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2016 unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tisa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha utekelezaji madhubuti wa sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa kutumia masharti ya sheria hizo na pia kuoanisha masharti ya sheria zinazorekebishwa na masharti yaliyopo katika sheria nyingine zilizopo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya masuala yaliyozingatiwa katika muswada huu ni kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadhi ya vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya, kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kupitia muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 *(The Civil Aviation Act, Cap 80);*

(ii) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191*(The Environmental Management Act, Cap 191);*

(iii) Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 *(The Higher Education Students' Loans' Board Act, Cap 178);*

(iv) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 *(The Public Service Act, Cap 298);*

(v) Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105 *(The Public Service Negotiating Machinery Act, Cap 105);*

(vi) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413 *(The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, Cap 413);*

(vii) Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317 *(The Transport Licencing Act, Cap 317);*

(viii) Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 *(The Treasury Registrar Powers and Functions Act, Cap 370);* na

(ix) Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 *(The Weights and Measures Act, Cap 340)*.

Mheshimiwa Spika, muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu kumi. Sehemu ya kwanza ya muswada inaainisha masharti ya utangulizi ikiwa ni pamoja na jina la sheria inayopendekezwa na tamko la marekebisho ya sheria mbalimbali zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho kupitia muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 *(The Civil Aviation Act, Cap 80)*. Marekebisho yanayopendekezwa kupitia Ibara ya 4 ya Muswada ni kuongeza kifungu kipya cha 10A kinachoweka masharti kuhusu mamlaka ya kuzuia na kukagua ndege *(the power to detain and search aircraft)* ili kumuwezesha Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga kuwa na Mamlaka ya kuingia, kukagua na kuzuia ndege yoyote pale anapoona kuna sababu za msingi za kuamini kwamba ndege hiyo inatumika kwa kukiuka masharti ya sheria hiyo au ina kitu chochote kinachoweza kutumika kama ushahidi kwa kosa lolote chini ya sheria. Marekebisho haya yanalenga kuwezesha hatua stahiki kuchukuliwa dhidi ya makosa yanayofanyika chini ya sheria hiyo mapema na kuhakikisha usalama katika usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ya muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 11A kinachoweka masharti kuhusu kuhamisha wajibu kwa

nchi nyingine yaani *transfer of responsibility*. Kifungu hicho kipya kinaelekeza kuwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga inaweza kuingia makubaliano chini ya Mkataba wa Usafiri wa Anga wa Chicago yaani *Chicago Convention on International Civil Aviation* na kuiruhusu mamlaka ya nchi nyingine kutekeleza majukumu au baadhi ya majukumu yake kwa ndege iliyosajiliwa hapa Tanzania na inafanya kazi nje ya nchi, au kuiwezesha Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania kutekeleza majukumu ya mamlaka ya nchi nyingine kwa ndege iliyosajiliwa katika nchi hiyo na inafanya kazi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia Ibara ya 5 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 11B kinachoweka masharti kuhusu ndege iliyozuiliwa *aircraft in distress* na kuainisha hatua zitakazochukuliwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga katika hali hiyo ikiwemo kuruhusu mamlaka husika ya anga ambako ndege hiyo imesajiliwa kutoa msaada unaotakiwa, kuratibu hatua za kuchukua pale ndege inapokuwa imepotea au haijulikani ilipo na msaada mwingine utakaohitajika. Kwa sababu hiyo, marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara hii kupitia vifungu vipya vinavyopendekezwa yamekusudiwa kuimarisha ushirikiano katika usimamizi wa masuala ya usafiri wa anga kwa mujibu wa Mkataba wa Usafiri Anga wa Chicago.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa katika sheria hiyo ni kuongeza kifungu kipya cha 19A kinachoweka masharti kuhusu kufuta au kusitisha kwa muda vyeti yaani *revocation and suspension of certificates* ikiwemo leseni, cheti au kibali kilichotolewa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga pale inapoonekana kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria ya Usafiri wa Anga. Hatua hizi zitawafanya watu na makampuni husika kutekeleza ipasavyo masharti ya sheria hiyo na hivyo kuimarisha usalama na sekta ya usafiri wa anga kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha usalama katika usafiri wa anga, muswada unapendekeza Kifungu kipya cha 19B kinachoweka masharti kuhusu ukaguzi utakaofanywa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga. Ukaguzi huo utahusiana ndege zilizopo Tanzania bila kujali nchi zilikosajiliwa, ndege zilizosajiliwa hapa Tanzania mahali popote zilipo, vifaa vya ndege and *flight compartment*, karakana za ndege *(aerodrome),* ajali za ndege na maeneo ya mtu mwenye leseni au kibali cha ndege, au nyaraka zilizotolewa na mamlaka hiyo.

Marekebisho ya mwisho yanayopendekezwa katika sehemu hiyo ni kurekebisha kifungu cha 26 cha Sheria ya Usafiri wa Anga kwa kuongeza kifungu kidogo cha (7) kinachoitaka Mamlaka ya Usafiri wa Anga kuhakikisha kwamba wakati inapotoa huduma ya usafiri wa anga hakuna muingiliano wa majukumu yake kama mdhibiti na yale ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yaani *The Environmmental Management Act*, Sura ya 191. Kifungu cha 16 cha sheria hiyo kinaanzisha Baraza la Usimamizi wa Mazingira yaani *the Environment Management Council* na kuainisha pamoja na mengineyo kuwa Baraza hilo linaweza kushtaki au kushtakiwa mahakamani.

Kwa kuwa, Baraza hilo ni Taasisi ya Serikali na kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali na taasisi zake kwa masuala yote ya sheria na anayo haki ya Kikatiba kuhudhuria na kusikilizwa katika mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 9 ya muswada inapendekeza kifungu hicho cha 16 kirekebishwe ili kuongeza masharti yatakayompatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali haki ya kuingilia kati shauri lililofunguliwa au kufunguliwa dhidi ya Baraza kwa kuliwakilisha Baraza hilo mahakamani katika shauri husika pale inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Aidha, Baraza limepewa wajibu wa kumfahamisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali pale linaposhtakiwa au kuishtaki mahakamani. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali katika Baraza hilo kuhusiana na mashauri yanayolihusu Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 42 cha Sheria hiyo kinaitaka kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandaa mpango wa utekelezaji wa mazingira katika eneo lake la kijiografia kwa kuzingatia Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kifungu hicho hakijaweka masharti kuhusu mahali pa kuwasilisha Mpango ya utekelezaji wa mazingira inayoandaliwa na Serikali za Mitaa. Hivyo Ibara ya 10 ya muswada inapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha 42(3) kinachoelekeza kuwa mipango itakayoandaliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa iwasilishwe kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira kwa hatua zake muhimu.

Marekebisho haya yanalenga kumwezesha Waziri kuratibu namna Serikali za mitaa zinavyotekeleza Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mazingira na kuchukua hatua muhimu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanahusu kifungu cha 57 cha sheria hiyo. Kifungu hicho kinaweka masharti kuhusu zuio kwa shughuli za kibinadamu zinazoathiri uhifadhi na ulinzi wa bahari, mito, mabwawa zisifanyike ndani ya mita 60 kutoka kingo za bahari, mito au mabwawa. Hatua hiyo

imekusudiwa kuimarisha ulinzi na usalama wa mazingira ya maeneo husika ya bahari, maziwa, mito na mabwawa.

Ibara ya 11 ya Muswada inapendekeza kifungu hicho kirekebishwe katika kifungu kidogo cha (2) ili kuwekwa mwongozo wa namna ya kupima umbali wa mita 60 kutoka kwenye kingo ya bahari, ziwa, mto au bwawa la maji ambapo shughuli zote za kibinadamu zimezuiliwa kufanyika. Kifungu hicho kitasomeka kama ifuatavyo; *For purpose of sub-section (1) the computation of sixty metres shall be reckoned-*

*(a) in the case of ocean or natural lake, from the highest water mark; and*
*(b) in the case of rivers, water dams or reservoirs, from the banks.*

Mheshimiwa Spika, tumezingatia maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) ili kutoa tafsiri ya meneno *highest water mark* kwa lengo kuwezesha wananchi kuelewa mahali ambapo umbali huo wa mita 60 unapoanza kuhesabiwa kutoka kwenye bahari au ziwa. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho hayo *the highest water mark* yatamaanisha *the level reached by sea or lake at high tide*.

Marekebisho haya yanalenga kuepusha mgogoro unaoweza kujitokeza kuhusiana na namna ya kupima umbali huo wakati wa usimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Kwa upande wa mito na mabwawa ya maji, Muswada unapendekeza kwamba mita sitini zitaanza kuhesabika kutoka kwenye kingo za mto au bwawa la maji husika. Aidha, utekelezaji wa masuala mengine ya hifadhi ya maliasili maji yaani *water resources* unasimamiwa na sheria nyingine ikiwemo, Sheria ya Usimamizi wa Maliasili Maji, 2009 yaani *The Water Resources Management Act, 2009* na Sheria ya Umwagiliaji Maji ya Taifa ya mwaka 2009 *(The National Irrigation Act, 2013)* hii ni ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inapendekeza pia marekebisho kwenye kifungu cha 184 kinachoweka masharti kuhusu makosa yanayohusiana na tathmini ya athari za mazingira. Ibara ya 12 ya Muswada inapendekeza kuwa kitendo cha mtu yeyote kushindwa au kukataa kufanya tathmini ya athari za mazingira *(environment impact assessment)* kwa mradi unaohitaji tathmini hiyo kufanyika iwe ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi bilioni moja au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka saba au vyote. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa adhabu ya faini isipungue shilingi laki tano na isizidi shilingi milioni kumi au vyote.

Mheshimiwa Spika, hivyo madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza adhabu hiyo ya faini kwa kuwa imepitwa na wakati jambo linaloweza kusababisha mtu au kampuni kukiuka masharti husika kwa kuwa tu ana uwezo wa kulipa faini hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumeondoa mapendekezo kuhusu kifungu cha 184(2) cha sheria hiyo kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho baada ya kuzingatia maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 187(1) cha sheria hiyo kinaweka masharti kuhusu kosa la kuchafua mazingira na kuainisha kuwa adhabu ya kosa hilo ni faini isiyopungua shilingi milioni tatu na isiyozidi milioni hamsini au kifungo gerezani kisichozidi miezi 12 au vyote. Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongeza kiwango cha adhabu ya faini isipungue shilingi milioni tano na isizidi shilingi bilioni kumi. Lengo la marekebisho haya ni kuzuia uwezekano wa mtu kuchafua mazingira kwa makusudi kwa kuwa tu ana uwezo wa kulipia adhabu hiyo ambayo kwa sasa inaonekana kuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 191 cha sheria kinaweka masharti kuhusu adhabu ya jumla kwa makosa yanayotendeka chini ya sheria hii na kuelekeza pamoja na mengineyo, kuwa adhabu ya juu ya faini isizidi shilingi milioni 50. Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza kuwa adhabu ya juu ya faini katika kifungu hicho isizidi shilingi bilioni moja ili kuiwezesha mahakama kutoa adhabu kulingana na kosa husika na kwa kuzingatia athari ya mazingira kwa kosa husika hasa yale yenye madhara ya moja kwa moja kwenye mazingira na kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Nne la Sheria hiyo ambalo linahusu Muundo na Uendeshaji wa Vikao vya Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Taifa wa Mazingira. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, mapendekezo ya kuongeza Wajumbe wa Bodi hiyo isizidi 11 yameondolewa ili idadi ya Wajumbe wa Bodi hiyo isizidi tisa kama ilivyo katika sheria ya sasa. Hii inatokana na mwongozo uliopo sasa Serikalini kuhusu kupunguza matumizi na gharama kubwa za uendeshaji wa shughuli za Bodi kwamba Wajumbe wa Bodi wasipungue saba lakini wasizidi tisa.

Aidha, muswada unapendekeza kupitia Jedwali la Marekebisho kuweka masharti yatakayoiwezesha bodi kualika mtu mwingine yeyote kushiriki katika vikao vya bodi iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo na kwamba mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 *(The Higher Education Students' Loan Board Act, Cap. 178)*. Ibara ya 17 ya muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 5 cha sheria hiyo kinachoweka masharti ya kuhusu Wajumbe wa Bodi. Kwa sasa bodi hiyo inaundwa na Wajumbe kumi na tano, muswada unapendekeza Wajumbe wa Bodi wapunguzwe ili kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za bodi lakini bila kuathiri utendaji wa bodi. Ibara hiyo ya 17 ya muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kuwa Bodi ya Mikopo iundwe na Mwenyekiti pamoja na Wajumbe nane kutoka Wizara yenye dhamana na Elimu ya Juu, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara yenye dhamana ya Fedha katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mwakilishi wa Muunganiko wa Vyama vya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na mwakilishi kutoka Vyuo Vikuu.

Aidha, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Wajumbe wengine walioongezwa baada ya kuzingatia maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria ni mwakilishi wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE)* na mwakilishi wa Wizara yenye dhamana ya Elimu ya Juu katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Pia kama inavyoonekana kwenyeJedwali la Marekebisho uwakilishi huu sasa utazingatia jinsia, yaani Waziri anapofanya uteuzi wa hawa Wajumbe anapaswa azingatie wawakilishi wa jinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 cha sheria hiyo kinaweka masharti kuhusu wajibu wa mnufaika wa mkopo *(liability and obligation of loan beneficiary)*. Muswada unapendekeza katika Ibara ya 18 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia majedwali mawili ya marekebisho baada ya kuzingatia maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria, kifungu hicho kimerekebishwa ili kuweka masharti kuhusu muda ambao mkopo unastahili kuanza kudaiwa. Inapendekezwa kuwa mkopo utastahili kuanza kulipwa au kurejeshwa mara baada ya mnufaika kumaliza au kusitisha masomo kwa sababu yoyote ile. Isipokuwa ataanza kulipa na kuwa *obliged* ukiona ile baada ya mwaka mmoja kupita.

Lengo la mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa mnufaika wa mkopo ambaye ana uwezo wa kulipa au kurejesha mkopo kuanza kulipa mkopo huo anapomaliza au kusitisha masomo. Kwa hiyo, chini ya muswada huu umewekwa fursa ya mwaka mmoja huyu mnufaika wa mkopo aanze kulipa. Pia imetoa fursa kwamba kwa yule anayeweza anaweza kuanza kulipa mara tu baada ya kuwa amesitisha masomo au kumaliza masomo.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kuwa wapewe muda usiozidi kulipia au kurejesha mkopo kwamba, Waziri atatunga Kanuni kwa ajili hiyo. Kwa sababu hiyo, mapendekezo yaliyokuwa kwenye muswada kwamba mnufaika wa mkopo aanze kulipa au kurejesha mkopo mara tu baada ya kumaliza au kusitisha masomo husika kwa sababu yoyote ile pasipokuwepo fursa ya muda mwingine wa kuanza kulipa au kurejesha mkopo huo yameondolewa na Serikali kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 ya muswada inapendekeza masharti yatakayomtaka mnufaika wa mkopo kutoa taarifa kwa Bodi ya Mikopo pindi anapopata ajira au kujiajiri ili kuwezesha mwajiri au mnufaika wa mkopo aliyejiajiri kuweka utaratibu wa kulipa mkopo huo kila mwezi na kuhakikisha kuwa malipo ya kila mwezi yanafanyika.

Aidha, muswada unapendekeza kuwa kiwango cha mkopo kinachopaswa kurejeshwa na mnufaika aliyejiajiri iwe kiasi kisichopungua shilingi 120,000 au asilimia kumi ya kipato chake kinachotozwa kodi *(taxable income)*. Tumefanya marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho sasa itakuwa ni shilingi 100,000. Pia kama inavyoonekana katika kifungu cha 19(7) kinachopendekezwa, masharti hayo kuhusu wajibu wa mnufaika wa mkopo yatatumika pia kwa mnufaika wa mkopo ambaye ameajiriwa na Serikali ya nje, Shirika la Kimataifa au kampuni yoyote. Masharti haya yako kwenye sheria ya sasa na yamelenga kuboresha makusanyo ya mikopo ya wanafunzi ili kuiwezesha Bodi kuwakopesha wanafunzi wengine na mtayaona haya Waheshimiwa kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 20 pamoja na kifungu cha 21 cha sheria hiyo. Kifungu cha 20 kinamtaka kila mwajiri kuifahamisha bodi kuhusu mwajiriwa ambaye ni mnufaika wa mkopo. Kwa kuwa siyo rahisi mwajiri kufahamu kama mtumishi anayeajiriwa ni mnufaika wa mkopo, muswada unaainisha kuwa mwajiri atatakiwa kuifahamisha Bodi ndani ya siku 28 baada ya kumwajiri mtumishi mwenye shahada au stashahada ili Bodi iangalie kama mwajiriwa huyo ni mnufaika wa mikopo. Kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, mwajiri ambaye atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu hicho atakuwa ametenda kosa la jinai ambalo adhabu yake sasa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho la pili adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni moja na isipokuwa hii adhabu sasa haina kifungo gerezani, ile imewekwa tu adhabu isiyopungua faini ya shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Spika, pia inapendekezwa kuwa baada ya Bodi ya Mikopo kuthibitishwa kuwa mwajiriwa husika ni mnufaika wa mkopo mwajiri atatakiwa

kuanza kukata asilimia 15 ya mshahara wa mwajiriwa huyo. Pia inapendekezwa kuwa Bodi au Mawakala wake wawe na mamlaka ya kukagua kumbukumbuku za waajiriwa kwa lengo la kutafuta taarifa zinazohusiana na wanufaika wa mkopo kwa hatua muhimu ipasavyo kuhusu ya mikopo hiyo. Hii pia imefanyiwa marekebisho kama inavyoonekana kwenye jedwali la mikopo hii itafanyika moja. Huyu Mkaguzi atafanya kwenye taarifa zinazohusiana tu na mnufaika wa mkopo lakini pia ataweza kwenda kukagua baada ya kuwa ametoa taarifa kwa yule mwajiri ili ajiandae na kuziandaa hizo taarifa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza mwanzo, Ibara ya 19 inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 21 cha sheria. Kifungu hicho kinaweka masharti kuhusu adhabu ya kuchelewesha makato ya mkopo na kuainisha kuwa mwajiri anayeshindwa kukata mkopo au anayeshindwa kuwasilisha mkopo husika baada ya kumkata mwajiriwa atatozwa asilimia 10 ya kiasi kinachodaiwa kwa kila mwezi ambapo malipo hayo yanaendelea kutolipwa. Muswada unapendekeza kuongeza msharti kwamba pale mwajiri anaposhindwa kuwasilisha makato ya kila mwezi na akashindwa kulipa tozo husika basi anatenda kosa la jinai ambalo adhabu yake ni malipo ya makato husika ambayo hayajawasilishwa au kifungo kisichopungua miezi sita na kwamba iwapo mwajiri ni kampuni, basi Mkurugenzi Mtendaji au Afisa Masuuli awajibike yeye binafsi kwa adhabu hiyo…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sekunde moja tu hapo hapo usiondoke.

Waheshimiwa Wabunge naongeza muda usiozidi nusu saa ili kazi hii iweze kwenda vizuri. Nawahakikishia tutamaliza kabla ya hiyo nusu saa haijafika.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tuendelee.

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo yanalenga kudhibiti waajiri ambao hawawasilishi makato ya mikopo kwenye Bodi na pia kuiwezesha Bodi kukusanya mikopo ili iendelee kuwakopesha wanafunzi wengine. Niseme tu mbele ya Bunge lako Tukufu utaratibu huu siyo mpya kwa mfano kwenye sheria za Mifuko ya Pensheni kama *NSSF* huu ndio utaratibu wao pia.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 20 inapendekeza kurekebisha aya ya 4 ya Jedwali la Sheria hiyo kwa kuongeza masharti yatakayoiwezesha Bodi kumwalika mtu mwenye taaluma, uzoefu au ushauri unaotakiwa na Bodi, kuhudhuria vikao vya Bodi na kwamba mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga

kura. Marekebisho haya yanalenga kuiwezesha Bodi kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi ipasavyo hasa pale jambo linalotakiwa kutolewa uamuzi linapohitaji utaalam, uzoefu au ushauri mahususi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 *(The Public Service Act, Cap. 298),* kifungu cha 3 cha Sheria hiyo kinachotoa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Sheria hiyo kinarekebishwa kwa lengo la kuongeza tafsiri ya maneno *Recruitment Secretariat.* Maneno hayo yametumika katika Sheria lakini hayakupewa tafsiri. Kwa namna hiyo, sasa meneno Sekretarieti ya Ajira *(Recruitment Secretariat)* yanamaanisha Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inayoanzishwa au kuundwa katika kifungu cha 29 cha Sheria hiyo ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 8 cha sheria hiyo kinaainisha mamlaka ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Utumishi kuwa ni pamoja na kufanya uchunguzi kwa ajili ya kuendeleza ufanisi wa watumishi wa umma na kuchukua hatua, kuratibu na kutunza taarifa zinazohusu watumishi wa umma, kufanya tathmini na kubadili malipo ya mishahara katika utumishi wa umma, na kuwezesha kuhama kwa watumishi kutoka kwa mwajiri mmoja hadi mwingine.

Ibara ya 23 ya muswada inapendekeza kurekebisha kifungu hicho ili kuweka masharti yatakayomwezesha Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma kuwa na mamlaka ya kurekebisha na kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengine ya watumishi wote wa umma.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuweka usawa wa maslahi kwa watumishi wa umma kulingana na kazi wanazofanya ikizingatiwa kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 31(2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, watumishi wa umma katika Wakala na Taasisi za Serikali wanasimamiwa na Sheria hiyo ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, pia marekebisho haya yanalenga kuhakikisha kuwa hakuna tofauti kubwa ya mishahara na marupurupu kwa watumishi wa umma wakati wote wanafanya kazi zinazolingana.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 24 ya muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 9A cha sheria kinachoweka masharti kuwa Taasisi, Wakala, Bodi au Tume za Serikali hazitakuwa na mamlaka ya kuidhinisha mishahara na marupurupu kwa watumishi wa taasisi hizo na badala yake kibali kwa ajili hiyo kitatolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma. Marekebisho haya yanalenga kuwa na mamlaka moja inayoratibu mishahara, posho na

marupurupu ya watumishi katika taasisi za Serikali na pia kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi wa taasisi hizo**.**

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, Ibara hiyo imefutwa na kuandikwa upya. Masharti yanayopendekezwa hayatatumika kwa mishahara, marupurupu na maslahi mengine kwa Bunge, Mahakama, Jeshi la Wananchi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Uhamiaji, Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Usalama wa Taifa ili kuwezesha utaratibu wa mishahara na marupurupu ya watumishi katika Taasisi hizo kuendelea kutumika kama ilivyo sasa katika Sheria zinazosimamia taasisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 20(1)(c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma kinaipa Tume ya Utumishi wa Umma mamlaka ya kutunga kanuni kuhusu usaili wa Watumishi wa Umma unaofanywa na Tume hiyo au Bodi. Ibara ya 25 ya muswada inapendekeza kuwa kifungu hicho kifutwe kwa kuwa sasa usaili kwa Watumishi wa Umma kwa sasa unafanywa na Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 26 ya muswada kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 32A kinachoweka masharti yanayowataka Watumishi wa Umma kutumia kwanza nafuu *remedies* iliyoko katika sheria hiyo kabla ya kutumia utaratibu ulioainishwa katika Sheria za kazi kwa masuala yanayohusiana na hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa mujibu wa vifungu vya 10(1)(e) na 25 vya Sheria ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma ina mamlaka ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi uliotolewa na Mamlaka ya Nidhamu ya Mtumishi wa Umma wakati ikitekeleza majukumu yake ya hatua za kinidhamu. Pia, kifungu cha hicho cha 25 cha Sheria ya Utumishi wa Umma kinaelekeza kuwa Mamlaka ya Nidhamu au Mtumishi wa Umma ambaye haitaridhishwa na uamuzi wa Tume ya Utumishi wa Umma akate rufaa kwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Sheria ilivyo sasa haijaweka masharti yanayowataka watumishi wa umma kumaliza kwanza utaratibu huo ulioanishwa katika Sheria hiyo kupata nafuu jambo linalosababisha baadhi ya Watumishi wa Umma hao na hasa waliokuwa kwenye *operational service* kutofahamu hatua stahili wanayotakiwa kuchukua kuhusiana na masuala yao ya kazi. Hivyo, marekebisho haya yanalenga kuweka mwongozo utakaowawezesha Watumishi wa Umma kutumia kwanza utaratibu ulioanishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma kabla ya kwenda katika vyombo vyingine ikiwemo Baraza la

Usuluhishi na Mahakama ya Kazi kwa kutumia sheria za kazi ambako jambo hilo linaweza kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 34 cha Sheria hiyo kinaweka masharti kuhusu Watumishi wa Umma wanaoumia kazini kulipwa fidia kwa mujibu wa kanuni zitakazotungwa na Waziri. Kwa kuwa Bunge limeshatunga Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008 *(The Workers Compensation Act, 2008)* ambayo imeanza kufanya kazi na kwa kuzingatia kuwa sheria hiyo inatumika pia kwa Watumishi wa Umma, muswada unapendekeza katika Ibara ya 27 kuwa kifungu hicho cha 34 kifutwe na kuandikwa upya.

Mapendekezo yaliyoko kwenye Muswada ni kwamba fidia kwa Watumishi wa Umma wanaoumia, kupata ajali au kufariki kutokana na kazi zao italipwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Sita inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105 yaani *The Public Service Negotiating Machinery Act, Cap. 105.* Ibara ya 30 ya Muswada inapendekeza kifungu cha 4(3)(b) kinachoelekeza kuwa Wajumbe wanaowakilisha wafanyakazi katika Baraza la Pamoja la Wafanyakazi *Service Joint Staff Committee* watachaguliwa na vyama husika vya wafanyakazi pamoja na Katibu kirekebishwe ili kumuondolea Katibu mamlaka ya kuteua Watumishi wa Umma wanaounda Baraza la Majadiliano ya Pamoja ya Watumishi wa Umma.

Hatua hii itawezesha vyama vya wafanyakazi kuteua wawakilishi wao pasipo kulazimika kumhusisha Katibu na hivyo kuwezesha wawakilishi hao kuwajibika kwa vyama hivyo. Aidha, kifungu kidogo cha 5 kinarekebishwa kwa kuweka masharti yatakayomwezesha Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma kuteua Katibu kutoka Wizara yenye dhamana na kada husika ya watumishi; masharti hayo hayako kwenye Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mwisho yanayopendekezwa katika Sehemu hii yapo katika Ibara ya 31 ya muswada ambayo inapendekeza kufuta kifungu cha 11 cha sheria ili kuondoa masharti yanayokataza Baraza la Pamoja la Wafanyakazi na Baraza la Pamoja la Watumishi wa Umma yaani *The Service Joint Staff Council* kushauri au kutoa mapendekezo kuhusiana na kima cha chini cha mshahara.

Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha suala la kima cha chini cha mishahara katika Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kushughulikiwa na Bodi za Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta husika kufuatia kuanzishwa kwa Bodi

hizo kupitia marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Taasisi za Kazi, 2004 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi 2015 *(The Employment and Labour Laws Miscellaneious Amendment Act, 2015.)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413 yaani *The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, Cap. 413*.

Ibara ya 33 ya muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 40A ili kuweka masharti kuhusu ufifilishaji wa makosa yaani *compounding of offences*. Inapendekezwa, pamoja na mengineyo kuwa pale mtu anapokiri kutenda kosa chini ya sheria hiyo na kabla ya shauri husika kufikishwa mahakamani, *SUMATRA* inaweza kumtoza mtu huyo faini isiyozidi nusu ya faini ambayo angeilipia baada ya kutiwa hatiani kwa kosa husika.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaowezesha kumaliza shauri husika mapema pale mkosaji anapokiri kosa na akawa tayari kulipia faini husika kuliko kusubiria utaratibu wa kimahakama ambao unachukua muda mrefu, pia hatua hii itaendeleza sekta ya usafirishaji nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara hiyo imeweka masharti kuhusu haki ya mtu ambaye hataridhishwa na uamuzi wa kufifilisha makosa chini ya kifungu hicho kukata rufaa Mahakama Kuu kwa kuzingatia kuwa Katiba katika Ibara yake ya 12(6)(a) inatoa haki ya mtu ambaye hajaridhika na uamuzi unaotolewa na mahakama au chombo chochote cha kimahakama kupewa fursa ya kukata rufani au kupata nafua nyingine ya kisheria. Pia msingi wa kutoa fursa ya kukata rufaa dhidi ya amri ya ufifilishaji wa makosa kutokana na ukweli kuwa anaweza kuwa hajakiri ipasavyo au faini iliyotolewa inaweza kuwa kinyume na sheria na hivyo kuhitaji Mahakama kuingilia kati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Leseni za Usafirishaji Sura ya 317, yaani *The Transport Lincencing Act, Cap. 317,* marekebisho yanayopendekezwa katika vifungu vya 11(6), 35(1), 41(1) na (2) na 42(2) yanalenga kuongeza adhabu katika vifungu hivyo ili adhabu hizo ziendane na wakati kama ifuatavyo:-

Ibara ya 35 ya muswada inapendekeza kurekebisha kifungu cha 11(6) kwa kuainisha kuwa adhabu ya kosa la kutumia gari kinyume na leseni inayotolewa chini ya kifungu hicho itakuwa faini isiyopungua shilingi 200,000 kwa mkosaji wa mara ya kwanza na sasa tumefanya mabadiliko kwenye lile Jedwali

la Marekebisho itakuwa ni shilingi 200,000 na badala faini isiyozidi shilingi 50,000 inayotajwa kwenye sheria ya sasa.

Iwapo itakuwa ni kosa la mara ya pili au kosa linalojirudia, inapendekezwa kuwa adhabu iwe faini isiyopungua shilingi 500,000 badala ya faini isiyozidi shilingi 100,000 inayotajwa kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge kama mtakavyoona kwenye Jedwali la Marekebisho Serikali imefanya marekebisho kwenye hii kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kwamba adhabu sasa itakuwa isiyopungua shilingi 250,000; lakini isiyozidi shilingi 500,000; kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Spika mapendekezo kuhusu mahakama kutoa amri ya kutaifisha gari linalohusishwa na kosa linalojirudia kwa mara ya pili na kuendelea yameondolewa na badala yake sheria ilivyo sasa itaendelea kutumika.

Ibara ya 36 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 35(1) cha Sheria kinachoweka masharti kuhusu adhabu ya kosa la kutozingatia masharti ya leseni ili iwapo kosa litafanyika kwa mara ya kwanza adhabu yake iwe faini isiyopungua shilingi 200,000 badala ya faini isiyozidi shilingi 10,000 inayotajwa kwenye sheria ya sasa. Pia, inapendekezwa iwapo kosa hilo litatendeka kwa mara ya pili au zaidi adhabu iwe faini isiyopungua shilingi 500,000 badala ya faini isiyozidi shilingi 20,000 inayotajwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Serikali imefanya marekebisho kwenye sehemu hizi kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho.

Ibara ya 37 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 41 cha sheria kinachoweka masharti kuhusu kughushi leseni; Inapendekezwa kuwa adhabu ya kosa hilo iwe faini isiyopungua shilingi 500,000 au kifungo gerezani kisichopungua miaka miwili. Sheria ya sasa inaeleza kuwa adhabu ya kosa hilo ni faini isiyozidi shilingi 50,000 au kifungo gerezani kisichozidi miaka mitano.

Aidha, Muswada unapendekeza kuwa adhabu kwa mtu anayetenda kosa la kutoa taarifa za uongo ili kupata leseni itakuwa faini isiyopungua shilingi 200,000 au kifungo gerezani kisichopungua miaka miwili badala ya faini isiyozidi shilingi 50,000 au kifungo gerezani kisichozidi miaka mitano inayotajwa kwenye sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, mbali na marekebisho hayo kuhusu adhabu, Muswada katika Ibara ya 38 unapendekeza kifungu kipya cha 47A ili kuweka

masharti kuhusu ufifilishaji wa makosa *(compounding of offences)*. Inapendekezwa kuwa iwapo mtu atakiri kutenda kosa chini ya sheria hiyo na kabla ya shauri husika kufikishwa mahakamani, *SUMATRA* inaweza kumtoza mtu huyo faini isiyozidi nusu ya kiasi cha faini ambacho angelipia baada ya kutiwa hatiani kwa kosa hilo. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu utakaowezesha kumalizika mapema kwa shauri husika kama mkosaji anakiri kosa na yuko tayari kulipia faini hiyo kuliko kusubiria utaratibu wa kimahakama ambao unachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kusema ambaye haridhiki na uamuzi huu wa *SUMATRA* ana haki ya kikatiba na kisheria kwenda mahakamani kukata rufaa, Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa ya muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 yaani *The Treasury Registrar Powers and Functions Act Cap.370*. Kifungu cha 3 cha sheria hiyo kinaelekeza, pamoja na mengineyo, kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina inaweza kushtaki au kushtakiwa yenyewe ikijitegemea. Marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza masharti yatakayompatia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama mshauri mkuu wa Serikali kwa masuala yote ya kisheria, akiwa na haki ya Kikatiba ya kuhudhuria na kusikilizwa katika Mahakama zote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haki ya kuingilia kati shauri lolote lililofunguliwa dhidi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina au kufunguliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuiwakilisha Ofisi hiyo katika shauri hilo. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali katika mashauri husika kwa kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ni Taasisi ya Serikali na inasimamia mali na mashirika au taasisi nyingine za Serikali.

Aidha, ili kumwezesha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza wajibu huo, muswada unapendekeza masharti kuwa Msajili wa Hazina amfahamishe Mwanasheria Mkuu pale Ofisi hiyo inaposhtakiwa au inapotaka kufungua shauri. Sheria ya Mashirika ya Umma yaani *The Public Corporations Act, Cap. 257* na Sheria nyinginezo zinazoanzisha Mamlaka za udhibiti *Regulatory Authorities* mbalimbali, Bodi na Taasisi nyinginezo za Kiserikali tayari zinayo masharti kama haya ili kuimarisha ulinzi na usalama wa kisheria wa mali na maslahi ya umma na Serikali katika taasisi hizo muhuimu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Vipimo; Sura ya 340 *(The Weight and Measures Act Cap. 340.)* Ibara ya 42 ya muswada inapendekeza marekebisho ya jumla kwenye sheria hiyo ili kuboresha matumizi ya maneno yaliyotumika katika sheria

hiyo. Mapendekezo hayo ni kufuta maneno *weighing and measuring instrument* kila yanapojitokeza katika sheria hiyo na kuweka badala yake maneno *measuring instrument or measuring system* na pia kufuta maneno *assizer* na kuweka badala yake neno *inspector*.

Aidha, Ibara hiyo inapendekeza kuongeza tafsiri ya neno *container* ambalo limetumika katika sheria hiyo ili kuwezesha watumiaji wa sheria kufahamu maana yake kwa muktadha wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 43 inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 2 kinachohusiana na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika sheria hiyo kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya neno biashara yaani *trade* ili kujumuisha huduma inayotolewa kwa kutumia vipimo pamoja na kipimo chochote kinachohusisha kifaa au mfumo wa kupimia. Taarifa iliyopo kwenye sheria ya sasa inaelezea tu kuwa biashara ni kuingia au kufanya makubaliano, manunuzi au mauzo ambapo thamani ya bidhaa inapimwa au kuhesabiwa. Kwa kuwa huduma inaweza kutolewa kwa kutumia vipimo au viwango, muswada unapendekeza marekebisho ya tafsiri ya neno hilo kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 44 ya muswada iliyokuwa inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria hiyo imefutwa kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho. Hata hivyo, masharti husika kuhusu Waziri mwenye dhamana ya vipimo kuwa na mamlaka ya kufanya marekebisho kwenye Majedwali ya Sheria hiyo pale itakapohitajika yanapendekezwa yaingizwe katika kifungu kipya cha 54A cha sheria hiyo.

Majedwali hayo yanaainisha viwango vya upimaji yaani *units of measurement,* viwango hivyo vinaweza kubadilika mara kwa mara kutokana na mahitaji ikiwemo yale ya *International System of Units* ambayo Tanzania ni mwanachama. Hivyo, hatua hii itarahisisha utekelezaji wa sheria hiyo kwa kufanya marekebisho ya viwango hivyo mapema kulingana na mahitaji badala ya kusubiria kuleta marekebisho ya sheria hiyo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinaweka masharti kuhusu uhakiki wa vipimo. Muswada unapendekeza katika Ibara ya 45 kuwa kifungu hicho kirekebishwe katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuelekeza kuwa tangazo la uhakiki litatolewa walau mara moja kwa mwaka. Sheria ilivyo sasa inaelekeza kuwa tangazo hilo litatolewa si zaidi ya mara moja kwa mwaka. Marekebisho haya yanalenga kuwezesha uhakiki wa vipimo kufanyika muda wowote pale inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Hatua hiyo itarahisisha utekelezaji wa Sheria hiyo.

Pia Ibara hiyo ya 45 inapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha (2) ili kuweka masharti yanayomtaka mtu anayemiliki kipimo kinachotumika au kinachokusudiwa kutumika kibiashara kukiwasilisha kwa Mkaguzi hata kama taarifa ya kufanya hivyo haikuwa imetolewa hapo awali. Muswada unapendekeza kuongeza kifungu kidogo cha (5) kinachoweka masharti kwamba vipimo visivyohamishika vitatakiwa kukaguliwa na kuhakikiwa katika sehemu au mahali vilipo. Madhumuni ya marekebisho ni kuhahakisha kuwa vipimo vinavyotumika viko sahihi na hakuna usumbufu wowote wa kuanza kusafirisha vitu ambavyo havihamishiki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 26 cha sheria hiyo kinaweka masharti kuhusu uuzaji kwa njia ya vipimo *(sale by net weight or measures)*. Ibara ya 46 ya muswada inapendekeza kifungu cha 26(2) kirekebishwe ili kuongeza masharti yanayomtaka mmiliki wa gari au mtu aliyekodishwa kubeba au kusafirisha bidhaa iliyofungashwa kufuata masharti ya ufungaji wa mizigo yaliyobainishwa katika Majedwali ya Sheria hii na kwamba mtu anayekiuka masharti ya kifungu hicho anatenda kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 47 ya muswada inapendekeza kifungu cha 30(2) kirekebishwe ili adhabu ya kosa la kukiuka masharti ya kifungu kicho kinachotaka uuzaji unaofanyika kwa kutumia vipimo ufanyike mbele ya mnunuzi, iwe faini isiyopungua shilingi 300,000 na isiyozidi shilingi milioni 50. Adhabu inayotajwa kwenye sheria ya sasa ni faini isiyozidi shilingi 200,000. Adhabu hiyo inaonekana kupitwa na wakati na pia inaweza kusababisha mtu kutenda kosa hilo kwa kutegemea kulipa faini hata kama akipatikana na hatia. Marekebisho haya yanalenga kuwezesha adhabu kutolewa kulingana na uzito au mazingira ya kosa husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 45 kinachoweka adhabu ya jumla kwa mtu anayekiuka masharti ya Sheria hiyo au Kanuni zake kinafutwa na kuandikwa upya. Marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 48 ya Muswada ni kwamba adhabu ya kosa hilo iwe faini isiyopungua shilingi laki tatu na isiyozidi shilingi milioni 50 na kifungo gerezani kisichozidi miaka miwili au vyote kwa mkosaji wa kwanza. Iwapo mtu huyo atarudia tena kutenda kosa hilo adhabu inayopendekezwa ni faini isiyopungua shilingi 500,000 na isiyozidi shilingi milioni 100 au kifungo gerezani kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Adhabu inayotajwa kwenye sheria ya sasa ni faini isiyozidi shilingi 10,000 au kifungo gerezani kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa mkosaji wa mara ya kwanza na faini isiyozidi shilingi 10,000 au kifungo gerezani kisichozidi miaka saba au vyote kwa pamoja. Hivyo, marekebisho haya yamelenga kuongeza adhabu

ya faini ili iendane na wakati na pia kuwafanya watu wazingatie ipasavyo masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa katika Ibara hiyo ya 48 ya muswada ni kuongeza masharti yatakayoiwezesha mahakama baada ya kumtia hatiani mshtakiwa kwa kosa chini ya sheria hiyo kutoa amri ya kutaifisha bidhaa au sehemu ya bidhaa au kifaa kinachohusika na kosa hilo.

Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa mtuhumiwa hanufaiki kwa kutenda makosa chini ya sheria hii ikiwemo kupima bidhaa isivyo halali na pia kuhakikisha kuwa watu wanatekeleza masharti ya sheria hii kwa uadilifu na uaminifu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 49 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 46 kinachoweka masharti kuhusu mamlaka ya Kamishna wa Vipimo katika kufifilisha makosa chini ya sheria hiyo. Malipo yanayotajwa kwenye sheria ya sasa kuwa yatatozwa na Kamishna wakati wa kufifilisha makosa ni kiasi kisichopungua shilingi 5,000. Kiwango hicho kimepitwa na wakati na hivyo muswada unapendekeza kwamba malipo yatakayolipwa kwa ajili hiyo yasipungue shilingi 100,000 na yasizidi shilingi milioni 20.

Aidha, sheria ilivyo sasa haijaweka masharti kuwa ufifilishaji wa makosa utafanyika pale mtuhumiwa anapokiri kosa. Hivyo, muswada unaongeza masharti kuwa ufifilishaji utafanyika baada ya mtu kukiri kosa husika.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya katika sehemu hii ni kuongeza kifungu kipya cha 53A kama inavyoonekana katika Ibara ya 50 ya muswada na kufanya marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho.

Kifungu kipya kinachopendekezwa kinaweka masharti kuwa mtu atakayeainisha vipimo vinavyotumika katika eneo lake la kiutawala azingatie ipasavyo vipimo yaani *prescribed measuring standards* vilivyoainishwa katika Sheria ya Vipimo. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha kuwa na vipimo vinavyofanana kulingana kama vilivyoainishwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo ya hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2016 yaani *The Written Laws Miscellaneous Amendment No.3 Act, 2016* na ninaomba Bunge lako Tukufu liujadili na kuupitisha katika hatua ya kusomwa

kwa mara ya pili na mara ya tatu ili hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwa)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**ISSN 0856 - 35X**

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***BILL SUPPLEMENT***

***No. 15***
***26th August, 2016***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.36 Vol.97 dated 26th August, 2016*
Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.3) ACT, 2016

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of certain written laws.

PART II
AMENDMENT OF THE CIVIL AVIATION ACT,
(CAP. 80)

3. Construction.
4. Addition of a new section 10A.
5. Addition of new sections 11A and 11B.
6. Addition of new sections 19A na 19B.
7. Amendment of section 26.

PART III
AMENDMENT OF THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT ACT,
(CAP.191)

8. Construction.
9. Amendment of section 16.
10. Amendment of section 42.
11. Amendment of section 57.
12. Amendment of section 184.
13. Amendment of section 187.
14. Amendment of section 191.
15. Amendment of the Fourth Schedule.

PART IV
AMENDMENT OF THE HIGHER EDUCATION STUDENTS' LOANS BOARD ACT,
(CAP. 178)

16. Construction.
17. Amendment of section 5.
18. Repeal of section 19.
19. Repeal of sections 20 and 21.
20. Amendment of the Schedule.

PART V
AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE ACT,
(CAP. 298)

21. Construction.
22. Amendment of section 3.
23. Amendment of section 8.
24. Addition of sections 9A and 9B.
25. Amendment of section 20.
26. Addition of new section 32A.
27. Repeal of section 34.
28. Amendment of section 35.

PART VI
AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE (NEGOTIATING MACHINERY) ACT,
(CAP. 105)

29. Construction.
30. Amendment of section 4.
31. Repeal of section 11.

PART VII
AMENDMENT OF THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT
REGULATORY AUTHORITY ACT,
(CAP.413)

32. Construction.
33. Addition of new section 40A.

PART VIII
AMENDMENT OF THE TRANSPORT LICENSING ACT,
(CAP. 317)

34. Construction.
35. Amendmentof section 11.
36. Amendment of section 35.
37. Amendment of section 41.
38. Amendment of section 47A.

PART IX
AMENDMENT OF THE TREASURY REGISTRAR (POWERS AND FUNCTIONS) ACT,
(CAP. 370)

39. Construction.
40. Amendment of section 46.

PART X
AMENDMENT OF THE WEIGHTS AND MEASURES ACT,
(CAP. 340)

41. Construction.
42. General amendments.
43. Amendment of section 2.
44. Amendment of section 3.
45. Amendment of section 19.
46. Amendment of section 26.
47. Amendment of section 30.
48. Repeal of section 45.
49. Amendment of section 46.
50. Addition of section 53A.

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,
26th August, 2016

**JOHN W. H. KIJAZI**
*Secretary to the Cabinet*

## A BILL
*for*

**An Act to amend certain written laws.**

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title

**1**. This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2016.

Amendment of certain written laws

**2.** The Written Laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II
AMENDMENT OF THE CIVIL AVIATION ACT,
(CAP. 80)

Construction

**3**. This Part shall be read as one with the Civil Aviation Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Cap. 80

Addition of a new section 10A

**4**. The principal Act is amended by adding immediately after section 10 the following new section:

"Power to detain and search aircraft

**10A**. Where the Director-General has reasonable grounds to suspect that an aircraft is used in contravention of this Act or that it contains any matter which may be used as evidence in respect of an offence under this Act, the Director General may detain, inspect, board on or recall that aircraft in flight."

Addition of new sections 11A and 11B

**5**. The principal Act is amended by adding immediately after section 11 the following new sections:

"Transfer of responsibili-ties to another state

**11A.** Notwithstanding any provision of this Act, the Authority may, by agreement made with the appropriate foreign civil aviation authority under the Chicago Convention:

(a) transfer to the concerned civil aviation authority of another state, all or part of the Authority's responsibilities for a Tanzania registered aircraft operated by a foreign operator; or

(b) vest in the Authority all or part of the responsibilities of the civil aviation authority of another state for an aircraft registered by that state and operated by a Tanzania operator.

Aircraft in distress

**11B.** Where an aircraft is in distress within the territory of the Authority, the Authority shall-

(a) permit, subject to control by its own

authorities, the owners of the aircraft or authorities of the state in which the aircraft is registered to provide such measures of assistance as may be necessitated by the circumstances rendering the distress;

(b) in the case where the aircraft is missing, search the missing aircraft in line with the coordinated measures prescribed by the Authority; or

(c) provide any other necessary assistance."

Addition of new sections 19A and 19B

**6**. The principal Act is amended by adding immediately after section 19 the following new section:

"Revocation and suspension of certificates

**19A**. Where the Director-General has reasonable grounds to believe that any person has violated this Act, he may make an order to prohibit, suspend, revoke or vary the privileges of a licence, certificate or any other authorization issued by the Authority to that person.

Inspection

**19B**. For the purpose of ensuring aviation safety, security, consumer protection and for any other reasons for which the Authority is established, the Authority shall have unrestricted access to inspect-

(a) any aircraft in Tanzanian territory regardless of its state of registry;

(b) Tanzania registered aircraft wherever it may be;

(c) flight compartment;

(d) aerodrome used for civil aviation operations;

(e) facilities and aircraft accident sites;

(f) premises of any regulated agent or premises of the holder of an air service licence, certificate,

authorization; or

(g) other approval document issued by the Authority or any records, information and explanation."

Amendment of section 26

**7**. The principal Act is amended in section 26 by adding a new subsection (7) immediately after subsection (6) as follows:

"(7) In providing air navigation services, the Authority shall ensure that a clear distinction and separation between its regulatory and operational functions is maintained."

PART III
AMENDMENT OF THE ENVIRONMENTAL MANAGEMENT ACT, (CAP.191)

Construction Cap. 191

**8**. This Part shall be read as one with the Environmental Management Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 16

**9**. The principal Act is amended in section 16 by adding immediately after subsection (2) the following new subsections:

"(3) Notwithstanding the provisions of this section, the Attorney General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by, or against the Council.

(4) Where the Attorney General intervenes in any matter pursuant to subsection (3), the provisions of the Government Proceedings Act shall apply in relation to the proceedings of that suit or matter as if it had been instituted by, or against the Government.

Cap. 5

(5) For the purposes of subsections (3) and (4), the Council shall have a duty to notify the Attorney General of any pending suit or intention to institute a suit or matter by, or against the Council."

Amendment of section 42

**10.** The principal Act is amended in section 42 by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) Local government authorities shall submit to the Minister environmental action plans prepared in

respect of their areas of jurisdiction."

Amendment of section 57

**11.** The principal Act is amended in section 57 by-

(a) designating its contents as subsection (1); and

(b) adding immediately after subsection (1) as designated, the following-

"(2) For the purposes of subsection (1), the computation of sixty meters shall be reckoned -

(a) in the case of ocean or a natural lake, from the highest water mark; and

(b) in the case of rivers, water dams or reservoirs, from the banks;"

Amendment of section 184

**12.** The principal Act is amended in section 184 by -

(a) designating its contents as subsection (1);

(b) deleting paragraph (a) appearing in subsection (1) as designated and substituting for it the following -

"(a) fails or refuses to conduct an Environmental Impact Assessment study in respect of a project for which the assessment is mandatory, commits an offence;"

(c) adding immediately after subsection (1) as designated the following-

"(2) A person who has paid a fine as a penalty for an offence of failing or refusing to conduct an Environmental Impact Assessment Study shall submit to the Council an environmental management plan for approval and guidance on how the project shall be implemented.

(3) Where the offence committed is that of failing or refusing to conduct an Environmental Impact Assessment study, the offender shall, upon conviction, be liable to a fine of not less than five million shillings but not exceeding one billion shillings or to imprisonment for a term of not less than two years but not exceeding seven years or to both."

Amendment of section 187

**13.** The principal Act is amended in section 187(1) by deleting the words "not less than three million shillings but not exceeding fifty million shillings" and substituting for them the

words "not less than five million shillings but not exceeding ten billion shillings"

Amendment of section 191

**14.** The principal Act is amended in section 191 by deleting the words "fifty million" and substituting for them the words "one billion".

Amendment of the Fourth Schedule

**15.** The principal Act is amended in paragraph 1 of the Fourth Schedule by-

(a) deleting the word "nine" and substituting for it the word "eleven"; and

(b) inserting immediately after item (i) the following-

"(j) three persons from the private sector who have proven knowledge, skills and experience in matters relating to the operations of funds."

PART IV
AMENDMENT OF THE HIGHER EDUCATION STUDENTS' LOANS BOARD ACT, (CAP. 178)

Construction Cap. 178

**16.** This Part shall be read as one with the Higher Education Students' Loans Board Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 5

**17.** The principal Act is amended in section 5 by-

(a) deleting subsections (1) and (2) and substituting for them the following:

**"**(1) The Board shall consist of a Chairman who shall be appointed by the President and six other members to be appointed by the Minister as follows:

(a) one member representing the Ministry responsible for higher education;

(b) a member from the Treasury;

(c) a Law Officer representing the Attorney General;

(d) a member representing the Ministry responsible for finance in the Revolutionary Government of Zanzibar;

(e) one representative from umbrella

students' association of higher learning institutions; and

(f) one member representing the Tanzania Commission for Universities."

(b) renumbering subsections (3) to (6) as subsections (2) to (5) respectively.

Repeal of section 19

**18**. The principal Act is amended by repealing section 19 and replacing for it the following:

"Liability and obligation of loan beneficiary

**19.**-(1) It shall be the duty of every loan beneficiary to repay the loan within the time and manner specified in the loan agreement-

(2) Repayment of loan shall become due upon-

(a) completion of studies in respect of which the loan was granted; or

(b) immediately where studies are terminated for any reason.

(3) The loan repayable shall be the total sum of money:

(a) calculated on the basis of the loan agreement, which shall be established by the Board as having been received by a beneficiary; or

(b) which the Board paid to the account of a higher learning institution where the beneficiary pursued studies.

(4) A beneficiary who secures employment shall-

(a) have the duty to notify the employer that he is a loan beneficiary;

(b) ensure that arrangement is made with the employer for deduction of monthly installment that shall include the principal, any fees, charges or penalties from the salary of the beneficiary;

(c) ensure that payments of monthly

deduction by the employer are remitted to the Board from the date such remittance is due and that the loan deduction schedule bear the name of the beneficiary, loan number, employment number or cheque number;

(d) inform the Board in writing of-
   (i) employer's name, address, telephone number and other necessary details;
   (ii) any change of names;
   (iii) the current address of the beneficiary and any subsequent changes of address;
   (iv) any thing that may be prescribed by the Board in accordance with this Act.

(5) A beneficiary who engages in self-employment, any trade, occupation or profession shall-

(a) arrange with the Board about the amount or installments and period during which the beneficiary shall make remittance to the Board;

(b) ensure that the remittance of monthly installment is made to the Board bearing the correct name, address and the loan number;

(c) inform the Board of the-
   (i) current postal and physical address;
   (ii) occupational and residential addresses;
   (iii) telephone numbers; and
   (iv) any subsequent changes of such particulars;

(d) comply with any other requirement as may be prescribed by the Board under this Act.

(6) For the purpose of subsection (5)(a), the amount payable by a self-employed

beneficiary on monthly basis shall not be less than one hundred and twenty thousand shillings or ten percent of the taxable income, whichever amount is greater.

(7) Subsection (4) shall apply *mutatis mutandis* to any beneficiary who is under employment of a foreign government, an international organization, a company, an agency or an association of any description."

Repeal of sections 20 and 21

**19**. The principal Act is amended by repealing sections 20 and 21 and replacing them with the following:

"Obligation of employer

**20.**-(1) For the purpose of identifying beneficiaries under this Act, every employer shall-

(a) notify the Board on employment of any person who is a holder of degree or diploma, within twenty eight days from the date on which such person is employed;

(b) upon confirmation from the Board that the person named in the notification is a loan beneficiary, deduct monthly installments of not less than fifteen percent of basic salary, wages or remuneration of the beneficiary, as the case may be;

(c) treat deduction as statutory and make such deductions as first charge over non statutory deductions; and

(d) inform the Board in writing of the status and rank of employment and any subsequent changes in the name, address, occupation and salary of the person who is a beneficiary.

(2) The employer shall remit every deduction from the beneficiary's salary, wages or remuneration to the Board within fifteen days after the end of each month.

(3) The Board or its agents shall have

power to inspect any record of the employer for searching the beneficiaries' information.

(4) Where an employer fails to notify the Board about the employment of a holder of degree or diploma in accordance with this Act, such employer commits an offence and is liable on conviction to a fine of not less than seven million shillings or to imprisonment for a term of not less than twelve months or to both.

Failure of employer to make deductions or remmittance

**21.**-(1) Where the employer fails to deduct or after making deduction from a beneficiary fails to remit such deductions to the Board within the prescribed period, the Board shall charge a sum of equal to ten percent of the total amount of the loan amount which is due for repayment for each month during which the repayment remains unremitted.

(2) Where the employer fails to remit monthly installments after deducting and is otherwise unable to pay the charge imposed under subsection (1), commits an offence and is liable on conviction to a fine of not less than the amount unremitted or to imprisonment for a term of not less than thirty six months.

(3) Notwithstanding any other law to the contrary, where an employer is a body corporate, the chief executive officer or any other accountable officer of such body shall be personally liable for the penalty.

(4) Any person who obstructs an employee of the Board or its appointed agent from doing any act authorized by this Act, commits an offence and is liable on conviction, to a fine of not less than seven million shillings or to imprisonment for a term of not less than twelve months or both."

Amendment of the Schedule

**20.** The principal Act is amended in paragraph 4 of the Schedule by inserting immediately after subparagraph (6) the following:

"(7) The Board may co-opt any person to assist the Board on deliberation of any issue or matter that requires the person's skills, expertise or advice, but the co-opted person shall have no right to vote in any meeting of the Board."

PART V
AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE ACT,
(CAP. 298)

Construction
Cap. 298

**21.** This Part shall be read as one with the Public Service Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 3

**22.** The principal Act is amended in section 3 by inserting in the appropriate alphabetical order the following new definition:

"Recruitment Secretariat" means the Public Service Recruitment Secretariat established under section 29;"

Amendment of section 8

**23.** The principal Act is amended in section 8(3) by-

(a) inserting immediately after paragraph (c) the following-

"(d) rationalize and harmonize salaries, allowances and fringe benefits in the Service;"

(b) renaming paragraphs (e) to (h) as paragraphs (f) to (i) respectively.

Addition of sections 9A and 9B

**24.** The principal Act is amended by adding immediately after section 9 the following new sections-

"Approval of Salary and incentives

**9A.**-(1) Notwithstanding the provisions of any other written laws, no public institution, Agency, Board or commission shall approve salaries, allowances, incentives and fringe benefits for its organization.

(2) Without prejudice to subsection (1), approval of salaries, allowances, incentives and fringe benefits in the Service shall be

determined by the Permanent Secretary (Establishments).

Conflict of laws in relation to remuneration

**9B.** Where there is a conflict between the provisions of this Act and the provisions of any other written laws, regarding remuneration, the provisions of this Act shall prevail."

Amendment of section 20

**25.** The principal Act is amended in section 20(1) by:

(a) deleting paragraph (c); and

(b) renaming paragraphs (d) and (e) as paragraphs (c) and (d) respectively.

Addition of new section 32A

**26.** The principal Act is amended by adding immediately after section 32 the following new section:

"Remedies under labour laws

**32A**. A Public servant shall, prior to seeking remedies provided for in labour laws, exhaust all remedies as provided for under this Act."

Repeal of section 34

**27.** The principal Act is amended by repealing section 34 and substituting for it the following:

"Compensa-tion for occupational disease and death Cap. 263

**34.**-(1) A public servant who suffers occupational disease or dies in the course of employment, shall be compensated in accordance with the Workers Compensation Act."

(2) For the purpose of this section "occupational disease" shall have a meaning to it under the Workers Compensation Act.

Amendment of section 35

**28.** The principal Act is amended in section 35(2) by:
(a) deleting "semi colon" appearing at the end of paragraph (d) and substituting for it a "full stop"; and
(b) deleting paragraph (e).

PART VI
AMENDMENT OF THE PUBLIC SERVICE (NEGOTIATING MACHINERY) ACT,
(CAP. 105)

Construction Cap. 105

**29.** This Part shall be read as one with the Public Service (Negotiating Machinery) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 4

**30.** The principal Act is amended:
(a) in section 4(3), by deleting the words "and the secretary" appearing in paragraph (b); and
(b) by inserting immediately after subsection (4) the following new subsection:
"(5) The Minister shall appoint a secretary of the Joint Staff Council from the respective service scheme."

Repeal of section 11

**31.** The principal Act is amended by repealing section 11.

PART VII
AMENDMENT OF THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT
REGULATORY AUTHORITY ACT,
(CAP.413)

Construction Cap. 413

**32.** This Part shall be read as one with the Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Addition of new section 40A

**33.** The principal Act is amended by adding immediately after section 40 the following new section:

"Compo-unding of

**40A.**-(1) Notwithstanding the provisions of this Act relating to penalties, where a person admits in writing that he has commited an offence under this Act, the Authority may, at

offence s

any time prior to the comencement of the hearing by a court of competent jurisdiction, compound such offence and order such person to pay sum of money, not exceeding one half of the amount of the fine to which such person would otherwise have been liable to pay if he had been convicted of such offence.

(2) Where an offence is compounded in accordance with subsection (1) and proceeding are brought against the offender for the same offence, it shall be a good defence for the offender to prove to the satisfaction of the court that the offence with which the offender is charged has been compounded under sub-section (1).

(3) Where any person is agrieved by any order under sub-section (1), he may within the prescibed period, appeal against such order to the High Court and the provisions of the Criminal Proceedure Act shall apply to every such appeal as if it were an appeal against sentence passed by a district court in the exercise of its original jurisdiction.

(4) Where the person fails to comply with the order issued under this section within the prescribed period, the Authority:

(a) shall, in addition to the sum ordered, require the person to pay an interest at the rate prescribed in the regulations; and
(b) may enforced the order in the same manner as a decree of a court for the payment of the amount stated in the order.

(5) The Minister shall make Regulations prescribing offences to be compounded and procedure for compounding of offences under this Act."

PART VIII
AMENDMENT OF THE TRANSPORT LICENSING ACT,

(CAP. 317)

Construction
Cap. 317

**34.** This Part shall be read as one with the Transport Licensing Act, hereinafter referred to as "principal Act".

Amendment of section 11

**35.** The principal Act is amended in section 11, by deleting subsection (6) and substituting for it the following:

"(6) A person who uses a motor vehicle in contravention of this section commit an offence and shall be liable, on conviction-

(a) in the case of the first offence, to a fine of not less than two hundred thousands,

(b) in the case of second and subsequent offence, to a fine not less than five hundred thousand shillings,

and in addition to the fine, the court may, in the case of the second or subsequent offence, order the forfeiture of the vehicle in relation to which the offence is committed, whether or not the previous offences were committed in relation to the same vehicle."

Amendment of section 35

**36**. The principal Act is amended in section 35(1), by-

(a) deleting the words " not exceeding ten" appearing between the words "fine" and "thousand" and substituting for them the words "of not less than two hundred"; and

(b) deleting the words "exceeding twenty" appearing between the words "not" and "thousand" and substituting for them the words "five hundred".

Amendment of section 41

**37.** The principal Act is amended in section 41, by-

(a) deleting the words "exceeding fifty" and "exceeding five" wherever they appear in subsection (1) and substituting for them the words "less than five hundred" and "less than two" respectively; and

(b) deleting the words "exceeding twenty" and "exceeding two" wherever they appear in subsection (2) and substituting for them the words "less than two hundred" and "less than two" respectively.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Amendment of section 47A

**38.** The principal Act is amended by adding immediately after section 47, a new section 47A as follows:

"Compounding of offences

**47A.**-(1) Notwithstanding the provision of this Act relating to penalties, where a person admits in writing that he has commited an offence under this Act, the Authority may, at any time prior to the comencement of the hearing by a court of competent jurisdiction, compound such offence and order such person to pay sum of money, not exceeding one half of the amount of the fine to which such person would otherwise have been liable to pay if he had been convicted of such offence.

(2) Where an offence is compounded in accordance with subsection (1) and proceeding are brought against the offender for the same offence, it shall be a good defence for the offender to prove to the satisfaction of the court that the offence with which the offender is charged has been compounded under sub-section (1).

(3) Where any person is agrieved by any order under sub-section (1), he may within the prescibed period, appeal against such order to the High Court and the provisions of the Criminal Proceedure Act shall apply to every such appeal as if it were an appeal against sentence passed by a district court in the exercise of its original jurisdiction.

(4) Where the person fails to comply with the order issued under this section within the prescribed period, the Authority:

(a) shall, in addition to the sum ordered, require the person to pay an interest at the rate prescribed in the regulations; and

(b) may enforced the order in the same manner as a decree of a court for the payment of the amount stated in the order.

(5) The Minister shall make regulations prescribing offences to be compounded and procedure for compounding of offences under this Act.

PART IX
AMENDMENT OF THE TREASURY REGISTRAR (POWERS AND FUNCTIONS) ACT, (CAP. 370)

Construction Cap. 370

**39.** This Part shall be read as one with the Treasury Registrar (Powers and Functions) Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 46

**40.** The principal Act is amended in section 3 by adding immediately after subsection (2) the following new subsections:

"(3) Notwithstanding the provisions of this section, the Attorney-General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by, or against the Board.

(4) Where the Attorney General intervenes in any matter in pursuance of subsection (2), the provisions of the Government Proceedings Act shall apply in relation to the proceedings of that suit or matter as if it had been instituted by, or against the Government.

Cap. 6

(5) For the purposes of subsections (3) and (4), the Treasury Registrar shall have a duty to notify the Attorney General of any impending suit or intention to institute a suit or matter by, or against the Board."

PART XI
AMENDMENT OF THE WEIGHTS AND MEASURES ACT, (CAP. 340)

Construction Cap. 340

**41.** This Part shall be read as one with the Weights and Measures Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

General

**42.** The principal Act is amended generally by-

amendments

(a) deleting the words "weighing and measuring instrument" wherever they appear in the Act and substituting for them the words "measuring instrument or measuring system".

(b) deleting the words "assizer" wherever they appear in the Act and substituting for them the words "inspector".

(c) Inserting in its appropriate alphabetical order the following new definition:

"container" means any form of packaging of goods as a single item, whether by enclosing the goods wholly or partly.

Amendment of section 2

**43.** The principal Act is amended in section 2 by deleting the definition of the word "trade" and substituting for it the following:

""trade" includes-

(a) the making, effecting or concluding of any contract bargain, sale, purchase or transaction, or any payment in connection therewith;

(b) any services rendered in which measurements are used;

(c) any other measurement within which a measuring instrument or system is used."

Amendment of section 3

**44.** The principal Act is amended in section 3 by adding immediately after subsection (7) the following:

"(8) The Minister may, by order published in the *Gazette*, amend the Schedules to this Act."

Amendment of section 19

**45.** The principal Act is amended in section 19 by-

(a) deleting the words "Not more than" at the beginning of sub section (1) and substituting for it the words "At least once";

(b) adding immediately after subsection (1) the following new subsection:

"(2) Notwithstanding subsection (1), a person who possesses any weight, measure, weighing or

measuring instrument which is used or intended to be used in trade, shall produce such weight, measure, weighing or measuring instrument to an inspector even if the notice in subsection (1) was not issued."

(a) renumbering subsections (2) to (6) as subsections (3) to (7) respectively.

(b) inserting immediately after (4) as renumbered the following new subsection:

"(5) Any immovable weight, measure, weighing or measuring instrument, shall be examined and verified in *situ* in addition to any preliminary test."

Amendment of section 26

**46.** The principal Act is amended in section 26 by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) Any person who owns or hired to carry or transport by any means prepacked goods shall comply with manner of packaging specified in 10th, 11th and 12th Schedules to this Act.

(3) Any person who contravenes or fails to comply with subsections (1) and (2) commits an offence."

Amendment of section 30

**47.** The principal Act is amended in section 30(2) by deleting the phrase "not exceeding two thousand shillings" appearing in subsection (2) and substituting for it the words "not less than three hundred thousand shillings and not exceeding fifty million shillings or to both".

Repeal of section 45

**48.** The principal Act is amended by repealing section 45 and replacing it with the following:

"General penalty

**45.** Any person who contravenes the provisions of this Act or Regulations made under this Act and which no specific penalty is provided shall commits an offence and on conviction, in the case of first offence to a fine of not less than three hundred thousand shillings and not exceeding fifty million shillings or to imprisonment for a term not exceeding two years or to both such fine and imprisonment;

and in the case of a second or subsequent offence, to a fine of not less than five hundred thousand shillings and not exceeding one hundred million shillings or to imprisonment for a term not exceeding five years or to both."

(2) On the conviction of any person for an offence under this Act, the court may, in addition to any other penalty which may be imposed, order the confiscation of all or any part of goods in respect of which the offence was committed, and all goods or instruments so confiscated shall be disposed of in a manner which the court directs."

Amendment of section 46

**49.** The principal Act is amended in section 46 by-

(a) deleting subsection (1) and substituting for it the following:

"(1) Where the Commissioner is satisfied that any person has committed an offence under this Act, he may by order, compound such offence by requiring such person to make payment of a sum of money, except that-

(a) such sum of money shall not be less than one hundred thousand shillings and not exceeding twenty million;

(b) the power or conferred under this section shall be exercised when a person admits that he has committed he offence under this Act;

(c) the Commissioner shall give to the person from whom he receives such sum of money, a receipt;

(d) subject to the provision of subsection (1), where proceedings are brought against a person for an offence under this Act, it shall be a good defence if that person proves that offence with which he is charged has been earlier compounded;

(e) any sum of money received under this section shall be dealt with as if the sum of

money were a fine imposed by the court of law for the offence;

(f) the order shall not be made under this section unless the person concern shall first had an opportunity of showing cause against the making of the order.

(2) In the addition to the fine, the Commissioner may ask the court to forfeit any weight or measure or weighing or measuring instrument or other item for which the offence was committed as directed by or under this Act or any regulations made under this Act.

(b) renumbering subsections (2) to (4) as subsections (3) to (5) respectively."

Addition of section 53A

**50.** The principal Act is amended by adding immediately after section 53 the following new section:

"Compliance with prescribed measurement standards

**53A.** Local Government Authorities, government agencies shall, in prescribing measurements applicable in their respective jurisdiction, have regard to the prescribed standards of measurements under this Act."

---

**OBJECTS AND REASONS**

---

This Bill proposes to amend Nine laws namely, the Civil Aviation Act, Cap. 80; the Environment Management Act, Cap.191, the Higher Education Student's Loans Board Act, Cap.178, the Public Service Act, Cap. 298, the Public Service (Negotiation Machinery) Act, Cap. 105, the Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, Cap. 413, the Transport Licensing Act, Cap. 317, the Treasury Registrar (Power and Functions) Act, Cap370; and the Weights and

Measures Act, Cap. 340.

The proposed amendments intend to keep the respective laws with changes so far observed in their implementation.

This Bill is divided into Ten Parts.

Part I deals with Preliminary Provisions which includes the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended, are amended in their respective Parts.
Part II of the Bill proposes to amend the Civil Aviation Act, Cap. 80. The amendments proposes to introduce a new section 10A, that empowers the Authority to inspect, board or detain an aircraft where has reasonable grounds to suspect that the aircraft is being used in contravention of the Act. It is further proposed to add a new section 11A for the purpose of complying with Article 83 of the Chicago Convention which provided for transferring of oversight functions to another state upon entering into an agreement. Furthermore, the Part introduces a new section 11B to implement article 25 of the Chicago Convention on providing assistance to aircraft in distress.

The new section 19A and 19B proposes to empower the Director General to suspend or revoke certificate or licence and to provide for the unrestricted access to aviation facilities. The Part also proposes to amend section 26 by adding a new subsection (7) that requires the Authority to ensure that a clear distinction and separation between its regulatory and operational functions is maintained when providing air navigation services.

Part III proposes to amend the Environment Management Act, Cap. 191, where section 16 is proposed to be amended for the purpose of giving the Attorney General right to intervene any suit or matter instituted by or against the Council by representing the Council in the court accordingly. The proposed amendments aim at protecting the Government's assets and interest.

Section 57 is amended by introducing a new subsection (2) which intend to provide guidance on how "sixty meters" shall be measured from the water bodies which is prohibited to carry out human activities.

The Part further proposes amendment to section 184, whereby paragraph (a) is proposed to be deleted and be substituted for purpose of creating an offence of failure or refusal to conduct an Environmental Impact Assessment study in respect of projects for which environmental impact assessment study is mandatory. It is also proposed to introduce new subsection (3) which shall

provide for a penalty to an offence of failing or refusing to conduct environmental impact assessment study. The proposed penalty to such offence shall be a fine of not less than five million shillings but not exceeding one billion shillings.

Section 187 is proposed to be amended by increasing the penalty from an amount that is not less than three million and not exceeding fifty million to an amount which is not less than five million and not exceeding ten billion. The purpose of this amendment is to enhance the penalty to an offence that bring about serious adverse effects to the environment and public health arising from mining operations or oil and gas explorations.

Section 191 which provides for the general penalty for offences committed under the Act, is proposed to be amended by deleting the words "fifty million" and substituting for them the words "one billion" for the purpose of enhancing penalty for offences commited under the Act that affect the environment and public health.

This Part also proposes amendment to the Fourth Schedule which deals with the composition and proceedings of the Board of Trustees of the Fund. The amendments are intended to increase the number of members of the Board, by dding three persons with proven knowledge, skills and experience in matters relating to the operations of the Funds.
Part IV of the Bill proposes to amend the Higher Education Students' Loans Board Act, Cap. 178. The part proposes to amend section 5 by limiting the number of Board members to seven for the porpse of minimizing administration costs. Section 19 of the Act is proposed to be repealed and replaced in order to create obligation to every loan beneficiary to disclose to the employer that he is a loan beneficiary. The new section also fixes the amount of loan repayment for the beneficiaries who are self employed to an amount which is not be less than one hundred and twenty thousand shillings or fifteen percent of the taxable income.

The amendments also proposes to repeal and replace section 20 for the purpose of imposing a mandatory requirement to employer to notify the Board about employment of any person who is a holder of degree or diploma and to deduct monthly installments form salaries of loan beneficiaries. The provision also intends to treat deduction as statutory and make such deductions as first charge over non statutory deductions. Section 21 of the Act is also proposed to be repealed and replaced for the purpose of introducing penalty to employers who fails to remit monthly installments after deductions.

The Bill further proposes to amend the Schedule by adding in paragraph 4 a new subparagraph (7) with the view to empower the Board to co-opt any person to assist the Board on deliberation of any issue or matter that requires the person's skills.

Part V of the Bill proposes to amend the Public Service Act, Cap. 298 for the purpose of defining the term "Recruitment Secretariat" that word has not been defined in the Act. Section 8 is proposed to be amended in order to empower the Permanent Secretary (Establishment) to rationalize and harmonize salaries, allowance and fringe benefits in the service.

This Part also proposes to add new sections 9A that intend to prohibit public institutions, agencies, boards and commissions to review salaries and other fringe benefits for its organization.

The proposed section 9B intend to create an overriding effect in the event of conflict between the Public Service Act and any other written law.

The Bill furthet proposes to add a new section 32A that requires the public servants to exhaust all remedies provided under the Sct before seeking remedies to other laws. It is also proposed to repeal section 33 and amend section 34 to reflect the amendments of the Workers Compensation Act that has established the Workers Compensation Fund.

Part VI proposes an amendment to the Public Service (Negotiating Machinery) Act, Cap.105. Section 4(3)(b) is proposed to be amended by removing the secretary from being an appointing authority for the Public Servants comprising Service Joint Staff Council. Nevertheless, it is proposed to amend the Act by introducing new subsection (5) of section 4 so as to warrant the Miniser to appoint a Secretary from the Ministry responsible for a respective Service Scheme. Further, it is proposed to repeal section 11 so as to part with the provisions prohibiting the Service Joint Staff Councl and the Public Service Joint Staff to recommend on the matters of wages.

Part VII propose the amendments to the Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, Cap.413 by introducing a new section 40A to provide for compounding of offences. The objective of the amendment is to facilitate deterrence of offences an amicable settlement of dispute and discouragement of lengthy court trial process with a view to support continuity in trade.

Part VIII of the Bill proposes to amend the Transport Licensing Act, Cap. 317. It

proposes to amend section 11(6), 35(1), 41(1) & (2) and 42(2) with a view to change the fines prescribed in the penalties so as to make them conform with the prevailing currency.

The Bill further proposes amendment to the Act by adding a new section 47A with a view to making provisions for compounding of offences so as to facilitate deterrence of offences and amicable settlement of disputes and the discouragement of lengthy court trial process and the support of continuity in trade.

Part IX of the Bill proposes to amend the Treasury Registrar (Powers and Functions) Act, Cap. 370. Section 3 is amended in order to give the Attorney General right to intervene in any suit or matter instituted by or against the Treasury Registrar by representing him in the court accordingly. These amendments are aimed at protecting the Government's assets and interest.

Part X of the Bill proposes to amend the Weights and Measures Act, Cap. 340. It proposes general amendment to the Act in order to make appropriate usage of the term "measurement" throughout the Act, the Bill further proposes general amendment by substituting the term "assaizer" with the term "inspector", the former being the internationally recognized terminology.

The Bill further proposes amendment to section 2 by deleting and substituting some of the definitions for the purpose of making better clarification of those definition which include the terms "trade" "container".

The Bill also proposes amendment to section 19 for the purpose of making it an obligation to a person who possesses any weight, measure, weight or measuring instrument which is used or intended to be used in trade, to produce such instrument for inspection at their own instance.

Section 26 is proposed to be amended to compel a person who owns or hired to carry or transport pre-packed goods to comply with manner of packaging specified in the Schedules to the Act. The section also creates an offence for a person who contravenes the provision of this section.

Section 30 is proposed to be amended to increase the penalty from an amount that does not exceed two thousand shillings to an amount which is not less than three hundred thousand shillings. It is also proposed to amend section 46 to extend the powers of the Commissioner to compound offences under the Act with the intention of facilitating deterrence of offences an amicable settlement

of dispute and discouragement of lengthy court trial process with a view to support continuity in trade.

The Bill proposes to introduce a new section 53A that makes provision aimed at making uniformity of prescribed standards of measurement by requiring local government authorities and government agencies engaged in prescribing measurements to adopt the prescribed measurements under the Act.

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Tisa ambazo ni Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80; Sheria ya Mazingira, Sura ya 191; Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178; Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298; Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105; Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413; Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317, Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 na Sheria ya Vipimo, Sura ya 340.

Mapendekezo ya marekebisho yanalenga kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo.

Muswada umegawanyika katika Sehemu Kumi, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha, jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80. Mapendekezo hayo yanalenga kuweka kifungu kipya cha 10A kinachoipa uwezo Mamlaka kukagua au kuzuia ndege yoyote pale inapokuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba ndege hiyo inatumika kwa lengo la kukiuka mashariti ya Sheria hii.

Aidha, inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 11A kwa lengo la kukidhi matakwa ya Ibara ya 83 ya Mkataba wa Chikago. Sehemu hii pia inapendekeza kuweka kifungu kipya cha 11B illi kutekeleza masharti ya Ibara ya 25 ya Mkataba wa Chikago unaohusu utoaji wa msaada wa ndege zilizo katika hatari. Vifungu vipya vya 19A na 19B vinapendekeza kumpa mamlaka Mkugurugezi Mkuu kufuta au kuaihirisha matumizi ya cheti au leseni ya matumizi ya huduma za anga. Vile vile, Sehemu hii inapendekeza kukifanyia marekebisho kifungu cha 26 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (7) kinachoipa Mamlaka sharti la kuhakikisha kwamba wakati inapotoa huduma ya usafiri wa anga hakuna muingiliano wa majukumu yake kama mdhibiti na yale ya uendeshaji.

Sehemu ya Tatu inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mazingira, Sura ya 191, ambapo kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa haki

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kuingilia kati shauri lililofunguliwa dhidi ya Baraza au kufunguliwa na Baraza kwa kuliwakilisha mahakamani ipasavyo. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali.

Kifungu cha 57 kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) ambacho kitakuwa kinaweka mwongozo wa namna ya kupima urefu wa mita sitini kwenye kingo ya bahari, ziwa, mto au bwawa la maji kinachozuiliwa kufanyia shughuli zozote za kibinadamu. Inapendekezwa kuwa upimaji wa mita sitini utapimwa kuanzia kwenye kingo za maeneo hayo.

Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 184 ambapo kipengele (a) kinapendekezwa kifutwe na badala yake kiwekwe kifungu kipya kwa lengo kuainisha ndani ya Sheria kosa la kushindwa au kukataa kufanya tathmini ya madhara ya kimazingira pale ambapo inatakiwa kuwa ni lazima tathmini hiyo kufanyika. Inapendekezwa pia kuweka kifungu kipya cha (3) ambacho kinaweka kuweka kosa ndani ya Sheria, inapendekezwa pia kuweka adhabu ya kosa hilo ambalo linapendekezwa kuwa ni adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi bilioni moja au adhabu ya kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka saba au vyote kwa pamoja.

Kifungu cha 187 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza adhabu kutoka kiwango kisichopungua shilingi milioni tatu na kisichozidi shilingi milioni hamsini, na kuwa kiwango kisichopungua shilingi milioni tano na kisichozidi shilingi bilioni kumi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza adhabu kwa makosa ambayo yana madhara ya moja kwa moja kwenye mazingira na kwa afya za jamii kutokana na uchimbaji wa madini au utafiti wa mafuta na gesi.

Kifungu cha 191 ambacho kinatoa adhabu ya jumla kwa makosa yanayotendeka ndani ya Sheria hii. Inapendekezwa katika kifungu hicho kufutwa maneno "milioni hamsini" na badala yake kuweka maneno "milioni mia tatu" ili kuongeza adhabu kwa makosa ambayo yana madhara ya moja kwa moja kwenye mazingira na kwa afya za jamii.

Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho kwenye Jedwali la Nne ambalo linahusiana na Muundo na Mwenendo wa vikao vya Bodi ya Wadhamini wa Mfuko. Marekebisho yanalenga kuongeza idadi ya Wajumbe wa Bodi. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuongeza idadi ya Wajumbe wa Bodi ambao wanatakiwa wawe ni watu ambao wana uelewa, ujuzi na uzoefu kwenye masuala yanayohusiana na masuala ya Mifuko.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178. Sehemu hii inapendekeza kufanyia marekebisho Kifungu cha 5 kwa kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi mpaka kufikia saba kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji. Kifungu cha 19 cha Sheria kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa madhumuni ya kuweka wajibu kwa munufaika wa mkopo kumuarifu mwajiri kwamba yeye ni munufaika wa mkopo. Kifungu hiki kipya pia kinabainisha kiwango cha mkopo kinachopaswa kurejeshwa na munufaika aliyejiajiri ambapo atalipa kiasi kisichopungua shilingi laki moja na elfu ishirini au asilimia kumi na tano ya kipato chake.

Marekebisho haya pia yanapendekeza kukifuta na kukiandika upya kifungu cha 20 kwa lengo la kuweka wajibu kwa mwajiri kuitaarifu Bodi kuhusu ajira ya mtu yeyote ambaye ana Shahada au Stashahada na pia kukata makato ya mwezi kutoka kwenye Mshahara wa munufaika wa mkopo. Kifungu hiki pia kinapendekeza kufanya marejesho ya mkopo kuwa ya Kisheria na kupewa nafasi ya awali katika orodha ya makato. Kifungu cha 21 cha Sheria pia kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuweka adhabu kwa waajiri wanaoshindwa kuwasilisha marejesho ya mwezi baada ya makato.

Muswada unapendekeza kufanyiwa marekebisho katika Jedwali kwa kuongeza katika ibara 4 ibara ndogo ya (7) ili kuiwezesha Bodi kumualika mtu kuhudhuria vikao vya Bodi na kuisaidia Bodi kufikia maamuzi mbalimbali yanayohitaji maamuzi ya kitaaluma.

Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 kwa lengo la kutoa tafsiri ya neno “recruitment Secretariat”, maneno haya yametumika katika Sheria lakini hayakuwa yamepewa tafsiri. Kifungu cha 8 kinapendekeza kufanyiwa marekebisho ili kumpa mamlaka Katibu Mkuu (Utumishi) kurekebisha na kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi wa umma.

Sehemu hii pia inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 9A kinachozizuia taasisi za umma, wakala, bodi na tume zisirekebishe au kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi.

Kifungu kipya cha 9B kinachopendekezwa kinakusudia kuipa nguvu Sheria ya Utumishi wa Umma pale itakapokinzana na sheria nyingine kwenye mambo yanayohusu mishahara, posho na marupurupu ya watumishi.

Muswada pia unapendekeza kuweka kifungu kipya cha 32A kinachomtaka mtumishi kukamilisha taratibu zote za utatuzi wa migogoro ndani ya Sheria hii

kabla ya kutumia taratibu zilizoainishwa kwenye sheria nyingine. Inapendekezwa pia kukifuta kifungu cha 33 na kukirekebisha kifungu cha 34 ili kuakisi marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Waajiriwa ambayo yaliainisha Mfuko wa Fidia.

Sehemu ya Sita inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kumuondolea Katibu mamlaka ya kuteua Watumishi wa Umma wanaounda Baraza la majadiliano ya pamoja ya Watumishi wa Umma. Aidha, inapendekezwa kufanya marekebisho kwa kuingiza kifungu kidogo kipya cha (5) ili kumuwezesha Waziri kuteua Katibu kutoka Wizara yenye dhamana na kada husika ya watumishi. Vile vile, inapendekezwa kufuta kifungu cha 11 ili kuondoa masharti yanayokataza Baraza la Majadiliano ya pamoja ya watumishi na Baraza la Pamoja la Watumishi wa Umma kutoa mapendekezo kuhusiana na ujira.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413 kwa kuongeza kifungu kipya cha 40A ili kuweka masharti yanayoruhusu ulipwaji wa faini pale mkosaji anapokiri kosa badala ya kila kosa kufuata taratibu za kimahakama.

Madhamuni ya marekebisho haya ni kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro pasipo kuhusisha mchakato mrefu wa kimahakama ambao umekuwa ni kikwazo katika kuendeleza na kukuza biashara katika sekta ya usafirishaji.

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Leseni za Usafirishaji Sura ya 317. Inapendekezwa kuvifanyia marekebisho vifungu vya 11(6), 35(1), 41(1) na (2) na 42(2) kwa lengo la kurekebisha adhabu zilizobainishwa katika vifungu hivyo ili viende na wakati.

Muswada pia unapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 47A ili kuweka masharti yanayoruhusu ulipwaji wa faini pale mkosaji anapokiri kosa badala ya kila kosa kufuata taratibu za kimahakama.

Madhamuni ya marekebisho haya ni kuweka utaratibu utatuzi wa migogoro pasipo kuhusisha mchakato mrefu wa kimahakama ambao umekuwa ni kikwazo katika kuendeleza na kukuza biashara katika sekta ya usafirishaji.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370. Kifungu cha 3 kinarekebishwa ili kumpa haki Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati shauri lolote lililofunguliwa dhidi ya Msajili wa Hazina au kufunguliwa na Msajili wa Hazina kwa kumwakilisha mahakamani ipasavyo. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Vipimo, Sura ya 340. Inapendekezwa kufanya marekebisho ya jumla kwenye Sheria kwa lengo la kukuboresha matumizi ya maneno "kifaa cha kupimia" na "mkaguzi".

Kifungu cha pili kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kutoa tafsiri ya neno "chombo" na kuboresha tafsiri ya neno "biashara".

Pia Sehemu hii ya Muswada inapendekeza kukifanyia marekebisho kifungu cha 3 ili kumpa mamlaka Waziri kufanya marekebisho kwenye Majedwali ya Sheria pale itakapohitajika kufanya hivyo. Inapendekezwa kukifanyia marekebisho kifungu cha 19 ili kumtaka mtu anayemiliki kipimo au kifaaa cha kupimia uzito ambacho kinatumika au kinachokusudiwa kutumika kibiashara kukiwasilishwa kwa mkaguzi hata kama taarifa ya kufanya hivyo haikuwa imetolewa hapo awali. Marekebisho kwenye kifungu hiki pia yanalenga kuwezesha vifaa vya kupimia vikaguliwe angalao mara moja kwa mwaka tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo vifaa hivyo vilikuwa vinakaguliwa si zaidi ya mara moja kwa mwaka. Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka mmliki wa gari au mtu aliyekodishwa kubeba au kusafirisha mizigo iliyofungashwa kufuata masharti ya ufungaji wa mizigo yaliyobainishwa katika Majedwali ya Sheria hii. Kifungu hiki pia kinatoa adhabu kwa mtu anayekiuka masharti ya kifungu hiki.

Kifungu cha 30 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza adhabu kutoka kiasi kisichozidi shilingi laki mbili hadi kiasi kisichopungua shilingi laki tatu. Kifungu cha 45 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu ambayo imepitwa na wakati. Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 46 ili kumuongezea Kamishna mamlaka ya kufifilisha makosa yaliyotendwa chini ya Sheria hii kwa lengo la kuwezesha utatuzi wa migogoro kwa njia ya amani.

Pia inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha 53A kwa lengo la kuweka jukumu kwa mamlaka za serikali za mitaa na wakala wa serikali kuzingatia

vipimo vilivyobainishwa katika Sheria hii.

Dar es Salaam, **GEORGE M. MASAJU**
15 Agosti, 2016 *Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ufafanuzi wa mapendekezo ya Serikali kuhusiana na mabadiliko mbalimbali yaliyoletwa.

Kwa hiyo, tutakaporudi jioni saa 11.00 jioni tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, na Maoni ya Upinzani kuhusu mambo yaliyo hapa, vilevile tutaweza kuchangia jambo hili nitaomba umakini mkubwa katika jambo hili ili tuweze kumaliza mapema ikiwezakana leo jambo hili tuweze kulifanyia haki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa haraka nitaje wageni tulionao, wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Spika ambao ni Wabunge kutoka Malawi ambao wanatoka katika Kamati ya Uongozi ya Malawi *(House Business Committee)* ambao ni Mheshimiwa Ralph Jooma, Mheshimiwa Lobin Lowe, Mheshimiwa Isabel Tambara na Mheshimiwa Kettie Kwalira. Karibuni sana kutoka Malawi, kule Lilongwe karibuni sana; najua mnajua Kiswahili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, ambao ni wasaidizi wake kutoka Jimboni, Ndugu Kasambe Hokororo, Ndugu Audiafast Ng'ombo, Ndugu Diones Malibiche na Ndugu Laurent Muya, pale mlipo karibuni sana kutoka Ruangwa. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambao ni viongozi mbalimbali kutoka Wizara yake wakiongozwa na Profesa Adolf Mkenda, Katibu Mkuu na Wageni wengine Ndugu Ally Gugu - Mkurugenzi Idara ya Biashara, Profesa Palamagamba Kabudi - Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Ng'wanza Kamata ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Dkt. Jingu John, Mhadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; popote pale mlipo karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ni Mheshimiwa Dkt. Abdallah Sadalla ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu mpaka juzi Bunge lililokwisha ambaye alikuwa Naibu Waziri Mstaafu wa Afrika Mashariki;

Mheshimiwa Sadalla uko wapi? Karibu sana na ahsante sana Mheshimiwa Sadalla karibu sana. Pia mtakumbuka alikuwa msaidizi wa Mheshimiwa Marehemu Mzee Sitta. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 27 wa Mheshimiwa January Makamba Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Bumbuli Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga, wakiongoza na Mheshimiwa Zubeda Titu - Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bumbuli na Ndugu Ramadhani Mahanyu - Katibu wa CCM Wilaya ya Lushoto, wengine ni Makatibu wa Mheshimiwa Mbunge Jimbo la Bumbuli ambao ni Ndugu Ahmed Abdallah na Mikidaki Mgeta. Wale wageni kutoka Bumbuli msimame wote, wako wapi? Wako kulia, karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wageni Watano wa Mheshimiwa Ally Ungando ambao ni wapiga kura wake kutoka Kibiti, Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Ndugu Hassan Kirungi, karibuni sana mkirudi huko wasalimieni wa Rufiji wote. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa ambaye ni Diwani wa Kata ya Kanoni kutoka Karagwe, Mkoani Kagera Mheshimiwa Sabby Rwazo, karibu sana Mheshimiwa Diwani tumeambiwa njaa kali tukajua utakuwa umekonda sana, lakini naona umeshiba mzee. *(Makofi/Kicheko)*

Mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimboni kwake Kilolo, Mkoani Iringa, karibu Sana. Pia tunao wageni nane wa Mheshimiwa Emmanuel Papian kutoka Kiteto ambao ni wapiga kura wake, karibuni sana majirani zangu. Pia tunao wageni 51 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma. Wanamaombi pale mlipo simameni; wametoka kidogo. Kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Halima Mdee ambao ni wapiga kura wake kutoka Kawe Jijini Dar es Salaam, karibuni sana.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, ambao ni mke wake na wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Ndugu Neema Mushi, mke wa Mheshimiwa. Wageni wetu kutoka Moshi, ahsante sana na karibuni popote pale mlipo.

Pia kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Sevelina Mwijage ambao ni familia yake kutoka Bukoba, Mkoani Kagera wakiongozwa na mdogo wake Ndugu Mariam Mwijage, karibuni sana popote pale mlipo.

Wageni wengine ni wageni 17 wa Mheshimiwa Deo Sanga ambao ni Madiwani wa Halmashauri wa Mji wa Makambako kutoka Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Makambako Hanana Mfikwa, Makamu Mwenyekiti Nevy Sanga na Katibu wa Mbunge Vasco Mgunda, karibuni sana toka Makambako kule. *(Makofi)*

Wageni 19 wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Itigi kutoka Manyoni, Mkoani Singida wakiongozwa na Mheshimiwa Ally Minja ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, karibuni sana. *(Makofi)*

Mwisho ni wageni 70 kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira Arusha, ambao wamekuja kwa safari ya mafunzo. Wageni wa Makumira karibuni sana wageni wetu kutoka Makumira, mjifunze mambo ya Bunge na mtupelekee salamu nyingi sana huko Makumira. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakumbuka tulitangaza kuhusu semina ya Wizara ya Afya ambayo itatolewa katika ukumbi huu kuhusiana na maambukizi ya VVU, Kifua Kikuu na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Tunawaomba tutakapoahirisha shughuli za Bunge mbaki kwa sababu chakula kimeandaliwa kwa ajili yenu lakini kitakuwa tayari saa 9.00 alasiri na semina hii haichukui zaidi ya saa moja. Kwa hiyo, ni vizuri basi mkaunganisha mkitoka hapo mnapata chochote kitu kabisa. Maana tukiwaruhusu muondoke saa hivi itakuwa tena imekuwa taabu kidogo, kwa hiyo tunaomba uvumilivu wenu.

Matangazo ya kazi Makamu Mwenyekiti Umoja wa Bunge Wanawake Tanzania *(TWPG)* Ndugu Susan Lyimo anaomba wanawake wa Bunge wote baada ya semina hii ya Wizara ya afya mkutane pale *dispensary* ya zamani Ukumbi wa Msekwa kuna ujumbe wenu maalum pale.

Mheshimiwa Anna Lupembe Mwenyekiti wa Ibada ya Makanisa ya *CCT* anawaomba kwamba baadaye hapo, baada ya semina hizi wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma watapenda mshirikiane nao katika ukumbi ambao mnafanyia ibada siku zote.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Khatib Haji alinichokoza kidogo akasema nimekuwa mtoro kidogo, nikaona ninyamaze lakini sasa nimjibu kidogo. Sijawa mtoro hata kidogo, nipo, nipo kabisa muda mwingi nakuwepo ofisini na mambo yote yanayoendelea tuko pamoja lakini hamnioni mara kwa mara kwa sababu za kimkakati tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, afya yangu kwa sasa imetengemaa haina mashaka yoyote naweza kuongoza kikao kutwa nzima bila mashaka yoyote yale. Ninafanya hivi kwa sababu nyingi; mimi ni mwanafunzi wa Marehemu Mzee Sitta katika shughuli hizi na yeye alikuwa katika baadhi ya mambo aliyokuwa anayaamini sana ni kujenga tuseme *succession* hivi kuhakikisha kwamba unajenga wenzako ili nao siku moja wawe kama wewe au wazidi hata wewe, unapokuwa kiongozi lazima utoe nafasi au siyo jamani? Kwa hiyo, ninachokifanya ni kutoa fursa ili kujenga misingi ambayo hata kesho na kesho kutwa Ndungai hayupo basi Bunge linaendelea kuwa imara zaidi. *(Makofi)*

Basi baada ya maelezo hayo naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni leo lakini baada ya hapa nawaomba muendelee kubaki ili Wizara ya Afya i-*take over* na baadae mwendelee. Ahsante sana.

*(Saa 7.27 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya njema na kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Pia kwa niaba ya wanasheria wenzangu nichukue fursa hii kutoa pole kwa mama yetu Margaret Sitta kwa kupotelewa na Mwanasheria mwenzetu ambaye katika *roll* ya Mawakili yeye yupo katika *roll* ya awali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Januari 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya 2016 (*The Written Laws Miscellaneous Amendment)* No. 3 of 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba ya Sheria iliupokea Muswada huu tarehe 13 Septemba, 2016 ili iufanyie kazi na mnamo tarehe 18 Oktoba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusu sababu na madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho katika sheria tisa mbalimbali kwa madhumuni ya kuondoa upungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho ni:

(i) Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 *(The Civil Aviation Act Cap. 8)*

(ii) Sheria ya Mazingira, Sura ya 191 *(The Environment Management Act, Cap. 191);*

(iii) Sheria ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 *(The Higher Education Student Loans Board Act);*

(iv) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 *(The Public Service Act);*

(v) Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105 *(The Public Service Negotiating Machinery Act)*

(vi) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura 413 *(The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act);*

(vii) Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317 *(The Transport Licensing Act);*

(viii) Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370; na

(ix) Sheria ya Vipimo, Sura ya 340.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Napenda Kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu. Naomba kutambua mchango wa wadau wafuatao:-

(i) Chama cha Mawakili Tanganyika *(TLS)*;

(ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(Legal and Human Right Centre);*

(iii) Chama cha Wamiliki Mabasi Tanzania *(TABOA);*

(iv) Chama cha Wamiliki Malori Tanzania *(TATOA);*

(v) Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(TAWLA)*;

(vi) Chama cha Wanasheria wa Mazingira Tanzania *(LEAT)*;

(vii) Jumuiya ya Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Sekta ya Afya (*TUGHE)*;

(viii) Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)*;

(ix) Mabalozi wa Usalama Barabarani Tanzania *(RSA)*;

(x) Chuo Kikuu Dodoma;

(xi) Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini;

(xii) Chuo cha Biashara, Tawi la Dodoma; na

(xiii) Wenyeviti wa Kamati za Kisekta za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika kazi ya uchambuzi wa Miswada ya Sheria ya Mabadiliko ya Sheria zilizopita, Kamati iliona kuna haja kwa wakati huu kuzishirikisha Taasisi za Serikali ambazo zinaguswa moja kwa moja na Sheria zinazobadilishwa ili Kamati ijiridhishe vya kutosha kuhusu Lengo na Kiini cha Mabadiliko haya *(Letter and Spirit of the Law)* na uamuzi huu wa Kamati uliongeza tija kubwa sana kwa Kamati katika kufanya uchambuzi wa sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huu Kamati inapenda kuzishukuru sana Taasisi zote za Serikali kama Mamlaka ya Udhibiti ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)*, Baraza la Mazingira la Taifa *(NEMC)*, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania, Ofisi ya Msajili Mkuu wa Hazina na Mamlaka ya Udhibiti wa Anga Tanzania *(TCAA)* ambazo zilifika mbele ya Kamati kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutoa maelezo ya kitaalam pale yalipohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na madhumuni ya Muswada huu wa marekebisho ya sheria yametajwa kwa kina katika hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na katika ukurasa wa 23 wa Muswada huu. Kwa faida ya muda na kwa ridhaa yako, naomba malengo na madhumuni ya Muswada kama yalivyo kwenye taarifa ya Kamati yaingie kwenye *Hansard* na uniruhusu sasa niendelee

moja kwa moja sehemu ya tatu ya taarifa hii inayohusu uchambuzi wa jumla wa Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana kwa karibu na Idara ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari na Sekretariati ya Kamati, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu wa Sheria kwa kupitia vifungu vyote 50 vya Muswada tarehe 17 Oktoba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya mapitio ya vifungu vyote na kujiridhisha na malengo na madhumuni ya sheria zinazobadilishwa katika Muswada huu. Kamati ilipokea hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mnamo tarehe 18 Oktoba, 2016 ambaye alieleza Kamati kinagaubaga kuhusu sababu za mapendekezo ya mabadiliko haya ya sheria kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia tarehe 19 mpaka 21 Oktoba, 2016, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Taasisi za Elimu ya Juu, Vyama vya Wafanyakazi, Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi ili kusaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kitaalam wa kisheria kwa kuchambua sheria mbalimbali zinazofanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa mabadiliko ya sheria zilizomo ndani ya Muswada huu na kwa sababu Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 imeruhusu Kamati kumwalika mtu yeyote kutoa maoni yake mbele ya Kamati, Kamati iliona kuna haja ya Muswada huu kuziita pia Taasisi za Serikali mbele ya Kamati ili kusaidia kutoa maelezo ya msingi pale yanapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu ulisaidia sana katika kufanya uchambuzi wa maoni ya wadau kutoka sekta zote. Kwa mfano maelezo yaliyotolewa na *SUMATRA*, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Mazingira yalisaidia sana katika kurahisisha uchambuzi wa Kamati katika maeneo yanayogusa Taasisi hizi katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maoni mbalimbali ya wadau kwa muda wa siku tatu mfululizo Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya wadau kwa kina ili kujiridhisha na maudhui yake. Kamati iliyapokea baadhi ya maoni ya wadau na kuyaacha mengine kwa sababu mbalimbali. Siku ya Jumanne tarehe 25 Oktoba, 2016, Kamati ilikutana na mtoa hoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kumpa nafasi kujibu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi iliofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikubaliana na mapendekezo ya Kamati. Yapo pia maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali kwa mfano ilikubali kuweka tafsiri ya Kisheria ya neno *Highest Water Mark* katika kifungu cha 11 cha Muswada. Katika Ibara ya 15, Serikali ilikubali kubadili Wajumbe wa Bodi ya Usimamizi wa Mazigira kutoka 11 na kuwa tisa na kupunguza Wajumbe wa Sekta Binafsi kutoka watatu waliopendekezwa na Serikali na kuwa mmoja iliyopendekezwa na Kamati ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Bodi na kuokoa pesa za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 17, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kuongeza Wajumbe wawili katika Bodi ya Mikopo, mmoja kutoka Wizara ya Elimu ya Zanzibar inayohusika na Elimu ya Juu na mwakilishi kutoka *NACTE* (Baraza la Taifa la Ithibati katika Elimu ya Ufundi) ambalo linahusika katika udahili wa Wanafunzi ya Elimu ya Ufundi kwa Vyuo vilivyo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi haya ni baadhi ya maeneo ambayo Serikali na Kamati zilikubaliana japokuwa mijadala iliendelea na baadaye Kamati pamoja na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikaa ilikutana na kujadiliana kuhusiana na jedwali la marekebisho ambayo kwa ujumla Kamati na Serikali ilikubaliana kwa hoja zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakukua na masuala yoyote yaliyoibua hoja za msingi kati ya Kamati na Serikali katika kifungu cha kwanza, pili, tatu, tano, sita mpaka kifungu cha 10, 16, 21, 22, 25, 28, 29, 30, 31, 32, 34, 39, 41, 42, 43, 46, 47 pamoja na kifungu cha 50. Baadhi ya hivi vifungu ni vya muundo zaidi yaani *Construction Provisions* na havina madhara katika maudhui ya Muswada na baadhi ya vifungu ni vya kimaudhui lakini visivyo na madhara katika kuathiri malengo na madhumuni ya Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo Kamati na Serikali hayakufikia muafaka. Kwa mfano, Kamati haikubaliani na pendekezo la Serikali kumtaka mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu kuanza kulipa deni la mkopo mara tu baada ya kuhitimu masomo yake kama inavyopendekezwa katika Kifungu cha 18 cha Muswada ambacho kinaweka kifungu kipya cha 19(1)(2)(a) kinachobeba pendekezo hili. Hata hivyo, naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba baada ya majadiliano pia Serikali ilikubali maoni ya Kamati na hapakuwa tena na mvutano kuhusiana na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikubaliani na mapendekezo pia ya Serikali kutoa adhabu kubwa za faini na vifungo kwa waajiri pale wanaposhindwa kutoa taarifa za wadaiwa wa mikopo au wanapozuia Bodi ya Mikopo au wakala wake kupata taarifa za wadaiwa wa mikopo kama inavyopendekezwa katika Ibara ya 19 ya Muswada huu. Baada ya majadiliano Serikali ilikubali pia kuondoa baadhi ya maneno ambayo Kamati iliona hayakufaa na pia kufanya marekebisho ambayo Kamati ilikubaliana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia haikukubaliana na Serikali kuhusu faini zinazopendekezwa na Serikali katika Ibara za 33, 34, 35, 36, 37 na 38 za Muswada. Vifungu hivi kwa ujumla vinaongeza mzigo mkubwa kwa wamiliki, wafanyakazi na wanufaikaji wa Sekta ya usafirishaji nchini na Kamati kwa kila kifungu ilipendekeza adhabu ambazo ni chini ya zile zilizopendekezwa na Serikali. Pia naomba nichukue fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilikaa pia na Serikali na kukubaliana katika maeneo haya na pia hakukuwa na mjadala tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na masuala mengine ya kimaudhui, Kamati iligundua kwamba kuna makosa mbalimbali ya kisanifu na uchapaji katika Muswada huu ambayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilitakiwa kurekebisha ili Muswada huu usomeke vizuri zaidi. Kwa mfano katika Kifungu cha 40 cha Muswada, Kifungu kinachobadilishwa ni Kifungu cha tatu (3) cha Sheria yaani *Principal Act,* lakini maelezo ya pembeni ya Muswada *Marginal Notes* yanaonyesha kwamba kifungu kinachobadilishwa ni Kifungu cha 46. Kifungu sahihi kinachotakiwa kubadilishwa katika maelezo ya pembeni ni Kifungu cha tatu (3) ambacho kimetajwa katika Kifungu cha 40 na siyo kifungu cha 46 kama kilivyo katika maelezo ya pembeni ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo pia makosa mengine ya kisanifu ambayo Kamati iliishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuyarekebisha ili lugha na uandishi iwe sanifu. Kwa mfano katika Kifungu cha 35(6), badala ya neno *commit* neno sahihi ni *commits* na Kamati ilishauri makosa kama haya yarekebishwe. Makosa ya namna hii yametokea katika baadhi ya vifungu kama 38 kifungu kipya cha 47(A)(4) ambapo neno *may enforced* limeandikwa kimakosa badala ya neno *may enforce*. Haya ni makosa ya uchapaji ambayo kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itakaa na kufanya kazi kwa umakini yanaweza kuepukika kabla ya Muswada haujasomwa Bungeni tena kwa mara nyingine kabla Muswada haujajadiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifungu ambavyo vilibeba maudhui ya msingi ambavyo Kamati ilihitaji majadiliano ya kina na Mwanasheria Mkuu wa Serikali

ni kifungu cha nne, tisa, 11, 12, na kifungu cha 13, pia 14, 15, 17, 18, 19, 20, 23, 24, 26, 27, 33, 35, 36, 37, 38, 40, 44, 45, 48 na 49. Vifungu hivi ndivyo vilivyobeba malengo na maudhui ya mabadiliko ya Sheria hizi na vilihitaji majadiliano ya kutosha kati ya Kamati na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mashauriano kati ya Kamati na Serikali, Serikali ilikubali kuondoa na kubadilisha baadhi ya vifungu na kuviboresha vingine. Kamati pia ilikubaliana na Serikali katika mapendekezo ya Mabadiliko katika Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80, Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105, Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 na Sheria ya Mazingira, Sura ya 191.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kumuunganisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kesi zinazohusiana na Baraza la Taifa la Mazingira, Mamlaka ya Anga Tanzania na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Hatua hii itatoa haki kwa Mwanasheria Mkuu wa Sheria kuingia katika mashauri ambayo yana maslahi kwa Serikali na yatatoa wajibu kwa taasisi husika kutoa taarifa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama zimeshtakiwa au kuna kusudio la kushtakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ambazo Kamati iliitaka Serikali kufanya mabadiliko na kuleta Jedwali la Mabadiliko ni zifuatazo; Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178; Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298; Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413; na Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mashauriano yaliyoendelea kati ya Serikali na Kamati mpaka kufikia siku ya jana na ahadi ya Serikali kuandaa Jedwali la Marekebisho, naomba sasa kabla ya kutoa maoni yangu nikiri kwamba, Serikali imefanya marekebisho yote ambayo Kamati ilitaka iyafanye. Naomba sasa nitoe maoni ya mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria, Na.3 kwa mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Kutokana na uchambuzi huu Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura 80; Kamati inapendekeza kuwekwe utaratibu maalum katika Kanuni utakaoainisha namna ambavyo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Anga atakavyokagua ama kuzuia ndege yoyote pale anapokuwa na sababu ya kuamini kwamba ndege hiyo imekiuka masharti ya Sheria. Pia Kamati ilipendekeza kuwepo utaratibu wa mtu

kulalamika endapo ataona ameonewa kutokana na maumivu au maamuzi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Mazingira, Sura 191; Kamati ilishauriana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na tafsiri ya neno *The Highest Water Mark* kama ilivyotumika katika Kifungu cha 11 cha Muswada huu ili yapewe tafsiri ili kuondoa mkanganyiko wowote unaoweza kujitokeza katika upimaji wa hizo mita 60.

Kamati inatambua kwamba upimaji wa hizi mita ni suala la kitaalam na linahitaji tafsiri ya kitaalam pia. Hata hivyo, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, tafsiri iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikubaliana na Kamati na hakukuwa na mgogoro wowote kuhusiana na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya mwananchi kufika katika maeneo yaliyotolewa katazo la kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 na hasa maeneo ya fukwe za bahari, mito ama ziwa ilindwe katika sheria. Hayo ni miongoni mwa maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 12 cha Muswada Kamati pia ilishauri kifungu hicho kiandikwe upya kwa sababu baada ya kuyaingiza marekebisho ya Serikali kitakaposomwa kitatoa maana yenye mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vifungu vya 13 na 14 vya Muswada, Kamati inashauri adhabu za faini zilizotajwa katika vifungu hivi iendane na hasara iliyosababishwa na mhusika. Hii inaendana na Kanuni muhimu sana katika usimamizi wa mazingira yaani Kanuni ya *Polluter Pays Principal* ambayo inamtaka mchafuzi wa Mazingira alipe fidia kulingana na uharibifu alioufanya. Kamati inafahamu kwamba kuna Makampuni makubwa katika Sekta ya Mafuta, Gesi na Madini ambayo yanaweza kufanya uharibifu mkubwa wa mazingira ambao hauendani na kiwango cha adhabu kilichowekwa kwenye vifungu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 15 ya Muswada Kamati pia ilishauri aongezwe Mjumbe mmoja badala ya watatu kutoka katika Sekta Binafsi katika Bodi ya Mfuko wa Usimamizi wa Mazingira. Kamati pia inaamini kwamba kuongeza Wajumbe watatu kutoka katika Sekta Binafsi katika Bodi hakutaongeza tija katika Bodi bali kutaongeza gharama za uendeshaji wa Bodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178, katika Kifungu cha 17 cha Muswada, Kamati ilishauri

katika Muundo wa Bodi ya Mikopo wa Wanafuzi wa Elimu ya Juu waongezwe Wajumbe wawili yaani Mjumbe mmoja kutoka Wizara ya Elimu ya Zanzibar na Mjumbe mmoja kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi yaani *NACTE* kwa sababu Wizara ya Elimu Zanzibar ndiyo Wizara Mama inayohusika na Elimu ya Juu kwa upande wa Zanzibar na *NACTE* kama ilivyo *TCU* inahusika pia na usimamizi wa vyuo na wanafunzi katika Vyuo vya Ufundi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 18 cha Muswada kuhusu muda wa mnufaika wa mkopo kurejesha mkopo, Kamati pia ilishauri kwamba muda wa mnufaika kurejesha mkopo uwe mwaka mmoja baada ya kumaliza masomo. Hii itatoa fursa kwa mnufaika wa mkopo kujiweka tayari kabla ya kuanza kulipa mkopo wake. Utaratibu huu unatumika katika nchi nyingi kama vile Kenya na Zambia. Pia naomba nichukue fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilikubaliana na maoni haya ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanufaika wa mkopo waliojiajiri, Kamati pia ilipendekeza kiwango cha kurejesha mkopo kisipungue Sh. 100,000 za Tanzania badala ya Sh. 120,000 kama ilivyopendekezwa na Serikali. Hata hivyo, nichukue fursa hii kukujulisha kwamba Serikali ilikubaliana na maoni haya ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipendekeza pia adhabu ya kulipa faini katika Ibara ya 21(4) kwa mtu yeyote atakayewazuia Maofisa wa Bodi ama Mawakala wa Bodi katika utekelezaji wa mujukumu yake ipungue kutoka shilingi milioni saba mpaka shilingi milioni tatu ama kifungo kwenda jela kutoka kifungo cha miezi 12 na kuwa miezi sita. Pia naomba nijulishe Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilikubaliana na maoni haya ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 20(3) ilipendekezwa kuweka utaratibu wa kumshirikisha Mwajiri kabla Bodi ama Mawakala wa Bodi kufanya ukaguzi kwa madhumuni ya kutafuta taarifa za wanufaika wa mkopo katika Ofisi za Waajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 20(4) kinatoa adhabu za faini ya shilingi milioni saba au kifungo cha miezi 12 jela au vyote kwa pamoja kwa mwajiri atakayeshindwa kutoa taarifa za mhitimu wa stashahada kwa mujibu wa sheria hii. Kamati haikukubaliana na kifungu hiki na iliishauri Serikali kifungu hiki kipitiwe upya kwa sababu kinatoa majukumu yasiyotekelezeka kwa waajiri na kinaweza kuleta usumbufu mkubwa usio wa lazima kwa waajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilijulishe Bunge lako Tukufu Serikali pia ilipitia maoni ya Kamati na kukubaliana na maoni yale ya Kamati yaliyotolewa.

Pia Kamati ilishauri kwamba, majukumu ya kutoa taarifa kwa Bodi ya Mikopo yawe kwa wadaiwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 21 cha Muswada Kamati inashauri kwamba mwajiri asipewe mzigo au jukumu la kufuatilia mwenendo wa malipo ya kurejesha mkopo ya mwajiriwa wake katika Bodi ya Mikopo. Kamati ilishauri Bodi ya Mikopo pia iweze kufanya marekebisho kwa namna hiyo ili iweze kuleta unafuu kwa mwajiri na si kuleta usumbufu kwa mwajiri. Endapo kifungu hicho kitabaki kama kilivyo inaweza kupelekea waajiri kuanza kuajiri waajiriwa wasiokuwa na mikopo ili kuepukana na usumbufu unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298, Kamati ilipendekeza kwamba, ili kulinda dhana ya mgawanyo wa madaraka Tume ya Utumishi wa Bunge na Tume ya Utumishi wa Mahakama zipewe uhuru katika kusimamia upangaji wa mishahara, posho na marupurupu mengine. Katika hili Kamati inapendekeza Kifungu kipya kidogo cha 3 ambacho kitasomeka kama ifuatavyo *''The provisions of subsection 1 and 2 shall not apply to the Parliamentary Service Commission and Judicial Services Commission"*.

Katika Kifungu cha 24, kinachopendekezwa Kifungu cha 9(b) Kamati ilishauri iongezwe sentensi mwishoni inayosomeka *"save for the National Assembly Administration Act, CAP 115 and the Judicial Administration Act"*. Lakini pia naomba nichukue fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, ushauri uliotolewa na Kamati Serikali iliupokea na kufanya marekebisho makubwa ambayo Kamati inakubaliana nayo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 26 cha Muswada, Kamati inapendekeza Kifungu kipya cha 32(a) kilicholetwa na Serikali kitumike kwenye masuala ya kinidhamu tu ili kuondoa urasimu unaoweza kutokea katika kutatua haki za Watumishi wa Umma endapo mtumishi akiamua kwenda mahakamani moja kwa moja.

Kamati pia ilishauri Sheria ya Utumishi wa Umma isiwe ndiyo Sheria mama katika utatuzi wa migogoro inayowahusu Watumishi wa Umma ili kutoa wigo mpana wa Kisheria kwa Watumishi wa Umma. Kwa muktadha huu Kamati pia ilishauri sentensi inayosomeka *''Any other written law''* isomeke baada ya neno *''Act"* katika kifungu cha 32(a) kinachoongezwa. Vile vile naomba nichukue fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ilikaa na Serikali na kukubaliana marekebisho ambayo yalifanywa na Serikali katika kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura 413; Kamati ilitaka Serikali kutoa ufafanuzi wa kina kuhusiana na suala la ufifilishaji wa makosa *(Compounding of Offences)* na ilishauri endapo mtu atakiri kosa na kuamua kulipa faini kama iliyopendekezwa katika Muswada, basi faini hiyo ikalipwe mahakamani wakati wa siku za kazi na siyo *SUMATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kupunguza mianya ya rushwa inayoweza kujitokeza na utaratibu kama huu unatumika nchini India. Pia niijulishe Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilikubaliana na Serikali mapendekezo haya na kwamba, Serikali ilikubali malipo hayo yasifanywe barabarani na badala yake yalipwe katika ofisi za *SUMATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317, katika Kifungu cha 35 cha Muswada Kamati inashauri kwamba adhabu ya kutaifisha gari kwa kushindwa kuwa na leseni ya usafirishaji ifutwe. Kama adhabu hii itapitishwa itakua ni hasara kubwa na mzigo kwa wamiliki wa magari. Hii inakinzana na Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatoa haki ya kila mtu kumiliki mali na haki ya hifadhi mali aliyonayo kwa mujibu wa Sheria. Ibara ya 24(2) ya Katiba inaweka marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali kwa madhumuni ya kutaifishwa au madhumuni mengine bila idhini ya Sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na kifungu hiki chote kilifutwa ili sasa Ibara ya 24(1) pamoja na Ibara ya 24(2) kiweze kuendelea kuwasaidia Watanzania katika kumiliki mali. Kamati pia inashauri kuwekwa utenganisho wa adhabu kwa madereva wa vyombo vya usafirishaji na adhabu kwa wamiliki wa vyombo vya usafirishaji kwa kuwa kumuadhibu mmiliki wa chombo cha usafirishaji kwa kosa la dereva siyo haki na haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipokea na kukubali ombi la Serikali kufanya mabadiliko katika Kifungu cha tatu (3) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo, Sura ya 178 ili kutoa nafasi kwa Wanafunzi wa Stashahada au Stashahada ya Juu kupewa mikopo katika maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana ataamua kutoka muda mpaka muda kutokana na vipaumbele vilivyopo katika Sera na Mipango ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ya mapendekezo ya Serikali ni kutokana na uhaba mkubwa ulioonekana wa Watumishi wa ngazi za kati hasa mafundi na Sekta zingine za kitaalam kama uhandisi ukilinganisha na wataalam

wa kitaaluma waliomo katika Sekta husika. Hata hivyo, baada ya majadiliano kati ya Serikali na Kamati ilionekana kwamba, utekelezaji wa mapendekezo haya ufanyike katika Muswada wa Mabadiliko ya Sheria, Na. 4 ambao utasomwa katika Bunge hili la Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya kupendekeza hivi ni kwamba Kifungu kinachopendekezwa na Serikali hakimo katika Muswada ambao ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 13 ,2016 na ni kinyume na taratibu bora *(best practices)* za utungaji wa Sheria ambao unataka Kifungu kinachojadiliwa na uchambuzi na Kamati kiwe ni kile kilichoandikwa kwenye Muswada wa Sheria na siyo kilicho nje ya Muswada wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itaruhusu mabadiliko haya ya Sheria yasomwe katika gazeti la Serikali na kusomwa mara ya kwanza Bungeni ili Wadau wapate muda wa kutoa maoni yao ili kuendana na Sheria na Taratibu bora za Utungaji Sheria kama ilivyofanyika katika Miswada mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa mara nyingine tena naomba niishukuru kwanza Serikali kwa kukubaliana na maoni yote ya Kamati, lakini pia nikushukuru wewe mwenyewe kwa kutoa kibali na Ofisi ya Spika ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kisekta ambao walipokea barua yangu ya mwaliko kuhusu kutoa maoni juu ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zinazohusu Sekta zao wanazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue na kwa kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao wa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii. Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Wajumbe waalikwa kwa weledi na umahiri wao waliouonesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge lako Tukufu hususan Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashilillah kwa Uongozi wake thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati hii. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athman Hussein, ambaye tumekuwa naye karibu sana na Kamati; Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga; Mkurugenzi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Sheria wa ,Ndg. Pius Mboya; Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Mossy Lukuvi na Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe,

Ndg. Thomas Shawa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rachel Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia, naomba nikiri na kutambua kwamba Serikali yetu hii sikivu ilipokea maoni ya Kamati, kuyafanyia kazi na kwa ujumla wa mapendekezo yote yaliyowasilishwa na Serikali. Mapendekezo haya yote yaliyowasilishwa na Serikali yalitokana na maoni ya Kamati yetu ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unga mkono hoja, unga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA. 3) WA MWAKA 2016, THE *WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, NO 3 OF 2016* – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI:**

**1.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2016 [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.3) Act of 2016.

**1.2 Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016 Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu tarehe 13 Septemba, 2016 ili iufanyie kazi, na mnamo tarehe 18 Oktoba, 2016, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alifika mbele ya Kamati iliyoketi katika ukumbi wa Serengeti uliyopo Ofisi za Hazina Dodoma na kutoa maelezo kuhusu sababu na Madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho katika Sheria tisa (9) mbalimbali kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho ni:

(i) Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80 *(The Civil Aviation Act (Cap. 80)*

(ii) Sheria ya Mazingira, Sura ya 191 (*The Environmental Management Act (Cap.191)*

(iii) Sheria ya Mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 *(The Higher Education Student Loans Board Act (Cap.178)*

(iv) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 *(The Public Service Act (Cap.298)*

(v) Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105 *(The Public Service (Negotiating Machinery) Act (Cap.105)*

(vi) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura 413 *(The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act (Cap.413)*

(vii) Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317 *(The Transport Licensing Act (Cap .317)*

(viii) Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370 *(The Treasury Registrar (Power and Functions) Act, (Cap.370) na;*

(ix) Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 *(The Weights and Measures Act (Cap.340)*

**1.4 Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitoa matangazo katika vyombo vya habari na kuwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**1.5** Napenda Kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu. Naomba kutambua mchango wa wadau wafuatao:-

i) Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS),
ii) Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC),

ii) Chama cha Wamiliki Mabasi wa Tanzania (TABOA),
iv) Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA),
v) Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA),
vi) Chama cha Wanasheria wa Mazingira Tanzania (LEAT)
vii) Jumuiya ya Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Sekta ya Afya (TUGHE),
viii) Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),
ix) Mabalozi wa Usalama Barabarani Tanzania (RSA),
x) Chuo Kikuu Dodoma (UDOM),
xi) Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP),
xii) Chuo cha Biashara (CBE) Tawi la Dodoma na
xiii) Wenyeviti wa Kamati za Kisekta za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika kazi ya uchambuzi wa Miswada ya Sheria za Mabadiliko ya Sheria zilizopita, Kamati iliona kuna haja kwa wakati huu kuzishirikisha Taasisi za Serikali ambazo zinaguswa moja kwa moja na Sheria zinazobadilishwa ili Kamati ijiridhishe vya kutosha kuhusu Lengo na Kiini cha Mabadiliko haya (***Letter and Spirit of the Law***) na uamuzi huu wa Kamati uliongeza tija kubwa sana kwa Kamati katika kufanya uchambuzi wa Sheria hizi. Kwa msingi huu Kamati inapenda kuzishukuru sana Taasisi zote za Serikali kama Mamlaka ya Udhibiti ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), Baraza la Mazingira la Taifa (NEMC), Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania (THESLB), Ofisi ya Msajili Mkuu wa Hazina na Mamlaka ya Udhibiti wa Anga Tanzania (TCAA) ambazo zilifika mbele ya Kamati kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kutoa maelezo ya kitaalamu pale yanapohitajika.

## 2.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Katiba na Sheria inapenda kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu maelezo ya jumla ya Muswada ambayo yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati kwa kushirikiana na Idara ya Kamati za Bunge, Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria chini ya Ofisi ya Bunge na ambayo kwa sehemu kubwa yamezingatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Maelezo haya ya jumla yanaongelea malengo na madhumuni ya mabadiliko ya kila Sheria ambayo inaguswa na Muswada huu.

### SEHEMU YA KWANZA YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi kama ifuatavyo; Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha, Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada.

## SEHEMU YA PILI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya pili ya Muswada inafanyia Marekebisho Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80. Mapendekezo hayo yanalenga kuweka Kifungu kipya cha 10A kinachoipa uwezo Mamlaka kukagua au kuzuia ndege yoyote pale inapokuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba ndege hiyo inatumika kwa lengo la kukiuka mashariti ya Sheria hii. Aidha, inapendekezwa kuongeza Kifungu kipya cha 11A kwa lengo la kukidhi matakwa ya Ibara ya 83 ya Mkataba wa Chicago. Sehemu hii pia inapendekeza kuweka Kifungu kipya cha 11B illi kutekeleza masharti ya Ibara ya 25 ya Mkataba wa Chicago unaohusu utoaji wa msaada kwa ndege zilizo katika hatari. Vifungu vipya vya 19A na 19B vinapendekeza kumpa Mamlaka Mkurugenzi Mkuu kufuta au kuaihirisha matumizi ya cheti au leseni ya matumizi ya huduma za Anga. Vile vile, Sehemu hii inapendekeza kukifanyia marekebisho Kifungu cha 26 kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (7) kinachoipa Mamlaka sharti la kuhakikisha kwamba wakati inapotoa huduma ya usafiri wa anga hakuna mwingiliano wa majukumu yake kama ya udhibiti na yale ya uendeshaji.

## SEHEMU YA TATU YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mazingira, Sura ya 191, ambapo Kifungu cha 16 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa haki Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kuingilia kati shauri lililofunguliwa dhidi ya Baraza au kufunguliwa na Baraza kwa kuliwakilisha mahakamani ipasavyo. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali.

Kifungu cha 57 kinarekebishwa kwa kuongeza Kifungu kidogo cha (2) ambacho kitakuwa kinaweka mwongozo wa namna ya kupima urefu wa mita sitini kwenye kingo ya bahari, ziwa, mto au bwawa la maji kinachozuiliwa kufanyia shughuli zozote za kibinadamu. Inapendekezwa kuwa upimaji wa mita sitini utapimwa kuanzia kwenye kingo za maeneo hayo.

Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho kwenye Kifungu cha 184 ambapo kipengele (a) kinapendekezwa kifutwe na badala yake kiwekwe Kifungu kipya kwa lengo la kuainisha ndani ya Sheria kosa la kushindwa au kukataa kufanya tathmini ya madhara ya kimazingira pale ambapo inatakiwa kuwa ni lazima tathmini hiyo kufanyika. Inapendekezwa pia kuweka Kifungu kipya cha (3) ambacho kinaweka kosa ndani ya Sheria inapendekezwa na kuweka adhabu ya kosa hilo ambalo linapendekezwa kuwa ni adhabu ya faini isiyopungua

Shilingi Milioni Tano lakini isiyozidi Shilingi Bilioni Moja au adhabu ya kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka saba au vyote kwa pamoja.

Kifungu cha 187 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza adhabu kutoka kiwango kisichopungua Shilingi Milioni Tatu na kisichozidi Shilingi Milioni Hamsini, na kuwa kiwango kisichopungua Shilingi Milioni Tano na kisichozidi Shilingi Bilioni Kumi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza adhabu kwa makosa ambayo yana madhara ya moja kwa moja kwenye mazingira na kwa afya za jamii kutokana na uchimbaji wa madini au utafiti wa mafuta na gesi.

Kifungu cha 191 kinatoa adhabu ya jumla kwa makosa yanayotendeka ndani ya Sheria hii. Inapendekezwa katika kifungu hicho kufutwa maneno "Milioni Hamsini" na badala yake kuweka maneno "Milioni Mia Tatu" ili kuongeza adhabu kwa makosa ambayo yana madhara ya moja kwa moja kwenye mazingira na kwa afya za jamii.

Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho kwenye Jedwali la Nne ambalo linahusiana na Muundo na Mwenendo wa vikao vya Bodi ya Wadhamini wa Mfuko. Marekebisho yanalenga kuongeza idadi ya Wajumbe wa Bodi. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuongeza idadi ya Wajumbe wa Bodi ambao wanatakiwa wawe ni watu wenye uelewa, ujuzi na uzoefu kwenye masuala yanayohusiana na masuala ya Mifuko.

**SEHEMU YA NNE YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178. Sehemu hii inapendekeza kufanyia marekebisho Kifungu cha 5 kwa kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi mpaka kufikia saba kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji. Kifungu cha 19 cha Sheria kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa madhumuni ya kuweka wajibu kwa mnufaika wa mkopo kumuarifu mwajiri kwamba yeye ni mnufaika wa mkopo. Kifungu hiki kipya pia kinabainisha kiwango cha mkopo kinachopaswa kurejeshwa na mnufaika aliyejiajiri ambapo atalipa kiasi kisichopungua Shilingi Laki Moja na Elfu Ishirini au asilimia kumi na tano ya kipato chake.

Marekebisho haya pia yanapendekeza kukifuta na kukiandika upya Kifungu cha 20 kwa lengo la kuweka wajibu kwa Mwajiri kuitaarifu Bodi kuhusu ajira ya mtu yeyote ambaye ana Shahada au Stashahada na pia kukata makato ya mwezi kutoka kwenye Mshahara wa mnufaika wa mkopo. Kifungu hiki pia kinapendekeza kufanya marejesho ya mkopo kuwa ya Kisheria na kupewa

nafasi ya awali katika orodha ya makato. Kifungu cha 21 cha Sheria pia kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa lengo la kuweka adhabu kwa waajiri wanaoshindwa kuwasilisha marejesho ya mwezi baada ya makato.

Muswada unapendekeza kufanyiwa marekebisho katika Jedwali kwa kuongeza katika Ibara ya (4) Ibara ndogo ya (7) ili kuiwezesha Bodi kumualika mtu kuhudhuria vikao vya Bodi na kuisaidia Bodi kufikia maamuzi mbalimbali yanayohitaji maamuzi ya kitaaluma.

**SEHEMU YA TANO YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 kwa lengo la kutoa tafsiri ya neno "recruitment Secretariat", maneno haya yametumika katika Sheria lakini hayakuwa yamepewa tafsiri. Kifungu cha 8 kinapendekeza kufanyiwa marekebisho ili kumpa Mamlaka Katibu Mkuu (Utumishi) kurekebisha na kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengine kwa Watumishi wa Umma.

Sehemu hii pia inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 9A kinachozizuia Taasisi za Umma, Wakala, Bodi na Tume kurekebisha au kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi.

Kifungu kipya cha 9B kinachopendekezwa kinakusudia kuipa nguvu Sheria ya Utumishi wa Umma pale itakapokinzana na Sheria nyingine kwenye mambo yanayohusu mishahara, posho na marupurupu ya watumishi.

Muswada pia unapendekeza kuweka Kifungu kipya cha 32A kinachomtaka mtumishi kukamilisha taratibu zote za utatuzi wa migogoro ndani ya Sheria hii kabla ya kutumia taratibu zilizoainishwa kwenye Sheria nyingine. Inapendekezwa pia kukifuta Kcha 33 na kukirekebisha Kifungu cha 34 ili kuakisi marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Waajiriwa ambayo yaliainisha Mfuko wa Fidia.

**SEHEMU YA SITA YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Sita inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kumuondolea Katibu Mamlaka ya kuteua Watumishi wa Umma wanaounda Baraza la majadiliano ya pamoja ya Watumishi wa Umma. Aidha, inapendekezwa

kufanya marekebisho kwa kuingiza Kifungu kidogo kipya cha (5) ili kumuwezesha Waziri kuteua Katibu kutoka Wizara yenye dhamana na kada husika ya Watumishi. Vile vile, inapendekezwa kufuta Kifungu cha 11 ili kuondoa masharti yanayokataza Baraza la Majadiliano ya pamoja ya Watumishi na Baraza la Pamoja la Watumishi wa Umma kutoa mapendekezo kuhusiana na ujira.

**SEHEMU YA SABA YA MUSWADA**

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413 kwa kuongeza Kifungu kipya cha 40A ili kuweka masharti yanayoruhusu ulipwaji wa faini pale mkosaji anapokiri kosa badala ya kila kosa kufuata taratibu za kimahakama.

Madhamuni ya marekebisho haya ni kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro pasipo kuhusisha mchakato mrefu wa kimahakama ambao umekuwa ni kikwazo katika kuendeleza na kukuza biashara katika sekta ya usafirishaji.

**SEHEMU YA NANE YA MUSWADA**

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Leseni za Usafirishaji Sura ya 317. Inapendekezwa kuvifanyia marekebisho Vifungu vya 11(6), 35(1), 41(1) na (2) na 42(2) kwa lengo la kurekebisha adhabu zilizobainishwa katika vifungu hivyo ili viendane na wakati.

Muswada pia unapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 47A ili kuweka masharti yanayoruhusu ulipwaji wa faini pale mkosaji anapokiri kosa badala ya kila kosa kufuata taratibu za kimahakama.

Madhamuni ya marekebisho haya ni kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro pasipo kuhusisha mchakato mrefu wa kimahakama ambao umekuwa ni kikwazo katika kuendeleza na kukuza biashara katika Sekta ya Usafirishaji.

**SEHEMU YA TISA YA MUSWADA**

Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370. Kifungu cha 3 kinarekebishwa ili kumpa haki Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati shauri lolote lililofunguliwa dhidi ya Msajili wa Hazina au kufunguliwa na Msajili wa Hazina kwa kumwakilisha mahakamani ipasavyo. Marekebisho haya yanalenga kulinda mali na maslahi ya Serikali.

**SEHEMU YA KUMI YA MUSWADA**

Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Vipimo, Sura ya 340. Inapendekezwa kufanya marekebisho ya jumla kwenye Sheria kwa lengo la kukuboresha matumizi ya maneno "kifaa cha kupimia" na "mkaguzi".

Kifungu cha pili kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kutoa tafsiri ya neno "chombo" na kuboresha tafsiri ya neno "biashara".

Pia Sehemu hii ya Muswada inapendekeza kukifanyia marekebisho Kifungu cha 3 ili kumpa Mamlaka Waziri kufanya marekebisho kwenye Majedwali ya Sheria pale itakapohitajika kufanya hivyo. Inapendekezwa kukifanyia marekebisho Kifungu cha 19 ili kumtaka Mtu anayemiliki kipimo au kifaa cha kupimia uzito ambacho kinatumika au kinachokusudiwa kutumika kibiashara kukiwasilisha kwa mkaguzi hata kama taarifa ya kufanya hivyo haikuwa imetolewa hapo awali. Marekebisho kwenye kifungu hiki pia yanalenga kuwezesha vifaa vya kupimia vikaguliwe angalau mara moja kwa mwaka tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo vifaa hivyo vilikuwa vinakaguliwa si zaidi ya mara moja kwa mwaka.

Kifungu cha 26 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumtaka Mmiliki wa gari au Mtu aliyekodishwa kubeba au kusafirisha mizigo iliyofungashwa kufuata masharti ya ufungaji wa mizigo yaliyobainishwa katika Majedwali ya Sheria hii. Kifungu hiki pia kinatoa adhabu kwa mtu anayekiuka masharti ya kifungu hiki.

Kifungu cha 30 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza adhabu kutoka kiasi kisichozidi Shilingi Laki Mbili hadi kiasi kisichopungua Shilingi Laki Tatu. Kifungu cha 45 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu ambayo imepitwa na wakati. Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 46 ili kumuongezea Kamishna Mamlaka ya kufifilisha makosa yaliyotendwa chini ya Sheria hii kwa lengo la kuwezesha utatuzi wa migogoro kwa njia ya amani.

Pia inapendekezwa kuongeza Kifungu kipya cha 53A kwa lengo la kuweka jukumu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala wa Serikali kuzingatia vipimo vilivyobainishwa katika Sheria hii.

**3.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kushirikiana kwa Karibu na Idara ya Mshauri Mkuu wa Bunge wa Sheria kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016 na Sekretariati ya Kamati, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu wa Sheria kwa kupitia vifungu vyote **50** vya Muswada tarehe **17/10/2016**. Baada ya kufanya mapitio ya Vifungu vyote na kujiridhisha na malengo na madhumuni ya Sheria zinazobadilishwa katika Muswada huu, Kamati ilipokea hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe **18/10/2016** ambaye aliieleza Kamati kinagaubaga kuhusu sababu za mapendekezo ya Mabadiliko haya ya Sheria kwa wakati huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kuanzia tarehe **19-21 Oktoba 2016** Kamati ilikutana na Wadau mbalimbali kutoka katika Sekta ya Umma, Taasisi za Elimu ya juu, Vyama vya Wafanyakazi, Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi ili kuisaidia Kamati kufanya uchambuzi wa kitaalamu wa Sheria mbalimbali zinazofanyiwa marekebisho katika Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kutambua Umuhimu wa Mabadiliko ya Sheria zilizomo ndani ya Muswada huu na kwa sababu Kanuni ya **84(2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 imeruhusu Kamati kumwalika mtu yeyote kutoa maoni yake mbele ya Kamati, Kamati iliona kuna haja kwa Muswada huu kuziita pia Taasisi za Serikali mbele ya Kamati ili kusaidia kutoa maelezo ya msingi pale yanapohitajika. Utaratibu huu ulisaidia sana katika kufanya uchambuzi wa maoni ya wadau kutoka sekta zote. Kwa mfano maelezo yaliyotolewa na SUMATRA, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Mazingira yalisaidia sana katika kurahisisha uchambuzi wa Kamati katika maeneo yanayogusa Taasisi hizi katika Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea maoni mbalimbali ya Wadau kwa muda wa siku tatu mfululizo Kamati ilijipa muda wa kupitia na kuchambua maoni ya wadau kwa kina ili kujiridhisha na maudhui yake. Kamati iliyapokea baadhi ya maoni ya wadau na kuyaacha mengine kwa sababu mbalimbali. Siku ya Jumanne tarehe **25/10/2016** Kamati ilikutana na mtoa hoja Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kumpa nafasi kujibu hoja mbalimbali za msingi ambazo Kamati iliziona kutokana na uchambuzi iliofanya.

**Mheshimiwa Spika**, yapo maeneo ambayo Kamati ilikubaliana na Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikubaliana na Mapendekezo ya Kamati. Yapo pia maeneo ambayo Serikali ilihitaji muda zaidi kwa ajili ya kufanya majadiliano ya ndani na kuandaa jedwali la marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa mfano ilikubali kuweka tafsiri ya Kisheria ya neno ''Highest Water Mark'' Katika Kifungu 11 cha Muswada. Katika Ibara ya 15 Serikali ilikubali kubadili Wajumbe wa Bodi ya Usimamizi wa Mazigira kutoka

Kumi na Moja (11) na kuwa (9) na kupunguza Wajumbe kutoka Sekta Binafsi kutoka Watatu (3) waliopendekezwa na kuwa 1(Mmoja) ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Bodi na kuokoa pesa za walipa kodi.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Ibara ya 17 Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kuongeza Wajumbe Wawili katika Bodi ya Mikopo, Mmoja kutoka Wizara ya Elimu ya Zanzibar inayohusika na Elimu ya Juu na Mwakilishi kutoka NACTE (Baraza la Taifa la Ithibati katika Elimu ya Ufundi) ambalo linahusika katika udahili wa Wanafunzi ya Elimu ya Ufundi kwa Vyuo vilivyo chini yake. Kwa ufupi haya ni baadhi ya maeneo ambayo Serikali na Kamati zilikubaliana.

**Mheshimiwa Spika**, Hakukua na masuala yoyote yaliyoibua hoja za Msingi kati ya Kamati na Serikali katika vifungu vya **1, 2, 3, 5, 6, 7, 8,10,16,21,22,25,28,29,30,31,32,34,39,41,42,43,46,47** na **50**. Baadhi ya hivi Vifungu ni vya Muundo zaidi (Construction Provisions) na havina madhara katika maudhui ya Muswada na baadhi ya Vifungu ni vya kimaudhui lakini visivyo na madhara katika kuathiri malengo na madhumuni ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, yapo maeneo ambayo Kamati na Serikali hayakufikia muafaka. Kwa mfano, Kamati haikubaliani na pendekezo la Serikali kumtaka mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu kuanza kulipa deni la mkopo mara tu baada ya kuhitimu masomo yake kama inavyopendekezwa katika Kifungu cha **18** cha Muswada ambacho kinaweka Kifungu kipya cha **19(1) (2) (a)** kinachobeba pendekezo hili. Pendekezo la Kamati ni kumpa muhitimu muda angalau wa mwaka mmoja ili aweze kuwa na uwezo wa kulipa mkopo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikubaliani na mapendekezo ya Serikali kutoa adhabu kubwa za faini na vifungo kwa waajiri pale wanaposhindwa kutoa taarifa za wadaiwa wa mikopo au wanapozuia bodi ya mikopo au wakala wake kupata taarifa za wadaiwa wa mikopo kama inavyopendekezwa katika Ibara ya 19 ya Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia haikukubaliana na Serikali kuhusu faini zinazopendekezwa na Serikali katika Ibara za **33, 34,35,36,37** na **38** za Muswada. Vifungu hivyi kwa ujumla vinaongeza mzigo mkubwa kwa Wamiliki, Wafanyakazi na Wanufaikaji wa Sekta ya usafirishaji nchini na Kamati kwa kila kifungu imependekeza adhabu ambazo ni chini ya zile zilizopendekezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na masuala mengine ya kimaudhui, Kamati iligundua kwamba kuna makosa mbalimbali ya kisanifu na uchapaji katika Muswada huu ambayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inatakiwa kurekebisha ili Muswada huu usomeke vizuri zaidi. Kwa mfano katika Kifungu cha **40** cha

Muswada Kifungu kinachobadilishwa ni Kifungu cha **3** cha Sheria Mama (Principal Act) lakini Maelezo ya pembeni ya Muswada (Marginal Notes) yanaonyesha kwamba kifungu kinachobadilishwa ni Kifungu cha **46.** Kifungu sahihi kinachotakiwa kubadilishwa katika Maelezo ya Pembeni ni Kifungu cha **3** ambacho kimetajwa katika Kifungu cha 40 na siyo kifungu cha **46** kama kilivyo katika Maelezo ya Pembeni ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, yapo pia makosa mengine ya kisanifu ambayo Kamati imeishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuyarekebisha ili lugha na uandishi uwe sanifu. Kwa mfano katika Kifungu cha **35(6**) badala ya neno ‘‘**commit**’’ neno sahihi ni ‘‘**commits**’’ na Kamati imeshauri makosa kama haya yarekebishwe. Makosa ya namna hii yametokea katika baadhi ya Vifungu kama **38** (Kifungu kipya cha 47A (4) (b) ambapo neno ‘‘may enforce**d’’** limeandikwa kimakosa badala ya neno ‘’may enforce’’. Haya ni makosa ya uchapaji ambayo kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itakaa na kufanya kazi kwa umakini yanaweza kuepukika kabla Muswada haujasomwa Bungeni kwa mara ya kwanza.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu ambavyo vilibeba maudhui ya msingi ambavyo Kamati ilihitaji majadiliano ya kina na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Vifungu vya **4, 9, 11, 12, 13, 14, 15, 17, 18, 19, 20, 23, 24, 26, 27, 33, 35, 36, 37, 38, 40, 44, 45, 48 na 49**. Vifungu hivi ndivyo vilivyobeba malengo na madhumuni ya mabadiliko ya Sheria hizi na vilihitaji majadiliano ya kutosha kati ya Kamati na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya mashauriano kati ya Kamati na Serikali, Serikali ilikubali kuondoa na kubadilisha baadhi ya Vifungu na kuviboresha vingine. Kamati pia ilikubaliana na Serikali katika mapendekezo ya Mabadiliko katika Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80, Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, Sheria ya Majadiliano ya Pamoja Katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105, Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 na Sheria ya Mazingira,Sura ya 191.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali Kumuunganisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kesi zinazohusiana na Baraza la Taifa la Mazingira, Mamlaka ya Anga Tanzania na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Hatua hii itatoa haki kwa Mwanasheria Mkuu wa Sheria kuingia katika mashauri ambayo yana maslahi kwa Serikali na yatatoa wajibu kwa taasisi husika kutoa taarifa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama zimeshtakiwa au kuna kusudio la kushtakiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ambazo Kamati iliitaka Serikali kufanya mabadiliko na kuleta Jedwali la Mabadiliko ni zifuatazo ; Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178, Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413 na Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mashauriano yaliyoendelea kati ya Serikali na Kamati na ahadi ya Serikali kuandaa Jedwali la Marekebisho, naomba sasa nitoe maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria, Na.3 wa Mwaka 2016.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika,**

**KATIKA SHERIA YA USAFIRI WA ANGA, SURA 80**

i) Kamati inapendekeza kuwekwe utaratibu maalumu katika Kanuni utakaoainisha namna ambavyo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Anga atakavyokagua ama kuzuia ndege yeyote pale anapokua na sababu ya kuamini kwamba ndege hiyo imekiuka masharti ya Sheria. Kamati inapendekeza kuwekwe utaratibu wa mtu kulalamika endapo ataona ameonewa kutokana na maamuzi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Anga.

**Mheshimiwa Spika,**

**KATIKA SHERIA YA MAZINGIRA, SURA 191**

ii) Kamati inashauri maneno "highest water mark'' kama yalivyotumika katika Kifungu cha 11 cha Muswada huu yapewe tafsiri katika Sheria ili kuondoa mkanganyiko wowote unaoweza kujitokeza katika upimaji wa hizo mita 60. Kamati inatambua kwamba upimaji wa hizi mita ni suala la kitaalamu na linalohitaji tafsiri ya kitaalamu pia.

iii) Haki ya Mwananchi kufika katika maeneo yaliyotolewa katazo la kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita sitini na hasa maeneo ya fukwe za bahari, mito ama ziwa ilindwe katika Sheria.

iv) Katika Kifungu cha 12 cha Muswada Kamati inashauri kifungu hicho kiandikwe upya kwa sababu baada ya kuyaingiza marekebisho ya Serikali kitakapo somwa kitatoa maana yenye mkanganyiko.

v) Katika Kifungu cha 13 na 14 ya Muswada Kamati inashauri adhabu za faini zilizotajwa katika Vifungu hivi iendane na hasara iliyosababishwa na muhusika.Hii inaendana na Kanuni Muhimu sana katika usimamizi wa Mazingira yani Kanuni ya "***Polluter Pays Principle''*** ambayo inamtaka mchafuzi wa Mazingira alipe fidia kulingana na uharibifu alioufanya. Kamati inafahamu kwamba kuna Makampuni makubwa katika Sekta ya Mafuta, Gesi na Madini ambayo yanaweza kufanya uharibifu mkubwa wa mazingira ambao hauendani na kiwango cha adhabu kilichowekwa kwenye vifungu hivi.

vi) Katika Ibara ya 15 ya Muswada Kamati inashauri aongezwe Mjumbe Mmoja badala ya Watatu kutoka katika Sekta Binafsi katika Bodi ya Mfuko wa Usimamizi wa Mazingira. Kamati inaamini kwamba kuongeza Wajumbe Watatu kutoka katika Sekta Binafsi katika Bodi hakutaongeza tija katika Bodi bali kutaongeza gharama za uendeshaji wa Bodi.

**Mheshimiwa Spika,**

**KATIKA SHERIA YA MIKOPO KWA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU, SURA YA 178**

vii) Katika Kifungu cha 17 cha Muswada Kamati inashauri katika Muundo wa Bodi ya Mikopo wa Wanafuzi wa Elimu ya Juu waongezwe Wajumbe Wawili yaani Mjumbe Mmoja kutoka Wizara ya Elimu ya Zanzibar na Mjumbe mmoja kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa sababu Wizara ya Elimu Zanzibar ndiyo Wizara Mama inayohusika na Elimu ya Juu kwa upande wa Zanzibar na NACTE kama ilivyo TCU inahusika pia na usimamizi wa vyuo na wanafunzi katika Vyuo vya Ufundi Tanzania Bara.

viii) Katika Kifungu cha 18 cha Muswada kuhusu muda wa mnufaika wa mkopo kurejesha mkopo, Kamati inashauri kwamba muda wa mnufaika kurejesha mkopo uwe mwaka mmoja baada ya kumaliza masomo. Hii itatoa fursa kwa mnufaika wa mkopo kujiweka tayari kabla ya kuanza kulipa mkopo wake. Utaratibu huu unatumika katika nchi nyingine kama Kenya na Zambia.

ix) Kuhusu wanufaika wa mkopo waliojiajiri Kamati inapendekeza kiwango cha kurejesha mkopo kisipungue Shilingi Laki Moja za Tanzania (100,000 Tshs) badala ya Shilingi Laki Moja na ishirini kama ilivyopendekezwa na Serikali.

x) Kamati inapendekeza pia adhabu ya kulipa faini katika Ibara ya 21(4) kwa mtu yeyote atakayewazuia Maafisa wa Bodi ama Mawakala wa Bodi katika utekelezaji wa mujukumu yao ipunguzwe kutoka Milioni Saba (7,000,000/=) mpaka Milioni Tatu (3,000,000/=) ama kifungo cha kwenda jela kutoka miezi kumi na mblili (12) na kuwa miezi 6.

xi) Katika Ibara ya 20(3) inapendekezwa kuwekwe utaratibu wa kumshirikisha Mwajiri kabla Bodi ama Mawakala wa Bodi kufanya ukaguzi kwa madhumuni ya kutafuta taarifa za wanufaika wa mkopo katika Ofisi za Waajiri. Kifungu cha 20(4) kinatoa adhabu ya faini ya Milioni Saba na Kifungo cha Miezi 12 jela au vyote kwa pamoja kwa mwajiri atakayeshindwa kutoa taarifa ya mhitimu wa shahada au stashahada kwa mujibu wa Sheria hii.Kamati haikubaliani na Kifungu hiki na inashauri kifungu hiki chote kifutwe kwa sababu kinatoa majukumu yasiyotekeleza kwa waajiri na kinaweza kuleta usumbufu usio wa lazima kwa waajiri. Kamati inashauri kwamba majukumu ya kutoa taarifa kwa bodi ya mikopo yawe kwa wadaiwa wenyewe.

xii) Katika Kifungu cha 21 cha Muswada Kamati inashauri kwamba mwajiri asipewe mzigo au jukumu la kufuatilia mwenendo wa malipo ya kurejesha mkopo ya mwajiriwa wake katika Bodi ya Mikopo. Kamati inashauri jukumu hili lifanywe na Bodi ya Mikopo yenyewe katika namna ambayo italeta unafuu kwa mwajiri na si kuleta usumbufu kwa mwajiri endapo kifungu hicho kitabaki kama kilivyo inaweza kupelekea waajiri kuanza kuajiri waajiriwa wasio na mikopo ili kuepukana na usumbufu unaoweza kujitokeza.

**Mheshimiwa Spika,**

**KATIKA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA, SURA 298**

xiii) Kamati inapendekeza kwamba ili kulinda dhana ya mgawanyo wa madaraka Tume ya Utumishi wa Bunge na Tume ya Utumishi wa Mahakama zipewe uhuru katika kusimamia upangaji wa mishahara, posho na marupurupu mengine. Katika hili Kamati inapendekeza Kifungu kipya kidogo cha 3 ambacho kitasomeka kama ifuatavyo ''**The provisions of subsection 1 and 2 shall not apply to the Parliamentary Service Commission and Judicial Services Commission**''. Katika Kifungu cha 24, kinachoongezwa Kifungu cha 9B Kamati inashuri iongezwe sentensi mwishoni itakayosomeka "**save for the National Assembly Administration Act, CAP 115 and the Judicial Administration Act".**

xiv) Katika Kifungu cha 26 cha Muswada, Kamati inapendekeza Kifungu kipya cha 32A kilicholetwa na Serikali kitumike kwenye masuala ya kinidhamu tu, ili kuondoa urasimu unaoweza kutokea katika kutafuta haki kwa Watumishi

wa Umma endapo mtumishi akiamua kwenda mahakamani moja kwa moja .Kamati pia inashauri Sheria ya Utumishi wa Umma isiwe ndiyo Sheria mama katika utatuzi wa migogoro inayowahusu Watumishi wa Umma ili kutoa wigo mpana wa Kisheria kwa Watumishi wa Umma. Kwa muktadha huu Kamati inashauri sentensi inayosomeka ''**Any other written law**'' isomeke baada ya neno ''Act'' katika kifungu cha 32A kinachoongezwa.

**Mheshimiwa Spika,**

**KATIKA SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI WA NCHI KAVU NA MAJINI, SURA 413**

xv) Kamati inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi wa kina kuhusiana na suala la ufifilishaji wa makosa (Compaunding of Offences), na inashauri endapo mtu atakiri kosa na kuamua kulipa faini kama iliyopendekezwa katika Muswada basi faini hiyo ikalipwe mahakamani wakati wa siku za kazi na siyo SUMATRA. Hii itasaidia kupunguza mianya ya rushwa inayoweza kujitokeza .Utaratibu kama huu unatumika nchini India.

**Mheshimiwa Spika,**

**KATIKA SHERIA YA LESENI ZA USAFIRISHAJI, SURA YA 317**

xvi) Katika Kifungu cha 35 cha Muswada Kamati inashauri kwamba adhabu ya kutaifisha gari kwa kushindwa kuwa na leseni ya usafirishaji ifutwe. Kama adhabu hii itapitishwa itakua ni hasara kubwa na mzigo kwa wamiliki wa magari. Ibara ya **24(1)** ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki ya kila mtu kumiliki mali, na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa Sheria. Ibara ya 24(2) ya Katiba inaweka marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengineyo bila idhini ya Sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili.

Kamati pia inashauri kuwekwe utenganisho wa adhabu kwa madereva wa vyombo vya usafirishaji na adhabu kwa wamiliki wa vyombo vya usafirishaji kwa kuwa kumuadhibu mmiliki wa chombo cha usafirishaji kwa kosa la dereva wake sio haki na haikubaliki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipokea na kukubali ombi la Serikali kufanya mabadiliko katika Kifungu cha tatu (3) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo, Sura ya 178 ili kutoa nafasi kwa Wanafunzi wa Stashahada au Stashahada ya Juu kupewa mikopo katika maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana

ataamua kutoka muda mpaka muda kutokana na vipaumbele vilivyopo katika Sera na Mipango ya Taifa. Hatua hii ya mapendekezo ya Serikali ni kutokana na uhaba mkubwa ulionekana wa Watumishi wa ngazi za kati hasa mafundi na Sekta zingine za kitaalamu kama uhandisi ukilinganisha na wataalamu wa kitaaluma waliomo katika Sekta husika.

Hata hivyo baada ya majadiliano kati ya Serikali na Kamati ilionekana kwamba utekelezaji wa mapendekezo haya ufanyike katika Muswada wa Mabadiliko ya Sheria, Na.4 ambao utasomwa katika Bunge hili la Tano. Sababu kubwa ya kupendekeza hivi ni kwamba Kifungu kinachopendekezwa na Serikali hakimo katika Muswada ambao ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwamba tarehe 13 Septemba 2016 na ni kinyume na utaratibu bora (**Best practices**) wa utungaji Sheria ambao unataka Kifungu kinachojadiliwa na kuchambuliwa na Kamati kiwe ni kile kilichoandikwa kwenye Muswada wa Sheria na siyo kilicho nje ya Muswada wa Sheria. Hatua hii itaruhusu mabadiliko haya ya Sheria yasomwe katika gazeti la Serikali na kusomwa mara ya kwanza Bungeni ili Wadau wapate muda wa kutoa maoni yao ili kuendana na Sheria na Taratibu bora za Utungaji Sheria kama ilivyofanyika katika Miswada Mingine.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia kazi Muswada huu. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kisekta ambao walipokea barua yangu ya mwaliko kuhusu kutoa maoni juu ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazohusu Sekta zao wanazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika**, naomba niwatambue na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria pamoja na Wajumbe Waalikwa kwa weledi na umahiri wao waliouonyesha wakati wa kuchambua Muswada huu na hatimaye kutoa mapendekezo ya msingi ya kuuboresha.

**Naomba Majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe

4. Mhe. Juma Hamadi Kombo, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
21. Mhe.Selemani Nchambi,Mb - Mjumbe
22. Mhe.Ussi Pondeza, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuu Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususan Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashilillah kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Mkurugenzi wa Ofisi ya Mshauri Mkuu wa Sheria wa Bunge Ndg. Pius Mboya, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mossy Lukuvi na Makatibu wa Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe, Ndg. Thomas Shawa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamlika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha. (*Makofi)*

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
**07 NOVEMBA 2016**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii.

**MHE. TUNDU A. LISSU – MSEMAJI MKUU KAMBI RASMI YA UPINZANI YA BUNGE KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge hili juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3), *2016*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 26 Agosti, 2016 na kusomwa kwa mara ya kwanza wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge lako Tukufu. Muswada huu ulikuwa unapendekeza marekebisho ya Sheria Mbalimbali tisa. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Usafiri wa Anga;heria ya Usimamizi wa Mazingira; Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; na Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma; Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini; Sheria ya Leseni za Usafirishaji; Sheria ya Madaraka na Majukumu ya Msajili wa Hazina; na Sheria ya Vipimo na Mizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, mapendekezo haya yanahusu sheria nyingi na muhimu. Sio hivyo tu, vifungu vinavyopendekezwa kurekebishwa katika sheria hizo ni vingi. Hivyo, kwa mfano, ukiachia vifungu kumi na moja vya kiutangulizi, Muswada huu unapendekeza kurekebisha vifungu thelathini na tisa vya msingi katika Sheria hizi tisa. Vilevile, marekebisho yanayopendekezwa yatapelekea mabadiliko makubwa ya kisera, kisheria na kitaasisi katika maeneo husika. Kwa vyovyote vile, hii siyo kazi ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inaamini kwamba, utaratibu wa kuleta marekebisho mengi ya sheria nyingi namna hii katika Muswada mmoja unalinyima Bunge lako Tukufu muda na uwezo wa kuyajadili kwa kina na kuyaelewa mapendekezo ya Serikali kabla ya kuyapitisha na kuwa sheria za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utaratibu huu sio tu ni kuligeuza Bunge lako Tukufu kuwa *rubber stamp* ya kuhalalisha maamuzi ya Serikali, bali pia unapelekea Bunge hili kupitisha sheria mbovu zinazoathiri haki za wananchi

wetu na ustawi wa Taifa letu na kusababisha migongano isiyokuwa ya lazima katika vyombo vya utekelezaji vya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, inaishauri Serikali hii ya CCM kuacha utaratibu huu mbovu wa utungaji sheria. Kwa sababu zitakazojionesha wazi hapa, tunapendekeza kuanza na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma; Muswada unapendekeza marekebisho mbalimbali katika Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwanza, inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria kuhusu tafsiri ya maneno 'Sekretarieti ya Ajira' yaliyopo katika Kifungu cha 29 cha Sheria hiyo. Pili inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 8(3) kwa kuongeza majukumu ya Katibu Mkuu Utumishi kuwa ni pamoja na "kurekebisha na kuoanisha mishahara, posho na marupurupu katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 24 ya Muswada inapendekeza marekebisho zaidi yanayohusu masuala ya mishahara ya watumishi wa umma. Kwa mfano, kifungu cha 9 cha Sheria ya Utumishi ya Umma kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuingiza kifungu kipya cha 9(a) ambacho kitaondoa mamlaka ya taasisi za umma, Wakala, Bodi au Tume ya kupitisha mishahara, posho na marupurupu mengine katika taasisi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake, kwa mujibu wa Kifungu kipya cha 9(a)(2) kinachopendekezwa, upitishaji wa mishahara, posho na marupurupu mengine katika Utumishi wa Umma yataamuliwa na Katibu Mkuu Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutilia nguvu masharti mapya yanayopendekezwa, Kifungu kipya cha 9(b) kinapendekeza kwamba, endapo kutakuwa na mgongano katika masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyinginezo, basi masharti ya Sheria hii ndiyo yatakayotiliwa nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapendekezo mengine ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa mfano, aya ya 25 ya Muswada inapendekeza kufutwa kwa Kifungu cha 20(1)(c) ambacho kinaipa Tume ya Utumishi wa Umma mamlaka ya kutunga kanuni za usaili wa watumishi unaofanywa na Tume au Bodi za Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, aya ya 26 inapendekeza kuingizwa kwa kifungu kipya cha 32(a) ambacho kitawazuia watumishi wa umma wenye

migogoro na waajiri wao kupeleka migogoro hiyo kwenye Mahakama za Kazi hadi kwanza wamalize taratibu za utatuzi wa migogoro zilizowekwa na Sheria ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, inapendekezwa kufuta Kifungu chote cha 34 cha Sheria na kuweka kifungu kipya kitakachowezesha watumishi wa umma wanaoumia au kufariki wakiwa kazini kupewa fidia kwa mujibu wa Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi. Utaratibu unaofutwa ulikuwa unampa mamlaka hayo Waziri kwa kutumia mamlaka yake ya kutunga kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Muswada huu yanayohusu usaili na fidia ya watumishi wa umma hayabadilishi sera, bali ni marekebisho yanayolenga kuboresha utekelezaji wa sera zilizopo. Kwa upande mwingine, mapendekezo ya marekebisho yanayohusu mishahara na malipo mengine ya watumishi ni mabadiliko ya kisera. Kwa sababu hiyo, mapendekezo haya yalihitaji, na yanahitaji, Muswada mahsusi wa kurekebisha Sheria ili kufanya mabadiliko ya kisera katika maeneo hayo. Tunaomba kutoa ufafanuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yake kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza kwamba "marekebisho haya yanalenga kuwa na mamlaka moja inayoratibu mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi katika Taasisi za Serikali na pia kuainisha mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi wa taasisi hizo. Suala muhimu linalohitaji majibu ni kwa nini utaratibu wa sasa hauna uwiano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya mabadiliko makubwa ya kisera yaliyofanywa na Serikali tangu miaka ya tisini, idara na taasisi nyingine za Serikali zilipewa mamlaka ya kuamua masuala ya kiutendaji ya idara na taasisi hizo. Aidha, taasisi kama vile Wakala wa Serikali *(Executive Agencies)* zilipewa mamlaka ya kujiendesha kibiashara bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Mabadiliko haya yalilenga kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika idara, wakala na taasisi hizo na *by extension*, kupunguza matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mabadiliko haya ya kisera ni kwamba mishahara, posho na marupurupu mengine, hasa watendaji wakuu na makada wa ngazi za juu wa taasisi hizo, ililipuka na kuongezeka kwa kiwango cha kutisha kwa nchi kama Tanzania. Mara tulianza kusikia Watendaji Wakuu, Wakurugenzi na Mameneja wa juu wa taasisi hizo wakilipwa makumi ya mamilioni ya shilingi kama mishahara, posho na stahiki nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara tulianza kuona mikutano ya Bodi za Wakurugenzi au Wadhamini wa Taasisi za umma ikifanyika katika nchi za kigeni kama Dubai au Afrika ya Kusini. Bila shaka Wabunge watakumbuka kashfa za Wajumbe wa Bodi za Mazao kama Korosho au Pamba au Kahawa au Chai, au Bodi za Wadhamini za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii waliokuwa wanalipwa mamilioni ya shilingi kama posho za kila siku za vikao vya bodi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilikuwa mbaya kiasi kwamba Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* alisemekana kugomea kuchukua mshahara wa zaidi ya shilingi milioni thelathini kwa mwezi kwa hoja kwamba mshahara huo ulikuwa mdogo na badala yake alifanya kazi kwa zaidi ya mwaka mmoja akilipwa posho tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, kwa sababu inazozijua yenyewe, Serikali hii ya CCM haijasema wazi kwamba marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma yanayopendekezwa, yanalenga kuondoa kashfa za aina hii katika malipo ya watumishi wa umma, ni wazi kwamba hili ndilo lengo kuu la mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hili ndio lengo la mapendekezo yanayohusu mishahara na malipo mengine ya watumishi wa umma, utaratibu unaopendekezwa unaweza kusababisha matatizo makubwa zaidi badala ya kuwa ndiyo tiba ya ugonjwa wa mishahara na malipo yasiyokuwa na uwiano katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuondoa mamlaka ya kupanga mishahara na malipo mengine kutoka kwenye taasisi husika na kuyapeleka kwa Katibu Mkuu Utumishi peke yake hakuondoi tatizo la malipo makubwa ya mishahara na posho na marupurupu ya Watendaji Wakuu na Mameneja wa Taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tatizo ni hilo, utatuzi wake unaweza kuwa kuweka viwango vya malipo hayo katika sheria au kanuni mahsusi zinazohusu idara, wakala au taasisi hizo. Mapendekezo ya marekebisho hayajaweka viwango vyovyote vya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mapendekezo haya yanarudisha ukiritimba wa madaraka (*centralization of power*) ndani ya Ofisi ya Rais na matatizo yote yanayotokana na ukiritimba wa madaraka kama vile urasimu utakaosababisha kukosekana kwa ufanisi katika utendaji wa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba lengo kubwa la *civil service reform programs* za tangu miaka ya Rais Mwinyi lilikuwa ni ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu (*Establishment*) kwenda kwenye taasisi na mashirika yanayojitegemea ili kuondoa urasimu, kuboresha ufanisi na kuongeza tija katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapendekezo haya, jitihada hizo za zaidi ya robo karne zinashambuliwa moja kwa moja. Kwa maneno mengine, mapendekezo haya yanaturudisha nyuma kwenye miaka ya Mwalimu Nyerere ambako Ikulu na Idara Kuu ya Utumishi zilikuwa ni *Alpha* na *Omega* ya kila kitu, kikubwa ama kidogo, katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya aya ya 26 ya Muswada yanaleta mabadiliko makubwa ya kisera vile vile. Itakumbukwa kwamba mwaka 2004, Bunge lako tukufu lilitunga 'Sheria za Kazi', yaani, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria ya Taasisi za Kazi. Sheria hizi mbili zilileta mabadiliko makubwa ya kisera katika masuala ya ajira na utatuzi wa migogoro ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, specifically, Sheria za Kazi zilianzisha Taasisi mpya za kutatua migogoro ya ajira zinazojulikana kwa *practitioners* kama Mahakama za Kazi, yaani Tume ya Upatanishi na Usuluhishi *(The Commission for Mediation and Arbitration)* na Mahakama Kuu, *division* ya Kazi. Kwa mujibu wa utaratibu huu, Wafanyakazi na waajiri wote wa Serikali au wa sekta binafsi wana haki ya kufungua mashauri katika Mahakama za Kazi. Kwa kiasi kikubwa, Mahakama za Kazi ziko huru katika kufanya maamuzi yake kwenye mashauri ya ajira na mahusiano kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa mapendekezo ya aya ya 26 ya Muswada, Mtumishi wa umma anayeingia kwenye mgogoro wa ajira na Mwajiri wake, hatakuwa na haki ya kwenda moja kwa moja kwenye Mahakama za Kazi kudai haki zake. Badala yake, Mtumishi huyo wa Umma atatakiwa kumaliza taratibu zote za utatuzi wa migogoro zilizopo chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Baada ya hapo ndio Mtumishi huyo wa Umma atakuwa na haki ya kwenda kwenye Mahakama za Kazi kutafuta haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, marekebisho haya yanalenga kuweka mwongozo utakaowawezesha Watumishi wa Umma kutumia kwanza utaratibu ulioainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma kabla ya kwenda katika vyombo vingine ikiwemo Baraza la Usuluhishi na Mahakama ya Kazi kwa kutumia Sheria za Kazi ambako jambo hilo linaweza kuchukua muda mrefu hiyo siyo kweli

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaopendekezwa na Muswada huu, badala ya kufupisha muda wa utatuzi wa migogoro ya ajira ya Watumishi wa umma, utarefusha muda huo zaidi na kuongeza gharama za utatuzi wa migogoro ya ajira katika Utumishi wa Umma. Kwanza, Mtumishi wa Umma aliyechukuliwa hatua za kinidhamu na Katibu Mkuu Kiongozi atatakiwa kama ni Mteule wa Rais kukata rufaa kwa Rais ambaye uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho. Hiyo ni kwa mujibu wa kifungu cha 25(1)(d) cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa mtumishi wa umma ambaye amechukuliwa hatua za kinidhamu na Katibu Mkuu, Mkuu wa Idara Inayojitegemea, Katibu Tawala wa Mkoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mkurugenzi wa Uhamiaji au na Kamishna wa Huduma za Moto na Uokoaji, mtumishi huyo anatakiwa kukata rufaa kwa Tume ya Utumishi wa Umma. Endapo hataridhika na uamuzi wa Tume, Mtumishi huyo anatakiwa kukata rufaa kwa Rais, ambaye uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho vile vile, kwa mujibu wa kifungu cha 25(1)(d) cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu unaopendekezwa na Muswada, mtumishi wa umma ambaye sasa ana haki ya kwenda moja kwa moja kwenye Mahakama za Kazi kudai haki zake, hatakuwa na haki hiyo tena. Badala yake, Mtumishi huyo wa Umma atatakiwa kwanza amalize utaratibu wa rufaa ulioelezewa hapa ndipo kama bado hajaridhika, aende kwenye Mahakama za Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi lengo la mapendekezo haya ni kuwazuia watumishi wa umma kwenda kutafuta haki katika Mahakama za Kazi ambazo ziko huru zaidi kulinganisha na utaratibu uliopo kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu haiwezi kukubaliana na mapendekezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile, kama ambavyo tumeonesha hapa, mageuzi yanayopendekezwa na Muswada huu katika masuala ya Utumishi wa Umma ni makubwa kwa sababu yanabadili mwelekeo wa sera za Serikali. Mapendekezo haya yalihitaji na bado yanahitaji, mjadala mpana zaidi ambao hautawezekana katika mazingira ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Ni Muswada mahsusi wa marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ambao ungeweza na unaweza kutoa fursa ya mjadala mpana ndani na nje ya Bunge lako Tukufu kuhusu masuala haya ya kisera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mwaka mmoja wa Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli, ni wazi sasa kwamba utumishi wa umma katika Taifa letu unakabiliwa na hatari kubwa ya kurudishwa nyuma kwa zaidi ya robo karne. Tangu utawala wa Serikali ya Rais Ali Hassan Mwinyi na hasa baada ya kurudishwa kwa mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1992, kumefanyika jitihada kubwa ya kufanya mageuzi makubwa ya kimfumo katika utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mageuzi haya yalilenga kuuondoa utumishi wa umma kutoka makucha ya mfumo wa chama kimoja cha siasa, uliojengeka toka miaka ya mwanzo ya uhuru wetu na kujenga utumishi mpya wa umma ambao umejengeka katika misingi ya uweledi yaani *professionalism* na kutofungamana na siasa za kivyama *(political non-partisanship)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Kanuni za maadili katika Utumishi wa Umma yaani *Code of Ethics and Conduct for the Public Service in Tanzania* zilizotungwa kwa mara ya kwanza tangu uhuru wakati wa utawala wa Rais Benjamin Mkapa, zilisisitiza Watumishi wa Umma kutofungamana kisiasa yaani kuwa na *political neutrality* na kuepuka ushawishi wa kisiasa yaani *political influence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ndio maana, kwa sababu ya mageuzi haya, kuna kada za utumishi wa umma ambazo zilipigwa marufuku kujihusisha na siasa za kivyama. Hivyo, kwa mfano, Ibara ya 74(14) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, imetamka kwamba, itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na chama chochote cha siasa. Watu wanaohusika na uchaguzi wametajwa kuwa ni pamoja na wasimamizi wote wa Uchaguzi katika miji na wilaya zote na kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Taifa, kila Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya atakuwa ni msimamizi wa uchaguzi kwa minajili ya kuendesha uchaguzi wa jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa makatazo haya ya Kikatiba yamewekwa kando na utawala huu wa Rais Magufuli. Mfano mzuri ni uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmashauri za Mitaa uliofanywa na Rais Magufuli mwezi Julai mwaka huu. Katika uteuzi huo, kati ya watu 195 walioteuliwa kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri na kwa hiyo Wasimamizi wa Uchaguzi, Wateule 62 walikuwa Wagombea Ubunge wa Chama cha Mapinduzi katika hatua ya kura za maoni majimboni au kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wateule wengine watano waligombea nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya CCM mwaka 2012. Wawili waligombea uteuzi wa nafasi ya Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano kwa tiketi ya CCM

mwaka 2015 na mmoja alikuwa Mgombea Ubunge wa chama cha *ACT*. Ndiyo kusema kwamba takriban asilimia 36 ya wateule wote wa nafasi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa hawana sifa za Kikatiba na kisheria za utumishi wa umma katika nafasi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio tu kwamba misingi ya *political neutrality* na *meritocratic principles* katika uteuzi wa Watumishi wa Umma wa nafasi mbalimbali unaelekea kuvurugwa na utawala huu wa Rais Magufuli. Madhara ya uteuzi huu haujazingatia taratibu mbalimbali za uteuzi wa Watumishi wa Umma. Wengi wa Wateule hawa hawana uzoefu wowote katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa vile tu hawajawahi kufanya kazi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; Godfrey Emmanuel Kunambi, ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma lilipo Bunge lako Tukufu, alimaliza masomo ya Chuo Kikuu mwaka 2014 na hajawahi kuwa Mtumishi wa Umma katika nafasi yoyote ile. Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, Mteule huyu aligombea Ubunge wa Jimbo la Mlimba kwa tiketi ya CCM na kushindwa vibaya na Mbunge wa sasa wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushindwa uchaguzi, ndugu Kunambi alikimbilia Mahakamani kufungua mashauri ya uchaguzi ambako pia alishindwa vibaya. Muda mfupi baadaye, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi mpya wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na sasa ndiye Afisa Masuhuli wa Halmashauri ya Manispaa hii na atakuwa Msimamizi wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu wa 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine wa uteuzi wa aina hii ni ule wa Abubakar Damian Assenga, Katibu Tawala mpya wa Wilaya ya Rombo katika Mkoa wa Kilimanjaro. Baada ya kumaliza masomo yake katika Chuo cha Sayansi ya Jamii cha Mwalimu Nyerere, hivi ndivyo alivyoiambia Mahakama, mwaka 2013, ndugu Assenga alifanywa Mwenyekiti au Mlezi wa Chipukizi wa Chama cha Mapinduzi. Baadaye mwaka 2015, Assenga aligombea Ubunge wa Jimbo la Kilombero ambapo alishindwa vibaya na Mbunge wa sasa wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kunambi, Assenga naye alikimbilia Mahakama Kuu kupinga matokeo ya uchaguzi ambako nako alishindwa vibaya. Siku chache baada ya kushindwa kesi ya uchaguzi na yeye pia aliteuliwa kuwa Katibu Tawala mpya wa Wilaya ya Rombo ambako sasa sio tu atakuwa Afisa masuhuli katika Ofisi ya Mkuu wa

Wilaya hiyo, bali pia atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Rufaa ya Wilaya wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji wa mwaka 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Yefredi Edson Myenzi aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa muda mrefu katika Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali ya Haki Ardhi ya Dar es Salaam. Mwaka 2015, Bwana Myenzi aligombea nafasi ya uteuzi wa Mgombea Ubunge wa Jimbo la Kilolo ambako alishindwa na Mbunge wa sasa wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Venance Mwamoto. Sasa Bwana huyu ndiye Mkurugenzi Mteule wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, ambako atatakiwa kusimamia fedha, mali na watumishi wa umma walio chini yake na pia kuwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa chaguzi zinazokuja mbeleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Utumishi wa Umma inampa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa Mamlaka ya kuteua, kupandisha vyeo na kudhibiti nidhamu ya Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa isipokuwa Wakurugenzi wa Jiji ambao ni Wateule wa Rais. Mamlaka haya yamefafanuliwa vizuri zaidi na sehemu (d) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009. Kwa sasa, kama inavyojulikana, Waziri huyo ni Mheshimiwa George Simbachawene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, uteuzi wa Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Serikali za Mitaa uliofanywa mwezi Julai ya mwaka huu, ulifanywa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa staili hii mpya ya Rais Dkt. Magufuli ya kunyoosha nchi bila kujali masharti ya Katiba wala sheria husika za nchi, ni wazi kwamba utumishi wa umma katika nchi yetu umeingia katika matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu yeyote anaweza kuteuliwa kuwa mtumishi wa umma wa ngazi yoyote bila kujali masharti na vigezo vilivyowekwa na Katiba wala sheria ya Utumishi wa umma. Sasa Mtumishi yeyote wa umma anaweza kutumbuliwa jipu hata kama kosa lake pekee ni kutoa ushahidi Mahakamani utakaopelekea Mgombea wa CCM kushindwa kesi kama ilivyotokea kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, ambaye alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero na Msimamizi wa Uchaguzi wa Majimbo ya Kilombero na Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sifa kuu na njia rahisi ya kuteuliwa Mkurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa au Katibu Tawala wa Wilaya ni kuwa Mgombea Ubunge wa Chama cha Mapinduzi aliyeshindwa, badala ya kuwa na *political neutrality* au kufuata *meritocratic principles.* Kwa maoni ya

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, utaratibu huu utaua kabisa Utumishi wa Umma katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; kwa msingi wa matakwa ya Kikatiba Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu umekosa uhalali kwa kuwa vipo vipengele ambavyo vimeanza kutumika kabla ya kukamisha matakwa ya Kikatiba na kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano; kuanzia Mwezi Septemba, mwaka huu, yapo malalamiko ya watumishi wa umma ambao wameanza kukatwa kiasi cha asilimia 15 katika mishahara yao kama makato ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambapo mapendekezo haya ya asilimia 15 yapo katika maboresho ya Muswada huu ulioko mezani. Je, Wizara imepata wapi uhalali wa kuanza kutoza asilimia 15 ilihali kifungu hicho cha sheria ndio kwanza kinaletwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya maboresho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu inamtaka Waziri aeleze mbele ya Bunge hili kuwa amepata wapi uhalali ya utekelezaji wa kifungu hiki ambacho bado hakijapata ridhaa ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema mwaka huu Rais Dkt. Magufuli aliliambia Taifa katika hotuba aliyoitoa katika chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa Serikali imeshatoa takribani shilingi bilioni 80 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ikiwa ni pungufu ya bilioni 40 ya fedha iliyotengwa katika robo ya kwanza ya bajeti ya mwaka wa 2016/2017. Hata hivyo, kauli ya Rais Magufuli inapingana na kauli ya Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, aliyoitoa tarehe 21 Oktoba, 2016, kuwa tayari Serikali imetoa shilingi bilioni 121 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa katika mwaka huu wa fedha, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 483 kwa ajili ya Bodi ya Mikopo. Hata hivyo, hadi leo wapo wanafunzi wengi wenye sifa na vigezo vinavyohitajika ambao hawajapata mikopo kwa ajili ya masomo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Tume ya Vyuo Vikuu nchini, mpaka sasa wamedahiliwa wanafunzi 61,590 kati ya hao wanafunzi 20,391 tu ndio waliopata mikopo mpaka sasa. Kwa mujibu wa Kauli ya Serikali iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa Waziri tarehe 4 Novemba, 2016, jumla ya wanafunzi 58,000 waliokuwa wamedahiliwa na kati yao 21,190 walikuwa wamekwishapata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Serikali ihakikishe inalipa deni la shilingi bilioni 60 kwa vyuo ambazo ni fedha za ada walizokopeshwa wanafunzi, lakini Serikali haikupeleka mkopo huo kwenye vyuo hivyo kwa mwaka wa masomo 2015/2016. Hii ina maana kwamba Serikali kuchelewa kulipa deni hilo kutasababisha vyuo vishindwe kumudu gharama mbalimbali za uendeshaji. Tukumbuke pia, migogoro mikubwa inayotokea vyuoni ni pamoja na kucheleshwa au kutolipwa kwa fedha za ada za wanafunzi ambapo vyuo husika hulazimika kuwasimamisha masomo wadaiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya sheria hii, kifungu cha tano kinachozungumzia kupunguza idadi ya wajumbe wa bodi kutoka 14 hadi 7 kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji. Kifungu hicho hakijazingatia umuhimu na uhitaji wa wawakilishi katika kuleta tija kwenye eneo hilo bali gharama za uendeshaji pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoonekana dhahiri hapa ni kuwa kuna maamuzi ambayo yanaweza kuamuliwa na bodi ambayo yanaweza kuwaathiri walengwa au wanufaika wa mikopo hiyo. Kwa mfano, katika marekebisho hayo nafasi ya mwakilishi wa elimu ya ufundi *(technical education)* imetolewa. Ilihali tunafahamu kuwa vyuo vilivyo chini ya *NACTE* navyo vinapata mikopo na vimekuwa vikikumbwa na changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuruhusu mwakilishi mmoja kutoka *TCU* na kuwaacha *NACTE* wakiwa hawana mwakilishi kunaweka ulakini katika muundo wa vyombo vya usimamizi wa elimu nchini. Pamoja na hayo, uwakilishi wa wanafunzi katika kifungu cha (5)(e) haujazingatia uwiano sawa wa uwakilishi wa wanafunzi kutoka Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu ni mojawapo ya masuala ya Muungano hivyo ni vyema uwakilishi ukazingatia pande zote za Muungano kwa kuwa mwamvuli unaokutanisha Wanafunzi wa elimu ya juu ni *TAHLISO* lakini uwakilishi wa vyuo vya Zanzibar ndani ya *TAHLISO* umekuwa ni wa kusuasua hivyo ni vyema Vyuo vya Zanzibar vikapata mwakilishi wao kwa kupitia Umoja wa Vyuo vya Wanafunzi Zanzibar, unaoitwa *Zanzibar Higher Learning Institution Federation*. Hivyo basi uwakilishi wa wanafunzi uzingatie uwiano sawa kwa pande zote mbili za Muungano. Pia, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako Tukufu, inashauri mwakilishi kutoka vyuo vya elimu ya ufundi awepo miongoni mwa wawakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine ambayo sijayasema yaingie katika *record* rasmi ya Bunge lako Tukufu, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, unga mkono hoja ya Serikali.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mwenyekiti sijakusikia.

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**WABUNGE FULANI:** Anasema unga mkono hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Eeehhh? Sijawahi kufanya hivyo tangu mwaka 2010. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MH. TUNDU A.M. LISSU, KUHUSU *MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI (NA. 3) WA 2016 [THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2016* (Kanuni ya 86(6) ya *Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016*) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

MAONI YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA, MH. TUNDU A.M. LISSU, KUHUSU *MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI (NA. 3) WA 2016 [THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 3) ACT, 2016*
(Kanuni ya 86(6) ya *Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016*)

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika,
*Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali (No. 3), 2016*, ulichapishwa kwenye *Gazeti la Serikali* la tarehe 26 Agosti, 2016, na kusomwa kwa mara ya kwanza wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge lako tukufu. Muswada huu ulikuwa unapendekeza marekebisho ya sheria mbali mbali tisa. Sheria hizo ni pamoja na *Sheria ya Usafiri wa Anga, Sura ya 80*; *Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191*; *Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178*, na *Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298*.

Sheria nyingine zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni *Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura ya 105*; *Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, Sura ya 413*; *Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317*; *Sheria ya Madaraka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370*, na *Sheria ya Vipimo na Mizani, Sura ya 340*.

Ni wazi, Mheshimiwa Spika, kwamba mapendekezo haya yanahusu sheria nyingi na muhimu. Sio hivyo tu, vifungu vinavyopendekezwa kurekebishwa katika Sheria hizo ni vingi. Hivyo, kwa mfano, ukiachia vifungu kumi na moja vya kiutangulizi, Muswada huu unapendekeza kurekebisha vifungu thelathini na tisa vya msingi katika Sheria hizi tisa. Vile vile, marekebisho yanayopendekezwa yatapelekea mabadiliko makubwa ya kisera, kisheria na kitaasisi katika maeneo husika. Kwa vyovyote vile, hii sio kazi ndogo.

Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaamini kwamba utaratibu wa kuleta marekebisho mengi ya sheria nyingi namna hii katika Muswada mmoja unalinyima Bunge lako tukufu muda na uwezo wa kuyajadili kwa kina na kuyaelewa mapendekezo ya Serikali kabla ya kuyapitisha na kuwa sheria za nchi yetu.

Matokeo ya utaratibu huu sio tu ni kuligeuza Bunge lako tukufu kuwa *rubber stamp* ya kuhalalisha maamuzi ya Serikali, bali pia unapelekea Bunge hili kupitisha sheria mbovu zinazoathiri haki za wananchi wetu na ustawi wa taifa letu na kusababisha migongano isiyokuwa ya lazima katika vyombo vya utekelezaji vya umma.

Kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu inaishauri Serikali hii ya CCM kuacha utaratibu huu mbovu wa utungaji sheria. Kwa sababu zitakazojionyesha wazi hapa, tunapendekeza kuanza na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA

Mheshimiwa Spika,

Muswada unapendekeza marekebisho mbali mbali katika Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwanza, inapendekezwa kufanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria kuhusu tasiri ya maneno 'Sekretarieti ya Ajira' yaliyopo katika kifungu cha 29 cha Sheria hiyo.[1] Pili, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 8(3) kwa kuongeza majukumu ya Katibu Mkuu (Utumishi) kuwa ni pamoja na *"kurekebisha na kuoanisha mishahara, posho na marupurupu katika Utumishi wa Umma."*[2]

Aya ya 24 ya Muswada inapendekeza marekebisho zaidi yanayohusu masuala ya mishahara ya watumishi wa umma. Kwa mfano, kifungu cha 9 cha Sheria ya Utumishi ya Umma kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuingiza kifungu kipya

[1] Aya ya 22

[2] Aya ya 23

cha 9A ambacho kitaondoa mamlaka ya taasisi za umma, Wakala, Bodi au tume kupitisha mishahara, posho na marupurupu mengine katika taasisi zao. Badala yake, kwa mujibu wa kifungu kipya cha 9A(2) kinachopendekezwa, "... *upitishaji wa mishahara, posho na marupurupu mengine katika Utumishi (Umma) yataamuliwa na Katibu Mkuu (Utumishi)."*[3]

Ili kutilia nguvu masharti mapya yanayopendekezwa, kifungu kipya cha 9B kinapendekeza kwamba endapo kutakuwa na mgongano katika masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyinginezo, basi masharti ya Sheria hii ndiyo yatakayotiliwa nguvu ya kisheria.[4]
Mheshimiwa Spika,

Kuna mapendekezo mengine ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa mfano, aya ya 25 ya Muswada inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 20(1)(c) ambacho kinaipa Tume ya Utumishi wa Umma mamlaka ya kutunga kanuni za usaili wa watumishi unaofanywa na Tume au Bodi za taasisi za umma. Aidha, aya ya 26 inapendekeza kuingizwa kwa kifungu kipya cha 32A ambacho kitawazuia watumishi wa umma wenye migogoro na wajiri wao kupeleka migogoro hiyo kwenye Mahakama za Kazi hadi kwanza wamalize taratibu za utatuzi wa migogoro zilizowekwa na Sheria ya Utumishi wa Umma.

Vile vile, inapendekezwa kufuta kifungu chote cha 34 cha Sheria na kuweka kifungu kipya kitakachowezesha watumishi wa umma wanaoumia au kufariki wakiwa kazini kupewa fidia kwa mujibu wa *Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi, Sura ya 263 ya Sheria za Tanzania*.[5] Utaratibu unaofutwa ulikuwa unampa mamlaka hayo Waziri kwa kutumia mamlaka yake ya kutunga kanuni.

Mheshimiwa Spika,
Mapendekezo ya Muswada yanayohusu usaili na fidia ya watumishi wa umma hayabadilishi sera, bali ni marekebisho yanayolenga kuboresha utekelezaji wa sera zilizopo. Kwa upande mwingine, mapendekezo ya marekebisho yanayohusu mishahara na malipo mengine ya watumishi ni mabadiliko ya kisera. Kwa sababu hiyo, mapendekezo haya yalihitaji, na yanahitaji, Muswada mahsusi wa kurekebisha Sheria ili kufanya mabadiliko ya kisera katika maeneo hayo. Tunaomba kutoa ufafanuzi wa jambo hili.

---

[3] Aya ya 24

[4] Aya ya 24

[5] Aya ya 27

Katika maelezo yake kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza kwamba "marekebisho haya yanalenga kuwa na mamlaka moja inayoratibu mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi katika taasisi za serikali na pia kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengine kwa watumishi wa taasisi hizo."[6] Suala muhimu linalohitaji majibu ni kwa nini utaratibu wa sasa hauna uwiano huo.

Mheshimiwa Spika,

Kama sehemu ya mabadiliko makubwa ya kisera yaliyofanywa na Serikali tangu miaka ya tisini, idara na taasisi nyingine za Serikali zilipewa mamlaka ya kuamua masuala ya kiutendaji ya idara na taasisi hizo. Aidha, taasisi kama vile Wakala wa Serikali (Executive Agencies) zilipewa mamlaka ya kujiendesha kibiashara bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini. Mabadiliko haya yalilenga kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika idara, wakala na taasisi hizo na, *by extension*, kupunguza matumizi ya Serikali.

Matokeo ya mabadiliko haya ya kisera ni kwamba mishahara, posho na marupurupu mengine, hasa watendaji wakuu na makada wa ngazi za juu wa taasisi hizo, ililipuka na kuongezeka kwa kiwango cha kutisha kwa nchi kama Tanzania. Mara tulianza kusikia watendaji wakuu, wakurugenzi na mameneja wa juu wa taasisi hizo wakilipwa makumi ya milioni ya shilingi kama mishahara, posho na stahiki nyingine.

Mara tulianza kuona mikutano ya Bodi za Wakurugenzi au Wadhamini wa taasisi za umma ikifanyika katika nchi za kigeni kama Dubai au Afrika Kusini. Bila shaka wabunge watakumbuka kashfa za wajumbe wa bodi za mazao kama korosho au pamba au kahawa au chai; au bodi za wadhamini za mifuko ya hifadhi ya jamii waliokuwa wanalipwa mamilioni ya shilingi kama posho za kila siku za vikao vya bodi hizo.

Hali ilikuwa mbaya kiasi kwamba Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) alisemekana kugomea kuchukua mshahara wa zaidi ya shilingi milioni thelathini kwa mwezi kwa hoja kwamba mshahara huo ulikuwa mdogo na badala yake alifanya kazi kwa zaidi ya mwaka mmoja akilipwa posho tu.

[6] Maelezo ya Ndugu George M. Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Akiwasilisha Katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2016 (The Written Laws [Miscellaneous Amendments] (No. 3) Act, 2016, uk. 12.

Pamoja na kwamba, kwa sababu inazozijua yenyewe, Serikali hii ya CCM haijasema wazi kwamba marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma yanayopendekezwa, yanalenga kuondoa kashfa za aina hii katika malipo ya watumishi wa umma, ni wazi kwamba hili ndilo lengo kuu la mapendekezo haya.

Mheshimiwa Spika,
Kama hili ndio lengo la mapendekezo yanayohusu mishahara na malipo mengine ya watumishi wa umma, utaratibu unaopendekezwa unaweza kusababisha matatizo makubwa zaidi badala ya kuwa ndio tiba ya ugonjwa wa mishahara na malipo yasiyokuwa na uwiano katika utumishi wa umma. Kwanza, kuondoa mamlaka ya kupanga mishahara na malipo mengine kutoka kwenye taasisi husika na kuyapeleka kwa Katibu Mkuu (Utumishi) peke yake hakuondoi tatizo la malipo makubwa ya mishahara na posho na marupurupu ya watendaji wakuu na mameneja wa taasisi hizo.

Kama tatizo ni hilo, utatuzi wake unaweza kuwa kuweka viwango vya malipo hayo katika sheria au kanuni mahsusi zinazohusu idara, wakala au taasisi hizo. Mapendekezo ya marekebisho hayajaweka viwango vyovyote vya mishahara.

Pili, mapendekezo haya yanarudisha ukiritimba wa madaraka (*centralization of power*) ndani ya Ofisi ya Rais na matatizo yote yanayotokana na ukiritimba wa madaraka kama vile urasimu utakaosababisha kukosekana kwa ufanisi katika utendaji wa watumishi wa umma.

Ikumbukwe hapa kwamba lengo kubwa la *civil service reform programs* za tangu miaka ya Rais Mwinyi lilikuwa ni ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu (*Establishment*) kwenda kwenye taasisi na mashirika yanayojitegemea ili kuondoa urasimu, kuboresha ufanisi na kuongeza tija katika utumishi wa umma.

Kwa mapendekezo haya, jitihada hizo za zaidi ya robo karne zinashambuliwa moja kwa moja. Kwa maneno mengine, mapendekezo haya yanaturudisha nyuma kwenye miaka ya Mwalimu Nyerere ambako Ikulu na Idara Kuu ya Utumishi zilikuwa ni *Alpha* na *Omega* ya kila kitu, kikubwa ama kidogo, katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika,
Mapendekezo ya aya ya 26 ya Muswada yanaleta mabadiliko makubwa ya kisera vile vile. Itakumbukwa kwamba mwaka 2004, Bunge lako tukufu lilitunga 'Sheria za Kazi', yaani, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (*Employment and Labour Relations Act, 2004*), na Sheria ya Taasisi za Kazi (*Labour Institutions Act,*

*2004*). Sheria hizi mbili zilileta mabadiliko makubwa ya kisera katika masuala ya ajira na utatuzi wa migogoro ya ajira.

*Specifically*, Sheria za Kazi zilianzisha taasisi mpya za kutatua migogoro ya ajira zinazojulikana kwa practitioners kama Mahakama za Kazi, yaani Tume ya Upatanishi na Usuluhishi (*the Commission for Mediation and Arbitration*) na Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi. Kwa mujibu wa utaratibu huu, wafanyakazi na waajiri wote – wa Serikali au wa sekta binafsi – wana haki ya kufungua mashauri katika Mahakama za Kazi. Kwa kiasi kikubwa, Mahakama za Kazi ziko huru katika kufanya maamuzi yake kwenye mashauri ya ajira na mahusiano kazini.

Sasa, kwa mapendekezo ya aya ya 26 ya Muswada, mtumishi wa umma anayeingia kwenye mgogoro wa ajira na mwajiri wake, hatakuwa na haki ya kwenda moja kwa moja kwenye Mahakama za Kazi kudai haki zake. Badala yake, mtumishi huyo wa umma atatakiwa kumaliza taratibu zote za utatuzi wa migogoro zilizopo chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Baada ya hapo ndio mtumishi huyo wa umma atakuwa na haki ya kwenda kwenye Mahakama za Kazi kutafuta haki.

Kwa maneno ya Mwanasheria Mkuu, "... *marekebisho haya yanalenga kuweka mwongozo utakaowawezesha watumishi wa umma kutumia kwanza utaratibu ulioainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma kabla ya kwenda katika vyombo vingine ikiwemo Baraza la Usuluhishi na Mahakama ya Kazi kwa kutumia sheria za kazi ambako jambo hilo linaweza kuchukua muda mrefu.*"[7]

Hio, Mheshimiwa Spika, sio kweli. Utaratibu unaopendekezwa na Muswada huu, badala ya kufupisha muda wa utatuzi wa migogoro ya ajira ya watumishi wa umma, utarefusha muda huo zaidi na kuongeza gharama za utatuzi wa migogoro ya ajira katika utumishi wa umma. Kwanza, mtumishi wa umma aliyechukuliwa hatua za kinidhamu na Katibu Mkuu Kiongozi atatakiwa – kama ni mteule wa Rais – kukata rufaa kwa Rais[8] ambaye, 'uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.'[9]

Pili, kwa mtumishi wa umma ambaye amechukuliwa hatua za kinidhamu na Katibu Mkuu, Mkuu wa Idara Inayojitegemea, Katibu Tawala wa Mkoa,

[7] Maelezo ya Mwanasheria Mkuu, uk. 13

[8] Kifungu cha 25(1)(a) cha Sheria ya Utumishi wa Umma

[9] Kifungu cha 25(1)(d) cha Sheria ya Utumishi wa Umma

Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mkurugenzi wa Uhamiaji au na Kamishna wa Huduma za Moto na Uokoaji, mtumishi huyo anatakiwa kukata rufaa kwa Tume ya Utumishi wa Umma. Na endapo hataridhika na uamuzi wa Tume, mtumishi huyo anatakiwa kukata rufaa kwa Rais, ambaye uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho vile vile, kwa mujibu wa kifungu cha 25(1)(d) cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kwa utaratibu unaopendekezwa na Muswada, mtumishi wa umma ambaye sasa ana haki ya kwenda moja kwa moja kwenye Mahakama za Kazi kudai haki zake, hatakuwa na haki hiyo tena. Badala yake, mtumishi huyo wa umma atatakiwa kwanza amalize utaratibu wa rufaa ulioelezewa hapa ndipo, kama bado hajaridhika, aende kwenye Mahakama za Kazi.

Ni wazi lengo la mapendekezo haya ni kuwazuia watumishi wa umma kwenda kutafuta haki katika Mahakama za Kazi ambazo ziko huru zaidi kulinganisha na utaratibu uliopo kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu haiwezi kukubaliana na mapendekezo haya.

Kwa vyovyote vile, Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeonyesha hapa, mageuzi yanayopendekezwa na Muswada huu katika masuala ya utumishi wa umma ni makubwa kwa sababu yanabadili mwelekeo wa sera za Serikali. Mapendekezo haya yalihitaji, na bado yanahitaji, mjadala mpana zaidi ambao hautawezekana katika mazingira ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Ni Muswada mahsusi wa marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ambao ungeweza, na unaweza kutoa fursa ya mjadala mpana ndani na nje ya Bunge lako tukufu kuhusu masuala haya ya kisera.

Mheshimiwa Spika,
Baada ya mwaka mmoja wa Serikali ya Rais John Pombe Magufuli, ni wazi sasa kwamba utumishi wa umma katika taifa letu unakabiliwa na hatari kubwa ya kurudishwa nyuma kwa zaidi ya robo karne. Tangu utawala wa Serikali ya Rais Ali Hassan Mwinyi, na hasa baada ya kurudishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, kumefanyika jitihada kubwa ya kufanya mageuzi makubwa ya kimfumo katika utumishi wa umma.

Mageuzi yalilenga kuuondoa utumishi wa umma kutoka makucha ya mfumo wa chama kimoja cha siasa, uliojengeka toka miaka ya mwanzo ya uhuru wetu, na kujenga utumishi mpya wa umma ambao umejengeka katika misingi ya uweledi (*professionalism*) na kutofungamana na siasa za kivyama (*political non-partisanship*). Ndio maana Kanuni za Maadili katika Utumishi wa Umma (*Code of Ethics and Conduct for the Public Service in Tanzania*) zilizotungwa kwa mara

ya kwanza tangu uhuru wakati wa utawala wa Rais Ben Mkapa zilisisitiza watumishi wa umma 'kutofungamana kisiasa' (political neutrality) na kuepuka 'ushawishi wa kisiasa' (political influence).[10]
Na ndio maana, kwa sababu ya mageuzi haya, kuna kada za utumishi wa umma ambazo zilipigwa marufuku kujihusisha na siasa za kivyama. Hivyo, kwa mfano, ibara ya 74(14) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania[11], imetamka kwamba: "*Itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na chama chochote cha siasa....*"

'Watu wanaohusika na uchaguzi' wametajwa kuwa ni pamoja na "*Wasimamizi wote wa Uchaguzi katika miji na wilaya zote.*"[12] Na kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Taifa, "*... kila Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya atakuwa ni msimamizi wa uchaguzi kwa minajili ya kuendesha uchaguzi jimbo....*"[13]

Sasa makatazo haya ya kikatiba yamewekwa kando na utawala huu wa Rais Magufuli. Mfano mzuri ni uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa uliofanywa na Rais Magufuli mwezi Julai mwaka huu. Katika uteuzi huo, kati ya watu 195 walioteuliwa kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri, na kwa hiyo Wasimamizi wa Uchaguzi, wateule 62 walikuwa wagombea ubunge wa Chama cha Mapinduzi katika hatua ya kura za maoni majimboni, au kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015.

Wateule wengine watano waligombea nafasi mbali mbali za uongozi ndani ya CCM mwaka 2012; wawili waligombea uteuzi wa nafasi ya mgombea uRais wa Jamhuri ya Muungano kwa tiketi ya CCM mwaka 2015, na mmoja alikuwa mgombea Ubunge wa chama cha ACT. Ndio kusema kwamba takriban asilimia 36 ya wateule wote wa nafasi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa hawana sifa za kikatiba na kisheria za utumishi wa umma katika nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika,

---

[10] Angalia Sehemu ya IX ya Kanuni za Maadili katika Utumishi wa Umma Tanzania.

[11] Sura ya 2 ya Sheria za Tanzania.

[12] Ibara ya 74(15) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

[13] Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Taifa, Sura ya 343 ya Sheria za Tanzania.

Sio tu kwamba misingi ya 'political neutrality' na 'meritocratic principles'[14] katika uteuzi wa watumishi wa umma wa nafasi mbali mbali unaelekea kuvurugwa na utawala huu wa Rais Magufuli. Madhara ya uteuzi huu haujazingatia taratibu mbali mbali za uteuzi wa watumishi wa umma. Wengi wa wateule hawa hawana uzoefu wowote katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa vile tu hawajawahi kufanya kazi serikalini.

Kwa mfano, Godfrey Emmanuel Kunambi, ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma lilipo Bunge lako tukufu, alimaliza masomo ya Chuo Kikuu mwaka 2014, na hajawahi kuwa mtumishi wa umma katika nafasi yoyote ile. Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, mteule huyu aligombea Ubunge wa Jimbo la Mlimba kwa tiketi ya CCM na kushindwa vibaya na Mbunge wa sasa wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga.

Baada ya kushindwa uchaguzi, 'ndugu' Kunambi alikimbilia mahakamani kufungua mashauri ya uchaguzi ambako pia alishindwa vibaya. Muda mfupi baadaye, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi mpya wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, na sasa ndiye afisa masuhuli wa Halmashauri ya Manispaa hii; na atakuwa Msimamizi wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Mfano mwingine wa uteuzi wa aina hii ni ule wa Abubakar Damian Assenga, Katibu Tawala mpya wa Wilaya ya Rombo katika Mkoa wa Kilimanjaro. Baada ya kumaliza masomo yake katika Chuo cha Sayansi ya Jamii cha Mwalimu Nyerere (zamani Chuo cha Chama Kivukoni) mwaka 2013, 'ndugu' Assenga alifanywa Mwenyekiti/mlezi wa Chipukizi wa Chama cha Mapinduzi. Baadaye mwaka 2015, Assenga aligombea Ubunge wa Jimbo la Kilombero ambapo alishindwa vibaya na Mbunge wa sasa wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali.

Kama ilivyokuwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa Kunambi, Assenga naye alikimbilia Mahakama Kuu kupinga matokeo ya uchaguzi ambako nako alishindwa vibaya. Siku chache baada ya kushindwa kesi ya uchaguzi, na yeye pia aliteuliwa kuwa Katibu Tawala mpya wa Wilaya ya Rombo ambako sasa sio atakuwa afisa masuhuli katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo, bali pia atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Rufaa ya Wilaya wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vijiji wa mwaka 2019.

---

[14] Angalia Sehemu ya X ya Kanuni za Maadili Katika Utumishi wa Umma Tanzania.

Kwa upande mwingine, Yefredi Edson Myenzi alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa muda mrefu katika taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya HakiArdhi/LARRRI (Land Rights, Resources and Research Institute) ya Dar es Salaam. Mwaka 2015, bwana Myenzi aligombea nafasi ya uteuzi wa mgombea ubunge wa Jimbo la Kilolo ambako alishindwa na Mbunge wa sasa wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Vinance Mwamoto. Sasa bwana huyu ndiye Mkurugenzi mteule wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, ambako atatakiwa kusimamia fedha, mali na watumishi wa umma walio chini yake, na pia kuwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa chaguzi zinazokuja mbeleni.

Mheshimiwa Spika,
Sheria ya Utumishi wa Umma inampa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa mamlaka ya kuteua, kupandisha vyeo na kudhibiti nidhamu ya Wakurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa[15], isipokuwa Wakurugenzi wa Jiji ambao ni wateule wa Rais.[16] Mamlaka haya yamefafanuliwa vizuri zaidi Sehemu D ya *Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009* (*Standing Orders for the Public Service, 3rd Edition, 2009*).[17]

Kwa sasa, kama inavyojulikana, Waziri huyo ni Mheshimiwa George Simbachawene. Hata hivyo, uteuzi wa Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Serikali za Mitaa uliofanywa mwezi Julai ya mwaka huu, ulifanywa na Rais John Pombe Magufuli. Kwa staili hii mpya ya Rais Magufuli ya 'kunyoosha nchi' bila kujali masharti ya Katiba wala sheria husika za nje, ni wazi kwamba utumishi wa umma katika nchi yetu umeingia katika matatizo makubwa.

Sasa mtu yeyote anaweza kuteuliwa kuwa mtumishi wa umma wa ngazi yoyote bila kujali masharti na vigezo vilivyowekwa na Katiba wala Sheria ya Utumishi wa Umma. Na sasa mtumishi yeyote wa umma anaweza 'kutumbuliwa jipu' hata kama kosa lake pekee ni kutoa ushahidi mahakamani utakaopelekea mgombea wa CCM kushindwa kesi ya uchaguzi, kama ilivyotokea kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, ambaye alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero na Msimamizi wa Uchaguzi wa Majimbo ya Kilombero na Mlimba.

Sasa sifa kuu na njia rahisi ya kuteuliwa Mkurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa au Katibu Tawala wa Wilaya ni kuwa mgombea Ubunge aliyeshindwa wa

[15] Kifungu cha 5(1)(a)(iii) cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

[16] Kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

[17] Angalia aya D.5(e) inayohusu 'Mamlaka za Uteuzi.'

Chama cha Mapinduzi, badala ya kuwa na 'political neutrality' au kufuata 'meritocratic principles.' Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Bunge lako tukufu, utaratibu huu utaua kabisa utumishi wa umma katika nchi yetu.

MAREKEBISHO YA SHERIA YA BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

Mheshimiwa Spika,
Kwa msingi wa matakwa ya Kikatiba Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu umekosa uhalali kwa kuwa vipo vipengele ambavyo vimeanza kutumika kabla ya kukamisha matakwa ya Kikatiba na kisheria. Mfano, kuanzia Mwezi Septemba mwaka huu (2016) yapo malalamiko ya Watumishi wa Umma ambao wameanza kukatwa kiasi cha 15% katika mishahara yao kama makato ya mikopo kwa wnafunzi wa elimu ya juu ambapo mapendekezo haya ya asilimia 15 yapo katika moboresho ya muswada huu ulio mezani. Je, Wizara imepata wapi uhalali wa kuanza kutoza asilimia 15 ilihali kifungu hicho cha sheria ndio kwanza kinaletwa mbele ya Bunge lako tukufu kwa ajili ya maboresho? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Waziri aeleze mbele ya Bunge lako tukufu kuwa amepata wapi uhalali ya utekelezaji wa kifungu hiki ambacho bado hakijaridhiwa na Bunge?

Mheshimiwa Spika,
Mapema mwaka huu Rais Magufuli aliliambia taifa katika hotuba aliyoitoa katika chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa serikali imeshatoa takribani shilingi bilioni 80 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ikiwa ni pungufu ya bilioni 40 ya fedha iliyotengwa katika robo ya kwanza ya Bajeti ya mwaka 2016/17. Hata hivyo, kauli ya Rais Magufuli inapingana na kauli ya Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, aliyoitoa tarehe 21 Oktoba 2016, kuwa tayari serikali imetoa shilingi bilioni 121 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa vyuo vikuu.

Ikumbukwe kuwa katika mwaka huu wa fedha, Bunge lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi Bilioni 483 kwa ajili ya Bodi ya Mikopo. Hata hivyo, hadi leo wapo wanafunzi wengi wenye sifa na vigezo vinavyohitajika ambao hawajapata mikopo kwa ajili ya masomo yao.

Mheshimiwa Spika,
Kwa mujibu wa Tume ya Vyuo Vikuu nchini (Tanzania Commision for Universities), mpaka sasa wamedahiliwa wanafunzi 61,590, na kati ya hao wanafunzi 20,391 tu ndio waliopata mikopo mpaka sasa. Na kwa mujibu wa Kauli ya Serikali iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa Waziri tarehe 4 Novemba 2016, jumla ya wanafunzi 58,010 waliokuwa wamedahiliwa na kati yao 21,190 waalikuwa wamekwisha pata mikopo.

Mheshimiwa Spika,
Pamoja na hayo serikali ihakikishe inalipa deni la shilingi bilioni 60.798 kwa vyuo ambazo ni fedha za ada (tuition fee) walizokopeshwa wanafunzi lakini serikali haikupeleka mkopo huo kwenye vyuo hivyo kwa mwaka wa masomo 2015/16. Hii ina maana kwamba serikali kuchelewa kulipa deni hilo kutasababisha vyuo vishindwe kumudu gharama mbalimbali za uendeshaji. Tukumbuke pia, migogoro mikubwa inayotokea vyuoni ni pamoja na kucheleshwa au kutokulipwa fedha za ada za wanafunzi ambapo vyuo husika hulazimika kuwasimamisha masomo wadaiwa.

Mheshimiwa Spika,
Katika marekebisho ya sheria hii kifungu cha 5 kinachozungumzia kupunguza idadi ya wajumbe wa bodi kutoka 14 hadi 7 kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji, lakini kifungu hicho hakikuzingatia umuhimu na uhitaji wa wawakilishi katika kuleta tija kwenye eneo hilo bali gharama za uendeshaji pekee.

Mheshimiwa Spika,
Kinachoonekana dhahiri hapa ni kuwa kuna maamuzi ambayo yanaweza kuamuliwa na Bodi ambayo yanaweza kuwaathiri walengwa au wanufaika wa mikopo hiyo. Mfano, katika marekebisho hayo nafasi ya mwakilishi wa elimu ya ufundi (technical education) imetolewa. Ilhali tunafahamu kuwa vyuo vilivyo chini ya NACTE navyo vinapata mikopo na vimekuwa vikikumbwa na changamoto nyingi sana. Kitendo cha kuruhusu mwakilishi mmoja kutoka TCU na kuwaacha NACTE wakiwa hawana mwakilishi kunaweka ulakini katika muundo wa vyombo vya usimamizi wa elimu nchini. Pamoja na hayo, uwakilishi wa wanafunzi katika kifungu cha (5)(e) haujazingatia uwiano sawa wa uwakilishi wa wanafunzi kutoka Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika,
Elimu ya juu ni mojawapo ya masuala ya Muungano hivyo ni vyema uwakilishi ukazingatia pande zote za Muungano kwa kuwa mwamvuli unaokutanisha wanafunzi wa elimu ya juu ni TAHLISO lakini uwakilishi wa vyuo vya Zanzibar ndani ya TAHLISO umekuwa ni wa kusuasua hivyo ni vyema Vyuo vya Zanzibar vikapata muwakilishi wao kwa kupitia Umoja wa Vyuo vya Wanafunzi Zanzibar, unaoitwa Zanzibar Higher Learning Institution Federation (ZAHLIFE).Hivyo basi uwakilishi wa wanafunzi uzingatie uwiano sawa kwa pande zote mbili za Muungano. Pia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Mwakilishi kutoka vyuo vya elimu ya ufundi (Technical Education) awepo miongoni mwa wawakilishi

Mheshimiwa Spika,
Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) kila mnufaika wa mkopo ambae kwa sababu yoyote ile ameshindwa kuendelea na masomo anatakiwa arudishe mkopo haraka iwezekanavyo. Hatuna budi tukumbuke kuwa katika vyuo vyetu wapo wanafunzi wanaoacha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo ugonjwa, au kushindwa kufaulu kunakotambulika kama discontinuation kutokana na sababu mbalimbali. Endapo watu hawa watatakiwa kulipa mkopo mara moja kutokana na sababu hizo je,kwa uhalisia wa maisha ya Kitanzania wanalipaje? Tukumbuke pia kuwa wanufaika wa mikopo ni vijana waliotoka katika kaya zenye kipato duni na wapo wanaofeli masomo kutokana na changamoto hizo za kimaisha. Kuwalazimu kulipa mkopo haraka iwezekanavyo ni kuzidi kuongeza umaskini juu ya umaskini, kunaweza kupelekea nchi yetu kuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wenye matatizo ya akili kutokana na msongo wa mawazo kama ilivyoezwa na Mganga Mkuu wa Serikali siku ya maadhimisho ya afya ya akili duniani tarehe 10 Mwezi Octoba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika,
Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kipengele hiki kitazamwe upya kwa kutoa tafsiri ya neno" immediately." Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza Bodi itoe angalau miaka miwili au zaidi ikiwa mnufaika huyo wa mkopo ameacha masomo kwa sababu yoyote.

Mheshimiwa Spika,
Kwa mujibu wa kifungu cha 20(a) ambacho kinamtaka mwajiri aweze kutoa taarifa ya mwajiriwa mwenye shahada au stashahada ndani ya siku ishirini na nane za mwanzo wa ajira yake na kifungu cha 20(b) ambacho kimeongeza kiwango cha asilimia ya makato ya marejesho ya mkopo kutoka 8% mpaka 15%.

Mheshimiwa Spika,
Kwanza kabisa vifungu hivi vimewekwa mahususi kwa ajili ya kukandamiza na kuwakatisha tamaa vijana wengi kujiunga na elimu ya juu nchini. Mfano, mshahara wa serikali hutolewa kwa kuzingatia utaalamu, elimu, muda wa ajira n.k Hivyo basi viwango hutofautiana. Mathalani wapo waajiriwa wanaopokea mshahara wa shilingi laki tatu na elfu kumi na tano (315,000/-)kama kiwango cha chini cha mshahara, wapo wanaopokea laki tano(500,000/-) milioni moja (1,000,000/-) n.k Mfano mtu mwenye mshahara wa shilingi 500,000/- akikatwa asilimia kumi na tano(15%) basi atakuwa amekatwa kiasi cha shilingi elfu sabini na tano (75,000/) na kubaki na 425,000/- tukumbuke katika mshahara huo bado inamlazimu kukatwa kodi ya mshahara (PAYE) pamoja na kodi nyingine mbalimbali zinazotokana na huduma anazozitumia au kuzihitaji katika kuendesha maisha yake.

Mheshimiwa Spika, tujiulize mkopo wa elimu nchini umelenga kumsaidia kijana wa Kitanzania au umelenga kumsababishia msongo wa mawazo unaotokana na ugumu wa maisha unaosababishwa na mishahara kidogo na makato makubwa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo majibu ya hoja yaliyotolewa kwa wajumbe wa kamati ya Sheria na Katiba yanaonyesha kuwa dhumuni la serikali katika kupandisha kiwango hicho cha asilimia ya marejesho ni kuhakikisha kuwa marejesho yanafanyika ndani ya kipindi kisichopungua miaka 10.

Mheshimiwa Spika, majibu haya sio tu hayakuzingatia hali halisi ya uchumi wa nchi yetu na pato la mtu mmoja mmoja lakini pia halikuzingatia mambo yafuatayo:

- Utofauti wa malipo ya ada vyuoni- kuna vyuo vinavyolipa ada kubwa na hivyo mkopo wake huwa ni mkubwa zaidi na marejesho yake yatatofautiana na wale wenye ada ndogo na pengine ndani ya miaka kumi wanaweza wasiwe wameamaliza mkopo huo.

- Utofauti wa mishahara- Wapo wanufaika wanaopokea mishahara kidogo kiasi kwamba ndani ya miaka kumi hawataweza kumaliza mkopo huo, hawa ni pamoja na wale walio katika sekta isiyo rasmi ambao kimsingi kipato chao hakitabiriki

- Utofauti wa muda wa kupata ajira- kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha (20) kuwa wanufaika waanze kulipa mkopo pindi wanapomaliza masomo, na malipo hayo yafanyike ndani ya miaka kumi, kwa asilimia 15% kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha (20) (b) . Ukweli ni kuwa muda wa marejesho hayo hauna uhalisia kwani watu hupata ajira kwa muda tofauti.

- Uwepo na upatikanaji wa ajira – kumekuwa na ongezeko la tatizo la ajira nchini japo kuna ongezeko la wataalamu pia. Jambo hili limeleta changamoto zaidi katika soko la ajira nchini. Hivyo basi wapo wataalamu wengi wanaomaliza masomo yao ya elimu ya juu lakini hawajapata ajira katika mfumo rasmi, hivyo kutaka wataalamu hawa warejeshe mkopo ndani ya muda usiozidi miaka 10 huku serikali bado haijatengeneza fursa za ajira nchini ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa mujibu wa majibu yaliyotolewa kwa kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba ilielezwa kuwa kuongezeka kwa kiwango cha

asilimia ya marejesho kutoka 8% mpaka 15% itaweza kupunguza muda wa urejeshwaji wa mikopo hivyo kulinda thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, tutambue kuwa vipo vifungu vipya vilivyoongezwa ambavyo kimsingi havikuwepo katika makubaliano ya mkopo haswa kwa wanafunzi waliosoma miaka ya nyuma Mfano, ulipaji wa deni unaozingatia kulinda thamani ya fedha , hivyo kuongezwa kwa vifungu hivi vya kulinda deni (retention) tena vikiwa na tozo mbalimbali zinazombana mdaiwa kimsingi ni kwamba serikali imeamua kufanya biashara kwa mtindo tofauti huku ikijinasibu kuwa mkopo huu wa elimu ya juu sio mkopo wa kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inatekeleza jukumu lake la kimsingi la kutoa huduma ya elimu yenye ubora, kuwekeza katika rasilimali watu kwa kuibua wataalamu watakaoweza kulisaidia taifa . Serikali ione umuhimu wa kutoa elimu bure mpaka chuo kikuu kwa kuwa nchi hii ni tajira sana kwa rasilimali na bado zipo rasilimali lukuki zinazozidi kuvumbuliwa kila siku kwa kuwa jambo hilo linawezekana. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani iko tayari kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wataalamu wa serikali ili kujadili kwa pamoja namna ya kufanya ili kuhakikisha elimu ya juu nchini inatolewa bure na kwa ubora wa hali ya juu ili kupata vijana wenye uwezo wa kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili taifa letu.

## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika,
Utunzaji wa mazingira ni jukumu la msingi la kila Mtanzania. Kumekuwa na ongezeko la uchafuzi wa vyanzo vya maji na pembezoni mwa kingo za bahari, maziwa, mito na mabwawa vinavyotokana na shughuli mbalimbali za binadamu zikiwemo shughuli za kilimo, ujenzi wa makazi na hoteli,uchimbaji wa madini, ukataji miti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika,
Ni dhahiri shughuli hizi zote zimekuwa na athari kubwa za kiafya na kimazingira nchini na duniani kwa ujumla. Kumekuwepo na usimamizi na utekelezaji mbovu wa sera na sheria mbalimbali zinazosimamia utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika,
Kwa mujibu wa kifungu cha 57(2) cha Sheria ya Mazingira ni muhimu serikali ikatoa elimu kuhusiana na mipaka hiyo ya mita sitini, na iweke bayana mipaka inayoonekana kwa wananchi ili kuepusha matatizo kwa wananchi wetu ambao kimsingi wengi hawana utaalamu na uelewa wa masuala ya kisheria

katika upimaji huo wa maeneo yaliyo karibu na kingo za mito, mabwawa, bahari au maziwa.

Mheshimiwa Spika,
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha inaweka mipaka kabla ya utekelezaji wa sheria hii ili kuwaepusha wananchi hususan wale waishio vijijini kujikuta mikononi mwa sheria kwa kushindwa tu kufahamu au kuelewa matakwa haya ya kisheria.

SHERIA YA LESENI YA USAFIRISHAJI

Mheshimiwa Spika,
Sekta ya usafirishaji ni moja ya sekta muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa. Ni moja ya sekta inayokusanya kodi kubwa kwa serikali na hata kutoa ajira kwa vijana. Kwa mujibu wa taarifa ya TATOA ya tarehe 13 Septemba 2016, sekta ya usafirishaji ilikua kwa asilimia 7.9% robo ya kwanza ya mwaka huu ikilinganisha na asilimia 14.5% ya ukuaji robo ya mwisho wa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika,
Kwa mantiki hiyo jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha kuwa kuna usimamizi wa kutosha katika sekta hii ya usafirishaji nchini ikiwa ni pamoja na utoaji wa leseni na utoaji wa adhabu kwa wale wanaokiukwa taratibu zote za usafirishaji nchini.

Mheshimiwa Spika,
Kwa mujibu wa kifungu cha 35 (b) cha muswada huu wa sheria kinazungumzia adhabu ya kutaifishwa kwa chombo cha usafiri kutokana na kujirudia kwa kosa la dereva la kutumia gari kinyume na leseni iliyotolewa chini ya kifungu hicho. Kifungu hiki kinapendekeza adhabu ya kutaifishwa (forfeit) kwa gari hilo endapo dereva wa gari hilo ametenda kosa hilo zaidi ya mara moja.

Kwa mantiki hiyo, kosa lililofanywa na dereva litapelekea kutaifishwa kwa gari ambalo kimsingi yeye sio mmiliki wake. Mfano, dereva anayefanya makosa kama kukimbiza chombo cha moto kupita kiasi (overspeeding) uendeshaji holela (reckless driving) kusababisha vifo au majeruhi n.k., ni makosa ambayo devera husika anapaswa kuwajibishwa mwenyewe na sio kutaifisha chombo cha usafiri ambacho sio mali ya dereva. Vile vile, kifungu hicho kinaitaka mahakama iwe na mamlaka ya kutoa amri ya kutaifishwa kwa gari lilohusiswa na kosa la kutokuzingatia masharti ya leseni kama ilivyoelezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika,
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafuatayo. Kwanza, kifungu cha (35) cha muswada huu kiweze kutofautisha makosa yanayofanywa na madereva na makosa ya wamiliki wa vyombo vya usafirishaji nchini.

Pili, kifungu hicho cha 35(b) kiachie mahakama itoe adhabu stahiki kwa mujibu wa makosa na sio kupendekeza au kuipangia mahakama aina ya adhabu inayopaswa kutolewa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 47(a) kinazungumzia ulipaji wa faini pale mkosaji anapokiri kosa ambapo mkosaji huyo anaweza kulipa nusu ya faini. Pamoja na kuwa kifungu hiki kinaweza kutoa fursa ya kupunguza mirundikano wa kesi Mahakani, lakini pia kinaweza kuwa ni kifungu kinachofungua milango ya rushwa hasa katika mchakato wa ufifilishaji wa kosa. Hii ina maana kwamba kifungu hiki kinatoa mwanya kwa mamlaka husika kufanya makubaliano (negotiations) na mtenda kosa ili kuweza kulipa nusu ya faini hiyo.

Mheshimiwa Spika,
Tunapotaka kutoa mwanya huo ni lazima tutambue hali halisi ya sasa kiuchumi na kisiasa nchini. Tukumbuke kuwa mpaka sasa serikali imefanya fedha ya makusanyo yatokanayo na makosa ya usafirishaji na yale ya barabarani kwa ujumla wake kuwa sehemu ya makusanyo ya mapato. Hii ni kutokana na kuwa vitengo vya usalama barabarani vimekuwa vikitangaza fedha iliyokusanywa kwa kila kanda ili kuongeza ushindani katika kukusanya mapato. Mfano, Mnamo Mwezi Februari jeshi la polisi lilikusanya bilioni 1.9 kutoka Kanda ya Pwani. Jambo hili sio muarobaini wa kupunguza makosa ya barabani bali linatengeneza tabia za kiuonevu kwa watumiaji wa vyombo vya moto barabarani ili kukusanya mapato.

## HITIMISHO

Mheshimiwa Spika,
Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini katika kujenga Taifa bora lenye watu wanaoweza kuisaidia serikali kutimiza wajibu wake na vilevile kuisaidia kuona mapungufu ya kiutendaji pale ambapo serikali hiyo haiyaoni. Hivyo basi ni jukumu la serikali kuyafanyia kazi masuala ambayo tumeyazungumzia katika maoni haya.

Mheshimiwa Spika,
Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha.

-----------------------------------------------
TUNDU A.M. LISSU (MB)
MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIBA NA SHERIA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sasa hivi ni saa 12 na tukiwa na wachangiaji sita tutamaliza saa moja, akiingia *AG* kujibu hoja zake, itabidi tuongeze muda. Kwa hiyo ruhusa nitatoa kwa nafasi sita na uwiano wa mbili upande huu wangu wa kushoto na nne kwa upande wangu huu wa kulia na kila muda itakuwa ni dakika 10. Tunaanza na Mheshimiwa Waitara.

*(Hapa Mheshimiwa Waitara hakusimama)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Mngwali, ajiandae Gekul.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na kutuwezesha kuwa hapa mchana huu ili kujadili mambo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti kama alivyosema Mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani, kazi tulinayo mchana huu si ndogo na kwa kuwa mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na sheria hata sisi kwenye Kamati tulijiona kwamba tuna kazi kubwa. Sheria ni nyingi, kwa hiyo ilituchukua muda na vikao kadhaa kuweza angalau kufikia pale tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya marekebisho ambayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameyaleta kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria yametoka kwenye mapendekezo ambayo Kamati tulikuwa tumeyafikia kwa sehemu kubwa sana na nyongeza ndogo tu ya kufanya katika maeneo mawili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja ni lile linalohusu mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na mengi katika ambayo yamesemwa ni namna ya kuwaweka waajiri mahali ambapo panawapa majukumu au panawaingiza katika makosa wakati wao mwanzoni hawakuwa sehemu ya mkataba huu. Kwa hiyo, maoni ya wengi ilikuwa ni kwamba waajiri waenziwe lakini pia…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaomba utulivu kwenye Bunge.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** ...lakini pia wapewe masharti nafuu sana ili na wao waweze kushiriki vyema katika zoezi hili la kusaidia kukusanya mikopo na

wasitishwe wala wakaona wanabebeshwa majukumu makubwa zaidi kuliko wale wenyewe ambao hawakuwa sehemu ya mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaopewa mikataba wanawadhamini wao, kwa hiyo, wadhamini wangekuwa wanabeba sehemu kubwa ya kuhakikisha kwamba mikopo hii inarejeshwa. Pia ni jambo ambalo linatakiwa lichukuliwe kwa tahadhari sana kwamba ikiwa tutawapa masharti magumu sana waajiri, basi tuwe na tahadhari kwani hii inaweza ikarejea kwa vijana wetu ikawa wanaonekana kama ni watu wasumbufu badala ya kuwasaidia pamoja na elimu zao ikawa tumewapa jukumu kubwa tena la kuwa wazururaji wa mitaani kwa kuwa waajiri wengi watakataa usumbufu na kwa hiyo watawaacha vijana wetu ambao ni wanufaika wa mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana haya tuyaangalie kwa umakini mkubwa yasije yakaturudia sisi ikawa ni hasara badala ya faida ambayo tunaitarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* nyingine ni kuongeza tu fikra katika suala la *SUMATRA*. Hili tulilijadili sana kwenye Kamati maeneo yale ya kutoza faini na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ameiweka hapa kwamba tahadhari kubwa ichukuliwe kwamba ile faini inalipwa vipi. Vile vile huyo anayetozwa faini, hilo neno kukubali kosa nalo pia linatakiwa liwekewe tahadhari kubwa kwa sababu na niliwahi kusema hapa kwamba, sentensi hiyo pia inatumiwa na Jeshi letu la Polisi wa Usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dereva unapofanya kosa barabarani, unajaziwa fomu halafu unaambiwa usaini kwa sababu fomu yenyewe imeshajazwa kabla ya kuulizwa wewe mhusika na vile vile wanamlazimisha mhusika yule alipe fani pale pale kwa yule askari tofauti na ambavyo ile karatasi inaeleza kwamba faini ile inaweza ikalipwa ndani ya siku saba katika ofisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kwa *SUMATRA* pia linahusika kwamba *SUMATRA* wasiwe wao wakusanya pesa barabarani tu na wala hii kumfanya mhusika wa kosa kulazimishwa kwa maana ya kujaziwa makosa kabla au kama ilivyowekwa kwenye hii Sheria kwamba wanamshawishi mtu eti kwa kumpunguzia adhabu alipe nusu ya faini ikiwa atakubali kulipa pale. Sidhani kama hii ni namna nzuri sana ya kuweka sheria ambazo tunatarajia zidumu na zilete ufanisi na zilete mtangamano katika makundi mbalimbali ya jamiii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bilago, ajiandae Mheshimiwa Ridhiwan.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Kwanza naomba niseme kwamba, kama wafanyakazi wa Tanzania wangefahamu kuna mabadiliko katika Sheria hii ya *Public Service Act* na *negotiating machinery* wangejaa humu. Viwanja vya Bunge vingejaa wafanyakazi wa Tanzania, lakini kwa sababu hawafahamu kinachokwenda kufanyika wapo kimya na Watanzania wetu ni wapole kama kondoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza bomu ambalo litalipuka kwa wafanyakazi wa nchi hii. Mabadiliko yanayokwenda kufanyika kwenye *Public Service Act,* yanapingana na *ILO Conventions, Convention* namba 98 ya mwaka 1949. Naomba niinukuu, *Convention 98, article 4* inasema hivi:

"*Measures appropriate to national conditions shall be taken, wherenecessary, to encourage and promote the full development and utilisation of machinery for voluntary negotiation between employers or employers'organisations and workers' organisations, with a view to the regulation of terms and conditions of employment by means of collective agreements.*" Naomba upigie mstari haya maneno; *by means of collecting agreement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanayotaka kuja kupewa Katibu Mkuu apange mishahara ya watumishi yanatoka wapi? Mimi sijui *AG* anataka ku-*achieve* nini katika hili. Utumishi wa umma hauwezi kuwa kama *grocery* ambayo mtu mmoja anaweza akapanga mishahara ya watu wote hawa. Akapanga posho za watu wote hawa, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya yanapingana na *CMA Commission for Mediation and Arbitration* (Tume ye Usuluhishi na Uamuzi) ambapo mtumishi yoyote akiwa *aggrieved,* kwa mfano amefukuzwa kazi lazima awe ameripoti kwenye Tume ya Utumishii na Uamuzi ndani ya siku 30. Hii imesema twende kwa Katibu, twende kwenye Tume ya *Public Service Act* au twende kwa Rais; atakuwa ameshapoteza haki ya kukata rufaa na kusikilizwa na hii itapoteza haki ya watumishi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie hii *ILO Conventions,* Tanzania ime-*ratify* tarehe 30 Januari, 1962; leo hii yote tumefunika kwa sababu ya kumfurahisha baba yetu. Tunatengeneza mabadiliko ya sheria kwa ajili ya ku-*favor* mtu na alisema atapunguza mishahara ya watu. *He had no grounds,* anatafutiwa *grounds* za kupunguza mishahara ya watu. Hii ni hatari katika nchi

hii. Ndugu zangu nawaambia hata upande wa CCM, watumishi wapo ambao ni wana-CCM wazuri lakini hili hawatalifurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuweka maisha ya wafanyakazi rehani, mtu mmoja anakaa kuamua mambo ya watu wengi. Mabadiliko haya yanapingana na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2003 *(Employment and Labor Relations Act)* ya 2004. Sijui *AG* anatuambia nini juu ya hili? Anatueleza nini juu ya Sheria zote hizi. Anakwenda kufuta kabisa haki ya mfanyakazi kudai haki yake, haki ya mfanyakazi kujadiliana na mwajiri wake juu ya maslahi yake. Hakuna maslahi yatakayojadiliwa bila kuwa na *collective bargaining.* Hawezi mtu mmoja akapanga mishahara na marupurupu ya wafanyakazi? Katibu Mkuu ni nani? Hizo ni sheria tulizo-*ratify* sisi wenyewe, tulikubali kwamba watakuwa wanakaa watatu; mwajiri, mtumishi na Chama cha Wafanyakazi kujadili maslahi ya wafanyakazi; mishahara na hayo marupurupu yanayofanana na kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria hiyo ambayo tunataka kwenda kuifanyia marekebisho, naomba niisome, inaipa mamlaka hii sheria iweze ku-*prevail* inapogongana na sheria zingine. *Public Service Negotiating Machinery Act* ya mwaka 2003 na yenyewe hii ime-*prevail,* ni ipi atakayochukua ndugu yangu *AG,* kati ya hizi mbili? *Public Service Negotiating Act* na yenyewe ina-*prevail* ambayo inazungumzia haki na maslahi ya wafanyakazi wa nchi hii. Hii nayo unataka i-*prevail* zote ziwe zina *prevail*, mtumishi atachukua ipi aache ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweka maslahi ya wafanyakazi rehani. Tunawaingiza kwenye mgogoro. Masuala ya utumishi yasifanywe kisiasa. Ndugu yangu Chiluba aliwahi kutunga sheria ambayo alisema atakayekuwa Rais asijihusishe na mambo ya siasa akistaafu. Alipostaafu yeye akaanza mambo ya siasa wakamchomolea waraka wa Sheria aliyotunga akiwa madarakani. Leo hii tunatunga sheria kudhibiti wafanyakazi na maslahi ya wafanyakazi kwa sababu tu ya maslahi ya mtu anataka watu waishi kama mashetani, hataki waishi kama malaika, haitawezekana. Kuna siku na yeye itakuja kula kwa watoto wake wakiwa watumishi watakapokuja kukosa haki kutokana na haya mabadiliko tunayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo gani juu ya utumishi wa wafanyakazi? Kwanza kupunguza mshahara wa mtu ni dhambi na ni kinyume cha sheria, alishaishi kwa *standard* ya mshahara fulani, leo hii tunatengeneza mazingira ambayo watu watakuwa wanapunguziwa mishahara yao. Mmoja ana-*regulate,* ana-*harmonize remuneration, allowances and other fringe benefits,* hiyo mliiona wapi *AG*? Nchi hii tutaonekana watu wa ajabu na hii

kwenye *ILO Conventions,* inaruhusiwa nchi kwenye kushtakiwa kwenye Shirika la Kazi Duniani inapo-*violate* sheria za wafanyakazi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ikishindikana humu ndani kwa sababu ya wingi wenu ni kuipeleka *ILO* na kuwaambia hawa watu wamevunja Sheria za Kazi na ita-*hold water* kwa sababu… muda umeisha?

**WABUNGE FULANI:** Endelea!

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** ...kwa sababu kinachofanyika hapa ni kufurahisha mtukufu, tusitunge Sheria ya kumfurahisha mtukufu, tutunge Sheria itakayolinda maslahi ya wafanyakazi katika nchi hii na tunazo Sheria nzuri sana kama ilivyoeleza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Sheria za utumishi ziko vizuri, tusizibadilishe kwa sababu ya kumfurahisha mtu mmoja, mtukufu. Hivyo kuliangamiza Taifa la wafanyakazi wanaokwenda kwenye hali ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kwenye hizi *remedies* ambapo kifungu cha 32(a) *A public servant shall, prior to seeking remedies provide for in labor laws, exhaust all remedies as provided for under this Act.* Hii ni hatari. Wafanyakazi watafukuzwa na hawatakuwa na pa kwenda, utakuwa ukifukuzwa ukirudi kwenye chombo cha kukusaidia wewe uliyefukuzwa urudi kazini wanakwambia ulishapoteza muda, ulishachelewa na kwa sababu walisema uende ku-*exhaust* huku na hii haikusema utakapo-*exhaust* hapa unaweza ukarudi kwenye sheria zingine kama *CMA* ambayo ni nzuri kabisa kwa wafanyakazi na imewaokoa wafanyakazi wengi kutopoteza haki zao za utumishi. Leo hii tunatengeneza sheria ya kupoteza haki za wafanyakazi na tunashangilia kabisa na *AG* anakuja na nguvu zake zote, anataka kubadilisha wafanyakazi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wanapoteza haki zao, 2020 ndiyo mtaanza kusema mnawapenda, leo mnawapenda kivipi? Wakati wa uchaguzi ndiyo mtawapenda, baada ya kuchaguliwa mnataka kuwaangamiza, itawakaanga hii, haitawasamehe, haitawaacha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ridhiwani, ajiandae Mheshimiwa Mmasi ndiyo mchangiaji wa mwisho, kuna mabadiliko.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba nzuri na mijadala mizuri ambayo inaendelea sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mwanasheria ningeomba nijikite moja kwa moja katika kuzungumzia sheria na sio mipasho kama wenzangu wengine waliotangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada wetu inazungumzia sheria ya vyombo vyetu vinavyoruka, lakini Sheria hii inampa mamlaka yule Mkurugenzi Mkuu wa viwanja vya ndege nafikiri kama tafsiri yake itakuwa sahihi, kuweza kukamata ndege, kuomba *reflection* na hata pia kuita ndege kama ikiwa inataka kuondoka katika kile ambacho kisheria kinatamkwa kwamba kufikiria kwamba kuna tatizo katika ndege hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ni Mwanasheria na napenda sana haki na haki ili itokee msingi mkubwa zaidi ni kufuata utaratibu wa kufanya maamuzi katika utaratibu wa Kimahakama. Katika lugha fupi tunasema katika *judicial proceedings,* sasa mtu mmoja kukaa ofisini na kufikiria kwamba ile ndege ina tatizo fulani aka-*order* hiyo ndege iwekwe chini au isiondoke, binafsi yangu sioni kama liko sawa. Isipokuwa kwa kuwa Mwanasheria Mkuu anajua nia madhubuti ya kutengeneza jambo hili, ningemwomba atakapokuja kutoa majumuisho basi atueleze nia ya Serikali juu ya jambo hili kabla hatujaamua kupiga kura na kupitisha au kukataa kipengele hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi niseme kwamba kipengele hiki kitatuweka kwenye matatizo. Kuna ndege kubwa ambazo hizo tunazijua hasa zile za nje zinataka ziende kufanya *connection* kwa maana ya *transit* huko nje. Ukiziweka hapa zinaweza zikachukua muda mrefu na baadaye tuka *discourage* hata usafiri wa watu wanokwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia kipengele kidogo kipya cha 19A ambacho kimeongezwa, binafsi yangu sijakielewa. Ningemwomba Mheshimiwa *AG* atoe maelezo ya kutosha katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia niwapongeze kwa kuweka vizuri utaratibu wa kukusanya fedha za wale ambao wamekopeshwa katika waliokwenda kusoma elimu ya juu. Pia niungane na wenzangu wa mwanzo kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kipengele cha kuwaambia wanafunzi walipe baada tu ya kumaliza masomo yao kwa kweli hiki hakijakaa vizuri na sababu kubwa kwangu ni hii ifuatayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu matatizo ya kupatikana kwa ajira kwetu bado yameendelea kuwa ni mtihani mkubwa na pia wanafunzi hawa wanapomaliza mpaka wajipange waweze kupata uwezo

wa kuanza kulipa nao wakati mwingine imekuwa ni mtihani mkubwa sana. Ningeomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu, pia aangalie kama Serikali uwezo wa kufungua milango mizuri ya ajira ili vijana hawa wapate kurudisha fedha mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niipongeze sana Serikali kwa kuleta Sheria ya mabadiliko katika *Public Service Act.* Waheshimiwa Wabunge mnaweza kukumbuka, katika Bunge lililopita, kumekuwa na shida kubwa sana na hata kulalamika sana kwa baadhi ya Wabunge nikiwa mimi mmojawapo juu ya marupurupu wanayojilipa hawa ambao wanajiita wafanyakazi na wanachama wa Bodi mbalimbali zile ambazo Serikali Kuu haina mkono mrefu ndani yake. Tumeshuhudia malalamiko hayo wafanyakazi wengi na bodi nyingi zikienda kufanyia Hong Kong, Marekani na maeneo mengineyo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tija ya safari zao ikiwa hatuzioni, binafsi yangu niipongeze Serikali kwa sababu sasa ule mwiba au mwarobaini wa ugonjwa ule unaletwa sasa. Niipongeze Serikali kwa kuona kwamba kuna kila sababu ya kuendelea kusimamia mambo hayo. Sheria yetu katika mabadiliko madogo ya kipengele cha 8(3) ambayo inampa mamlaka Katibu Mkuu Utumishi ya kuoanisha na kuainisha mishahara, posho na marupurupu mbalimbali wanayojilipa hao wenzetu kwenye bodi huko na hata wakati mwingine ilipokuja kuambiwa kwamba Wabunge sio *member wa board* wengi tulilialia kwa sababu tunajua kwamba sasa mzee ulaji nao umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo pia kupitia Sheria hii niipongeze Serikali kwamba, sasa inaweka uhusiano mzuri au uwiano mzuri juu ya mshahara, maana kuna bodi nyingine zilikuwa zinajipangia tu mishahara halafu unasikia tu huko kwamba "bwana Mkurugenzi wa Bodi fulani analipwa mabilioni ya fedha halafu kazi ambayo anafanya wakati mwingine haionekani" japokuwa kuna wengine najua watahuzunika kwa kipengele hiki. Binafsi niseme naunga mkono sana hoja kwenye kipande hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuendelee kuangalia maeneo mbalimbali na hasa tuzingatie zaidi yale maeneo ambayo mkono wetu au mkono wa Serikali usije kujikuta unaingia katika kukabiliana na *interest* nyingine. Mfano, katika eneo kama la Mahakama ambao wana chombo chao ni eneo ambalo kidogo ingebidi Serikali iangalie vizuri na kuona utaratibu utakapokuja basi tusiingie kwenye migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia nizungumze kidogo katika jambo zima la mamlaka ya leseni. Niipongeze Serikali kwa kuleta sheria hii pia ninayo maneno machache ya kusema juu ya utaratibu wa kugawiwa kwa leseni. Nimeona pamoja na utaratibu ambao umewekwa pia liko jambo ambalo sasa ni jipya limeingizwa jambo la utoaji wa adhabu.

Mheshimiwa Menyekiti, ningemba sana Serikali inapokuja kutoa majumuisho hapa ione sababu ya kutenganisha juu ya nafsi hizi tatu katika utaratibu mzima wa uendeshaji wa vyombo vya moto. Natambua yako magari, wako wenye magari na wako watu wanaitwa madereva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuhukumu gari kwa kosa alilofanya dereva si jambo zuri. Natambua kwamba, katika marekebisho yake Mheshimiwa *AG* ametenganisha jambo hilo, lakini bado adhabu kuondolewa kwenye magari ni jambo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na mwisho sio kwa umuhimu sana, nizungumzie jambo la mazingira, *Management of Environment Act,* kwa kipindi kirefu sana hasa mimi ninayetokea Chalinze, nimekuwa nalalamika sana juu ya uharibu wa mazingira hasa katika eneo letu la Wami Mbiki. Mazingira yameharibika sana, kiasi kwamba imefikia sehemu sasa hivi hata wanyama wakali kama tembo wanafikia sehemu ya kuingia kwenye Mji wa Chalinze, kwa sababu tu mazingira katika maana ya njia zao, watu wameanza kujenga nyumba, pia ng'ombe wengi waliojaa katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii kusema kwamba ng'ombe hawa hawafai, lakini nataka niwaeleze ndugu zangu, ukweli kwamba mifugo hii ya ng'ombe imekuwa inaharibu sana mazingira. Leo hii, tunapozungumza hapa Bonde la Mto Rufiji, linataka kupotea, bonde la Mto Wami linataka kupotea, maeneo mengine mengi sana ya mabonde yetu na mito yetu nayo pia yanapotea. Nakumbushwa hapa kwamba kuna Mto unaitwa Mbwemkuru nao pia unapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana huyu Mheshimiwa Waziri wa Mazingira anapokuja, pamoja na kutuambia mambo mazuri haya, naomba ndugu yangu Mheshimiwa January Makamba atambue kwamba kilio cha uharibu wa mazingira kinagusa kila mtu. Mazingira yetu kama hatukuyaweka vizuri leo, kesho ndio kilio chetu kitakuwa kikubwa sana. Ningemwomba sana, pamoja na sheria hii ya *management* ya mazingira, basi atakapokuwa anatengeneza zile sheria ndogo aangalie juu ya uhifadhi wa mabonde yetu haya ili kwenda kuweka uoto wetu wa asili vizuri, maji yetu yapate kupatikana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana naingalia Chalinze yangu na mradi mkubwa wa maji ambao tunatengeneza pale naweza kufika ndani ya miaka mitano tukabakiwa na mitambo mitupu halafu maji yakawa hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja ya Serikali lakini pia nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wengine wanapokuja…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester M. Mmasi na Mheshimiwa Bashe utapata dakika tano.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Bunge lako hili Tukufu. Kwanza napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kumtendea haki kijana wa Kitanzania ili naye aweze kupata fursa ya kuweza kwenda elimu ya juu, kwa maana kwamba fursa ile ya mkopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinasema kwamba, kwenye bajeti ya mwaka 2015/2016, Bodi ya Mikopo ama Wizara ya Elimu iliweza kutenga shilingi bilioni 340 na wanufaikaji katika Mfuko huo walikuwa ni wanafunzi 90,000. Hata hivyo, baada ya Mheshimiwa Rais kuingia madarakani na kupitia ilani na ahadi yake kwa wananchi alitambua dhamana yake aliyopewa na wananchi na hata kuongeza fursa ile ya mkopo kutoka bilioni 340 mpaka bilioni 473 kwa kipindi cha miezi mitatu; hili tunabidi tutoe pongezi za dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza kuchangia kwenye Muswada huu au Mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria hii ya Bodi ya Mikopo, naomba nianze kujikita kwenye kifungu kile cha 17 ambacho kinaongelea *board composition* ya Bodi hii ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameletwa mapendekezo kwako kwamba na *NACTE* pengine na wao wapate nafasi. Mimi nimeenda mbali nikaona kwamba, suala la *affirmative action* ni suala muhimu sana kwetu sisi akinamama, nafikiri tunahitaji *representative from women collision platform* ambaye atakuwepo pale katika kutetea maslahi mazima ya masuala ya *gender*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu, suala la *gender* au suala la usawa wa kijinsia ni suala nyeti sana. Hii ni agenda ya kidunia, ni agenda ya Watanzania, lakini pia ni agenda yetu sisi wanawake wa Bunge hili, yaani *Women Parliamentary Conquers*. Tunaomba nafasi ya mwakilishi kutoka *platform* ya wanaharakati wa masuala ya *gender*.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda pia kifungu cha 18 utaona pale tunaongelea *liability and obligation of loan beneficiary.* Ukisoma pale 19 *section (1)* inaongelea kwamba ni wajibu wa *loan beneficiary* kuweza kurudisha mkopo ndani ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda *section* 19(5)(a) inaongelea kwamba, *beneficiary who engage in self-employment*, *any trade or occupation of professional shall,* yaani hapa Serikali inajaribu kumtambua kijana ambaye ame-*struggle* aliko *struggle,* akafika sehemu akajipatia kipato ili aweze kulipa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunafika hapa kuona kwamba suala la ajira ni suala la kijana aweze ku-*struggle* mwenyewe na kuweza kutoka. Ni dhahiri kwamba Serikali, pengine inajivua jukumu hili, sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye bajeti iliyopita, tulisimama hapa tukasomewa mipangilio ya Serikali yetu hii katika kumkwamua kijana wa Kitanzania. Kwa sababu, bila ajira hakuna kulipa hayo madeni na kinachotukalisha hapa ni ajira kwa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema kwamba Mfuko wa Vijana wa Taifa, utengewe bilioni moja. Kaka yangu Mavunde pale, amekuwa na jitihada kubwa sana za kutaka kusaidia vijana wenzake, lakini atakwama kama Mheshimiwa Mpango hataweza ku-*release* zile pesa ziende pale kujenga ajira ya Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tofauti na mpangilio wa ajira, ni kwamba tunao utaratibu mbovu sana kwenye Bodi hii ya Mikopo. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, kwenye hili nitaomba tusikilizane. Iko hivi, nasema utaratibu mbovu pamoja na changamoto tulizonazo, kwamba pesa hizi hazirudi, lakini pia kuna utaratibu mbovu ndani ya *board* hii. Mheshimiwa Waziri ni shahidi. Ukienda pale Chuo cha Kampala *International University (KIU),* Bodi ya Mikopo ina-*release* pesa nyingi kuwasomesha vijana wa Kitanzania kwenye fani ya Ufamasia, lakini ukienda kwenye Baraza la Mafamasia Tanzania, vijana wale hawaajiriki popote. Huu ni utaratibu mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namsihi Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aliangalie hili suala kwa macho yenye upana, kwa sababu inawezekana tukatambua nguvu zake na jitihada zake, lakini bado akakwamishwa na watendaji ambao bado hawajielewa kwenye nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivi inashindanika nini kwa Bodi ya Mikopo ku-*release* pesa za kutosha kuongeza *enrolment* kwa chuo hiki cha Dodoma ambapo tayari…

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mwenyekiti taarifa

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ambapo tayari kuna…

**MWENYEKITI:** Taarifa

**TAARIFA**

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) ambayo sipendi niisome. Mheshimiwa Mbunge wakati anachangia…

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Zungumza na kiti.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mbunge wakati anachangia sasa hivi, amesema kwamba katika mwaka wa fedha wa 2015/2016. Bunge lilipitisha shilingi bilioni 370, kwa ajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu, lakini kwa mujibu wa *record* zilizopo hapa, fedha iliyopitishwa katika mwaka huo ni bilioni 473 na katika mwaka huu wa fedha, Bunge limepitisha bilioni 481, ni ongezeko la shilingi bilioni 10 tu na siyo bilioni 100 ambayo yeye amesema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikataa taarifa hiyo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa!

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninasema kwamba tusikilizane, nilichosema kwenye bajeti ya mwaka 2014/2015, bajeti iliyokuwa imetengwa ni shilingi bilioni 340. Bajeti ya mwaka 2015/2016 ilitengwa shilingi bilioni 473. Kwa hiyo, nilichoongelea hapo ni mafaniko ambayo tunayapata ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu naomba kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nilichokuwa nimejenga hoja yangu ni kwamba, hebu tuone umuhimu wa kuweza kudahili wanafunzi wa kutosha kwa chuo chetu cha *UDOM* kwa sababu pale kuna *College of Health* ambayo nafikiri tukijengea uwezo tukamaliza hii miundombinu ambayo iko pale, ambayo pengine tunafikiri bado inaweza isi-*accommodate* vijana kwa kiwango kile tunachokitaka. Tukimalizia *infrastructure* ambayo iko pale *UDOM* ni dhahiri kwamba tutapeleka pale vijana, watakopesheka na ni dhahiri wataingia kwenye mfumo wa kuajirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nasema hivi kwa sababu, ukiangalia takwimu, hizi ni takwimu za juzi tu, nimezipata siku ya Ijumaa. Tunasema kwamba, kwenye *enrolment of this academic year*, ninavyoongelea Ijumaa iliyopita. Takwimu zinasema hivi, tulikuwa na wanafunzi 7311, ambao walikuwa wanatakiwa kudahiliwa Chuo Kikuu cha *UDOM*, lakini mpaka siku ya *Friday* kulikuwa na wanafunzi 3906 sawa na asilimia 50.3 ambayo tayari walikuwa wamepata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukijaribu kufunga Mfuko ambao unavuja, kule *KIU* tukauleta pale *UDOM* ni dhahiri wanafunzi hawa wataingia kwenye mfumo wa ajira. Kwa hiyo, huu utaratibu uangaliwe upya, sio utaratibu wenye afya na sio utaratibu ambao utaweza sisi kutufikisha kwenye azma ya kumsaidia mtoto wa Kitanzania na kwenye azma ya kuona kwamba, Mfuko huu unashindwa kukidhi malengo ya Tanzania tunayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala hapa ukisoma *section* 19. Pale naanzia (a) ambayo inaongelea hiyo hiyo *liability and obligation of loan beneficiary.* Utaona kwamba ni jukumu la mfanyakazi au la mtumishi aliyeajiriwa kuhakikisha kwamba pesa zinakatwa. Lakini pesa hizo, ahakikishe yeye pamoja na majukumu ya mwajiri, huyo huyo ahakikishe pesa inaingia *Loans Board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifike kusema kwamba yawezekana labda *Loans Board* imepungukiwa uwezo wa kuleta ufanisi katika *board* ile. Basi ninachoshauri ni kwamba, kwa kuwa tunaona majukumu ya *Board* tumpe na

mtumishi ambaye ameajiriwa, kwenye utumishi wa umma, kwamba iwe ni jukumu lake kuhakikisha pesa zinakatwa na mwajiri, pesa zinaenda *Loans Board*. Pengine tuone umuhimu wa kuweza kushirikiana na *financial institutions* na kutoa hili jukumu la *Loans Board,* kulipeleka kwenye *financial institution* na sisi tukalipa *management fee* ili tuweze kuondokana na mizigo ambayo tunafikiri kwamba haitatufikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, bajeti nzima ya kuendesha haya masuala ya uratibu wa Mfuko huu, inafika karibu bilioni 30. Kama tutapeleka kwenye *financial institution* ni dhahiri kwamba hizi pesa bilioni 30, tutaokoa *billions of money* tukapeleka kwenye Mfuko huu na vijana wetu wakazidi kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kwenda kwenye *section* ya 20 ambayo inaongelea *obligation* ya *employer*. Tunaona pale kwenye *section* ya 21(1) inaongelea kwamba kutakuwa na adhabu, pale ambapo mwajiri atakuwa amekata makato ya mwajiriwa ambaye ni *loan beneficiary* wa *Loans Board* na akashindwa kuwasilisha pesa ile *Loans Board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba nina mashaka ipo changamoto kwamba mifumo ya *board* haisemezani yenyewe kwa yenyewe. *Central system admission* haisemezani na *Loans Board, Loans Board* haisemezani… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele ya pili. Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kuchangia maeneo mawili tu madogo. La kwanza, ni marekebisho ya Serikali kwenye Sheria ya Mazingira. *Subsection* 15 kuna *composition* ya *trustee* ambayo itakayokuwa inasimamia masuala ya mazingira. Mapendekezo ya awali, naomba ninukuu ilikuwa inasema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the principal act is amended* kwa kuongeza idadi ya *members* kutoka tisa mpaka 11 kwamba na katika hao *members* watakaongezwa wengine watatoka katika *private sector*. Hata hivyo, *amendment* aliyoleta *AG*, anasema *the Board of Trustee may invite any person, who is not a member to participate in the deliberation of any meeting of the Board of Trustee by any person, so invited shall not be entitled to vote.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hoja yangu? Hoja yangu ni moja, ningeshauri Serikali, *Board of Trustee* kwa ajili ya kuijengea *credibility* na kwa ajili ya kuweza kusaidia ku-*mobilize funds* kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira. Tukielewa kwamba hali ya Serikali na namna ambavyo tunabana matumizi, tunaamini kwamba *board* hii itaweza ku-*source fund* kutoka nje ya mfumo wa kawaida wa kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshauri Serikali, kwamba, waruhusu katika *composition* ya *board* waweze kuacha kipengele kilichokuwa *proposed* waongezwe watu kutoka katika *private sector* ili kuijengea *credibility, board* hii kwenda kutafuta fedha nje ya mfumo rasimu wa kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kipengele hiki cha *invitation* kiendelee kuwa *retained* ambacho Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameleta. Hii itatoa fursa kwa *board* ku-*invite even international organizations* kuja kwenye hii *Boards of Trustee* na itaijengea *credibility* katika suala la kwenda kutafuta fedha. Hicho ni kipengele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili ni *section* 12(2) inasema "*A person who has paid a fine as penalty for an offence of failing or refusing to conduct an Environmental Assessment Study, shall submit to the Council an environmental management plan, for approval and guidance on how the project shall be implemented*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matokeo ambayo yanajitokeza sasa hivi, watu wanafanya *environmental assessment,* anapopewa *certificate* nyuma ya *environmental assessment certificate* kunakuwa kuna *guidelines,* lakini *most of the organizations* au taasisi nyingi hazifuati zile *guidelines.* Kwa hiyo, ninachotaka nishauri, kwa hali ya mazingira ilivyo sasa hivi, mapendekezo ya *AG* ni ku-*delete* kipengele hiki, ningeshauri Serikali ikiache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tungeongeza *enforcement* kwamba unapokabidhiwa *certificate* ya mazingira usipokwenda kufuata masharti yaliyoelekezwa katika *certificate* ile basi uweze kuadhibiwa. Bila ya hivyo kutakuwa hakuna sababu ya kumpatia mtu *certificate* yoyote ile baada ya kufanya *environmental assessment*. Hili ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nataka nishauri Serikali, hii *Public Service Act,* dunia inabadilika, *competition* ina-*grow.* Haya mambo ya kuweka *ceiling* ya mishahara, ku-*control remuneration* ya watu na sisi leo hii tunakwenda na *competition* duniani hali inavyobadilka, hebu *imagine* tutapoteza *best brains. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hofu sana katika jambo hili. Ku-*control* maposho na namna ya kulipana posho na nini, *is a good thing,* lakini mshahara, dunia ina *competition*, leo hii, tunapoweka *ceiling* kwa Mkurugenzi Mkuu wa *ATC*, tunapowawekea *ceiling,* Wakurugenzi au taasisi hizi ambazo tunatarajia watu waende ku-*perfom* vizuri, waweze kufanya kwa sababu naamini kwamba *you pay someone out of productivity* na uwezo wake wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niishauri Serikali pamoja na nia njema, ni vizuri Serikali ikalitazama hili jambo. *Is very danger* tunapoumiza morali ya *civil servant,* ni hatari kwelikweli kwa maslahi ya nchi yetu na kwa maslahi ya Taifa hili. Ni vizuri mno tukatafakari mara mbili maamuzi haya tunayoyaweka tuweke *frame work* lakini lazima tufikiri mara mbili, *what do we want to attain,* nini tunataka tupate siku ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni-*conclude* kwa kusema kwamba, hili la *Board* ya *Trustee* tunaomba ni vizuri Serikali na *AG* akakubali wazo lililoletwa na Wizara la kuomba kwamba *members* wawe 11, kuijengea *credibility board* hii ili iweze kutafuta fedha nje ya mfumo wa kawaida wa kibajeti. Tumeona hapa namna gani wakati wa bajeti tulivyopata shida kuwawekea fedha katika Mfuko wao wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nape dakika tano, Mheshimiwa Mbarawa dakika tano, Mheshimiwa Anjela dakika 15.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mifumo inayoendeshwa kidemokrasia kama wa kwetu, baada ya uchaguzi, kazi ya Serikali iliyoko madarakani ni kutekeleza *agenda* waliochaguliwa na wananchi kuingia nayo madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya ajenda kubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano, ni kurudisha nidhamu ya utumishi wa umma katika nchi yetu. Hili tuliliahidi na ndio ilikuwa moja ya sifa ambayo Watanzania walituamini nayo, wakatupa kura nyingi tukachaguliwa kuongoza Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kutekeleza ajenda mambo mawili ni ya muhimu sana. La kwanza, ni kuangalia sheria mlizonazo ni jinsi gani zinawasaidia kutekeleza ajenda ambayo mmepewa dhamana ya kuitekeleza.

Ndiyo maana Miswada ya namna hii inakuja ili isaidie katika kutekeleza agenda hiyo.

La pili, ni watu mnaowaweka kwenye maeneo mbalimbali ambao kwanza wanaamini agenda mliyonayo, lakini mbili wana uwezo wa kuitekeleza hiyo ajenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Kambi ya Upinzani moja ya kazi yao ya msingi ambayo nadhani wanaifanya vizuri, ni ya kujaribu kuzuia msifanye hayo mabadiliko yatakayowasaidia kutekeleza ajenda ili waje watumie mwanya huo kuwahukumu kwa wananchi wakati wa uchaguzi unapokuja. Pili, watahakikisha kila uteuzi mnaofanya ambao utawapeleka kwenye kutekeleza ajenda yenu wanaukosoa na kuupigia kelele vya kutosha ili msifanikiwe kutekeleza ajenda yenu. Kwa hiyo, walilolifanya si jambo la ajabu, ni jambo la kawaida na wanatimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umezungumzwa hapa uteuzi ambao umekuwa ukifanywa na Mheshimiwa Rais. Kaka yangu Mheshimiwa Tundu Lissu anajua kwa sababu ni mwanasheria, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 36, naomba niinukuu inasema hivi:-

*"Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii na ya Sheria nyingine yoyote, Rais atakuwa na mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais ana mamlaka ya kufanya uteuzi kwenye maeneo yoyote kwa mujibu wa Katiba hii. Kwa hiyo, uteuzi alioufanya hakuvunja Katiba hata kidogo, ameteua Wakurugenzi, ameteua Wakuu wa Wilaya hakuvunja Katiba lakini pia amezingatia *principle* ya kuteua watu ambao watakwenda kutekeleza ajenda ambayo ndiyo imemweka madarakani kwa sababu mwisho wa siku ndiye atakayekuja kuulizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kaka yangu Mheshimiwa Lissu anajua, amejaribu ku-*twist* maneno hapa kwamba Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene lakini anajua huyu anaitwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, mwenye Wizara yake ni Rais. Kosa la Rais hapa ni nini? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Nashangaa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye Wizara hiyo ni Rais, ndiyo maana ofisini kwake kuna Wizara mbili, haitwi Waziri tu, anaitwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, UTUMISHI na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema maneno haya tuyapuuze kwa sababu lengo lake ni kutaka kutotupeleka kwenye kutekeleza ajenda tuliyonayo na ni ajenda ya muhimu, tuna miaka mitano ya kutekeleza. Kazi ya kwanza tutengeneze na kurekebisha sheria zetu. Kazi ya pili, tuweke watu wenye imani na ajenda tuliyonayo na hao ndiyo watatupeleka huko tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nisisitize upotoshaji wa namna hii ni wa kuupuuza na sisi tusonge mbele. Rais amefanya sawasawa na aliowateua hakuvunja sheria, hakuvuja Katiba, wala hakupotoka popote…

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Amefanya sawasawa kwa sababu tunataka kutekeleza ajenda na tuna sababu ya kusonga mbele katika hili. Wangesifia ingebidi tukae kujiuliza lakini kwa kuwa wamekosoa na kupiga kelele, uamuzi huu ni sahihi na tusonge mbele. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbarawa dakika tano.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia Muswada ulioko mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa kuwasilisha vizuri na naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mawili nataka kuchangia. La kwanza, ni kuhusu Marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA),* Sura ya 413 kwa kuongeza kifungu kipya cha 40A ili kuweka masharti yanayohusu ulipwaji wa faini pale mkosaji anapokiri kosa badala ya kumpeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu una faida kubwa, kwanza unaondoa tatizo la kwenda Mahakamani ambapo baadhi ya wakati kesi zinachukua muda mrefu. Pili, utaratibu huu unapunguza sana gharama za kuendesha kesi huko Mahakamani. Utaratibu huu unatumiwa na wadhibiti wengi, kwa mfano *TCRA* na *EWURA* na unafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuzungumzia machache kuhusu Ibara ya 35 ya Muswada inayopendekeza kurekebisha kifungu cha 11(6) kwa kuainisha kuwa adhabu ya kosa la leseni za usafirishaji chini ya kifungu hicho sasa itakuwa shilingi laki mbili kwa kosa la kwanza na utakaporejea kosa kiwango hicho sasa kiwe si zaidi ya shilingi laki tano. Sheria ya zamani ya Leseni ya mwaka 1973 ilikuwa inatoa faini ya shilingi elfu kumi kiwango cha chini na kiwango cha juu ilikuwa ni shilingi elfu hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lina faida kubwa sana, kwanza ni kuweka viwango vya faini vinavyoendana na wakati. Viwango vya mwaka 1973 vimedumu kwa muda wa miongo minne na hivyo vimepitwa na wakati. Kwa mfano, shilingi elfu kumi mwaka 1973 ilikuwa sawa na dola za Kimarekani 1,400/= kwa *exchange rate* ya Dola moja shilingi saba. Kama utachukua faini hiyo leo itakuwa sawa na shilingi milioni 3. Hata hivyo, kwa kutambua changamoto zilizopo sisi tumeweka kiwango cha chini kuwa ni shilingi laki mbili na cha juu kisizidi shilingi laki tano ambapo tunaamini kabisa kiwango kama hiki kitapunguza sana ajali za mabasi barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonesha nchi ambazo wana faini kali pamoja na kutoa elimu na kutumia teknolojia ya kisasa hasa TEHAMA kwa kiasi kikubwa zimefanikiwa kupunguza ajali za barabarani. Kwa hiyo, nasi kwa kuweka faini hizi pamoja na kutumia teknolojia ya kisasa ya TEHAMA na kuendelea kutoa elimu kwa watu wanaotumia vyombo hivyo tutapunguza kwa asilimia kubwa sana ajali za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yanayopendekezwa yanalenga kuhuisha adhabu ambazo zitatolewa kwa watoa huduma watakaofanya biashara bila ya kuwa na leseni au wale watakaokiuka masharti ya leseni. Kwa mfano, gari la abiria lenye leseni linatakiwa liwe na hali ya usalama na ubora, kama gari haliko kwenye hali ya usalama itabidi walipe faini hiyo. Mfano mwingine, dereva wa gari la abiria anayeajiriwa anatakiwa awe na sifa zinazostahili kwa ajili ya kuendesha gari hilo, kama dereva huyo hana leseni sheria hii itatumika na mengine mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba niongelee mabadiliko ya sheria kuhusu usafiri wa anga. Kwenye usafiri wa anga tunataka kufanya mabadiliko hayo, ili kuleta usalama…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Angellah dakika 15, Mheshimiwa Dkt. Ndalichako na *AG* wajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kabisa kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja ya Muswada huu uliowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia kwenye Muswada nianze kuzungumzia maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Kwanza kabisa, tumemsikia na nashukuru Mheshimiwa Nape amelieleza vizuri sana kwamba Rais amekuwa akiteua viongozi mbalimbali bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Ibara ya 37(1 na (2) zimeeleza bayana kabisa utaratibu na mamlaka ya Rais katika utendaji na utekelezaji wa shughuli zake. Rais ndiye anayeteua viongozi wakuu, Rais ndiye anayeteua viongozi wanaosimamia na kutekeleza sera, lakini vilevile Wakurugenzi hawa wanaotajwa ndiyo watekelezaji wakuu au moja ya makundi ya watekelezaji wa sera, kwa hiyo, Rais wala hajakiuka chochote hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *The Ministers' Discharge of Duties Act* na katika *GN* ya 144 ya Aprili 2016, imeeleza kabisa majukumu ya Wizara moja baada ya nyingine. Ukiangalia katika Ofisi ya Rais *(the Presidency)* imeweka kabisa majukumu na mojawapo likiwemo la Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, yeye mwenyewe ndiye Waziri, lakini vilevile ana mamlaka ya kuweza kuteua. Niseme tu kwamba *delegation does not mean application* na hamna chochote ambacho kimekiukwa, lakini hata wale wateule wa Rais wanatekeleza majukumu yao kwa kufuata taratibu pamoja na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kujikita sasa katika suala zima la Sheria hii ya Utumishi wa Umma. Nimesikia hapa wako wanaosema kuna *ILO Convention* imekiukwa. Wako wanaosema kwamba haijazingatia masuala mbalimbali ya Vyama vya Wafanyakazi na wako wanaosema kwamba tunatengeneza bomu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Bilago anajua kwanza Muswada huu ulitangazwa na ukasomwa kwa Mara ya Kwanza ili watu wajiandae wausome watoe maoni. Hata hivyo, Kamati ya Katiba na Sheria ya Bunge ilialika wadau mbalimbali kuja kutoa maoni kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tunayo Sera ya Malipo na Mishahara na Motisha ya mwaka 2010. Kwa mujibu wa sera hii na imeelezwa bayana kabisa dhumuni la kuoanisha na kuwianisha mishahara na maslahi mbalimbali katika utumishi wa umma. Nimemsikia hapa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani akisema watu walikuwa wakifanya mikutano Dubai, akisema hapa watu walikuwa wanajilipa mishahara mikubwa, hivi kweli anataka au tunataka tubaki katika hali hiyo? Hivi kweli tunataka kuwa na tofauti ya mishahara wengine wana milioni zaidi ya 40 kweli katika utumishi huu huu wa umma? Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma tulikuwa na Shirika/Taasisi yetu ya *SCOP* si kitu cha ajabu hata kidogo, ilikuwa ikioanisha na ilikuwa ikiwianisha mishahara yetu. Baada ya kugundua tatizo hili, Tume ya Ntukamazina ilikuja na hoja na ndiyo maana tarehe 3 Juni, 2011 iliundwa Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Hivi ninavyoongea hapa kiko chombo kwa ajili ya kazi hiyo na kazi yake ni kumshauri Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu Utumishi wa Umma, lakini vilevile kumshauri Mheshimiwa Rais kutokana na tafiti mbalimbali inazozifanya kuhusiana na motisha, maslahi na mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa ni kutaka tu kuchanganya watu. Nimeona katika mitandao mbalimbali, nimeona *distortion* kubwa ambayo imekuwa ikifanyika kwamba posho zote zinafutwa, si kweli ndugu zangu! Labda tuoneshwe kifungu kimoja tu kinachosema kuna posho fulani itafutwa! Tunachokisema hapa, tunamwongezea mamlaka Katibu Mkuu Utumishi kwa mujibu wa kifungu cha 8(3) cha Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na majukumu yake mengine basi aweze kuoanisha na kuwianisha mishahara, motisha, marupurupu na maslahi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepunguza mishahara ya baadhi ya wakuu wa taasisi kuanzia Julai hakuna anayepata zaidi ya shilingi milioni 15. Tumeshuhudia wakuu wa taasisi wengine baadhi ya posho za nyumba wanajilipa mshahara mzima!

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Anajikuta anapata mshahara wa milioni 30 na posho yake ya

nyumba ni *equivalent* kwa mshahara wake wa mwezi mmoja! Haiwezekani! Wako ambao wana magari zaidi ya matatu, ana gari lake, la mke wake na lingine liko nyumbani kwa ajili ya *pool! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwogope Mwenyezi Mungu. Tumekuja kwa nia njema na mapendekezo haya na si nchi ya kwanza kufanya hili na sisi pia tulishapita huko. Kenya wanafanya hivyo, wanayo *Salary and Remuneration Commission*. Ireland, *South African* na nchi nyingine pia wamekuwa wakifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwarejeshe Waheshimiwa Wabunge katika kifungu cha 8(3)(e), Katibu Mkuu kupitia kwa Bodi ya Mishahara wanayo mamlaka ya kufanya tathmini ya kazi kwa ajili ya kupanga upya madaraja mbalimbali ya mishahara na miundo. Zoezi hilo tumeshaanza kupitia Bodi ya Mishahara na linakwenda vizuri, lakini kwa sasa hakuna posho yoyote inayofutwa ila itakapofikia kuna maombi mbalimbali ni lazima tuangalie uwezo wetu wa kibajeti na miundo yetu ya kiutumishi ilivyokaa na mambo mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niliweke hilo bayana ili kuweka rekodi sawa na lengo hasa la kuleta Muswada huu. Ukiangalia katika sheria mbalimbali katika miaka ya 1990 na 2000 wakala mbalimbali zimekuwa zikitunga sheria zikizipa bodi zao mamlaka za kutoa kibali cha kupandisha mishahara, haiwezekani! Ukiangalia Ofisi ya Rais, Utumishi ndiyo wana mamlaka ya kuangalia *payroll management* nzima, ni lazima waweze kujua, je, uwezo huo tunao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako ambao wanasema bodi zao zinazalisha fedha za kutosha lakini tukumbuke fedha hizi ni za umma. Hata kama shirika lako limezalisha ziada ni lazima zirudi katika chungu kikuu, ni lazima upendekeze kwa utaratibu wa kawaida na ndipo baadaye utaweza kuidhinishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Bunge, Bunge haliidhinishi mishahara yake peke yake. Bunge linapendekeza na hatimaye Rais ndiyo anayeidhinisha na ndicho tunachokifanya hapa. Bodi hazikatazwi kupendekeza, taasisi hazikatazwi kupendekeza nyongeza ya mishahara na mambo mengine, lakini mwisho wa siku tunataka tuwe na mamlaka moja itakayopitia, itakayokuwa na kumbukumbu sahihi ili kuhakikisha kwamba hatuendi nje ya mstari na bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wanaosema kwamba tunakiuka dhana ya ugatuaji wa madaraka. Hakuna popote tunapokiuka dhana hii, lakini tuseme

ni lazima kuwa na uwiano wa kipato. Nitashangaa kama kuna Serikali yoyote ambayo haiangalii uwiano wa kipato baina ya watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika suala la mashauri ya nidhamu katika kifungu cha 26 na yenyewe imezungumziwa sana. Ukiangalia katika utaratibu wa sasa liko wazi kabisa. Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma imeainisha mamlaka za nidhamu na ajira katika utumishi wa umma. Inajulikana kabisa katika masuala ya kuthibitishwa kazini, kupandishwa cheo, kuthibitishwa ajira, kufukuzwa kazi na mengine, mtu anaanzia katika mamlaka ya ajira, anaweza kukata rufaa katika mamlaka ya kwanza katika Tume ya Utumishi wa Umma na hatimaye kufikia kwa Mheshimiwa Rais. Hizi ni taratibu *administratively* lakini bado haizuii mtu atakapokuwa ame-*exhaust administrative measures* na *administrative organs* baada ya hapo kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaleta mapendekezo haya kwa sababu tumekuwa tukishuhudia wako watu katika utumishi wa umma mara tu wanapokuwa *charged* kwenye mamlaka ya ajira au katika Tume, akishafikishwa Tume tu anaenda kufungua shauri katika Baraza la Usuluhishi, haiwezekani! Ni lazima aweze kutumia nafuu zote zilizoko katika utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mwingine ameenda Tume, rufaa yake ikishakataliwa badala ya kukata rufaa kwa Mheshimiwa Rais yeye tayari ameshakwenda Mahakamani au katika Baraza la Usuluhishi, tunasema hii hapana! Ni lazima tuweke *consistency,* ni lazima tufuate sheria kama ilivyoainishwa ili kuhakikisha kwamba tunakwenda sawa. Hatumkatazi mtu kwenda Mahakamani lakini ni baada ya kuwa ameshapitia nafuu na taratibu zilizopo katika utumishi wa umma anaweza akaenda kupitia *judicial review* katika Mahakama zetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ndalichako dakika kumi na tano na Mheshimiwa *AG* ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nianze moja kwa moja kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza zaidi katika sehemu ya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Niseme tu kwanza haya mapendekezo ya marekebisho yamekuja kwa kuchelewa. Nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia pamoja na Kamati ya Sheria na Katiba kwa mchango mzuri ambao kimsingi umelenga katika kuboresha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya kuleta marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika urudishaji wa mikopo na kufanya Mfuko wa Mikopo kuwa himilivu na endelevu ili kuwawezesha Watanzania wengi ambao wana uhitaji wa mikopo waweze kuendelea kunufaika na mikopo ambayo imewekwa kwa lengo la kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia vipengele ambavyo vimechangiwa na wazungumzaji wengi. Kwanza kabisa, jambo ambalo limezungumziwa sana ni suala la muundo wa Bodi ya Elimu ya Juu. Niseme tu kwamba kazi ya Bodi ni kuiongoza na kuisimamia ile taasisi. Kwa hiyo, tukielekeza zaidi uchaguzi wa Bodi katika uwakilishi wakati mwingine kuna mambo mengine ya msingi ambayo yanaweza yasitekelezeke kwa sababu kazi na majukumu ya Bodi yameainishwa katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imezingatia maoni na mapendekezo ya wadau na katika *Schedule of Amendment* ambayo tunaileta tumekubaliana na pendekezo la kuongeza Mjumbe kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar na vilevile tunaongeza mjumbe kutoka *NACTE*. Kwa hiyo, suala hilo limezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa na suala la kuzingatia uwiano wa *gender*. Mimi Waziri ambaye pia ni mwanamke siwezi kuwaangusha akinamama wenzangu, lakini pia hiyo tumeilinda katika kuiweka kwenye sheria ili anapokuja Waziri mwingine yeyote ahakikishe kwamba uteuzi wa Bodi unazingatia *gender*. Kwa hiyo, hilo suala tumelizingatia na lipo katika *Schedule of Amendment* ambayo tunaleta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumzwa sana ni muda wa marejesho ya fedha baada ya mwanafunzi ama kuhitimu mafunzo yake au kusitisha mafunzo kwa sababu mbalimbali. Serikali ilikuwa imependekeza kwamba mwanafunzi aanze kurudisha mkopo wake mara moja kwa sababu tunatambua kwamba pamoja na tatizo la ajira lililopo, lakini wapo wanafunzi wengine ambao mara baada ya kumaliza mafunzo yao huwa wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza mapendekezo na maoni kutoka kwa Kamati, kwa waliochangia kwa maandishi na waliozungumza, Serikali imekubaliana na pendezo la kuweka muda wa mwaka mmoja tangu kumaliza lakini haimnyimi fursa yule ambaye atakuwa na uwezo wa kurejesha moja aweze kurejesha. Kwa hiyo, muda wa marejesho utakuwa ni mwaka mmoja lakini kwa yule ambaye atabahatika kupata kazi mapema arejeshe hata kabla ya huo muda wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa mwenyekiti, eneo lingine lililokuwa linazungumziwa ni eneo la kuwapa adhabu waajiri kwa kutowasilisha makato. Naomba itambuliwe kwamba makato ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ni sehemu ya makato kama yalivyo makato mengine ya kisheria. Hivyo basi tunavyosema kwamba mtu ambaye hatarejesha atapewa adhabu ni kama ambavyo inakuwa kwenye mfuko wa *NSSF na LAPF*. Kwenye hii mifuko ya kijamii mtu ambaye hapeleki makato kwa wakati anapewa adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo siyo kuwakomoa waajiri ni kuwakumbusha wajibu wao. Kwa kuzingatia hilo hata ile adhabu tuliyokuwa tumependekeza tumeipunguza, tumeiacha kama ambavyo ilikuwa kwenye sheria hii. Kwa hiyo, katika *Schedule of Amendment* tunasema kwamba adhabu lazima iwepo ili kuwakumbusha waajiri kwamba nao wana wajibu wa kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba hii mikopo inarejeshwa. Kwa hiyo, katika *Schedule of Amendment,* Ndugu yangu Mheshimiwa Riziki tumebadilisha, adhabu itakuwa ni shilingi milioni moja tu. Kwa hiyo, tunaomba waajiri nao wajione kwamba wana wajibu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa na ndugu zetu Kambi Rasmi ya Upinzani linahusu suala la Mheshimiwa Rais kutoa takwimu za fedha ambazo zinatofautiana na zile ambazo nilizitoa. Mheshimiwa Rais alizungumzia shilingi bilioni 80 kama fedha ambazo zimetolewa na Serikali kwa ajili ya posho ya kujikimu wanafunzi mimi nilizungumzia shilingi bilioni 120 nikiwa nimejumuisha kiasi cha shilingi bilioni 40 ambazo zimetolewa katika *financial year* hii kwa ajili ya *tuition fees* za vyuo. Hata katika taarifa yao wanazungumzia kwamba kuna madeni kwa vyuo ya shilingi bilioni 60, tunayalipa na ndizo hizi shilingi bilioni 40 ambazo tayari Serikali imekwishatoa kwa vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, taarifa yangu ilikuwa inajumuisha kiasi cha shilingi bilioni 80 ambazo tumezitoa mahsusi kwa ajili ya wanafunzi pamoja na shilingi bilioni 40 ambazo tumezitoa kwa ajili ya *tuition fee*. Kwa hiyo, hakuna kugongana kwa taarifa, inategemea mtu anarejea kitu lakini hakuna kupishana kwa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala ambalo limezungumzwa hapa kwamba Serikali inakuwa kama inafanya biashara kwenye mikopo. Serikali haifanyi biashara. Mikopo imetolewa kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye uhitaji.

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata mapendekezo ya kiasi ambacho tumeleta mbele ya Bunge lako cha 15% ni kidogo tu kwa sababu katika utumishi wa umma, mtumishi anaweza akakatwa mpaka abaki na moja ya tatu (1/3) ya kipato chake. Serikali hatukutaka kwenda huko, tunakata 15% tu anabaki na asilimia 85. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhana kwamba tunafanya biashara, tunatengeneza faida kwa kuwakata wanafunzi. Hakuna riba inayotozwa kwenye mikopo isipokuwa kuna tozo la kuchelewesha. Sasa kama hutaki kukatwa hiyo tozo lipa kwa wakati hakuna mtu atakayekudai, lipa kwa wakati ili watoto wengine waendelee kunufaika. Kwa hiyo, Serikali haifanyi biashara ila tunawakumbusha vijana wanaopata hii siyo ruzuku, ukikopa mkopo lazima urejeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhana hapa kwamba mwanafunzi mwingine anaweza akaacha masomo kwa sababu ameugua. Hayo yote yameelezwa wazi kwenye kanuni kwamba mwanafunzi akifariki au akiugua nini kifanyike. Kwa hiyo, ni masuala ambayo Serikali inatambua kwamba kila mtu anaweza akawa na matatizo na yote hayo yamekwishazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo, niseme tu kwamba, naomba Waheshimiwa Wabunge wote tuunge mkono mapendekezo haya ambayo kwa kweli yana lengo jema kabisa la kuhakikisha kwamba vijana wengi wananufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala alilozungumzia Mheshimiwa Ester Mmasi kuhusiana na vyuo ambavyo havina sifa. Nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba kama kuna vyuo vinaendesha programu zozote ambazo ama hazitambuliki na *Professional Bodies* mwaka huu wa fedha itakuwa ndiyo mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumza ziko timu za wataalam zinakagua vyuo vyote. Kwa hiyo, kama kuna programu zozote ambazo zinaendeshwa kinyume na taratibu tutazifungia. Pia kama kuna chuo

kikuu ambacho kilianzishwa na hakina wataalam mwaka huu wa fedha ndiyo mwisho, hii hadithi hatutaisikia tena. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuongeza udahili katika vyuo vya umma hilo tutalizingatia na hasa katika fani ya afya ambapo Chuo Kikuu cha Mloganzila tumeshakamilisha *teaching hospital*. Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba angalau katika mwaka wa masomo unaokuja 2017/2018, wawepo wanafunzi angalau ile hospitali inapotumika na mafunzo yawe yanaendelea ili tuongeze wigo wa kufundisha madaktari kwa sababu vyuo vya madaktari vimekuwa vichache. Kwa hiyo, ushauri huo utazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumziwa ni kwamba, Serikali bado haijapanga mikopo kwa wanafunzi wengi na kwamba mpaka sasa hivi ni wanafunzi 21,000 tu ndiyo wamepata mikopo. Naomba niseme kwamba tangu nilipotoa ile taarifa yangu zoezi hili la kuendelea kupanga mikopo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza limekuwa likiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi jumla ya wanafunzi 25,228 wa mwaka wa kwanza wamekwishapangiwa mikopo. Tofauti na nilivyokuwa nimetoa taarifa wiki iliyopita hadi leo kiasi cha Sh. 73,153,910,172 zimekwishatumwa na zoezi bado linaendelea kwa sababu kulikuwa na wanafunzi wengine ambao wanadahiliwa kupitia *NACTE* ambapo majina yao hayakufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kabisa baada ya ufafanuzi huu, Waheshimiwa Wabunge wote wataunga mkono hoja hii ili tuongeze tija katika makusanyo ya mikopo ili vijana wetu wasiendelee kutaabika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa *AG* dakika ishirini.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nikushukuru kwa kunipatia fursa ili niweze kuichangia hoja hii nikitoa ufafanuzi kwa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Labda kwa sababu tumekuwa na mambo mengi bado tuna majonzi tangu jana na asubuhi tumekuwa na mambo mengi lakini nilipokuwa nawasilisha hoja asubuhi, hotuba yangu ile ilikuwa *very comprehensive* na baadhi ya hoja ambazo zimezungumzwa na baadhi ya

Waheshimiwa Wabunge hapa zinajibiwa na hotuba ile. Hata hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri ambao wamepata pia fursa ya kufafanua baadhi ya hoja ambazo zimeulizwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mhshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo napenda kulisemea hapa, kwa sababu limezungumzwa kwa namna ya kupotoshwa ni hili suala la *role* ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya kuwa na jukumu la kuridhia mapendekezo ya mishahara na marupurupu mengine au posho yanayotoka kwenye taasisi nyingine za Serikali. Limezungumzwa kana kwamba hapa tunarudi nyuma na kwamba tunataka watu waishi maisha ya kishetani, hiyo siyo kweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimikwa Mwenyekiti, lakini wakati haya yanazungumzwa pia kuna mifano imetolewa hapa namna gani ambavyo baadhi ya wenzetu kwenye taasisi hizi za umma walivyokuwa wanaishi maisha *so much lavishly* lakini pia kwa namna ambayo ilikuwa na ufujaji mkubwa sana wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesikia hoja ikizungumzwa hapa na mzungumzaji mmoja akieleza namna jinsi ambavyo hata mikutano mingine ya Bodi ilikuwa inafanyika nje ya nchi, sasa tunafurahia hili? Wote sera yetu si ni kupambana na ufisadi na kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumika vizuri? Kwa hiyo, mapendekezo haya yanakuja kwa nia nzuri kabisa ili kushughulikia kasoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati haya yanazungumzwa, Bunge hili lilishajitungia Sheria ya *The National Assembly Administration Act* ya mwaka 2009, inatambua na inaweka utaratibu kwamba hata wakati ambapo Bunge lina utaratibu wa kujipangia mishahara yake na ya watumishi wake na marupurupu na kadhalika lakini inapeleka kwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imeweka masharti, msome kifungu cha 20 na 21 ya sheria hii, kwamba pamoja na Tume ile kuwa na mamlaka hayo lakini itazingatia *National economy,* uchumi wa Taifa unaruhusu, *the wage bill* na kuangalia sera nyingine katika utumishi wa umma zinazotawala masuala ya maslahi. Sheria ya Mahakama ambayo ilitungwa mwaka 2011 nayo inasema hivyo hivyo kwenye vifungu vya 30 na 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mihimili muhimu sana katika nchi hii, lakini ninyi wenyewe mliona pamoja na kujiwekea mamlaka hayo mkasema muweke utaratibu mapendekezo yetu tunayojiwekea ya mishahara, posho na

marupurupu pia yaendane na uwezo ambao Taifa linaweza likauhimili kiuchumi. Sasa kama ninyi Waheshimiwa Wabunge ambao ni mhimili na Waheshimiwa Majaji na Mahakama zao ambao nao ni mhimili waliona hilo ni muhimu sembuse hizi taasisi za umma ambazo ni za Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limeletwa kwa nia njema kabisa na siyo kila wakati ambapo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inapopata fursa ya ku-*regulate* au kuidhinisha maslahi haya ni lazima ipunguze. Nimeeleza vizuri, tunataka kuoanisha tu maana baadhi ya watu wamelalamika wanasema kuna tofauti kubwa sana ya kipato kati ya mtu wa chini na wa juu. Kwa hiyo, niliona nilifafanue hili lakini moja, hakuna Katiba ilipokiukwa na pia hakuna sehemu yoyote ambapo sheria imekiukwa, ni kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mlio na sheria maana sheria hizi natembea nazo, *The Judiciary Administration Act* ninayo hapa, nendeni msome kifungu cha 30 na 31. Mamlaka ya kupendekeza maslahi ya *Judiciary* yamewekwa kwenye *Judicial Service Commission* ya Mahakama (Tume ya Utumishi wa Mahakama). Vilevile kwenye *National Assembly Administration Act,* 2009, kifungu cha 20 na 21, mamlaka haya yamewekwa kwenye Tume ya Utumishi wa Bunge, lakini bado wanazingatia haya. Hizi sheria zinazozungumzwa sasa za mashirika ya umma, *regulatory authorities*, *bodies* hazikuwa na masharti hayo kama yalivyo kwenye hizi sheria za Mahakama na ya Bunge. Ndiyo maana Serikali inakuja hapa sasa na Muswada huu ili tuoanishe vitu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2009, Sheria hii ya Utumishi wa Umma ilifanyiwa mabadiliko kwenye kifungu cha 31. Kifungu kile kilikuwa kinasema kwamba taasisi hizi zitaendeshwa na sheria zilizozianzisha lakini ikawekwa kifungu kidogo cha (2) kinachosema pia Sheria ya Utumishi wa Umma itatumika. Mwaka jana kwenye Sheria Na.17 ya mwaka 2015 kupitia kifungu cha 22, Bunge hili lilifanya mabadiliko pia kwenye kifungu cha 34 kikaongezwa kifungu kipya cha 34(A). Kifungu hiki kilisema hivi:-

"*Where there is an inconsistency between the provision of this Act and any other written law governing executive agencies, public institutions or such as public service offices, the provision of this Act shall prevail*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *that is the essence* kwamba tumeondoa yale mapendekezo yaliyokuwa kwenye kifungu cha 26 cha Muswada huu. Msingi wake ni kuwa na vitu vya aina hii, una-*harmonize*. Si kwamba Katibu Mkuu Utumishi wa Umma yeye anakaa anaanza kupanga, mapendekezo yanatoka kwenye taasisi husika, wanajenga hoja. Kama ni mashirika ya umma labda

yamezalisha sana, lazima akubali tu kwamba hawa jamaa wamezalisha au wamebana matumizi lazima tuwape *incentives* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme hili wazi kusudi twende na uelewa wa pamoja, ni kitu ambacho kilinigusa sana. Kwa hiyo, baada ya kulisema hilo nadhani Waheshimiwa Wabunge watakuwa wamelielewa hili. Mengine yamezungumzwa lakini nadhani Wabunge hawakupata nafasi ya kusoma, Serikali imeshaleta majedwali mawili, kwa hiyo, mengine yote haya yameshakuwa *taken care of*. Naomba Waheshimiwa Wabunge muikubalie hoja hii nzuri ipite tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameulizwa maswali hapa, maana nikiwa nimekaa hapa Waheshimiwa Wabunge wameendelea kuleta michango, hivi msingi wa mabadiliko kwenye ile sheria inayozungumzia mita 60 kwa ajili ya ulinzi wa mazingira ulikuwa ni nini? Hii imekuwepo hata kwenye Sheria ya Mazingira lakini shida ilikuwa ni kwamba unaanzaje kuzihesabu hizi na nimesema kwenye hotuba yangu, *how to calculate this one, where do you begin and where do you end*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa mgogoro huo ndiyo tukasema sasa tunaleta hiyo tafsiri na kuweka *clarity*. Kwa mfano, wewe una shughuli zako kwenye eneo la mita 60 au umejenga mle, mimi naweza kusema aah, aah mimi niko nje. Sasa kunapokuwa na migogoro kama hii labda anashtakiwa, ndiyo tunataka kuondoa huo utata. Huo ndiyo msingi wa mabadiliko yale, kwa hiyo, naona muunge mkono hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba kulisemea hapa limezungumzwa na Mheshimiwa Bashe kuhusu ile Bodi ya Mfuko wa Mazingira. Tulikuwa na *proposal* kutoka Serikalini tuongeze watu watatu ili wafike kumi na moja na watu hawa ilidaiwa kwamba walitakiwa wawe na ujuzi na utaalam kwenye mambo ya uendeshaji wa Mifuko. Nadhani ilikuwa ni *oversight,* Serikali yenyewe tumeshajiwekea mwongozo kwamba katika hizi hatua za kubana matumizi yasiyokuwa ya lazima kwa kuwa na Bodi nyingi, nyingine ndiyo mnasema zinafanyia mikutano Dubai na kadhalika, basi tu-*streamline* ili Bodi moja wawe aidha wajumbe saba wasizidi tisa. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge mnaona kwenye ile Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu walikuwa wajumbe 15 tumewapunguza, lakini pia kwenye Muswada huu tumeweka fursa ya kualika mtu mwingine ili ku-*co-opt* watu wengine wanaotaka kuwasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tungeenda hivi Serikali ingekuwa inajikanyaga yenyewe. Hapa unaleta watu wengine eti kwa sababu wana utaalam wa uendeshaji wa Mifuko unaongeza gharama kule halafu Bodi ya

muhimu sana kama hii ya Mikopo ya Elimu ya Juu unawapunguza wale watu. Kwa hiyo, ndiyo maana tukaondoa pale ili warudi tisa lakini tumefanya mabadiliko kwenye *Schedule of Amendment* Waheshimiwa Wabunge ambapo sasa huu Mfuko unapata fursa ya kumwalika mtu mwingine yeyote siyo kutoka kwenye mifuko ya uendeshaji bali mtu yeyote kwa maana kama anaweza kuja kuwasaidia namna ya ku-*combat* na kuimarisha vita dhidi ya uharibifu wa mazingira awasaidie siyo utaalam wa kuendesha Mifuko tu. Kwa hiyo, naomba hili Waheshimiwa Wabunge mlikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu pia ndiyo ulikuwa ushauri wa Kamati. Ndiyo msingi wake lakini mtu yeyote kama ana utaalam, anaweza akatusaidia ku-*mobilize availability* ya *funds* kwa ajili ya *running of the activity of this fund,* anakaribishwa. Kwa kweli siamini kabisa kwamba kwa kuweka wale watu mle ndani ndiyo fedha zinaweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri sana *on this one with a serious note,* hali ya uharibifu wa mazingira ni mbaya sana, *if this does not going to be checked accordingly then we are in a mess*. Kwenye suala hili Serikali na Wabunge lazima tuungane tuwe kitu kimoja tupambane na vita kali ya uharibifu wa mazingira, mimi hii naiona ni vita kubwa *second to* ufisadi. Unajua hiyo ndiyo *survival* ya nchi yenyewe. Kwa hiyo, hilo nilifikiri nilifafanue namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeulizwa swali hapa wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia wakitaka nieleze msingi wa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga ikiwa amekamata ndege. Msingi wake nimesema ni pale ambapo hiyo ndege inakuwa kwa namna yoyote wamefanya makosa ya sheria hiyo, lakini makosa ambayo ni kinyume na utaratibu wa Mkataba wa Chicago wa Usafiri wa Anga (*Chicago Convention on International Civil Aviation)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu siyo mpya, upo kwenye sheria hii ambayo leo tunaibadilisha. Kwa hiyo, huo ndiyo msingi wake tu, tunataka sasa kukidhi zaidi masharti ya mkataba ule na ni kwa nia njema kwa ajili ya usalama wenyewe, ndiyo msingi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtu ambaye labda hakuridhika na uamuzi ule anafanyaje? Ukienda Sehemu ya XI ya *Civil Aviation Act* unaona kuna utaratibu pale wa *review and appeals procedures,* haya ni mambo *technical,* hayawezi kwenda moja kwa moja kwa Waziri. Kwa hiyo, wameweka utaratibu pale kuna *Internal Review Committee* na mambo mengine kwa sababu ndege

zenyewe nazo hazipaswi kukaa sana. Kwa hiyo, utaratibu ule upo kwa mtu ambaye amekuwa *aggrieved* na maamuzi yaliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitushauri kwamba tuweke utaratibu huo kwenye Kanuni na Mheshimiwa Waziri anasema anaboresha zile Kanuni zake vizuri kufuatia kuingizwa kwa mabadiliko haya katika sheria. Kwa hiyo, Kanuni ita-*take care* hakuna mtu atakayeweza kudhulumiwa. *At any given point in time* kama mtu hakuridhika na uamuzi wa *review panel* au wa Waziri au wa Mkurugenzi anaweza akaenda Mahakamani. Hilo nalo pia niliona nilifafanue ili liweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niseme mambo kadhaa. Kuna hoja hapa imejengwa kwamba siyo vizuri kuleta Muswada wa Sheria Mbalimbali. Ukweli ni kwamba Bunge linaruhusu Miswada yote ya aina mbili, Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali na Muswada unaojitegemea wenyewe. Kanuni wala Katiba haikatai na ni utaratibu mzuri tu na tumesema kwa nini. Kwa mfano, hapa tunabadilisha sheria tisa yaani hapa sasa leo tungekuwa na Miswada tisa inayojitegemea inawasilishwa na Mawaziri na wakati sheria nyingine labda unabadilisha kifungu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja kwamba haya ni mambo ya kisera, mambo ya kisera siyo ya Bunge ni ya Serikali. Kama Muswada unakuja hapa Serikali tayari huko imeshafanya maamuzi ya kisera. Wajibu wa Bunge sasa ni kutunga sheria ama unaikubali au unaikataa tu.

**MBUNGE FULANI:** Naam! *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa hiyo, kuletwa kwa Muswada huu eti kwa sababu ni wa kisera na hakuna sheria au kanuni inayosema kwamba kwenye mambo ya kisera na Miswada yote *anyway* ni ya kisera tu. Kwa sababu Miswada ya sheria si inatokana na sera? Unaanza na sera ndiyo unakuja kuitungia sheria. Hakuna panaposema kwamba ikiwa ni suala la kisera *you bring a stand-alone kind of a Bill.* Niliona hilo na lenyewe nilifafanue ili lieleweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine ya uwakilishi kwenye Bodi na kadhalika tumeyazingatia kama unavyoona kwenye *Schedule of Amendment*. Nataka kulizungumza moja ambalo Mheshimiwa Kairuki amelizungumzia. Imesemwa hapa kwamba hatua hii ya Rais kuteua Wakurugenzi na watendaji wengine ni kuvunja Katiba, hapana. Mimi ni mtaalam wa Katiba na mimi siyo mtaalam pekee ninayejua Katiba, kuna wanasheria wengi tu waliopo hapa na wasiokuwepo hapa. Ukweli ni kwamba kwa hatua hiyo hakuna sehemu yoyote ambayo Rais anavunja Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza amepewa mamlaka chini ya Ibara ya 36, lakini pia Sheria ya Utumishi wa Umma imesema kuwa hawa Wakurugenzi watateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya *Local Authorities.*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *The Ministers (Discharge of Ministerial Functions) Act,* Rais na yeye mwenyewe ni Wizara anaweza akapanga akajiachia madaraka yake. Hata hivyo, kwa mujibu wa mwongozo ule mliokuwa mnaudai wakati ule, haya ni mojawapo ya mambo ambayo ameyaacha Wizarani kwake, yeye ndiye mwenye dhamana. Kwa hiyo, hakuna ambapo sheria imevunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine tena nikushukuru na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Waziri wa Nchi.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ratiba ya siku hii ya leo kama tulivyokuwa tumesema asubuhi imekuwa na shuguli nyingi na kwa mujibu wa ratiba ya Bunge ni lazima shughuli zote zilizopangwa leo tuzimalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba nitumie tena Kanuni ya 153 na kwa sababu inajulikana sitaisoma ili niweze kutoa hoja kwamba Bunge hili sasa liweze kuendelea mpaka pale tutakapokuwa tumemaliza shughuli hii ambayo ilipangwa kwenye *Order Paper* kwa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda, shughuli inaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15
*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto unataka kusema nini?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hoja kwenye Ibara ya 15.

**MWENYEKITI:** Imeshapita na Bunge limeshahojiwa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, Ibara hiyo imeshahojiwa, *please* kaa! *(Makofi)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruth.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naona itapita hii kwa sababu Serikali imefanyia marekebisho, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina marekebisho kama ilivyotamkwa kwenye Ibara ya 17 na nina hoja nne. Ni kweli kwamba kuna marekebisho yamefanywa na Serikali lakini wame-*consider* Mawaziri wa pande zote mbili; upande wa Zanzibar na upande wa Bara kwa maana ya elimu ya juu. Napendekeza kwenye hii Bodi kuwe na uwakilishi wa *private universities* na *public universities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwenye kipengele (e) napendekeza kuwe na uwakilishi wa mwanafunzi kutoka mwamvuli wowote wa wanafunzi wa vyuo vikuu. Ni muhimu kuwe na uwakilishi wa wanafunzi kutoka elimu ya juu kwa maana ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Bodi wakati inaanza kazi nilikuwepo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hata namna ambavyo huyu mtu anapatikana ilikuwa ni shida maana Waziri anaamua kupendekeza mtu ambaye hata wanafunzi

wenyewe hawakumpendekeza. Ndiyo maana naleta mapendekezo haya. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako liende na mapendekezo ya Serikali kwa sababu zifuatazo. Kwanza, Mheshimiwa Mbunge anapendekeza kwamba tuweke chuo kikuu cha umma na chuo kikuu binafsi. Hii inazingatiwa kwa sababu kutakuwa na mjumbe anayeiwakilisha *TCU* na katika *TCU* kunakuwa na *composition* ya wajumbe binafsi, vyuo binafsi na vyuo vya umma. Kama nilivyosema Bodi ni chombo cha kufanya maamuzi siyo chombo cha uwakilishi. Kwa hiyo, kwa hawa waliopo, walikuwa wajumbe saba tumeongeza wamefika tisa wanatosha

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu kwa upande wa wanafunzi ni kwamba, mwanafunzi ujumbe wake unakuwa *valid* pale anapokuwa mwanafunzi. Kwa hiyo, anapo-*cease* hata kama kipindi cha Bodi kinaendelea tutakuwa tunafanya *rotation*. Suala la kupata majina, wanaletwa na wanafunzi wenyewe, Waziri mimi siwajui wanafunzi, watapendekezana wao wenyewe. Kwenye Kanuni tutaweka kwamba watakuwa wana-*rotate* kwa upande wa Bara na Zanzibar, hilo litazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mapendekezo ya Serikali yakubaliwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwanza hiyo *rotation* anayoizungumza wanafanya *rotation* wakati gani? Tunataka sheria itamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, hao wote anaosema *TCU* walipelekwa kwa malengo mengine, kazi ya Bodi ni tofauti na kazi ya *TCU*. Tulisema katika michango mbalimbali mojawapo ya *confusion* iliyopo ni namna ambavyo *TCU* inaingilia mamlaka ya namna ya kudahili wanafunzi badala ya ku-*regulate* mambo mbalimbali ya *academic issues* katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitoe hoja ili tupate michango mingine ya Waheshimiwa Wabunge. Naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya na Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, wawili wanatosha.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 wakati sheria hii inapitishwa nilikuwa Rais wa Chuo Kikuu cha Tumaini na nilikuwa miongoni mwa Marais wa kwanza waliopigania sheria hii kupita. Pia nilikuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Marais wote nchi nzima wa vyuo vikuu vya Serikali. Natambua kabisa umuhimu wa kuwa na uwakilishi wa wanafunzi kwenye Bodi ya Mikopo kwa sababu maamuzi sahihi yatafanywa na watu ambao wanawafahamu wanafunzi. Ukienda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ni chuo kikuu cha Serikali na chuo kikuu *private,* mazingira ya vyuo vikuu hivi vyote ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana kwenye Bodi ya Mikopo wanafunzi wote wa *public* na *private* wawepo kama wawakilishi sahihi kwa sababu mazingira ya vyuo hivi vyote ni tofauti. Kwa hiyo, naiunga mkono vizuri sana hoja ya Mheshimiwa Waitara. Kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Ndalichako ambaye ni Waziri wa Elimu siyo sahihi hata kidogo kulinganisha *TCU* na Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba marekebisho yaliyoletwa na Serikali yabakie kama yalivyo. Sababu za kwanza naunga mkono zile ambazo ameziongea Mheshimiwa Waziri wangu, lakini pili ukiangalia wajumbe hawa ambao wameainishwa katika hii Bodi, utakuta kila mmoja ana jukumu la muhimu sana katika kuisaidia Bodi hii. Kama tulivyosema kwamba siyo lengo letu kuwa mkutano wa Bodi yaani mkutano wa watu wengi wako pale. Lengo letu ni kuona tunakuwa na Bodi ambayo ni *effective.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika misingi hii ukiangalia waliowekwa *either* kama ni mtu wa *Treasury* tunajua kwamba fedha nyingi zinazohusika kwenye Bodi zinatoka huko. Ukiangalia wajumbe wanaotoka upande wa pili wa Muungano Zanzibar tunahitaji uwakilishi wao lakini wanafunzi pia wapo hapo. Sasa huyu *private sector* ni sawa na yeye tunam-*consider* lakini kwa hali hii hapa hatujawa katika shughuli maalum ile ya uendeshaji wa vyuo, tupo katika shughuli ya kuhakikisha kwamba mikopo inapatikana kwa wakati lakini vilevile inawafikia hawa wadau kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani wakati mwingine tuwe na nafasi ya kukubaliana na Serikali inapokuwa imefanya jambo kwa tathmini kubwa kama hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ukiangalia kwenye Ibara ya 20(7) inatoa fursa sasa kwa Bodi ku-*co-opt* mtu yeyote yule aende mle ndani. Kwa hiyo, hata kama hawapo kama wawakilishi wa jumla pale ambapo Bodi itataka kupata maoni yao kuhusu namna gani hii mikopo inakuwa *disbursed* au kuna *any kind of stumbling blocks and whatever,* bado wanaweza wakamwalika mtu kutoka kwenye hizi taasisi anazozizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sababu ya pili ni suala hili la kudhibiti tu matumizi haya, kuendesha hizi Bodi siyo kazi rahisi, ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo, *spirit* ileile ambayo pia tumeikatalia kwenye hii Bodi ya Mifuko ya Mazingira tukubali na hii ibaki hivi hivi, hatuwezi kuwa na *double standard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ushauri wangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara funga hoja yako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na maelezo yaliyotolewa. Kwanza, wenyewe wamekubali kwamba *TCU* ina kazi zake maalum tofauti na Bodi. Mimi nimekuwa Rais wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mwanzoni nimeshiriki kwenye hii Bodi, maamuzi yanayofanyika ni *very crucial* kwa mustakabali wa wanafunzi. Kwa hiyo, uwakilishi wa wanafunzi kwenye Bodi hii ni muhimu kwa sababu wanafanya maamuzi. Hoja ya fedha kwamba gharama za uendeshaji Bodi zitakuwa kubwa siyo sahihi. Kama mnataka kutenda haki lazima kuwe na uwakilishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hoja hii iamuliwe kwa kura ili rekodi iseme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwamba angalau Serikali kwa sasa imefanya marekebisho, mwanzoni ilikuwa haioneshi ni kwa muda gani wataanza kurejesha mkopo, lakini sasa wamesema ni baada ya mwaka mmoja. Hata hivyo, tunakubaliana kwamba kuna shida kubwa sana ya ajira katika nchi hii, *being it* ya Serikali au ya watu binafsi. Naona kwa mwaka mmoja bado ni muda mchache sana na kuna *fine* zimeorodheshwa humu kama mtu atashindwa kurudisha mkopo ina maana anaweza akawajibishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa sababu ya mazingira haya, maana tusitunge sheria kwa kujiangalia sisi, tutunge sheria kwa hali halisi ilivyo huko mtaani, ugumu wa ajira na watu wanavyopata shida. Naomba angalau tuongeze iwe miaka miwili ili huyu mtu kama ataweza kujitafutia fedha au apate kazi aanze kurejesha. Hayo ndiyo mapendekezo yangu kwamba itoke mwaka mmoja angalau iwe miaka miwili kwa kuzingatia hali halisi ya ajira Tanzania na hali halisi ya vijana na mazingira tuliyonayo kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba tayari Serikali imekwishaongeza muda. Mwanzoni tulikuwa tunapendekeza kwamba iwe *immediately,* lakini baada ya mapendekezo tumeweka mwaka mmoja. Naomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono kwa sababu vijana wanaohitaji mikopo wako wengi na siyo kweli kwamba wanafunzi wote wanaomaliza ndani ya mwaka mmoja wanakuwa hawana uwezo wa kurejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mapendekezo ya Serikali yabaki kama yalivyo bila marekebisho ya Mheshimiwa Waitara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sikubaliani na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu hali halisi kila Mtanzania anajua kwamba kupata kazi siyo jambo rahisi. Wapo vijana mtaani ambao wamepata mikopo mnataka wakamatwe wafungwe miaka miwili, miaka mitatu, minne hadi mitano kazi hawajapata wako mitaani wanahangaika. Sasa ikitokea kipindi kama hiki ambacho Mheshimiwa Rais amezuia ajira, wapo mtaani na wana *qualifications* lakini hawawezi kuajiriwa kwa sababu Rais amezuia, anafanya uhakiki wa watumishi hewa. Sasa mazingira kama haya unayachukuliaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ili tupate maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwa upana wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Kikwete.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tunapaswa tulitazame kwa mapana sana na naomba Waziri wa Elimu na Serikali ilitazame jambo hii vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana au mtu yeyote anapomaliza elimu anakwenda kupata ajira. Kwa mfano, amepata ajira mara moja, huwezi ukaanza kumkata mkopo mara moja. Unapaswa umpe muda wa kujipanga kwenye maisha ndiyo aanze kukatwa mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wafanyabiashara humu watanielewa, ukienda benki kuomba mkopo *private sector* unapewa *gestation period* kwa ajili ya kuanza kuzalisha ndiyo unaanza kulipa mkopo. Hii *principle* ya kwamba ukimaliza chuo ndani ya mwaka uanze kulipa mkopo, tumeitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa kiongozi wa Serikali ya wanafunzi *(DARUSO),* jambo hili tulilijadili sana na tulikubaliana baina ya viongozi wa Serikali za wanafunzi kwamba ni lazima tutoe *gestation period.* Kipindi kile tuliweka miaka miwili kwamba miaka miwili baada ya kupata ajira.

**WABUNGE FULANI:** *Yes!*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Kwa hiyo, sasa hivi mnasema mwaka mmoja baada ya kumaliza chuo, haitawezekana! Tuimarishe mifumo ya vijana hawa kuweza kulipa na kwenye Kamati tulimpatia Mheshimiwa Waziri namna gani ya

kufanya ili watu hawa waweze kulipa lakini msiwabane vijana hawa walipe *immediately* baada ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara na tupate *consensus* hapa kwamba iwe ni mara baada ya kupata ajira na siyo baada ya kumaliza…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Miaka miwili baada ya kupata ajira.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Sawa! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami siko mbali sana na Mheshimiwa Waitara, mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilisema, mazingira yetu ya sasa yanafahamika na sisi ndiyo wawakilishi wa watu hao. Tutaongopa hapa na tutajiongopea sisi wenyewe na kizazi chetu na wote wanaotutazama wakitegemea kwamba sisi wawakilishi wao tutazungumza ya ukweli, kama tutasema ndani ya mwaka mmoja mtu huyu alipe hizi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza hapa katika mchango wangu ajira zenyewe zimekuwa ngumu, vijana hawa mnataka walipe baada ya mwaka mmoja watatoa wapi pesa hizi? Napenda niungane na Mheshimiwa Waitara kwamba kama suala la hata asiye na ajira ajitafute basi miaka miwili iwe ni kipimo cha kutosha. *Otherwise* tuangalie vijana hawa watakapopata ajira waanze kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara kwamba kiuhalisia tukiangalia wanafunzi wanaomaliza masomo wengi wao hawapati ajira moja kwa moja. Wanakaa mitaani miaka miwili, mitatu, minne, kuna wengine mpaka miaka sita wako mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kiuhalisia kama tunataka tuwasaidie Watanzania tuweke miaka miwili baada ya kupata ajira. Maana hata ukipata ajira bado utahitaji wewe mwenyewe kujiweka sawa. Kwa hiyo, tuwape miaka miwili ya kujiweka sawa wao wenyewe *then* baada ya pale ndiyo waanze kulipa mikopo. Hivi tulivyoiweka sasa hivi haitaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kabisa Waheshimiwa Wabunge tuwasaidie Watanzania wanaomaliza chuo wanakaa mitaani hawana kazi, mwisho wa siku hapa tutakuta wanaenda kuuza ardhi ili wakalipie mikopo ikiwa tutaweka kama Serikali ilivyopendekeza. Nashauri iwe miaka miwili baada ya kupata ajira ndiyo watakiwe kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyefahamu kwamba suala la ajira nchi hii ni tatizo sana. Hakuna *guarantee* ya mtoto akimaliza chuo kikuu anaenda kupata ajira ya uhakika. Kama kungekuwa na *guarantee,* hicho Serikali mnachokisema kiko sahihi ilivyo sasa haitaweza kutekelezeka. Hao wanafunzi watamaliza vyuo halafu mtawataka ndani ya mwaka mmoja warejeshe mikopo, hakika mtaenda kuwaumiza vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waitara kwamba iwe ni baada ya miaka miwili, wajipange ndipo waanze kulipa hiyo mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengwerwa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Afuate Haonga baada ya Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tulipata fursa ya kutosha kujadili suala hili. Nami nataka niwaambie Watanzania tunao vijana wetu wengi ambao wanahitaji mikopo hii. Iwapo tutaruhusu suala hili la kufanya *extension* ya muda, vijana wetu wengi watakosa mikopo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vizuri marekebisho ya sheria husika tuliongeza kifungu cha kuruhusu yule ambaye hajapata ajira kuweza kutoa shilingi laki moja kila mwezi.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Anatoa wapi?

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiruhusu hili Watanzania wataendelea kuwa wavivu…

**MBUNGE FULANI:** Ajira ziko wapi?

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Tunasema haya wazi kabisa. Wapo vijana ambao hawajasoma lakini wamejiajiri na wanapata kipato cha kutosha.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Serikali yako vizuri na sisi Kamati tulijiridhisha kwa kina kwamba kipindi cha mwaka mmoja kinatosha. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa…

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Haonga hapa naendelea kuchangia hata bila ya kuniruhusu maana huniruhusu wewe. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nani yule Ulega?

**MBUNGE FULANI:** Kingu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Haonga, Haonga!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu endelea.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia suala hili kwa heshima kabisa ya Watanzania vijana wetu, wadogo zetu na kwa uzalendo wa nchi yetu. Nataka nikupe mfano, mimi binafsi nina mdogo wangu ambaye ni wa mwisho katika familia yetu, amemaliza *University of Dodoma* leo ana mwaka wa nne mtaani hajapata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na Mawaziri wetu tunazungumza kwa nia njema kwa maslahi ya watu maskini wa hii nchi. Ikifika mahali tukashindwa kuona hali halisi ya Taifa, tukashindwa kuona hali halisi ya Watanzania na tukatumia nafasi yetu kama Wabunge, kwa nia njema kabisa naomba Mawaziri mtuelewe nia yetu Wabunge ni kuwasaidia Watanzania ambao watakwenda kuathirika nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi msimamo wangu naungana na kaka yangu Mheshimiwa Waitara kwamba *tu-extend* muda ili kusudi watoto wa Kitanzania wafaidike. Ndugu zangu ngoja niwaambie tu kweli, leo tunazungumza masuala ya ajira ndiyo tuko kwenye *phase* za kutaka ku-*industrialise* hii nchi, leo tukisema watu wamalize chuo kikuu wakatengeneze ajira na kujiajiri na kupata kipato ni wangapi wanaweza wakamudu? Kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa unajua nakupenda na najua wewe ni kichwa lakini mtoto hana ajira hiyo Sh.100,000/= anaitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika hili kwa maslahi ya watu tunaowawakilisha tusimame na tuseme kwamba hapana vijana wetu wapewe angalau hiyo miaka miwili na iwekewe *clause* kwamba pale tu watakapokuwa wamepata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Aha, aha, Mheshimiwa Flatei.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Bahati nzuri mimi nimesoma, nakataa moja kwa moja kumfanya mwanafunzi aliyemaliza chuo hajapata kazi aendelee kulipa Sh.100,000/= anaweza kulipa kwa kutumia nini? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Very true, very true. (Makofi)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwana CCM, naipenda sana CCM na naipenda sana Serikali, lakini kwa kuzingatia *background* ya watoto wetu wanaotoka katika familia maskini hawataweza. Kwa mfano, mimi leo nimesoma kwa kujitegemea, mkopo sijapata nikiambiwa nirejeshe hizo fedha nazitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa nia njema kabisa na nawashawishi Wabunge wenzangu mlioko humu, mkubaliane na hili kwamba kwa kweli wasubiri mtu atakapopata kazi hapo hapo ndiyo aanze kulipa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Tupige kura.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Aise usiwe *bias,* angalia kote kote bwana.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naona hoja hii imechangiwa kwa hisia kubwa sana.

Mheshimiwa Mweyekiti, niseme kwamba dhamira ya Serikali ya kuweka kipengele hiki ilikuwa njema ukizingatia kwamba hata sasa hivi tunavyoongea wapo wanafunzi wengi ambao wanahitaji mkopo lakini hawajaweza kupata. Lengo lilikuwa wale ambao wanakuwa na uwezo warejeshe fedha mapema ili wengine waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza haya maelezo na majadiliano ambayo yameendelea kuhusiana na kipengele hiki, Serikali kama nilivyosema ilikuwa imeleta hili jambo kwa nia njema, lakini pia michango iliyotolewa naamini imetolewa kwa nia njema hiyohiyo. Kwa hiyo, Serikali inakubaliana na mapendekezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipengele chetu ambacho tulikuwa tumeongeza kwamba yule ambaye anapata aanze kulipa kinabaki kama kilivyo. Kwa hiyo, tunaweka miaka miwili lakini yule ambaye atapata mapema aweze kuanza kulipa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji, kifungu hiki…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza hoja.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, subirini basi kwanza. Mheshimiwa AG unaiwekaje?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki sasa kitasomeka hivi:-

"*Repayment of loans shall become due after completion of studies in respect of which the loan was granted or where studies are terminated for any reason:*

*Provided that, the beneficiary shall be obliged to commence repayment of loan after the period of two years upon completion or termination of studies*".

**WABUNGE FULANI:** Aah, aah!

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Ndivyo alivyopendekeza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo hiyo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapa tunatunga sheria, naomba AG apewe nafasi ya kusema, kama kuna hoja mtapewa nafasi ya kujibu. Masuala ya makelele hapa siyo sokoni.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Haya ndiyo mapendekezo ya Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Marekebisho yaliyokuja ni ya Mheshimiwa Waitara.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Ndiyo mapendekezo yaliyokuja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Na tumeyakubali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Tumeyaboresha.

**MWENYEKITI:** Mwenye hoja ni Mheshimiwa Waitara na Serikali imekubali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Ndiyo! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa iweke vizuri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kile kifungu kidogo cha (4) kinabaki ambacho kinasomeka hivi:-

"*Without prejudice to subsection (3), the beneficiary may commence repayment of loan at any time immediately after completion or termination of studies*". Yaani anapewa fursa yule mwenye uwezo aanze kulipa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, wewe ndiyo mwenye mapendekezo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maboresho ya Waheshimwa Wabunge walio wengi… *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aha, aha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuelewane, kwa sababu kimsingi wala siyo kwamba tunapambana na Mheshimiwa Waziri wala Serikali. Waheshimiwa Wabunge, wanatoa maoni kutokana na hali halisi iliyopo mtaani kwamba tukishakubaliana hapa tukapitisha, utekelezaji unakuwaje? Sasa wanapendekeza iwe miaka miwili baada ya kupata ajira, ndiyo Wabunge wengi wameboresha namna hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG!*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kulikuwa na mapendekezo ya msingi kwa sababu hapa *technically,* hata tukienda kwenye sheria…

**WABUNGE FULANI:** Tumeboresha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *schedule* yake yeye mwenyewe kuna *technically error* kwa sababu Ibara ya 19 anayoizungumzia siyo yenyewe. Sisi tumefanya tu hapa hekima kwa sababu ni jambo linalowagusa watu wote. Kwa hiyo, *technicality this could have not passed through*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Ni *wrong citation*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa sababu ya *wrong citation* na kwa *principle* hii hatuikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba mapendekezo ya Serikali jinsi yalivyo kwenye Muswada yabaki hivyohivyo isipokuwa kuwe na *amendment* tulipoweka mwaka mmoja iwe miaka miwili na Waziri apate fursa ya kuanza kutengeneza Kanuni. Vinginevyo, kama hali ikiwa ni hivi hata hao wengine hawataweza …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** *Speaker's guidance.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, subirini! Mheshimiwa Waitara, *amendment* yako ya mapendekezo ya miaka miwili yamekubaliwa…

**WABUNGE FULANI:** Tumeboresha.

**MWENYEKITI:** Umetaka *one pound of flesh* umepewa sasa unataka *another drop of blood? Merchant of Venice hiyo, you have to give in* maana Serikali imeshakubali *two years. (Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo yangu ambayo yameungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge lakini Serikali ione umuhimu wa kuboresha kadri Waheshimiwa walivyopendekeza hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara ndiyo mwenye hoja na kwa mujibu wa Kanuni umeshakubali kaa chini.

**WABUNGE FULANI:** Tuliboresha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji...

**WABUNGE FULANI:** Tumeboresha.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo. Kwanza naomba tupate *spirit* ya *consensus* yaani tusishindane, tuwe na *consensus* tu. Kwa hiyo, naomba tumsikilize na *AG* anavyozungumza kwa sababu yeye ndiyo mtalaam wa sheria, atatusaidia namna gani ya kuweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *problem* yangu ni kwamba, hii *amendment* ambayo Serikali ilikuwa imeileta ukiachana na kifungu kilichokuwemo kwenye Muswada iko *detailed* sana. Tukiichukua tu bila kukubaliana hapa tutajikuta tumeacha baadhi ya mambo mazuri yaliyomo kwenye hii *amendment* kwa sababu tu ya kubishana kuhusu *one year or two years, employment or before employment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninakiomba *AG* atusaidie, mapendekezo ambayo Mheshimiwa Waitara ameyaleta na maoni ambayo Wabunge wameyatoa aya-*incorporate* ndani ya ile *amendment* ambayo yeye alikuwa ameileta kwa sababu inatoa *freedom* kubwa zaidi na *flexibility* kwa Serikali kwa namna ya kuweza ku-*implement*. Naomba aiangalie ile *amendment* yake kabla hujatuhoji kwa sababu kuna kitu tutakipoteza.

**MWENYEKITI:** Kwa vile tunatunga sheria, tunataka tutoke hapa wote tumeelewana, *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyokuwa kwenye *First Schedule of Amendment* ingekuwa na shida lakini hii *Further Schedule of Amendment* imekuwa *so much clear.* Kwa hiyo, hapa haiwezi ikaleta shida yoyote. Suala lilikuwa ni muda gani huyu mwanafunzi aliyenufaika na mkopo aanze kulipa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mkiangalia kwenye *Further Schedule of Amendment,* kwenye *clause B,* tumesema:-

*"Repayment of loan shall become due after completion of studies in respect of which the loan was granted or where the studies are terminated for any reason:*

*Provided*, *provided* ni sharti, sasa sijui kwa Kiswahili wanasemaje, *provided that the beneficiary shall be obliged to commence repayment of loan after the period of two years upon completion or termination of his studies*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna vitu viwili, moja ni wakati gani deni linaiva? Deni tumesema linaiva wakati huyu bwana anapokamilisha masomo yake au wakati ambapo kwa namna yoyote ile masomo yake yamesitishwa au yamekatishwa kwa namna yoyote ile haendelei lakini sasa ni wakati gani aanze kulipa? Ndiyo sisi tulipendekeza awe na *grace period* ya mwaka mmoja na Waheshimiwa Wabunge mnasema sasa iwe miaka miwili na Serikali inakubali, ndiyo aanze kulipa.

**MBUNGE FULANI:** Miaka miwili baada ya kupata ajira.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeweka sharti kwamba, kwa sababu kuna watu wengine ambao kwa namna yoyote ile labda wanapata uwezo au wanapata kazi mapema au wanajiajiri *whatever,* yule ambaye ana uwezo wa kuanza kurudisha mkopo mapema kwa hiari yake kabla ya hata hiyo miaka miwili naye awe na fursa hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* umeeleweka.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* ameeleweka na mwenye *amendment* amekubali.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**MWENYEKITI:** Sasa nawahoji kuhusiana na mapendekezo ya Ibara hii.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Katibu.

Ibara ya 20

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napendekeza kwamba mwajiri atoe taarifa kwa *Loan Board* baada ya miezi mitatu badala ya siku ishirini na nane ambazo zimewekwa kwenye Muswada.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, miezi mitatu badala ya siku ishirini na nane.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lake Mheshimiwa Dkt. Sware la miezi mitatu sijafahamu ni kwa nini kwa sababu utamaduni ni kwamba mtu anapoajiriwa anajaza zile *particulars* zake moja kwa moja, mambo ya *medical check up,* mambo ya mfuko atakaoweka, sijui kwa nini hili la Bodi ya Mikopo lisubiri.

Waheshimiwa Wabunge, hizi fedha Serikali tunaweka kwa nia njema kabisa kwamba, ziweze kuwanufaisha watu. Sasa mtu ameshapata ajira tumeisogeza miaka miwili halafu akipata ajira isogee miezi mitatu, naomba akubaliane na mapendekezo ya Serikali kwamba mtu anapoajiriwa *notification* ifanyike ndani ya siku ishirini na nane ili tuweze kuanza kurejesha mapema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nili-*suggest* baada ya miezi mitatu kwa sababu mtu anapokuwa amepata ajira huwa kunakuwa na *probation period.* Kwa hiyo, nilikuwa nimetoa miezi mitatu ambayo ni *standard,* wengine wanakwenda mpaka miezi sita lakini angalau miezi mitatu, pale anapopata *confirmation letter of employment* basi yule mwajiri ndiyo atoe taarifa. Maana unaweza ukawa unatoa taarifa, una-*update* una-*lose track* au unakuwa unamwonea yule kijana ambaye unataka kumwambia alipe huo mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaona hiyo mantiki kwa sababu ukipata ajira, umeajiriwa. Hilo suala la *probation* wengine inachukua mwaka mzima kutofautiana na kazi na wengine

ni miezi sita. Kwa hiyo, nafikiri mnufaika na mwajiri wawe na wajibu wa kutoa taarifa, hayo mambo ya kwamba atakuja kufukuzwa kazi yatakuja kujitokeza pale tutakapofika. Sioni sababu ya kuanza kuvuka mto kabla hatujafika kwenye mto wenyewe, tukifika mtoni ndiyo tutavuka, lakini atoe taarifa, kama kutakuwa na changamoto itatolewa taarifa, mimi sioni kuna tatizo gani katika hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware, kama kuna changamoto taarifa itatolewa.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Bado nasisitiza, wengine pia tumetoka kwenye hizo ajira ama *private* au Serikalini, lakini kunakuwa kuna *probation period* yaani hupati *confirmation* siku ambayo umeambiwa umepata kazi. Kwa hiyo, ili kutokuchanganya mambo, kutoa *information* kwa *Loans Board* kila baada ya miezi sita, ndiyo maana na-*suggest at least* baada ya miezi mitatu *then* una uhakika huyo kijana ameajiriwa hiyo sehemu ndiyo yule mwajiri atoe taarifa kwa *Loans Board.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kama Wabunge wanataka kujadili hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Kangi na Mheshimiwa Angellah. Tuanze na Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono sana hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware kwa sababu ni kweli kwamba unapoajiriwa leo mahali pengine wanakaa mwaka mmoja ndiyo wanapata *letter of confirmation.* Tumesikia hata Wabunge humu ndani jinsi ambavyo kumekuwa na tatizo kubwa la *data.* Kwa hiyo, nadhani hakuna sababu ya Bodi ya Mikopo leo wamepelekewa majina halafu keshokutwa baada ya miezi miwili yule mtu hayuko kazini. Kwa hiyo, nadhani hoja ni ya msingi sana kwamba angalau wakae miezi mitatu ili yule mtu awe ameshapata *letter of confirmation, then* wanakuwa na uhakika kwamba huyu ni mwajiriwa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yetu na nadhani ni ya msingi sana na naiunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi.

**MHE. KANGI A.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ama kweli usemi wa kukopa harusi kulipa matanga ndiyo unajitokeza katika hoja ya Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Dkt. Sware. Umeshapata mkopo, umeshasoma

umemaliza, kuna mahali umepata kazi mpaka na barua ya ajira wakakupatia sasa suala la kusubiri tu *confirmation* limzuie mwajiri wako asiwasiliane na Bodi ya Mikopo kwamba huyu mtu wenu jamani yuko hapa?

Mheshimiwa Dkt. Sware, hebu tuwe wawazi, umesha-*enjoy* sana hapa, leo taarifa tu na taarifa hizi kwenye *database* hazitamgharimu huyu mwajiri ambaye baadaye hata asipom-*confirm* ikaonekana kwamba baadaye anatoa taarifa huyu mtu hatukum-*confirm* au aliacha kazi aliona ujira ni mdogo, mawasiliano haya hayawagharimu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba akubaliane tu na pendekezo la Serikali, tena hata siku ishirini na nane ni nyingi, unatakiwa unaajiriwa leo, kesho taarifa zinatolewa kwamba huyu mtu yuko hapa, kwa hiyo twende na hizi siku ishirini na nane. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Maghembe.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo inayotolewa kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu ni kama *revolving fund* kwamba wale ambao wameshafaidika na mikopo hiyo wakishaanza kazi walipe ili na wengine nao wapewe mikopo hiyo. Kwa hiyo, ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na *compliance* lazima kila mmoja aeleze alipo na siku ishirini na nane ukiwa umepata kazi kueleza kama uko hapo siyo kwamba unaanza kulipa unaeleza kwamba niko hapa nimepewa kazi. *What is the worry,* unataka kujificha?

Mikopo hii siyo zawadi, mikopo hii ni *revolving fund* inayotolewa kwa watoto wa Tanzania ili waweze kusomesha wanafunzi waliopo na baadaye mikopo watakayolipa isomeshe wenzao. Kwa hiyo, naunga mkono mapendekezo ya Serikali ya ku-*notify within twenye eighty days. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angellah.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami niunge mkono mapendekezo ya Serikali ibaki hivyohivyo siku ishirini na nane hasa ukizingatia kwamba hapa ni *obligation* tu ya *employer* kutoa taarifa kwamba katika taasisi yake ina mwajiriwa mpya.

Pili, ukienda katika kifungu kidogo cha (b), Bodi sasa ikishaangalia katika orodha yake baada ya kuwa imepokea *notification* kwa mwajiri, ikiona kwamba yule mtumishi ni mtu ambaye alikuwa *loan beneficiary* ndiyo itaanza

kukata malipo. Kwa hiyo, nadhani wasiwe na hofu, siku ziwe ishirini na nane, baada ya hapo watakuja kupitia orodha na kama kweli ni mnufaika basi ndiyo makato yataanza kufanyika, siku tisini kwa kweli ni nyingi sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya michango hiyo, naomba ibaki kama ilivyoletwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dkt. Sware, Serikali imesimamia *twenty eight days*.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka tu tena kufafanua zaidi, nimetoa hii *suggestion* ili kuondoa mkanganyiko wa *information* zinazoenda *Loans Board.* Namba moja, nimesimamia kwamba kwenye *employment* yoyote kuna *probation period,* kwa nini usisubirie mpaka *probation period* ikaisha ukapata *confirmation letter then* unatoa *information* ambayo ina uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, tumetoka kupitisha hapa kwamba unaanza kulipa *loans two years after being employed,* kwa nini sasa hivi tunakimbilia kutoa taarifa *within twenty eight days* wakati naanza kulipa ule mkopo *after two years?* Kwa nini tusiwe na *information* ambayo inaeleweka kuliko kila saa kuanza ku-*counter check* watumishi hewa au *data* hazieleweki. Kwa hiyo, pendekezo hili nataka kuisaidia Serikali ili kuwa makini na tunachokifanya na uhakika wa unachokifanya *then at least three months* baada ya kuwa *employed,* ni hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa nitahoji, hatuwezi kurudi tena Serikalini.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye Ibara ya 20 hakijaisha, kuna mapendekezo yangu na ya Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MWENYEKITI:** Huna mapendekezo Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Ninayo.

**MWENYEKITI:** *Schedule* yako hii hapa ipo Mezani kwangu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Ya Mheshimiwa Dkt. Sware yapo *the same*.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Waitara.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina mapendekezo yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Sware Ibara yako ni ya 20.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Ibara ya 20(a)(b).

**MWENYEKITI:** Kinahojiwa pamoja, hakina (a) na (b). Lazima mpate ushauri wa kisheria mnapoandika hizi *amendments* zenu, Ibara hii tumeshahoji imekwisha.

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, endelea na Ibara ya 21.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwendo kasi, sawa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Ibara ya 21 iondolewe ingawa umetuondoa kwenye hoja ya msingi sana asilimia hiyo ni kubwa. Maelezo ya Ibara ya 21 kipengele cha (2),(3) na kuendelea hayana shida lakini pale wanaonesha kama wanataka kuwa na *retention fee,* kifungu hicho hakipo kwenye mkataba wa mkopo wa mwanafunzi na hakiko kwenye makubaliano, ni kitu kipya ambacho kinaibuliwa. Ndiyo maana napendekeza Ibara ya 21(1) iondolewe na aweze ku-*renumber* zile namba nyingine ambazo zinafuatia pale, ndiyo hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21 anayoizungumzia ni ile inayosema:-

"*This Part shall be read as one with the Public Service Act, hereinafter referred to as the "Principal Act".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukikiondoa hiki maana yake ni kwamba hutafanya tena mabadiliko kwenye hiyo sheria yote. Ndiyo maana uko sahihi unapomwambia Mheshimiwa Mbunge Waitara kwamba hiyo anayoisema haipo, *unless* tunakubali kwamba hata mabadiliko yote kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma tuyaondoe. Naomba kushauri na Mheshimiwa Waitara, mabadiliko yake haya ayaondoe kwa sababu kwanza hayana tija yoyote baada ya kupata ile tija kubwa kwenye mikopo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado sisi siyo wageni hivyo kwenye masuala haya. Mwombe ushauri wa kisheria wakati mnaleta *amendments* zenu. Siyo jambo zuri kuleta vitu halafu baadaye ukajikuta unachanganyikiwa. Kwa hiyo, mwanzo ni mgumu naelewa, lakini tuwe *very careful* wakati tunaleta *amendments* kwenye Bunge.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 44

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 48

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49
Ibara Mpya ya 50

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja. *(Makofi)*

## T A A R I F A

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2016)* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2016),* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo tisa kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu kwa hatua hii sheria hii imeshapitishwa na Bunge, sasa itakwenda kwa Mheshimiwa Rais kwa hatua ya *signature* kwa idhini yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, *AG,* Serikali yote kwa ujumla lakini pamoja na Wabunge wa pande zote mbili kwa michango mizuri. Tulisema Serikali hii ni sikivu, imeongeza miaka miwili bila matatizo yoyote, kwa hiyo msilalamike Serikali hii haisikilizi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, wanafunzi watafurahi kwa sababu Bunge lao na Serikali yao imewakubalia mikopo ilipwe baada ya miaka miwili. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Miaka miwili baada ya ajira.

**MWENYEKITI:** Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.17 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 9 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*